23 APRILI, 2013

# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIA NO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA KUMI NA MOJA

**Kikao cha Kumi na Moja - Tarehe 23 Aprili, 2013**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Job A. Ndugai ) Alisoma Dua*

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati Ifuatayo Iliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:**

Randama za Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Maji kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014.

**MASWALI NA MAJIBU**

Na. 86

**Kupeleka Umeme – Sekondari za Kata.**

**MHE. HEZEKIAH N.CHIBULUNJE (K.n.y. MHE. DKT. DAVID M. MALLOLE)** aliuliza:-

Chanzo kimojawapo kinachosababisha taaluma katika shule zetu za Kata kushuka ni ukosefu wa Nishati katika maabara, Maktaba na kwenye Mabweni ya wanafunzi.

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kupeleka umeme shule za Kata hasa zile za Bweni ili kuimarisha taaluma kwenye shule hizo?

(b) Je, shule za Kata za Kikombo, Mpunguzi na Ipagala katika Jimbo la Dodoma Mjini watapata lini umeme ambao wameahidiwa kwa muda mrefu sasa?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (ELIMU)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. David Mciwa Mallole, Mbunge wa Dodoma Mjini, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, kupitia mpango wa Elimu ya Sekondari awamu ya pili, Serikali itakamilisha ujenzi wa shule za sekondari 1,200 kwa kuweka miundombinu muhimu ikiwemo umeme, awamu ya kwanza imeanza kwa shule 264 kwa thamani ya shilingi bilioni 56.3 ambapo suala la umeme wa gridi ya Taifa au umeme wa jua limepewa kipaumbele.

Aidha, Serikali kupitia mfuko wa wakala wa usambazaji umeme Vijijini (*REA)*imedhamiria kusambaza umeme katika zahanati, shule na visima vya maji vilivyo katika maeneo yatakayonufaika na huduma hii ya umeme Vijijini.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, mpaka sasa Serikali imewezesha shule za sekondari 3,385 sawa na asilimi 75 ya shule zote za sekondari nchini kuwa na huduma ya umeme.

Kuanzia mwezi machi 2011,shule ya sekondari Kikombo ilianza kutumia mfumo wa umeme wa jua kupitia mradi wa *TASAF.* Aidha, kuanzia mwezi februari 2013,shule za sekondari Mpunguzi na Mbambala zilianza kutumia umeme wa gridi ya Taifa baada ya Shirika la Umeme Tanzania *(TANESCO)* kukamisha upatikanaji nguzo za umeme katika maeneo ya shule.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali itaendelea kashirikiana na Wadau na kupitia miradi mbalimbali ya maendeleo kuhakikisha dhamira ya kuziwezesha shule na maeneo mengine yanayotoa huduma za jamii yanakuwa na huduma ya uhakika ya umeme.

**MHE.HEZEKIAH N.CHIBULUNJE:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri ninapenda kuuliza, maswali mawili ya nyongeza.

(a) Kwa kuwa, Mheshimiwa Naibu Waziri amesema kuwa uko mpango ambao unalenga kupeleka nguvu za umeme katika maeneo ya shule Zahanati na kadhalika. Sasa ninataka kujua Serikali i itaweka Bajeti katika shule za sekondari zote ili kuweza kuzipatia umeme kadiri inavyowezekana?

(b) Kwa vile kuna shule nyingi za sekondari sasa hivi amabzo ziko karibu na njia za umeme kama vile Manchali na maeneo ya Itiso. Je, katika mpango huo Serikali inaweza ikaelekeza Wizara inayohusikakufikisha umeme maeneo hayo ambayo yako karibu sana na nguzo za umeme?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (ELIMU):** Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda nimhakikishie Mbunge kuwa mpango wa Serikali kuhakikisha kuwa shule zetu zinapata nishati ya umeme upo na tumefikia hatua nzuri kwa sababu hadi sasa tunazo shule elfu moja mia moja na saba zina umeme wa gridi,tunazo shule elfu na thelathini na tisa zina umeme wa sola, lakini pia tuna shule elfu moja, mia mbili ishirini na saba zina umeme wa jenereta na shule kumi na mbili zinatumia umeme wa *biogas* na katika hili ninataka kutoa wito katika Halmashauri zetu nchini ziweke taratibu zake kupitia mapato ya ndani kuwezesha shule zetu zote kuwa na umeme moja kati ya maeneo haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, umeme unaweza kuwa wa gridi kama nguzo zitakuwa zimepita katika eneo hilo au kutumia sola ambazo sasa hivi zinapatikana katika maduka mengi. Lakini pia kutumia nishati hii tuliyonayo jirani ya *biogas,* ili kuwezesha shule zetu kuwa na umeme uweze kuwasaidia walimu na wanafunzi walioko katika maeneo hayo.

Lakini pia inao mpango kupitia njia kuu za umeme zinazopita njia ya karibu ya Taasisi zinazotoa huduma kama ambavyo nimeeleza ikiwemo shule, vituo vya afya na maeneo ambayo ni muhimu sana kama vile visima vya maji vinavyotakiwa kuvuta maji kwa hiyo, mpango upo na tutaendelea kuutekeleza.

**MHE. LETICIA M. NYERERE:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa mtindo uliopo sasa hivi wa kuwataka wanafunzi kwenda shuleni wakiwa wakiwa wamebebeshwa majembe, mafagio sijui sululu na mashoka unaleta *distruction* kwa watoto wanashindwa ku- *focus* katika masomo.

Je, Serikali haioni kuwa huu mtindo umepitwa na wakati na ni Tanzania peke yake ambapo asubuhi ukiamka unaona watoto wamebeba majembe, mafagio na sululu *(Vicheko).*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Leticia swali la msingi lilihusu Nishati lakini Mheshimiwa Naibu Waziri tafadhali majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (ELIMU):** Mheshimiwa Naibu Spika,naomba kujibu swali la Mheshimiwa Nyerere ambaye amekaripia sana watoto wetu kubeba nyundo na nini, jambo hili ninataka kulieleza kuwa wala halikuwa geni toka huko tulikokuwa tukisoma shule pale ambapo shule inaona kuna umuhimu wa kufanya usafi katika maeneo yao lakini pia kuendeleza kipindi kile cha Elimu ya Kujitegemea.

Tunachosema siyo utamaduni na wala siyo maagizo ya Kiserikali kwamba shule zianze kubebesha watoto majembe, mafagio na kila kitu tunaomba shule zetu zote ziweke

utaratibu wa kuwa na stoo wakishakusanya kuwe na stoo inayotunza majembe, kuwe na stoo inaweka mafagio badala ya kubebesha watoto hawa kila siku barabarani ili kuondoa usumbufu uliopo. Mheshimiwa Leticia, jambo hili kwa agizo hili nina amini litatekelezwa katika shule zetu. *(Makofi)*

**MHE. HENRY D.SHEKIFU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru; kwa kuwa utekelezaji wa mradi wa *MCC* maeneo mengine yamerukwa na umeme haukufika kwenye taasisi na imepita kwenye taasisi kama vile Jimbo la Lushoto eneo la Mkuzi, Kwefingo pamoja na shule ya Mkuzi Juu. Serikali inatamka nini maana hili limezusha mgogoro mkubwa wa malalamiko ili shule hizi zilizorukwa zipate umeme?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (ELIMU):** Mheshimiwa Naibu Spika, kufuatia miradi hii ya *MCC* ambayo pia tunaitekeleza katika maeneo yetu ya elimu lengo ni kuhakikisha kuwa shule zetu hizi zinakuwa na mwamko na mabadiliko kadiri ambavyo sisi tunakusudia ili kufikia malengo haya ya *Millenium Challenge* ili kuzipa mwelekeo mzuri, mvuto mzuri kw maana ya maeneo ya shule na taasisi zetu ziwe ni mahali ambapo taaluma inaweza kutolewa na inaweza kumfikia mtoto ili aweze kupata mabadiliko haya, kulingana na mabadiliko ya sayansi na teknolijia.

Kwa hiyo, mpango wetu Serikali ni kuimarisha mikakati hii ili shule zetu zipate mashiko ya kuweza kuhakikisha kuwa shule hizi zinapata mabadiliko makubwa. *(Makofi)*

Na. 87

**Ukamilishaji wa Ujenzi wa shule za sekondari Rombo**

**MHE. JOSEPH R. SELASINI** aliuliza:-

Kutokana na uhaba wa ardhi katika Kata ya Keni, Shimbi, Mrao Keryo, katika Jimbo la Rombo, wananchoi wameamua kujenga shule za sekondari kwa mtindo wa

ghorofa na shule hizo ni pamoja na sekondari za Keni,Bustani na Shimbi.

Je, Serikali itakuwa tayari kuchukua shule hizo na kukamilisha ujenzi wake ili kuunga mkono juhudi za wananchi wa Rombo wa kuwapa nafasi kuchangia miradi mingine.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (ELIMU)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu naomba kujibu swali la Mheshimiwa Joseph Roman Selasini, Mbunge wa Rombo, kama nilivyolijibu tarehe 7 Juni, 2012 kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango mmoja wapo wa wananchi katika kufanikisha ujenzi wa shule za sekondari za Kata ni kuwezesha upatikanaji wa ardhi kupitia Serikali za vijiji. Kutokana na ufinyu wa ardhi wananchi wa Rombo waliamua kujenga shule za sekondari za Kata kwa mtindo wa ghorofa ni shule ya sekondari Keni inayojengwa katika Kata ya Keni, shule ya Sekondari Shimbi inayojengwa katika Kata ya Shimbi na shule ya Sekondari Bustani inayojengwa katika Kata ya Mrao Keryo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2010/11Serikali katika kuunga mkono jitihada za wananchi kupitia Halmashauri ya Wilaya ya Rombo ilitoa jumla ya shilingi milioni 625 kwa ajili ya miradi ya maendeleo ya elimu katika shule zote 41 za Serikali. Kwa kuzingatia gharama za ujenzi wa ghorofa shule hizo tatu zilipata mgao ufuataoo:-

Shule ya sekondari Bustani ilipewa shilingi milioni 57.6, Keni ilipewa shilingi milioni 53.9 na Shimbi ilipewa shilingi milioni 53.9.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ujenzi wa shule za sekondari za Kata ni ubia kati ya wananchi, Halmashauri na Serikali Kuu. Shule za sekondari za Kata zinazojengwa ni mali ya Halmashauri husika. Katika mwaka wa fedha 2013/2014

Halmashauri ya Wilaya ya Rombo imeomba kuidhinishiwa shilingi milioni 234 kwa ajili ya kuendeleza ujenzi wa shule za sekiondari Bustani, Keni na Shimbi. Aidha, Halmashauri imewasilisha maombi maalum ya shilingi bilioni 2 kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa shule hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninatoa wito kwa Halmashauri kusimamia matumizi sahihi ya fedha hizi na kuhakikisha maelezo ya Serikali ya kukamilisha miradi ya zamani yanazingatiwa kabla ya kuanza miradi mipya ukiwamo ukamilishaji wa ujenzi wa shule ya Sekondari Keni, Bustani na Shimbi.

**MHE. JOSEPH R. SELASINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ninashukuru kwa majibu ya Waziri na pia ninamshukuru sana kwa agizo lake alilotoa jana kwamba wale walimu walioanza ajira zao mwaka huu walipwe kwa kuwa walikuwa hawajalipwa kwa muda wa miezi mitatu ninadhani litazingatiwa. Pamoja na hayo nina maswali mawili madogo ya nyongeza.

Swali la kwanza kwa kuwa majengo haya yameanza kuchakaa na kwa kuwa wananchi sasa uwezo wa kuendelea kuchangia umekuwa ni mdogo. Je, Serikali inawaambiia nini wananchi haya maombi ambayo yametolewa na Halmashauri yamezingatiwa katika Bajeti ya mwaka ujao wa fedha 2013/2014?

Swali la pili, Halmashauri ya Rombo wananchi waliitikia vizuri sana katika kuchangia ujenzi wa hizi shule za Kata, ambapo kuna shule karibu 41 za kidato cha nne. Sasa Serikali iko tayari kuruhusu shule ya sekondari ya Mahida iliyoko katika Kata ya Mahida na shule ya sekondari Orombo iliyoko katika Kata ya Mkuu zipandishwe hadhi na kupewa kidato cha tano na cha sita?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (ELIMU):** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu maswali mawili ya Nyongeza Mheshimiwa Selasini, Mbunge wa Rombo, kama ifuatavyo:-

Kwanza juu ya maombi halali ambayo pia nimeyaeleza kwenye jibu la msingi ya shilingi bilioni 2 kwa kuwa tayari Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu TAMISEMI imeshapita hapa kwenye hatua za awali yataendelea kuangaliwa ili pia yaweze kusaidia harakati za kuhakikisha shule zetu kule zinapata fedha ya kutosha kuweza kukamilisha miundo mbinu yake na shule ziweze kuendelea katika hali ambayo tunaihitaji.

Swali la pili, la shule hizi za Mahida na Rombo kuomba kuwa kidato cha tano na cha sita kwa mujibu wa taratibu za Wizara ya Elimu ambayo pia ndiyo inatoa kibali cha kupandisha kuwa kidato cha sita kama maombi yameshawasilishwa na Halmashauri kwa Wizara, Wizara itatuma wataalam wa idara ya ukaguzi kutoka katika kanda yenyewe watafanya ukaguzi wa awali na baada ya ukaguzi wataandika taarifa na itaenda Wizara ya Elimu na baadaye Wizara ya Elimu inaweza kuridhia.

Wito wangu kwenu ni kuhakikisha kuwa vigezo vyote vinavyotakiwa kukamilisha shule hizo kuwa kidato cha sita sasa vikamilishwe ili mtakapoita timu ya ukaguzi ili mpate kibali kile iwe rahisi kuruhusiwa na jambo hilo linaweza kuamriwa mara tu vigezo vitakapokamilika.

Na. 88

**Kuipandisha Hadhi Barabara ya Mchingo Kijiweni kuwa ya Mkoa**

**MHE. SAID M. MTANDA** aliuliza:-

Barabara ya Mchinga hadi Kijiweni ni muhimu sana kwa shughuli za kiuchumi, ulinzi na usalama:-

(a) Je, ni lini barabara hii itapandishwa hadhi na kuwa barabara ya Mkoa?

(b) Je, ni fedha kiasi gani zinazohitajika katika matengenezo ya barabara hiyo ili iweze kupitika kwa mwaka mzima?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Said Mohamed Mtanda, Mbunge wa Mchinga, kama ifuatavyo:-

(a)Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ninatambua jitihada kubwa ambazo Mheshimiwa Mbunge anafanya katika kuhakikisha barabara hii inatengenezwa na kupitika wakati wote. Barabara ya Mchinga Kijiweni ina urefu wa kilomita zipatazo 37.3. Nilipokuwa katika ziara Mkoani Lindi nilikagua barabara hii na nilishuhudia kuwa iko katika hali mbaya kiasi cha kuhitaji matengenezo makubwa na maalum.

Kwa mantiki hii nakubaliana kabisa na pendekezo la Mheshimiwa Mbunge la kuipandisha hadhi barabara hii ili iwezre kuhudumiwa na Mkoa. Aidha, pendekezo la kupandishwa hadhi barabara hii litapelekwa katika Wizara ya Ujenzi ambayo ndiyo yenye dhamana kwa mujibu wa Sheria baada ya kupitishwa katika vikao vya Baraza la Madiwani, Kamati za Ushauri za Wilaya na Mkoa pamoja na Bodi ya Barabara.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, katika Bajeti ya Wizara ya Fedha 2012/2013 barabara hii ilitengewa kiasi cha shilingi milioni 112.1 kwa ajili ya matengenezo ya mara kwa mara *(routine maintanace)* urefu wa kilomita 35 na matengenezo ya muda maalum urefu wa kilomita 4.5. Halmashauri ya Wilaya ya Lindi imefanya makisio ambapo fedha kiasi cha shilingi milioni 337.5 zinahitajika kwa ajili ya kuweka changarawe katika sehemu iliyobaki ya barabara ili iweze kuwa katika hali nzuri na iweze kupitika wakati wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Bajeti ya mwaka 2013/2014, Halmashauri imewasilisha maombi maalum Wizara ya Fedha na Uchumi ya shilingi milioni 380.0 kwa ajili ya matengenezo ya barabara hii. Aidha, Halmashauri ya Wilaya ya Lindi inashauriwa kuweka barabara hiyo katika vipaumbele vyake vya Bajeti ili iweze kupata matengenezo yatakayoifanya ipitike wakati wote.

**MHE. SAID M. MTANDA:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Mchinga nimshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa kazi kubwa aliyoifanya alipotembelea Jimbo hili na kukagua barabara kadhaa ikiwemo barabara hii. Llakini kwa kuwa ujenzi wa barabara hii ikiambatana na ujenzi wa tuta kubwa au daraja pale Mchinga ilikuwa ni ahadi ya Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, katika kipindi cha Uchaguzi Mkuu uliopita.

Kwa kuwa Mheshimiwa Waziri Mkuu alinitaka nipeleke vielelezo na maandishi mbalimbali yanayoonyesha kwamba barabara hii ni muhimu sana kwa wakazi wa maeneo ya Mchinga na Kijiweni. Je, Serikali sasa iko tayari kutoa waraka maalum kwa Halmashauri ya Wilaya ile ukielekeza barabara hii sasa ijengwe kwa kiwango cha changarawe ili kuepusha usumbufu unaojitokeza kila mara kwa kurudiarudia fedha nyingi za wananchi zinapotea kwa kujenga kwa kiwango cha udongo.

(b) Kwa kuwa tuliomba shilingi milioni 380 ili kuweza kujenga daraja lile au kuinua tuta pale Mchinga ili wananchi waweze kupita na kwa kuwa, maombi hayo tuliwasilisha toka mwaka jana na Serikali hapa Bungeni ilikubali kuyafikisha maombi hayo Wizara ya Fedha. Je, Wizara ya Fedha kwa kuwa imo humu ndani, Waziri wa Fedha yupo, Manaibu Mawaziri wapo, wapo tayari sasa kutueleza kwamba maombi yale maalum yamekubaliwa na fedha hiyo shilingi milioni 380 tutapata ili ujenzi wa tuta lile kubwa au daraja lile la Mchinga liweze kukamilika. (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Spika, mimi namwomba ndugu yangu rafiki yangu Said Mtanda asitumie nguvu kubwa sana hapa, kama alivyokiri hapa na Waziri wa Nchi yupo hapa Mheshimiwa Hawa Ghasia alinituma mimi niende nikakague barabara hii, katika jibu letu tumekiri. Mimi Bamvua kwanza nilikuwa sijui maana yake, nilikuwa nafikiri kama ni mto hivi unapita kumbe kuna wakati Bahari inakupwa basi unakuta maji yamejaa pale halafu baadaye unaweza ukapita pale ukaiona barabara iko vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka niseme kwamba Mheshimiwa Said Mtanda anakumbuka kwamba nilienda kukagua barabara hii usiku na tuliionana na tumekiri katika jibu hili kusema kwamba ni kweli anachosema Mbunge pana tatizo pale.

Sasa kuhusu suala la kupandisha hadhi, anayepandisha hadhi barabara, mapendekezo yanatoka kutoka kwenye Halmashauri yanakwenda kwenye *Regional Consultative Committee* na yanakwenda kwenye Bodi ya Barabara ya Mkoa.

Lakini hatimaye anayesema sasa nakubali barabara hii ipande hadhi ni Waziri wa Ujenzi, yeye ndiye anatamka hivyo na akishatutamkia basi barabara ile inahama na Bajeti zake zinakwenda kwenye Bajeti za Mkoa.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara hii inayozungumzwa hapa fedha zinazohitajika hapa ni shilingi milioni 380, Halmashauri ya Wilaya ya Lindi fedha yake ambayo imetengwa ambayo itapita hapa sasa kama itakubalika, hii tumeshaipitisha hapa ni shilingi milioni 667. Kwa hiyo akichukua nusu ya pesa ile akapeleka pale maana yake ni kwamba barabara nyingine zote zitakuwa hazina kitu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nikubaliane kwa niaba ya Waziri Mkuu na Mheshimiwa Mtanda kwamba ni kweli *he has a point*, niombe hapa kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu, sisi kwa sababu mwaka jana tulimjibu swali hilo na mwaka

huu tumemjibu tena hivyo kusema kwamba tunaendelea tuombe wenzetu wa Wizara ya Fedha, tukae nao wote kwa pamoja TAMISEMI na Wizara ya Fedha tuzungumzie jambo hili kwa pamoja na Mheshimiwa Mtanda nimwombe tuwe wote kwa pamoja, kwa sababu maombi maalum ni maombi maalum Serikali itakubali au kukataa kufuatana. Tukae wote watatu tukishakaa wote watatu tuweze kuondoka katika tatizo hili.

**MHE. MWIGULU L. M. MADELU:** Mheshimiwa Naibu Spika ahsante sana. Hizi barabara zinapopandishwa hadhi kuwa za Mkoa zinachelewa sana kutengewa fedha na wakati ule ule zinakuwa hazitengewi tena fedha na Halmashauri kwa kuwa zimeshapandishwa daraja na hivyo kusababisha hata zisipitike. Mfano ni barabara ya Shelui, Ntwike kwenda Kidaru na barabara ya shelui-Mtoa kwenda Urugu.

Kwa kuwa Serikali ni moja. Je, Waziri atakuwa tayari kusema kwamba Serikali sasa itakuwa inatenga fedha angalau za kuwezesha barabara hizo zipitike wakati hazijatengewa Bajeti rasmi?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli nchi yetu tumegawa barabara katika makundi manne makuu, kwanza kuna barabara Kuu, halafu tuna barabara za Mikoa, tuna barabara za Wilaya na barabara za Vijiji. Barabara Kuu na Barabara za Mikoa zinahudumiwa na *TANROADS,* na barabara za Wilaya na Vijiji zinahudumiwa na TAMISEMI. Yameletwa maombi mengi sana kuhusu kupendekeza barabara zipandishwe hadhi kutoka barabara za Wilaya ziende barabara Kuu na za Mikoa kwa mategemeo kwamba ziweze kutengenezwa vizuri zaidi. Lakini barabara hizi nyingi ambazo zimeletwa nyingi hazikidhi vigezo ambavyo vinatakiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili barabara ya Mkoa kwa mfano ili kutoka Wilaya ipande daraja ni lazima kwanza iunganishe makao makuu ya Wilaya na na Makao Makuu ya Wilaya nyingine hicho ni kigezo cha kwanza.

Naomba sana Bodi za Mikoa ziwe zinaangalia vigezo hivi vilivyoainishwa kwenye sheria kabla ya kupeleka kwa Waziri wa Ujenzi. Waziri wa Ujenzi hawezi kwenda kinyume na sheria ambayo amepewa mamlaka kupandisha daraja.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la kuhusu kwanini hazijatengenezwa, ni kweli barabara nyingi ambazo zimependekezwa na zikapitishwa nyingi ya barabara hizo kwanza unakuta ni kama palio la ng'ombe haipo barabara, kwa hiyo ina maana inahitaji bajeti kubwa ili iweze kutengenezwa. Serikali inaendelea kutafuta fedha za ziada ili kusudi barabara hizi ambazo zimependekezwa zipandishwe hadhi ziweze kutengenezwa katika kiwango kinachotakiwa kuitwa barabara ya Mkoa. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mchemba, tunakushukuru kwa swali zuri, ama kweli wananchi wa Iramba wana Mbunge mahiri. Swali linalofuata ni la Mheshimiwa Deogratias Aloyce Ntukamazina. (*Makofi/Kicheko*)

Na. 89

**Shilingi Elifu Kumi (10,000/=) kwa ajili ya *Capitation Grant* kwa kila Mwanafunzi**

**MHE. DEOGRATIAS A. NTUKAMAZINA** aliuliza:-

Wakati wa Mpango wa MMEM I Serikali ilikuwa inatoa shilingi 10,000 kama *Capitation Grant* kwa kila mwanafunzi wa shule ya msingi kwa ajili ya kununulia vitabu, chaki na vifaa vingine vya kufundishia; Shule za Msingi katika Jimbo la Ngara zina matatizo makubwa ya ukosefu wa vitabu kwa sababu ya kupewa shilingi 200 tu ya *Capitation Grant* badala ya shilingi 10,000/= kwa kila Mwanafunzi:-

(a) Je, Serikali inawaambia nini wananchi wa Ngara juu ya kumaliza tatizo hilo?

(b) Je, ni lini Serikali itarejesha *Capitation Grant* ya shilingi 10,000 kwa kila Mwanafunzi badala ya shilingi 200 ambayo haitoshi kununulia vitabu na vifaa vingine?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA(ELIMU)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri Mkuu naomba kujibu swali la Mhehsimiwa Deogratias Aloyce Ntukamazina, Mbunge wa Ngara, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Kupitia Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi Serikali imekuwa ikitoa fedha za uendeshaji wa shule *Capitation* kwa kiwango cha shilingi elfu kumi kwa kila mwanafunzi. Awamu ya kwanza ilitekelezwa kuanzia mwaka 2002 hadi mwaka 2006 na awamu ya pili ilitekelezwa kuanzia mwaka 2007 hadi mwaka 2012.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika awamu hii Serikali imekuwa inatuma fedha za uendeshaji kadiri zilivyokuwa zinapatikana. Asilimia 40 ya fedha za uendeshaji wa shule zimekuwa zinatumika kwa ajili ya ununuzi wa vitabu na Serikali imekuwa inatekeleza mpango huu kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imekuwa inahakikisha kiasi cha shilingi elfu kumi kwa mwanafunzi kinafikiwa kwa kuendelea kutoa fedha za uendeshaji kila robo ya mwaka. Hadi kufikia mwezi Machi, 2013 Serikali imeshatoa jumla ya shilingi bilioni 60 za *Capitation* kwa shule za msingi nchini kote. Kiasi hiki ni sawa na shilingi 7,565 kwa mwanafunzi ambayo ni sawa na asilimia 75.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa Halmashauri ya Wilaya ya Ngara jumla ya shilingi milioni 465 zimeshapelekwa ambazo ni sawa na shilingi 6,816 kwa mwanafunzi ambayo ni asilimia 68.2. Aidha, Serikali imekamilisha mikataba ya zabuni ya shilingi bilioni 30 kwa ajili ya ununuzi wa vitabu kwa shule za msingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nimhakikishie Mbunge kuwa Serikali itaendelea kutoa kiasi kilichobaki cha wastani wa shilingi 3000 kwa mwanafunzi kadiri ya makusanyo ya Serikali yatakavyopatikana hadi kufikia mwishoni mwa mwaka wa fedha wa 2012/2013.

**MHE. DEOGRATIAS A. NTUKAMAZINA:** Mheshimiwa Naibu Spika ahsante sana. Pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri ninalo swali moja la nyongeza.

Kwanza nianze kwa kusema kwamba swali hili nililipeleka kwa Katibu wa Bunge mwaka 2011 leo ndiyo linajibiwa, kwa kuwa linajibiwa leo, nitamwomba Naibu Waziri atakapokuja kujibu swali langu la nyongeza aongeze shule za sekondari kwa sababu na zenyewe zina matatizo makubwa ya uhaba wa vitabu. Ninajua kwamba kutokana na Mpango wa MMES kila mwanafunzi wa sekondari anastahili kupata shilingi 25,000 kwa ajili ya vitabu na mambo mengine.

Mhehsimiwa Naibu Spika, niliuliza swali hili mwaka 2011 baada ya kufanya utafiti katika shule za msingi na kuona kuna uhaba mkubwa wa vitabu, sasa pia nimetembelea shule za sekondari kuna uhaba mkubwa sana. Nilikuja nikawaona viongozi Watendaji Wakuu wakakubaliana na mimi kwamba kuna tatizo hilo na wakasema kuna mkakati.

Je, ni lini mkakati huo wa kusambaza vitabu katika shule za msingi na shule za sekondari katika Wilaya ya Ngara na nchi nzima utaanza kutekelezwa?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA(ELIMU):** Mheshimiwa Naibu Spika, kama ambavyo nimesema kwenye jibu la msingi kwamba ununuzi wa vifaa kama vitabu kwa shule za msingi na sekondari umeandaliwa katika maeneo mawili, moja ni kupitia *capitation* ambayo tunaitoa, na kwa elimu ya msingi tumesema eneo la vitabu tumetenga asilimia 40 kwa ajili ya ununuzi wa vitabu. Lakini pia kwa sekondari tuna asilimia 50 ya *capitation* yake kwa ajili ya ununuzi wa vitabu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo tunayo mipango ya kununua vitabu nje ya utaratibu huu. Kwa shule za msingi tuna nyongeza ya bilioni thelathini ambazo tumezitenga na zabuni zake zimeshatolewa tayari na kwa hiyo usambazaji wake unaweza ukaanza wakati wowote. Lakini zaidi ya hiyo kwa shule za msingi kwa idadi kubwa waliyonayo tuna zile fedha za marejesho ya Rada ambayo tulitenga bilioni 55.2 kwa ajili ya ununuzi wa vitabu pekee ikiwa ni asilimia 75 ya fedha zote za fedha za Rada.

Kwa hiyo, bado tuna mkakati mzuri wa kupata vitabu vingi vya kutosha na utaratibu wa kusambaza vitabu hivyo zabuni hizi zitakapokamilika, kwa sababu wachapishaji wameshapatikana tayari kwa hiyo watalaam wanakamilisha taratibu za mwisho ili wasambazaji wapeleke vitabu moja kwa moja mpaka shuleni. Hivyo hivyo kwa sekondari.

Mhehsimiwa Naibu Spika, kwa shule za Sekondari pamoja na *capitation* ambayo tumekwishatuma bilioni 40 kufikia mwezi machi tayari zimeshasambazwa na kama nilivyosema kwamba asilimia 50 kwenye ile bilioni 40 ya kila shule ni kwa ajili ya vitabu pekee.

Lakini hata hivyo, tuna bilioni 31 ambazo pia nazo tumetuma kwa ajili ya ununuzi ikiwa ni fedha iliyotengwa na TAMISEMI kwa ajili ya kununua vitabu pia kwenye eneo hilo. Tuna uhakika mkakati wetu wa kumfanya mtoto kwa somo kuwa na kitabu kimoja tutaufikia baada ya kipindi kifupi.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Naibu Waziri, swali fupi sana la nyongeza Mheshimiwa Assumpter Mshama.

**MHE. ASSUMPTER N. MSHAMA:** Mheshimiwa Naibu Spika ahsante sana. Kwa kweli ningeomba tu kumwuliza Waziri, hivi ni kweli sisemi kwamba anadanganya lakini nataka nipate uhakika kwa sababu katika Wilaya yangu ya Misenyi nimezunguka Wilaya nzima nikiwauliza walimu kama *capitation* inakuja wanasema hawajapata, sijui ni Wilaya yangu tu iliyobaki tu ambayo haijapewa au na Wilaya zingine zipo ambazo na zenyewe hazipata?

Mheshimiwa Waziri naomba kusaidiwa.

**NAIBU SPIKA:** Jibu kwa kifupi sana Mheshimiwa Naibu Waziri Majaliwa Kassim Majaliwa.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (ELIMU):** Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nimhakikishie kwamba fedha za *capitation* tumezipeleka kwenye Halmashauri zote nchini na kama kuna mashaka ya fedha hizo kufika kwa agizo hili, Wakaguzi wa Ndani wa Halmashauri hii ya Misenyi waende kwa Mkurugenzi waone kama fedha zote zilizoingia kutoka TAMISEMI kwa ajili ya *capitation* ya shule za Msingi na shule za Sekondari kwamba zote zimepelekwa. Kama taarifa hiyo haijapatikana basi Mbunge nadhani utapata taarifa kutoka kwenye Halmashauri yako tujulishe kama fedha hiyo haijafika kwenye Halmashauri lakini tuna hakika imeshaifika.

Je, wameshapeleka kwenye shule za Msingi au Sekondari. Kama haijafanyika hilo tutachukua hatua dhidi ya Mkurugenzi. *(Makofi)*

Na. 90

**Leseni za Kuchimba Madini**

**MHE. PROF. KULIKOYELA K. KAHIGI** aliuliza:-

Makampuni kama *TANCAN, Resolute* na kadhalika yalikuja nchini siku nyingi na kupata leseni za utafiti ambao umefanyika kwa muda mrefu:-

Je, ni lini Kampuni hizo zitachukuliwa leseni za kuchimba Madini Bukombe na Mbogwe ili yaanze kazi hiyo na kulipa kodi ili kuchangia maendeleo katika maeneo husika?

**NAIBU WAZIRI NISHATI NA MADINI (MHE. STEPHEN J. MASELE)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini naomba kujibu swali la Profesa Kulikoyela Kanalwanda Kahigi, Mbunge wa Bukombe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa uzoefu uliopo shughuli za utafutaji madini zinachukua muda mrefu kabla ya mgodi kuanza, kwa mfano migodi ya Bulyanhulu na Geita ilifunguliwa takribani miaka 30 ya utafiti uliofanywa na kampuni mbalimbali ikiwemo *STAMICO* katika maeneo yenye migodi hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, maeneo ya Bukombe, Mbogwe yaliyopo Mkoani Geita ni maeneo maarufu kwa shughuli za madini hususani dhahabu. Kampuni mbalimbali pamoja na wachimbaji wadogo wamekuwa wakijishughulisha na utafutaji na uchimbaji wa madini hayo katika maeneo kadhaa. Kampuni kubwa za utafutaji madini kama *TANCAN* na *Resolute T. Ltd,* kupitia kampuni tanzu ya Mabangu *Minerals Ltd, African Barrick Gold, Pangea Minerals Ltd* na mengineyo yamekuwa yakijishughulisha na utafutaji wa madini katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kampuni za *TANCAN* na *Resolute T. Ltd*, zimeonesha mafanikio kiasi katika utafiti wa madini katika maeneo ya Nyakafuru ambapo takribani mashapo yenye wakia 700,000 za dhahabu yamebainishwa. Mradi huo upo katika hatua za awali za upembuzi yakinifu na utafutaji zaidi wa madini unahitajika ili kuongeza kiasi cha mashapo ya dhahabu kufikia angalau wakia milioni moja ambapo mgodi mkubwa wa dhahabu unaweza kuanzishwa. *(Makofi)*

Tunamwomba Mbunge awe na subira ili utafiti unaofanywa na kampuni ya *Resolute* eneo la Nyakafuru ukamilike kwa mujibu wa leseni ya utafutaji madini iliyotolewa katika maeneo hayo kabla ya kuchukua leseni ya uchimbaji. *(Makofi)*

**MHE. PROF. KULIKOYELA K. KAHIGI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru ninayo maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Naibu Waziri alisema kuwa utafiti wa madini Nyakafuru umegundua mashapo yenye wakia laki saba za dhahabu, lakini hakutaja mashapo ya huko Kigosi ambako *TANCAN* imefanya utafiti imegundua wakia kiasi gani za dhahabu?

Swali la pili; umewataja wachimbaji wadogo, Je kuna mpango gani wa kuwasaidia wachimbaji wadogo wadogo katika maeneo ya Bukombe na Mbogwe?

**NAIBU WAZIRI NISHATI NA MADINI (MHE. STEPHEN J. MASELE):** Mhehsimiwa Naibu Spika, ni kweli nimetaja kiwango cha mashapo cha utafiti unaofanywa na Kampuni ya *Resolute* kiasi cha wakia 700,000 na taarifa mpaka hivi sasa kwa maana ya ripoti ya utafiti ya kampuni ya *TANCAN* hawajatuletea kuona kwamba mpaka sasa tunavyozungumza wamegundua kiasi gani cha mashapo katika eneo wanalofanya utafiti.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye majibu yangu ya msingi sikuzungumzia wachimbaji wadogo, lakini kwa kuwa umeuliza niseme tu kwamba katika eneo la Mbogwe, Ushirombo tumetenga maeneo kwa ajili ya wachimbaji wadogo hasa kwenye eneo la Ng'anzo ambapo palikuwa na mgogoro wa leseni na maeneo mengine tunaendelea kuzungumza na makampuni makubwa ambapo mashapo yale kwa ajili ya uchimbaji mkubwa ugunduzi uliofikiwa mpaka hivi sasa hautoshelezi kufanya mradi ule kuwa *commercial,* basi maeneo yale tumeomba makampuni yaweze kufikiria kuyaachia kwa ajili ya wachimbaji wadogo.

**NAIBU SPIKA:** Maswali ya nyongeza ya mwisho ya Mheshimiwa Vicky Kamata na Mheshimiwa Kabwe Zitto yatakuwa ya mwisho. Mheshimiwa Vicky Kamata.

**MHE. VICKY P. KAMATA:** Mheshimiwa Naibu Spika ahsante. Kwa kuwa, Serikali iliamua kuanzisha Mikoa minne katika nchi yetu na Geita ikiwa mojawapo na ili mikoa hii iweze kupiga maendeleo kwa kasi ni lazima iweze kuvutia wawekezaji wa ndani na wawekezaji wa nje, lakini mpaka sasa ninavyoongea nilikuwa Geita kuanzia siku ya Ijumaa, Jumamosi na Jumapili Geita hakuna umeme kabisa, umeme unawaka dakika tano unakatika siku nzima, unawaka dakika mbili unakatika siku tatu, yaani siyo umeme wa uhakika. Kwa namna hii kweli tunaweza tukapiga maendeleo katika Mkoa wetu wa Geita?

**NAIBU SPIKA:** Majibu kwa kifupi Naibu Waziri japo naona swali limehama.

**NAIBU WAZIRI NISHATI NA MADINI (MHE. STEPHEN J. MASELE):** Mheshimiwa Naibu Spika, nakiri kweli swali limehama lakini kwa taarifa tulizonazo, eneo la Geita na maeneo mengine ya Maswa tuna matatizo makubwa ya miundombinu ya umeme kwa maana ya zile *transmission* line zimekuwa zina matatizo, mvua zikinyesha kubwa zinakuwa nguzo za umeme zinaanguka. *TANESCO* wanalazimika kuzima umeme kwa ajili ya kufanya matengenezo hayo.

Kwa hiyo, nataka nimhakikishie Mbunge kwamba Wizara ya Nishati na Madini imejizatiti kuhakikisha kwamba tatizo la mgawo wa umeme halipo na matatizo yanayojitokeza haya madogo madogo ni kwa sababu ya matatizo ya kiufundi na mafundi wetu wanalazimika kuzima umeme kwa ajili ya kurekebisha.

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Naibu Spika nashukuru kwa kunipa nafasi. Pale Nzega katika mgodi ambao umemaliza muda wake na kufungwa hivi sasa wa *Resolute* kulikuwa kuna makubaliano kati ya kampuni ya *Golden Pride,* Kampuni ya *Resolute* na Chuo Kikuu cha Dar

es Salaam kwamba eneo lile mara baada ya shughuli za uchimbaji kukamilika litageuzwa kuwa *University Collage* kwa ajili ya kuwafundisha Watanzania namna gani masuala ya Jiolojia na kadhalika.

Lakini taarifa ambazo zipo hivi sasa ni kwamba mmeamua eneo lile liwe Gereza. Hivi Serikali haioni aibu kugeuza eneo ambalo linaweza kuwa la mafunzo kwa ajili ya Watanzania kuweka wafungwa?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. STEPHEN J. MASELLE):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na madini, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Zitto Zubeir Kabwe, Mbunge wa Kigoma Kaskazini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, si kweli kwamba, eneo la Mgodi wa Nzega, limegeuzwa kuwa litakuwa Magereza. Kawaida mgodi unapofikia mwisho kuna utaratibu wa *Mining Closure Plan,* ambayo kunakuwa na Kamati inayojadili ni hatua zipi zitafuata baada ya mgodi kufungwa.

Kamati hii ina uwakilishi kutoka kwenye Halmashauri husika, eneo husika; kwa kesi ya Nzega, Halmashauri ya Nzega, inakuwa na uwakilishi wa mgodi wenyewe. Lakini pia wanakuwa na uwakilishi wa Wizara kwa maana ya Serikali, ambapo *Chief Inspector* wa Madini ndiye anayekuwa Mwenyekiti wa Kamati hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa katika Kamati ile ndipo wanapojadili ni matumizi yapi yatafuata baada ya mgodi kufungwa na taratibu zote kwa mujibu wa Sheria kama zimefuatwa na mgodi husika katika kufuata taratibu za ile *Mining Closure Plan. (Makofi)*

Kwa misingi hiyo, yako mawazo mengi yalikuja katika vikao hivyo, ikiwemo kwamba, Idara ya Magereza iliomba eneo lile ilitumike kwa ajili ya magereza. Lakini kama Wizara na Kamati, maamuzi ambayo sisi tumeyafikia ni kwamba, eneo lile litaendelea kutumika kama ambavyo ilivyokusudiwa mwanzo iwe ni sehemu ya mafunzo kwa ajili ya wanafunzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nipende kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge pamoja na Wabunge wote na Watanzania na wananchi wa Nzega kwamba, taarifa za kwamba, mgodi ule unakwenda kuwa Magereza, siyo za kweli. Pengine wategemee taarifa rasmi kutoka kwa Serikali. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge, mkitazama pale juu mtaona tuna wageni ambao ni wanafunzi wenye matatizo ya kusikia, viziwi na kuna mtu ambaye anafanya tafsiri kwa kutumia lugha ya alama. Kwa hiyo, naomba sana msishangae kuona nini kinaendelea.

Swali la Mheshimiwa Jenista Joakim Mhagama.

Na. 91

**Mradi wa Maji Peramiho**

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA** aliuliza:-

Katika Bajeti ya Mwaka 2011/2012 Serikali, iliahidi kusaidia uanzishwaji wa mradi wa umeme wa maji katika maporomoko ya Lingatuta Mahanje, Tarafa ya Makiba, katika Jimbo la Peramiho:-

Je, ni kiasi gani cha fedha kimetengwa, ili mradi huo uanze?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Jenista Joakim Mhagama, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 1996 Serikali, kupitia Kampuni ya Kijerumani iitwayo *Lahmeyer International,* ilifanya utafiti wa uzalishaji umeme katika maporomoko ya Lingatuta yaliyoko mto Njegeya, karibu na *Mahanje Mission* na Madaba.

Aidha, ulifanyika utafiti katika maporomoko ya mito Lumeme, Ngongi, Luaita, Luwiko na Lupilo. Matokeo yalionesha kuwa maporomoko ya Lingatuta yangeweza kuzalisha *Mega Watt 3.6* na Nakatuta *Mega Watt 9.2.* Sambamba na utafiti huu, utafiti mwingine ulifanywa na Serikali ya Tanzania na Norway katika maporomoko ya mto Masigira na kuonesha uwezo wa kuzalisha *Mega Watt 118.*

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali, inayo dhamira ya kuendelea miradi yote hii kwa ushirikiano na Sekta Binafsi. Mradi wa Lingatuta, unaendelezwa kwa kupitia Wakala wa Nishati Vijijini *(REA),* kwa ushirikiano na Serikali ya Urusi. Kwa sasa Mshauri Mwelekezi *Global Village Partnership (GVEP),* anakamilisha upembuzi yakinifu, ambapo wananchi wa Kijiji cha Mahanje na Vijiji jirani kwa ushirikiano na Dayosisi ya Songea ya Kanisa Katoliki chini ya Usimamizi wa *REA* wanashirikiana kuendeleza mradi huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, miradi ya Nangatuta na Masigira, nayo iko katika hatua mbalimbali za kuendelezwa kwa ushirikiano na Sekta Binafsi. Aidha, kwa sasa Serikali, imeelekeza nguvu zaidi katika utekelezaji wa mradi mkubwa wa Makambako – Singea, utakaohusisha shughuli zifuatazo:-

(i) Ujenzi wa njia ya usafirishaji umeme yenye uwezo wa *kV 220*.

(ii) Ujenzi wa Kituo cha kupozea umeme chenye misongo ya *kV 230/33.* Kituo hiki kitajengwa maeneo ya Madaba na umeme utakaozalishwa Lingatuta utaunganishwa Madaba kwa kuzingatia ushauri na maombi ya muda mrefu ya Mheshimiwa Mbunge, Jenista Mhagama.

Mheshimiwa Naibu Spika, dhamira ya mradi huu ni kuunganisha Mkoa wa Ruvuma na Gridi ya Taifa. Aidha, Wilaya za Njombe, Ludewa, Njombe, Mbinga, Songea Mjini, Songea Vijijini, Namtumbo na Nyasa, zinazopitiwa na mradi huu zitapatiwa umeme.

Kwa Songea Vijijini umeme utawekwa Vijiji vya Madaba, Mahanje, *Peramiho Medical College,* Lilondo, Wino, Igawisenga, Kifanya, *Kilocha Priest Seminary,* Itipula, Pigan, Yonga, Magingo, Mkongotema, Tanga, Lumecha, Mageuzi, Milayoyo, Likalangilo, Mtyangimbole, Gumbiro na Nagadinda.

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi huu unatarajiwa kuanza mwezi Oktoba, 2013 na kukamilika mwaka 2016, kwa gharama ya shilingi bilioni 189, chini ya ufadhili wa Serikali ya Sweden.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ni marefu, lakini hata hamjajibu swali kabisa. Swali linasema ni kiasi gani?

Mheshimiwa Jenista Mhagama?

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawali ya nyongeza.

Kabla ya maswali yangu, kwanza nimpongeze sana Mhashamu Askofu Mkuu Mtega, kupitia Jimbo Kuu Katoliki Songea, kwa kukubali kusaidia mradi huu wa ujenzi wa umeme kwenye Maporomoko ya Lingatuta. Lakini namwomba Mhashamu Baba Askofu, afanye haraka kama mazungumzo yetu tulivyokubaliana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, maswali yangu ni haya yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, nimeuliza *REA* imetenga kiasi gani cha fedha, ili mradi huo sasa uweze kuanza? Kwa sababu, *REA* ndio washika dau wakubwa kwa niaba ya Serikali, na ndio watakaosadia kusambaza umeme huu kupitia vijiji vyote vinavyozunguka umeme mpaka kule katika maeneo ya Peramiho, *REA* wana mpango huo. Sasa ni kiasi gani cha fedha kimetengwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini swali la pili. Mheshimiwa Naibu waziri, ameonesha hapa *commitment* kubwa sana ya Serikali, kwenye mradi huu wa umeme wa gridi kutoka Makambako kwenda Songea. Mwaka 2011/2012 zilitengwa bilioni tatu, 2012/2013 bilioni tisa, 2013/2014 zimetengwa bilioni 12, mabilioni haya yanatengwa kila siku, lakini bado mradi haujaanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ninachotaka kujua kwa kiu ya wananchi wa Mkoa wa Ruvuma, Naibu Waziri atuambie, haya mabilioni yote yametengwa siku zote yamefanya kazi gani? Na ananiambia mradi utaanza mwezi wa 10 mwaka huu? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Jenista Mhagama, Mbunge wa Peramiho, kama ifuatavyo:-

Kama nilivyosema katika jibu langu la msingi kwamba, inashirikiana na Kanisa Katoliki na wananchi wa maeneo yale ya vijiji vile vinavyozunguka eneo la mradi kwa ajili ya uzalishaji. Hapa niseme tu kwamba, ni Sera ya Serikali, kwamba, Sekta binafsi inaweza ikashiriki au watu katika maeneo yao wanaweza wakaungana na kuanzisha mradi ambao Serikali, itasaidia *facilitation.*

Kazi hii inafanywa na *REA,* lakini umiliki unabakia kuwa wa kwao kwa hivyo, *REA* kwa sababu, wao wana-*facilitate* ule mradi kama mchango wa Serikali, kwa kuungana na wananchi na Bajeti ya *REA* inakwenda kulingana na muda ambapo kinatakiwa kifanyike kitu fulani; kwa sababu, nafikiri Wabunge, wanafahamu fedha ya *REA* inapatikanaje. Kwa hivyo, sio lazima ikaonekana imetengwa katika Bajeti hii. Lakini pale itakahitajika jambo linalotakiwa basi litafanyika kwa msaada na maombi maalum yatakayofanywa na wanaohusika.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kuhusu mradi wa Makambako Songea, kwamba, zimekuwa zikitengwa fedha, ni kweli. Lakini awali, mradi huo ilikuwa uwe wa uwezo wa *132 kV,* msongo huo, lakini baadaye tukabadilisha na kuweka msongo wa *220 kV.* Kwa hiyo, utaona hata *study* zile zilibadilika na kwa hiyo, kuna fedha baadhi ilibidi zitumike. Lakini katika haya mashirikiano na nchi wahisani, kwa kiasi fulani ni lazima na Serikali, nayo ioneshe *commitment* kwa kuweka kiasi cha fedha na ndio maana unaona baadhi ya fedha zinaonekana hata katika Bajeti ya mwaka huu. *(Makofi)*

Na. 92

## Maeneo ya Kihistoria Kuvutia Utalii

**MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMED** aliuliza:-

Majengo ya zamani pamoja na magofu yaliyojengwa kati ya Karne ya 14 na 15 ni kati ya vivutio katika sekta ya utalii na ni eneo moja kati ya vitega uchumi vya Taifa na maeneo ya kihistoria.

(a) Je, ni maeneo gani ya kihistoria nchini ambayo Serikali, inayatambua Kisheria?

(b) Je, ni hatua zipi zinachukuliwa kuhifadhi, kulinda na kuendeleza historia hizi kwa ajili ya kutoa elimu kwa vizazi vijavyo?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Rajab Mbarouk Mohamed, Mbunge wa Ole, lenye sehemu *(a)* na *(b),* kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Sheria inayosimamia Mambo ya Kale, Sura ya 333, jumla ya maeneo ya majengo 128 ya kihistoria yametangazwa katika Gazeti la Serikali na kuhifadhiwa. Maeneo hayo yamegawanyika katika makundi makuu yafuatayo: Maeneo ya akiolojia/paleontologia kama vile *Olduvai Gorge,* Maeneo ya Kihistoria kama vile Magofu ya Kaole, Miji ya Kihistoria kama vile, Mji wa Bagamoyo, Mji wa Mikindani na Mji Mkongwe wa Zanzibar. Makazi ya Kijadi kama vile Bweranyange, Mkoani Kagera. Majengo ya kihistoria kama vile Jengo la Ikulu – Dar-es-Salaam. Maumbile asilia kama vile, Mapango ya Amboni Mkoani Tanga na michoro ya Miambani kama vile Kolo, Wilayani Kondoa.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu imechukua hatua mahususi katika kuhifadhi, kulinda na kuendeleza historia hizo kwa kufanya mambo yafuatayo: Kwanza, tumetangaza katika gazeti la Serikali, maeneo yote ambayo yamefanyiwa tafiti na kuona kuwa, yanafaa kuingizwa katika orodha ya Kumbukumbu na Urithi wa Utamaduni wa Taifa *(National Monuments).*

Pili, Wizara inaandaa Sheria Mpya ya Mali Kale, kulingana na maelekezo ya Sera ya Mali Kale ya Mwaka 2008 na tatu, tunaboresha taarifa katika vituo vya mambo ya Kale pamoja na kuendelea kujenga Vituo vya

Kumbukumbu na Taarifa katika maeneo muhimu ya Malikale. Wizara inaendelea kuhamasisha na kuelimisha jamii kupitia vyombo vya habari na ushiriki wa maonesho ya ndani na nje ya nchi, ili wananchi watambue umuhimu wa uhifadhi na uendelezaji wa Malikale pamoja na kuendelea kutoa mafunzo ya watumishi katika fani za utafiti, uhifadhi na uendelezaji wa Malikale za Taifa letu. Vilevile, tunahamasisha Halmashauri za Wilaya, Taasisi binafsi, mashirika yasiyokuwa ya Kiserikali na watu binafsi kuajiri Wataalamu wa sekta ya Malikale, ili waweze kusimamia na kuendeleza Malikale zinazopatikana katika maeneo yao.

**MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMED:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, ambayo yamenipa mashaka katika uelewa mzima wa historia ya Mambo ya Kale, naomba niulize maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 1412, Kisiwa cha Kilwa, kilikuwa na Serikali na Utawala kamili na fedha zake. Mwaka 1987, Kisiwa hiki kilitangazwa kama ni Urithi wa Dunia. Ambapo katika Karne ya 15, utawala wa kisiwa hiki ulikuwa unatawala maeneo ya Malindi, Mombasa, Pemba, Unguja, Mafia, Komoro, Sofila na hata Madagascar.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashangaa kwamba Waziri, anashindwa kulitaja eneo hili ambalo ni kubwa kihistoria.

Je, Mheshimiwa waziri, huoni kwamba, huu ni uhasaba katika maeneo haya? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili. Moja kati ya maeneo ambayo ni ya kihistoria ambayo, vilevile ni kivutio kikubwa cha utalii, ni suala zima la utamaduni, mila, silka na desturi.

Je, Mheshimiwa Waziri, Wizara yako ina mpango gani mahsusi na wa kimkakati, kuyatambua na kuyatangaza makabila kama vile Wahadzabe, Wasonyo, Wandorobo, Wamasai, Wasandawe, Wairak, Wabarbeig na hata rafiki

zangu wale Wamatumbi, akina Mheshimiwa Mangungu, ambao wana historia kubwa ya Kinjeketile na Vita vya Majimaji?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii, naomba nijibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Rajab Mbarouk Mohamed, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, moja, nimwondoe tu wasiwasi Mheshimiwa Mohamed. Serikali, imelijibu vizuri sana swali lake katika majibu ya msingi. Tumetaja maeneo yote ambayo yana historia na yanahifadhiwa.

Labda tu niseme katika maeneo yote 128 ambayo tumeyataja, yako yanasimamiwa na ile Sheria yetu ya Mambo ya Kale, Sura Namba 333 katika Kitabu cha Sheria za Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili; tunatambua vilevile umuhimu wa Kisiwa hiki cha Kilwa na ni sehemu ya Urithi wa Dunia, ambao umeshatangazwa na unaendelea kusimamiwa. Naomba nisisitize na niseme tena Wizara yangu, kama ambavyo tumeshaeleza katika jibu la msingi, tutaendelea kuhakikisha kwamba, tunasimamia tunahifadhi na tunaendeleza utamaduni huu na urithi huo wa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika utamaduni wa asili au urithi wa utamaduni wa Mtanzania, Wizara kupitia Taasisi zake, tumeweka bayana umuhimu wa kuhifadhi historia hii ya utamaduni. Ameyataja makabila ya Wahadzabe, lakini makabila yako mengi na tunaendelea kuratibu, tunaendelea kuweka hii historia. Kama nilivyosema, tunaendelea kujenga maeneo ya kumbukumbu katika maeneo yote 128 yaliyo Tanzania, ili historia hii aliyoitaja na ile ambayo tunaifahamu na ile ambayo vijana wetu wanaendelea kuifanyia utafiti, iweze kuhifadhiwa.

**NAIBU SPIKA:** Pamoja na muda kuwa mdogo, lakini Mheshimiwa Mangungu, swali fupi sana la nyongeza.

**MHE. MURTAZA A. MANGUNGU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Ningependa kumwuliza tu swali moja la nyongeza kwamba, Kilwa ni sehemu tajiri na ilijitawala na ikawa na fedha zake kama historia inavyosema. Leo hii wananchi wa Kilwa Kisiwani, ambako kuna utalii na kuna pesa ambazo zinatolewa na *UNESCO* kwa ajili ya urithi wa Dunia. Kwa nini, hawapati mapato yanayotokana na vyanzo hivi?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nijibu Swali la nyongeza la Mheshimiwa Mangungu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, na ninaomba nirudie tena kwamba, Kilwa, ilikuwa nchi katika historia ambayo inabaki. Ndio sehemu ambayo ilikuwa na fedha zake, ilikuwa na utawala wake na historia ile daima itaendelea kukumbukwa. Serikali, inasisitiza na tunaongeza juhudi za kuimarisha utalii wa ndani. Tunapenda wananchi wengi waweze kutembelea eneo hili la kihistoria la Kilwa na wageni wanaotoka nje ya nchi kwa ajili ya shughuli za utalii waweze kutembelea maeneo haya ya Mambo ya Kale, ikiwa ni pamoja na Kilwa. Tuna mpango wa kuhakikisha kwamba, mali au fedha zinazopatikana kutokana na shughuli hizi za kitalii zinawafaidisha wananchi kupitia ushiriki wa Halmashauri na wananchi mbalimbali wanaojishughulisha na shughuli za kibiashara, hususan biashara ya utalii. *(Makofi)*

Na. 93

**Kufanya Ukaguzi wa Afya na Usalama Mahali pa Kazi**

**MHE. AMINA N. MAKILAGI** aliuliza:-

Ilani ya *CCM* ya Mwaka 2010, Ibara ya 80 (b), imetamka bayana kuwa, Serikali, itafanya ukaguzi wa Afya na Usalama Mahali pa Kazi:-

Je, Serikali, imefikia hatua gani katika kutekeleza dhamira hii yenye lengo la kuimarisha utendaji katika sehemu za kazi?

**NAIBU WAZIRI WA KAZI NA AJIRA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kazi na Ajira, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Amina Nassoro Makilagi, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kutekeleza Ilani ya *CCM* ya Mwaka 2010, Ibara ya 80, Kifungu (b), Wizara yangu kupitia Wakala wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi *(OSHA),* imechukua hatua zifuatazo:-

(i) Imetoa mafunzo mbalimbali yanayohusu Usalama na Afya sehemu za kazi ikienda sambamba na uundwaji wa Kamati za Usalama Mahali pa Kazi.

(ii) Imeongeza idadi ya magari ambayo yatawezesha wakaguzi hawa kuzifikia sehemu za kazi nyingi zaidi.

(iii) Jitihada pia zimefanyika katika kuongeza idadi ya wakaguzi binafsi *(Private Inspectors),* kati ya 30 na 45 ambao wakisaidiana na wakaguzi wa ndani wapatao hamsini, sehemu nyingi za kazi zitafikiwa.

Aidha, Serikali, ipo katika mchakato wa kuridhia mikataba mitatu ya Shirika la Kazi Duniani *(ILO),* inayohusu masuala ya Usalama na Afya Mahali pa Kazi. Mikataba hiyo ni Namba 167 wa mwaka 1988, Namba 185 wa mwaka 2003 na Mkataba Namba 187 wa mwaka 2006.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2011/2012 *OSHA* pia imetekeleza yafuatayo:-

(i) Jumla ya kaguzi 5995 za kawaida ambazo ni sawa na 85% ya kaguzi zilizopangwa na kaguzi maalum 12,549 sawa na 89% za kaguzi zilizopangwa zilifanyika.

(ii) Jumla ya wafanyakazi 16,767 walipimwa afya zao sawa na zaidi ya 129% ya wafanyakazi 13, 000 waliotegemewa kupimwa afya zao.

(iii) Waajiri wameendelea kushauriana na kutakiwa kuzingatia sheria na Kanuni za Usalama na Afya mahali pa kazi. Aidha wale waliokaidi maagizo walipelekwa mahakamani na wengine kufungiwa kabisa shughuli zao hadi kufikia mwezi Mei, 2012 jumla ya kesi 16 zipo mahakamani.

(iv) Mafunzo ya usalama na afya mahali pa kazi yalitolewa kwa wafanyakazi 1004.

(v) Wakala umeendelea kujitangaza kupitia njia mbalimbali ikiwemo vyombo vya habari na tovuti yake ya *www.osha.go.tz.* Aidha siku ya kimataifa ya usalama na afya mahali pa kazi iliadhimishwa Mkoani Dar es Salaam mwaka jana Aprili, 28 ikiwa na kauli mbiu isemayo kuboresha Afya na usalama mahali pa kazi katika uchumi wa kijani.

Aidha mwaka huu 2013 siku hii itaadhimishwa Mkoani Arusha tarehe 28 Aprili, 2013 ikiwa na kauli mbiu ya kuzuia magonjwa yatokanayo na kazi. *(Makofi)*

**MHE. AMINA N. MAKILAGI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi niweze kuuliza maswali mawili. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza kwa kuwa ipo sheria ya fidia kwa wafanyakazi wanaoumia kazini iliyotungwa mwaka 2008 na kwa kuwa sheria hii bado haijaanza kutumika. Je, Serikali sasa ina mkakati gani ili sheria hii ya mwaka 2008 iweze kutumika na wafanyakazi wanaoumia kazini waweze kupata fidia zinazostahili?

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kwa kuwa Serikali kwa kushirikiana na *OSHA* wamekuwa wakifanya kazi nzuri ya kuwafikia wafanyakazi na kwa kuwa jibu la msingi la Waziri limeonyesha kwamba *OSHA* haijafanya kazi yake kikamilifu.

Je, sasa Serikali ina mkakati gani wa kuiwezesha *OSHA* ili iweze kwenda mbali zaidi na kuwafikia wafanyakazi na hata katika sekta zisizo rasmi ambayo inawaunganisha wafanyakazi walio wengi? Ahsante sana.

**NAIBU WAZIRI WA KAZI NA AJIRA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa kazi na ajira napenda kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Amina N. Makilagi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kabisa kwamba sheria ya fidia kwa wafanyakazi wanaoumia kazini ilipitishwa na Bunge hili mwaka 2008 hii ni baada ya kuona kwamba Sheria ya zamani ilikuwa kwa kweli haiwafai sana wafanyakazi kwa sababu kima cha mwisho cha kulipwa ilikuwa ni shilingi laki moja na nane.

Baada ya hii Sheria kupitishwa mwaka 2008 tukiri tu kwamba imechelewa kuanza kazi kwanza tulikuwa tunatengeneza Kanuni ambazo tumeshakamilisha kuzitengeneza lakini pili Wizara ikawa inatatizwa na upatikanaji wa fedha za kuanzisha mfuko huu kwa sababu sheria hii inaendana na kuanzisha mfuko uwe na Ofisi ya mfuko, uwe na Bodi ya mfuko, uwe na Mtendaji Mkuu na wafanyakazi wengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hili limechelewa kwa sababu ya upatikanaji wa fedha lakini kwa bahati nzuri niseme hapa Bungeni kwamba kwa mwaka wa fedha unaoanza Julai kama mtapitisha Bajeti yetu hapo tarehe 3 mwezi wa sita basi tumewekewa fedha za kuanzisha mfuko huu na ili sheria hii ianze kufanya kazi kuanzia Julai mwaka huu 2013.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili ni kwamba *OSHA* bado haina uwezo mkubwa mpaka sasa kama mnavyoiona ipo katika Kanda sita tu za nchi yetu ipo Dar es Salaam kanda ya pwani, ipo Mbeya, ipo Arusha, Mwanza, Dodoma na Mtwara na ofisi ndogo pale Tanga na Moshi.

Kwa hiyo, bado tunajikusanya kama Wizara, kama Serikali na *OSHA* wenyewe kwa kujitafutia fedha ili waweze kutanuka zaidi hii ndiyo sababu ambayo inafanya *OSHA* kwa kweli haijafikia, hawajafanya kaguzi nyingi kama ambavyo inavyotakiwa.

Kwa mfano wameweza kusajili tu maeneo ya kazi 6,599 ukilinganisha na maeneo ya kazi 27,000 yaliyopo nchini. Kwa hiyo kadiri tunavyoendelea kupata uwezo tutaendelea kuiwezesha *OSHA* ili iweze kufanya kazi yake ipasavyo.

**MHE. CATHERINE V. MAGIGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza kwa kuwa tumekuwa tukishuhudia kina mama wanaofanya usafi barabarani wakifanya usafi katika vumbi kubwa vilevile magari yakipita na kuhatarisha usalama wa afya zao.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuyabana makampuni husika ili kina mama hawa wapatiwe bima ya maisha na bima ya afya?

**NAIBU SPIKA:** Kwa kweli Mheshimiwa Naibu Waziri hili la kina mama kufagia barabara hili, Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KAZI NA AJIRA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa kazi na ajira napenda kujibu swali la Mheshimiwa Catherine Magige, la nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi ya *OSHA* kwa kweli ni kukagua maeneo ya kazi yaliyosajiliwa lakini vilevile katika maeneo haya ya kazi panatakiwa kuwepo na kamati hizi za afya na usalama mahali pa kazi ambayo yanajumuisha vile vile na wafanyakazi na viongozi wa wafanyakazi.

Sasa pale ambapo tunapata taarifa za eneo la kazi ambalo kuna wafanyakazi ambao wanahitajiwa kupimwa afya tunafanya hivyo kupitia *OSHA*.

Sasa hawa hawa akina mama ambao wanafagia barabarani yako makampuni yao, makampuni ambayo yamewaajiri kazi ya *OSHA* itakuwa ni kufuatilia na kuona kwamba: Je, wafanyakazi hawa wanapimwa afya zao na wanatumia vile vifaa vinavyotakiwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba bado *OSHA* wale wanaofanya kazi ya kufagia barabarani lazima wataendelea kufanya la msingi.

Je, wana nyenzo za kuweza kuvaa puani na miguuni ili wasiathirike. Lakini kuhusu suala la bima sasa hilo ni suala lingine ambalo halihusu Wizara yetu. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana, swali la mwisho kwa siku ya leo Waheshimiwa naona muda hauko upande wetu swali la Mheshimiwa Said Mussa Zubeir, Mbunge wa Fuoni.

Na. 94

**Tume ya Ajira na Mafao kwa Askari Polisi/Magereza**

**MHE. SAID MUSSA ZUBEIR** aliuliza:-

(a) Je, Serikali, inayo Tume ya Ajira na Mafao kwa ajili ya Askari Polisi na Magereza?

(b) Je, Tume hiyo imeweka utaratibu gani wa kulipa askari pensheni na motisha pale wanapomaliza kazi bila matatizo?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Said Mussa Zubeir, Mbunge wa Fuoni, lenye sehemu *(a)* na *(b),* kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali, haina Tume ya pamoja ya Ajira na Mafao kwa ajili ya Askari Polisi na Magereza, isipokuwa kuna Tume ya Utumishi ya Polisi na Magereza.

Kazi za Tume hii ni kumshauri Mheshimiwa Rais juu ya mambo yanayohusiana na Jeshi la Polisi na Magereza, kufanya mapendekezo ya uteuzi wa Maafisa wa juu wa Polisi na Magereza, kuwapandisha au kuwashusha vyeo na kuthibitisha adhabu dhidi ya Maafisa wa Polisi na Magareza wenye vyeo kuanzia Mkaguzi Msaidizi hadi Kamishna Msaidizi, zilizopendekezwa na Kamati za nidhamu za Polisi na Magereza.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, Askari Polisi na Magereza hulipwa pensheni kwa mujibu wa Kifungu Namba 8 na 9 cha Sheria ya Mafao ya Hitimisho la Ajira kwa Watumishi wa Umma, Sura Namba 371 na Kifungu Namba 15, 16, 17, na 18 cha Sheria ya Mfuko wa Akiba ya Wafanyakazi Serikalini *(GEPF),* Sura Namba 51 ya Sheria za Tanzania. Motisha mbalimbali kwa Askari Polisi na Magereza, hulipwa kwa namna na sababu tofauti.

**MHE. SAID MUSSA ZUBEIR:** Mheshimiwa Naibu Spika, asante pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri nina maswali mawili ya nyongeza madogo tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi ni *formula* gani wanatumia inayotumiwa na Serikali kwa hawa wastaafu hususan waliotimiza zaidi ya miaka 30 kwenye hili jeshi la polisi halafu walipwe kiinua mgongo cha 785,000/= akimaliza mtu na nafasi ya u-*sergeant* hilo ni (a).

Mheshimiwa Naibu Spika, (b) kama mtu au watu hawa hawakuwa na matatizo wakati wa ufanyaji wao wa kazi ambayo kwamba ingewapelekea labda kwenye kiinua mgongo chao kukatwa fidia.

Je, Serikali haioni kwamba kufanya hivi ni kuwadhurumu hawa watu?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi napenda kujibu maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa Said Mussa Zubeir, kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, malipo ya kiinua mgongo kwa ajili ya Polisi na Jeshi la Magereza hulipwa kwa mujibu wa vifungu vya Sheria ya Hitimisho la Ajira.

Lakini katika sheria hii ambayo ilianza mwaka 1999 huko nyuma kulikuwa wanalipwa kwa mujibu wa kifungu 68 cha Jeshi la Polisi ambacho kimsingi Askari Polisi alikuwa anakisiwa atumie miaka 21 katika jeshi la Polisi kwa maana ya miaka 12 akiwa kwenye utumishi wa mkataba na miaka 9 kwa wale *constables* kuweza kutimiza miaka 21.

Kwa hiyo, *formula* kwa wakati ule ilikuwa 21 kwa maana ya miaka na mara mshahara anaolipwa mara mbili juu ya tatu. Hata hivyo baada ya kubadilisha sheria hii na kuja kwa sheria nyingine ya Hitimisho la Ajira Sura ya 371 sasa hivi wanalipwa kwa mujibu wa sheria za mifuko ya *GEPF* na *PSPF.*

Mheshimiwa Naibu Spika, Je, inawezekena mtu kulipwa laki 785,000/= hii inategemea pia ni lini alistaafu kwa sababu huko nyuma viwango vya mshahara ambao ndiyo sehemu kubwa *factor* kubwa katika kukokotoa ilikuwa kwa sababu ya hali ya uchumi vile vile ilikuwa thamani ya pesa mishahara ilikuwa ni midogo sana.

Hata hivyo kwa mawazo yangu hii si dhuluma kwa sababu ya kuona pengine wafanyakazi maafisa pamoja na Askari hawapati mafao ya kutosha ndiyo Serikali ikabadilisha Sheria na sasa pengine hali inaweza ikawa afadhali kuliko hapo mwanzo.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge kwa sababu ya muda kama mtakavyoona tumeshapita kabisa muda ambao tunatakiwa kuutumia kwa hiyo naomba tusonge mbele.

Nina tangazo moja tu la kikao cha Kamati ya Wabunge Kamati ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala Mheshimiwa Dkt. Pindi Chana anawatangazia Wajumbe wa kamati hiyo ya Katiba, Sheria na Utawala saa saba mchana wakutane ghorofa ya kwanza Ukumbi 133, Sheria, Katiba na Utawala Ukumbi 133 ghorofa ya kwanza. *(Makofi)*

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2013/2014
### Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika

(*Majadiliano yanaendelea)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge majadiliano yanaendelea tunaanza na Mheshimiwa Dkt. Lucy Nkya na Mheshimiwa Dkt. Titus Mlengea ajiandaye.

**MHE. SUBIRA K. MGALU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kunipa fursa na mimi kuchangia hotuba ya Wizara ya Kilimo naomba nianze kwa kuunga mkono hoja iliyowasilishwa na Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, lakini naomba katika kupitia mapitio ya utekelezaji wa Bajeti ya mwaka 2012/2013 niombe tu Wizara ya fedha wakati inapeleka mafungu ya Wizara mbalimbali itupie jicho la huruma Wizara hii ya Kilimo, Chakula na Ushirika kwa kuwa mwaka wa fedha huu unaokaribia kwisha mpaka mwezi wa tatu ni 19% tu.

Lakini mapato makubwa ya Serikali yanachangiwa na bidhaa zinazozalishwa na sekta ya kilimo na mazao mbalimbali ambayo yanakuwa *exported* nje ya nchi yanachangia pato la Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, niombe tu Wizara ya Fedha ihakikishe kwa kweli hela za maendeleo za Wizara hii zinapelekwa kwa wakati kwa sababu shughuli nyingi zinazotegemewa kufanywa na Wizara hii kupitia fungu la maendeleo ni shughuli ambazo zinatarajia kumlenga mkulima.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu wa pili ni kuhusu pesa ambazo zimeonekana kwenye taarifa ya Wizara hii zimebaki *carry over funds* ambazo ni takribani bilioni 25.

Naomba niliombe Bunge na Waheshimiwa Wabunge tuangalie hii miradi ya umwagiliaji, miradi ni mingi lakini pesa zenyewe zinapelekwa kidogo kidogo hazileti tija ifike wakati tuainishe miradi michache kila mwaka tutekeleze miradi michache ikamilike halafu tija inaweza ikapatikana.

Lakini suala la kuwa na miradi mingi ambayo haikamiliki kutokana na fedha zenyewe kwenda kidogo kidogo mimi nilikuwa naomba tuainishe miradi michache tukubaliane kama Wabunge wengine tuendelee kusubiri na wengine itekelezeke ili ikimalizika ilete tija na hasa miradi ambayo ni ya umwagiliaji iliyo katika mradi huu wa *SAGCOT.*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna maeneo ambayo yametengwa kama Mikoa ya kuzalisha chakula na maeneo ambayo yametengwa kama ghala la taifa la chakula. Niombe *scheme* zile za umwagiliaji katika maeneo hayo zipewe kipaumbele ili zizalishe chakula kwa ajili ya matumizi ya nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu mwingine nitajielekeza kwenye mazao ya biashara hasa zao la korosho ambalo ni zao muhimu katika Mikoa ambayo inalima zao hili la korosho. Hapa naomba nishukuru hatua ambazo zimechukuliwa na Serikali juu ya watendaji wa vyama vya msingi katika Mkoa wa Pwani ambao wamesababisha pesa nyingi kupotea na hatimaye wakulima wa korosho katika Mkoa huo kutopata stahili zao zinazotakiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza niishukuru Serikali ya awamu ya nne ilijitahidi kufuatia madeni ya Vyama Vikuu vya Ushirika katika Mikoa mbalimbali.

Lakini la kushangaza vyama hivyo vimeendelea tena kuzalisha madeni mengine. Niwaombe wakulima wa maeneo hayo kuchagua viongozi waaminifu ili tusiendelee kulea viongozi wa vyama vya ushirika wasiokuwa waaminifu na ambao wataendelea kuzalisha madeni. *(Makofi)*

Lakini pia nipongeze Serikali kwa mpango wa matarajio ya uanzishaji wa Tume ya Ushirika. Nadhani Mswada huo utakapowasilishwa Bungeni naomba Waheshimiwa Wabunge tuunge mkono ili Ushirika ambao unategemewa kwa kiasi kukubwa na wakulima wa nchi hii uweze kufanikiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia naomba niwaombe wakazi wa vijiji vya Matipwili na Kiwangwa ambako mradi mkubwa wa miwa Wilaya ya Bagamoyo unataka kuanzishwa niwaombe tu kuwa na subira, wasubiri wakati Serikali inapofuatilia madai yao.

Lakini tusikwamishe mradi huu kwa sababu una nia njema ya kuwawezesha kuanzisha mashamba ya kibiashara ya kilimo cha miwa. Nchi yetu bado ina uhaba wa sukari. Kwa hiyo, niwaombe wasikilize Serikali inasema nini na nadhani haki zao za msingi zitazingatiwa ili mradi huu uanze kutekelezwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niungane na Mheshimiwa Mbunge wa Korogwe vijijini kuiomba Serikali kuangalia hususan Wizara ya kilimo na Wizara ya Ardhi kuangalia mashamba ya Mkonge ambayo wengi wananchi waliachwa mashamba yale yalipotaifishwa waliachwa mle ndani hawakulipwa fidia, hawakulipwa mafao yao baadaye leo mashamba yale wanapokuja wakulima wakubwa wanataka kuwatoa hakuna pa kuwapeleka.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi niombe na kazi ya wale maeneo mengine tumeshafanya ya kuwasilisha maombi ya kufuta zile Hatimiliki na nadhani jambo hili likifanywa kwa haraka inaweza ikasaidia.

Lakini niwaombe hata wakulima wakubwa waliochukua hayo mashamba haimkiniki unamiliki heka 10,000 una watu umewakuta hawana ardhi na wao nawaomba wawe na moyo wa huruma wawafikirie wale wananchi waliopo katika mashamba hayo wawamegee haiwezekani?

Uwekezaji wowote unaendana na amani kuwepo kwa wananchi wale ambao hawana hatima yao wakiwapa zile heka chache inaweza ikasaidia na wao uwekezaji wao ukawa wa msingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo mimi niombe hili suala ni kubwa kwa kweli wale wananchi wale waliopelekwa kwenye mashamba ya Mkonge wametoka maeneo mbalimbali Tanzania nzima. Wamekaa miaka 20, miaka 30 na sisi Mikoa mingine ambayo mashamba hayo yapo Morogoro, Pwani, Tanga yenyewe, kazi ilishafanyika ya kuangalia ukubwa wa hayo maeneo.

Lakini cha kushangaza pia nimeona Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika imeipa hela Rubada ipime hayo maeneo, maeneo ambayo wananchi walishavamia leo mtu amekaa miaka 30 unamwitaje mvamizi.

Mimi niombe Shirika hodhi *Consolidated Holdings Company* lishirikiane na Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika na Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi, waharakishe huo mchakato na sisi wengine tupo tayari kuwasaidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia naomba niishukuru RUBADA kwa kupitia uwekezaji wa *program* ya kilimo kwa vijana hasa huu uanzishaji wa kambi ya vijana Mkongo, Rufiji. Naomba huu mpango uharakishwe, wako vijana wengi, wanahitaji kujiunga kwenye sekta hii ya kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini naomba niseme kuhusu Vyuo vya Kilimo, vyuo hivi vingi kwa kweli vimechoka. Niombe Wizara, kupanga ni kuchagua, inapopata *ceiling* yake hebu ivitazame, tunategemea Maafisa Ugani katika maeneo hayo, mfano Chuo cha Mlingano, Muheza. Kwa kweli, kile Chuo kiangaliwe kwa huruma kwa kuwa kinatoa mafunzo ya zana za kilimo. Serikali imejitahidi kukopesha matrekta, kukopesha *power tillers,* lakini tunategemea wataalam watakaozalishwa na vyuo hivi kuendelea kuwapa huduma wakulima katika suala zima la matengenezo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, naomba Serikali kupitia Wizara hii ya Kilimo, kuwatazama wakulima waliozalisha vyakula; mpunga na mazao mengine, ambao leo hawana soko kwani mapato makubwa ya nchi hii yanachangiwa na sekta hii ya kilimo na inaajiri zaidi ya asilimia themanini. Leo kwa nia njema tu ya Serikali ya kuleta chakula na kupunguza bei, lakini niwaombe wafanyabiashara nao, wawatazame hawa wakulima ambao wamezalisha chakula cha ndani.

Mheshimiwa Naibu Spika, niwaombe Watanzania, tuendelee kutumia mchele unaozalishwa nchini kwetu. Tuwasaidie hawa wakulima; leo tunaweza tukajivunia kuna mchele umeingia sokoni mwingi, lakini Waswahili wanasema usimtegemee jirani. Tuwaunge mkono, tununue bidhaa hizo, mchele ule ni mzuri kwa afya yetu na ni bora.

Kwa hiyo naiomba Serikali na huu Mfuko unaotaka kuanzishwa wa *Stabilization Fund*, wadau waitwe haraka mwezi wa Tano wachangie na Muswada huo uletwe haraka, ili basi wakati wa anguko la bei, wakulima wafidiwe kama ambavyo ilishawahi kutokea wakati wa mdororo wa uchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema haya, naomba niishie hapa na nishukuru sana Serikali. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa John Cheyo, atafuatiwa na Mheshimiwa Abdulsalaam Ameir. Mheshimiwa John Cheyo!

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Kwanza kabisa niseme kuwa, mkulima anahitaji vitu vitatu vya maana; kwanza ni maji, pili ni ardhi na pia mbegu bora, nguvu atatoa. Sasa hivi adui yetu mkubwa katika Tanzania na katika nchi nyingi ni tabia nchi. Hatujui lini mvua itanyesha na hatujui lini mvua itakauka. Wakulima wanafanya kazi nzuri, wanalima mahindi, yanakaribia kuiva, mara moja jua linakuja, wanapoteza.

Mheshimiwa Naibu Spika, hasara inaonekana moja kwa moja, mwaka huu tumetumia zaidi ya bilioni 30 kwa ajili ya kutoa chakula cha misaada kwa wananchi. Kwa kawaida wananchi hawapendi chakula cha kupewa, wananchi wanataka chakula ambacho wamelima wao wenyewe kwa sababu hiyo ni heshima ya kibinadamu kwamba, umeweza kujilisha wewe mwenyewe.. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kama Serikali imeweza kutumia bilioni 30, lakini ukiangalia kwa miradi ya umwagiliaji, unaona kiduchu, hii ina maana gani? Kweli Serikali haioni tatizo hili? Naiomba Serikali ihakikishe tangu kipindi cha kumi na nne, kumi na tano, tunaona hekta milioni moja zinawekewa fedha za kutosha. Mabonde yapo, maji yapo, ni maaamuzi tu. Tukiamua kama vile tulivyoamua kujenga barabara, tutahakikisha kuwa maji tena siyo tatizo kwa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la pili, ni ardhi. Watu sehemu ambazo tunalima wengi, kama sehemu hizo za *Sukuma land*, sisi ni wakulima, sisi tunajua *Igembe Sabho!* Yaani jembe ndiyo mali, tunajua kulishika na popote pale ambapo tumekwenda tumelima sawasawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeona hapa Serikali imeweza kupata hekta laki moja na nusu kwa ajili ya *SAGCOT*. Tunataka *SAGCOT* nyingi na *SAGCOT* hizi zisiende tu kwa wakulima wakubwa, tunataka vijana ambao hawana ardhi sasa hivi vijijini, badala ya kukaa vijijini au kuhamia mjini, waende kwenye *SAGCOT* hizi, na ziwe mahali popote. Ziwe Mpanda, Kigoma na sehemu yoyote Tanzania, kwa sababu ardhi yetu bado ni kubwa katika sehemu nyingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini tumeanza uchoyo; hapa ni kwangu, hapa ni kwa wale, tuachene uchoyo. Nchi hii ni yetu wote, kama kuna sehemu watu ni wavivu, hawalimi na kuna watu wengine ambao wana uwezo wa nguvu na nia ya kulima, hao ndiyo tuwashikirie na wafanye kazi yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hilo, nataka kusema jambo lingine juu ya ardhi. Tunasema sisi ambao tunafuga na ambao pia tunalima, tungependa kwa mfano, sehemu ambazo tunapakana na hifadhi ya wanyama kama vile *game reserves* za Maswa na *controlled areas* za Maswa. Kama ilivyo Ngorongoro, sioni kwa nini tusiwe na *multiple land use*. Yaani kama vile wanavyofanya Ngorongoro, wanalima kidogo na wanafuga na wanyama wanakuwepo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukifanya hivyo, ardhi ambayo sasa hivi tunaitumia kwa ajili ya mifugo, tutaitumia pia kwa ajili ya kulima. Tukipata hiyo ardhi, nawahakikishia kama mvua itaweza kunyesha au umwagiliaji utafanyika, kama vile inavyofanyika Zimbabwe, nina hakika nchi hii haitakuwa na njaa tena.

Mheshimiwa Naibu Spika, siwezi kuacha kuzungumzia juu ya pamba, mahali ambapo natoka na wananchi wanategemea. Nataka kusisitiza jambo moja tu, nimengalia fedha ambazo zimetolewa kwa ajili ya pembejeo. Nyingi zinakwenda kwenye mbolea na fedha kidogo sana inabakia kwa ajili ya madawa ya pamba. Kama kuna uwezekano wa bajeti hii kuweza kurekebishwa, naomba pesa ya madawa ya pamba iwepo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini siyo hivyo tu, naiomba Wizara hii iangalie wakulima wa pamba. Najua mwaka huu mmezungumzia juu ya utaratibu wa kuweka Mfuko wa Kudhamini Bei au *Price Stabilization*. Hilo ni jambo jema, lakini kwa nini mkulima tunamwondoshea hela ambayo ni halali yake? Mkulima anakatwa shilingi arobaini kwa kila kilo, ili kuwapelekea watu wa *CDTF* eti Mfuko wa Maendeleo ya Pamba, lakini hiyo pesa ni kwa jili ya kununua pembejeo na Serikali inapeleka pesa kwa ajili ya kununua pembejeo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka huu wakulima wamekatwa zaidi ya bilioni 12. Sasa unanunua yale madawa kwa hela ya mtaji wa mkulima, halafu unampelekea mkulima tena; Unamwuzia. Huu ni wizi wa moja kwa moja! Siwezi nikakupa mtaji, unakwenda kununua, mahitaji yangu halafu unarudi unanidai tena, unaniuzia. Utaratibu huo haufai na naomba Waziri aliangalie hilo, kwa sababu hiyo ni kuchukua *public finance* bila kutumia utaratibu ambao ni wa haki. Huwezi ukachukua pesa ya mkulima, ukaenda kununua dawa, halafu unakuja kumuuzia tena.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama inawezekana turudi tena kwenye utaratibu ambapo kila mmoja alikuwa na *account* yake, tuuboreshe kwamba, kila mkulima kama ameweka sh. 40,000/= aone sh. 40,000/= zinamrudia kwa njia ya pembejeo. Huu utaratibu wa kwamba, nimetoa sh. 40,000/ = halafu nakuja kupewa madawa ambayo gharama yake ni 3000 tu hainifai.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nafikiri kwamba, kama tukiangalia utaratibu huu, wala haitakuwa lazima Serikali kuweka pesa ya madawa kwa ajili ya pembejeo. Tutakuwa na fedha za kutosha kabisa kununua madawa yote ambayo yanahitajiwa na wananchi. Kama tukijitengenezea Mfuko wa watu kula fedha za wakulima, utaratibu huu haufai.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilimwomba Mheshimiwa Waziri, aangalie huu Mfuko aupeleke kwa CAG, ukakaguliwe. Kwa sababu hizi fedha ni *public finance*. Kwa sababu tuna Bodi ya Pamba, kuna Sheria ya Pamba ndiyo maana watu

wanakatwa. Kwa hiyo, kama watu wanakatwa ndiyo kusema *this is public finance*, ni pesa ya umma. Kama ni pesa ya umma, huwezi ukamkabidhi mtu tu aile, aishone anavyotaka. Lazima ikaguliwe ili kuhakikisha kwamba kweli pesa za wananchi zinatumika inavyopaswa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo kubwa kwa nini bei zetu zinaanguka upande wa pamba? Ni kwamba, wale wanaonunua zile pamba ni kama vile hawajaijua ile biashara sawa sawa, kwani tunangonjea mpaka msimu umeanza ndiyo tunaanza kutafuata masoko. Ulimwenguni kote wanatafuta masoko kwa sasa, kabla pamba haijaanza kuonekana. Huu utaratibu ndio ufuatwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Abdulsalaam Amer atafuatiwa na Mheshimiwa Kidawa Hamid Saleh. Mheshimiwa Abdulsalaam Selemani Ameir!

**MHE. ABDULSALAAM SELEMANI AMEIR:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii kuchangia Wizara ya Kilimo. Naunga mkono hoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia hotuba ya Mheshimiwa Waziri ni nzuri, lakini bajeti ni finyu sana, kama alivyoongea Mwenyekiti wa Kamati kwamba, hata nusu ya asilimia kumi haijafikiwa. Hoja yangu, bajeti nzuri iliyopangwa na Wizara, lakini pesa hawapati kwa wakati kama wao walivyopanga.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama wenzangu wa Kaskazini walivyosema kuhusu mambo ya pamba, mimi naelekea upande wa miwa. Wakulima wa miwa wa Bonde la Luhembe, Wilaya ya Kilosa wana tatizo sana kuhusu miwa yao waliyoiuza kwenye Kiwanda cha Sukari.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo sukari imejaa kiwandani, wakulima wanadai asilimia tano ya, pesa walizouza miwa

kiwandani, hawajalipwa na wanasema kwamba sukari imejaa *godown*, lakini sukari kutoka nje imeagizwa, wanasema bei itapungua lakini naona bei ni ile ile. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wakulima wa miwa kwa kweli wanavunjika mioyo. Bonde la Luhembe ni tegemeo kubwa kwa Kiwanda cha K2 (Kilombero *two*) chini ya Kampuni ya Ilovo ambao wanaendesha hiki Kiwanda. Wakulima wanalalamika kuhusu pesa yao iliyobaki, lakini kiwandani wanasema hawawezi kutoa kwa sababu mauzo ya sukari hakuna. Sukari imejaa pale, lakini mauzo hakuna.

Mheshimiwa Naibu Spika, hapo wakulima wa miwa wanapata wakati mgumu na kusababisha wakulima kuvunjika moyo na kilimo cha miwa. Sasa wakulima wameamua kulima mpunga na mpunga nao wanalalamika, umejaa Mbarali, hivyo soko hakuna. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la pembejeo. Kwa kweli, mpango wa Serikali ni mzuri sana, lakini baadhi ya Halmashauri hazina asilimia sabini ya kuchangia. Naiomba Serikali ipange mkakati maalum wa kuwasaidia wakulima wa mazao ya biashara, mfano tumbaku, miwa, korosho na pamba wenye uwezo mdogo ili waweze kuwakopesha moja kwa moja kwa dhamana ya Serikali, waweze kupata mkopo wa pembejeo hasa *tractor* na vifaa vya kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wakulima wa miwa wana matatizo mengi. Jambo la kwanza, mfano mkulima wa miwa katika heka moja ya miwa anatoa tani 30 za miwa kwa kiwango cha chini. Wanalipwa kwa leo shilingi 63 kwa tani moja. Anapata milioni moja laki moja na themanini kwa hekari moja. Lakini mkulima huyo huyo ana makato mengi sana mpaka anavunjika moyo na kilimo. Mkulima hawezi kukopesheka, kwa sababu kodi nyingi wanalipa. Ningeomba Wizara ya Kilimo iangalie suala hili linalohusu makato ya wakulima wa miwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nipende kuzungumzia suala la mashamba ya mkonge. Sisi kwetu Wilaya ya Kilosa,

mashamba mengi ni mapori. Wawekezaji wapo pale kwa jina tu lakini hawa hawaonekani mpaka leo. Kuna wananchi pale toka Kiwanda cha Mkonge kinaanza yuko pale pale ana wajukuu na watukuu. Leo anambiwa aondoke aende wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baadhi ya wawekezaji walichukua mashamba yao kwa ajili ya kupata mikopo kwa maslahi yao binafsi, lakini mashamba yale hayaendelezwi. Ningewaomba ndugu zangu wa Mkoa wa Tanga tuungane kwani matatizo yetu yako sawa na yao. Naomba Serikali ifuatilie suala hilo ili kuwanusuru wananchi wake ambao wako pale kwa muda mrefu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine naomba kuungana na Mbunge mwenzangu Mbunge Jitu kuhusu suala la kodi ya pembejeo za kilimo. Leo utaona pampu ndogo ya kumwagilia maji unapata dola 80 mpaka dola 120 kutoka China. Lakini hapa kwetu tunauziwa laki nne na nusu mpaka laki tano. Sasa Serikali inajua suala hilo na imesema imetoa lakini bado, wanabaki wafanyabiashara kama ni mradi wa kujipatia utajiri wa haraka. Sasa huyo mkulima mdogo anunue mashine laki nne na nusu atapata wapi hela ya kununua? Kwa kweli ni mzigo mkubwa kwa wakulima wadogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kumalizia suala langu la mwisho kuhusu mpango wa Serikali kuangalia kodi za pembejeo. Naomba Serikali iangalie sana, mikopo kwa watu maalum kama wakulima wadogo. Nina uhakika mkulima mdogo wa miwa ana uwezo wa kulipa trekta kwa muda wa miaka mitatu au mitano kutokana na kipato anachopata.

Mheshimiwa Naibu Spika, pale katika ofisi za Halmashauri za Wilaya, watendaji wanakaa wanakwambia bajeti ya kwenda Wizarani hatuna. Hata ripoti ya Wizarani hazina uhakika, inawezekana ni za kubuni au ni za miaka iliyopita. Nadhani Wizara ina taarifa zile ambazo siyo sawasawa na si za wakati muafaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru.

**NAIBU SPIKA:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Abdulsalaam Selemani Ameir.

Waheshimiwa Wabunge kuna tangazo la Mwenyekiti wa Kamati ya Ardhi, Maliasili na Mazingira, Mheshimiwa Lembeli; anawaomba wajumbe wa Kamati hiyo 7.15 mchana, ukumbi namba mia 227.

Tunaendelea, Mheshimiwa Kidawa Salehe, atafuatiwa na Mheshimiwa Rachel Mashishanga na Rebecca Mngodo ambao watagawana dakika tano tano. Mheshimiwa Kidawa Saleh!

**MHE. KIDAWA HAMID SALEH:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi, nami nichangie mchango wangu wa jumla katika bajeti hii ya Wizara ya kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, wote tunakubali kwamba, kilimo ni sekta tegemeo na kimbilio kwa Watanzania walio wengi. Karibu asilimia sabini na tano ya Watanzania wanaishi Vjijini na Watanzania wote tunategemea kilimo kwa maisha yetu. Kwa sababu tunang'ara, tunanenepa matumbo na mashavu kwa sababu ya wakulima kuwa wanalima na wanatulisha. Kwa hiyo, kilimo kina umuhimu mkubwa kwetu sisi sote. Umuhimu huu wa kilimo unahitaji Serikali iwekeze zaidi na bajeti ya Wizara ya Kilimo iongezwe ili kuonesha kweli kuna umuhimu wa kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, *Maputo Declaration* ilitaka angalau bajeti ya Sekta ya Kilimo ifikie asilimia kumi, lakini naona bado tuko mbali kufikia lengo hilo. Kwa hiyo, Serikali iwekeze zaidi ili kufikia angalau asilimia hiyo kumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukuaji wa kilimo umekuwa ukiyumba yumba. Mwaka 2010/2011, kilimo kilikuwa kwa 4.2%. Mwaka 2011/2012 kilimo kilishuka kwa 3.6% na mwaka huu unaomalizika tunambiwa kilimo kitakuwa kwa 4.3%.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukiangalia ongezeko la ukuaji wa watu la wastani wa 2.9% kwa Tanzania nzima na yumkini kwamba, kule katika sekta ya Kilimo ukuwaji wa watu ni 3%, kwa sababu takwimu zinaonyesha wastani wa kaya ni watoto watano, lakini kule kwenye sekta ya kilimo ni watoto saba na kwenda juu. Kwa hiyo, yumkini ukuaji huu wa kilimo hautoshelezi kabisa kukidhi ukuaji wa watu tulionao.

Mheshimiwa Naibu Spika**,** kwa hiyo, kuna kazi kubwa ya kufanywa na ndiyo maana kuna malalamiko kwamba, Serikali inasema uchumi wa nchi hii unakua kwa asilimia 6.9, lakini walio wengi wanalalamika mbona hali ya umaskini imebakia vile vile au umaskini unaongezeka? Uchumi huu unakua kwa kiasi gani? Kumbe ni kwamba, watu walio wengi hasa katika Sekta ya Kilimo, hawajaguswa na ukuaji huu wa uchumi, kwa sababu sekta zinazosabisha kukua kwa uchumi, siyo sekta ya kilimo!

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kuna kazi kubwa ya kufanya katika sekta ya kilimo, uwekezaji wa hali ya juu unatakiwa kuwepo katika sekta ya kilimo, ili sekta ya kilimo ikue na kila mmoja aone kama kweli uchumi unakua. Kila mmoja aguswe na ukuaji wa uchumi ndani ya nchi yake na umaskini uweze kupungua.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunajua kuna changamoto nyingi katika sekta ya kilimo na Serikali inajaribu ku-*address* changamoto hizo. Kwa mfano, katika maeneo ambayo yamelalamikiwa sana hapa ni kwamba, kilimo chetu bado kinaendeshwa kwa jembe la mkono na wakulima walio wengi ni wazee ambao hawana nguvu tena za kulima. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kilimo cha matrekta, maksai ni muhimu sana, angalau watu waanze kufundishwa. Maeneo mengine hata kulima kwa maksai hawajui, ng'ombe wanawaogopa. Kama kule kwetu Zanzibar ukisogeza ng'ombe hapo mbele watu wengi wanakimbia, lakini ni kitu muhimu kwa kuanzia.

Mheshimiwa Naibu Spika**,** lakini na matrekta ni jambo muhimu, angalau kila Kata, kungewekwa matrekta mawili mawili yangesaidia sana wakulima wetu na wakulima wakawekewa lengo, labda kila Kaya ilime heka nne, au zaidi, si chini ya heka nne na pembejeo zikafika kwa wakati, naona hali ingebadilika.

Mheshimiwa Naibu Spika**,** lakini kuna tatizo hata la mbegu bora, ni kitu cha aibu kabisa! Tunapigia kelele watu walime, lakini mbegu hazipatikani ndani ya nchi yetu kwa asilimia 100, mbegu zinaagizwa mbegu kutoka nje kwa asilimia 75, tunategemea nini? Asilimia 75 mbegu zinatoka nje! Ardhi tunayo ya kutosha! Kwa nini hatuzalishi mbegu bora hapa kwetu! Vyuo vya utafiti vikafanya tafiti, lakini na humu humu ukaandaliwa mpango madhubuti wa kuzalisha mbegu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini mbegu zinaagizwa kutoka nje na zikifika nyingine hazifanyi kazi, kwa sababu utafiti wa udongo hapa kwetu unatofautiana na zile mbegu zinazotoka huko nje. Watu wanalalamika, wananunua mbegu kwa bei ya juu, lakini zikifika hazifanyi kazi, ni hasara tupu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tujiulize kulikoni ndani ya Tanzania, hata mbegu basi tuagize kutoka nje? Matrekta tuseme hatuna Viwanda vya Trekta, lakini mbegu pia tunashindwa kuzalisha hapa kwetu! Kwa kweli ni kitu cha aibu! (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ni kwamba, vijana wetu hawapendi kilimo na hawapendi kilimo, siyo kuwa hawapendi tu hivi hivi, lakini wana sababu! Vijana wanataka wafanye kazi za haraka haraka, za kuwapatia kipato cha haraka haraka. Kwa hiyo, kuwe na motisha ya kuwafanya vijana wapende kilimo, lakini kama hakuna motisha kijana gani atapenda kilimo. Tutalalamika kuna Wamachinga wengi huko mjini, lakini ndiyo hali halisi ilivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, Serikali naipongeza kwa kuanza ile *program* ya kuwatengea ardhi vijana na kuwasaidia kuweza kushiriki katika kilimo. Basi wapewe ardhi, wapewe miundombinu yote ya kuwasaidia kulima, wapewe matrekta, lakini vile vile wasaidiwe kupata nyumba zile za bei nafuu! Ili wa-*settle* pale walipo, wafanye kazi ya kilimo na naamini watazalisha. Kilimo cha mboga mboga, matunda na maua vina faida kweli, vijana wetu wahamasishwe na wasaidiwe kushiriki katika kilimo hiki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nchini kwetu kuna tatizo la mfumko wa bei na huu mfumko wa bei unatokana na upungufu wa chakula, mbali ya kuwa tuna *imported inflation* ya mafuta ambayo hatuna uwezo nayo. Kwa hiyo ile adhima ambayo imejadiliwa kwenye *Lab*, ya kuongeza uzalishaji wa chakula, mahindi, mpunga na miwa, Serikali ishikilie hapo hapo, ifanye jitihada, chakula kipatikane kwa wingi, lakini na masoko ya chakula ya mazao hayo yaweko.

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wanazalisha, katika Mikoa mingine, wanazalisha hatimaye unaona mifuko ya mpunga na mahindi yanagalagala tu, wakati maeneo mengine wanakosa chakula. Hata uwezo wa kusomba basi chakula kutoka Mkoa mmoja kupeleka Mkoa mwingine watu wasife njaa hatuwezi? Tuna tatizo gani? Watu wanalima, wana-*toil*, wanalima, lakini hata kusambaza kile chakula na kununua tunashindwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali tunaomba ijitahidi katika hayo, lakini vile vile, Serikali ihamasishe kulima chakula kinachostahimili ukame. Unajua katika nchi yetu na ulimwengu mzima, tuna tatizo la tabia nchi, maeneo mengine kuna mafuriko, maeneo mengine kuna ukame. Kwa hiyo, tujaribu kutumia hali hii inayojitokeza, lakini watu wetu tuwanusuru wasife njaa!

Mheshimiwa Naibu Spika, kule ambako kuna ukame, watu wafundishwe kulima mazao mengine kama mtama, mhogo, viazi, vyote ni vyakula, wasishikilie tu mahindi, mahindi

kwa kuwa ndiyo tumezoea. Matokeo yake, watu wanakosa chakula na wanapata shida, inabidi watafutiwe chakula labda kutoka nchi za nje na nini, lakini tukiwahamasisha kulima vyakula vinavyostahmili ukame, inaweza ikanusuru tatizo la njaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie ajira kwa vijana na viwanda vya kusindika mazao. Tumekuwa tukipiga kelele siku nyingi hapa, matunda yanaoza, mboga zinaharibika, tunasema Serikali ihamasishe basi uwekezaji katika hivi viwanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru na naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Kidawa Saleh. Kama nilivyosema Mheshimiwa Rachel na Mheshimiwa Rebecca watagawana dakika tano, tano. Mheshimiwa Rachel Mashishanga!

**MHE. RACHEL M. ROBERT:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kabla sijazungumza kwa mara ya kwanza kabisa kupitia mdomo wangu huu, natamka kwamba siiungi mkono bajeti hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie suala la pamba. Zao hili limekuwa likichangia pato la Taifa kwa asilimia kubwa sana mpaka sasa hivi, lakini limekuwa na changamoto nyingi sana ambazo zilikuwa zikiwakabili wakulima. Naomba nizitaje kwa haraka haraka hizi changamoto pengine ndiyo zinaweza zikasaidia mkulima akanufaika kwa zao hili la pamba.

Mheshimiwa Naibu Spika, ruzuku ya pembejeo; tumejionea maeneo mengi sana ruzuku hizi za pembejeo zimekuwa zikichelewa, kwa mfano, kwa Mikoa ya Shinyanga na Simiyu, wakulima walikuwa wakilima pamba kuanzia mwezi wa Novemba, lakini zinakuja mwezi wa Tatu. Hii inachangia wafanyabiashara ambao wamekuwa wakileta ruzuku, baada ya kuona ruzuku za Serikali zinachelewa, kuja

kuwauzia wakulima kwa bei ya juu sana. Naomba Mheshimiwa Waziri aliangalie hili ili msimu ujao hiki kitu kisitokee.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kuna tatizo la bei, bei hii imekuwa haieleweki, kadri miaka inavyokwenda bei inakuwa haieleweki, wakulima wa pamba wamekuwa wakikata tamaa sana. Vile vile, kwa nini Serikali isifikirie hili suala la kuwepo na *stimulus package* kwa ajili ya pamba. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkoa wa Shinyanga na Simiyu ni wakulima wa pamba sana, sasa tunavyowatelekeza tunakuwa tunawakatisha tamaa na ni zao ambalo linategemewa sana kwa ajili ya kuinua uchumi wao. Hivyo, pamoja na kuwa wakulima wamekuwa wakililima, lakini hakuna kitu wanachokipata.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini bado kuna matatizo, wakulima hao wanapokwenda kuuza pamba yao kwa wanunuzi, wamekuwa wakikatwa kilo moja katika kila mzigo, kilo moja hiyo inakatwa kwa sababu ya kile wanachobebea ambacho inakuwa ni nguo. Hivi kwa akili ya kawaida, mtu labda amefungia *khanga*, anakatwa kilo moja, hivi *khanga* kweli inaweza ikawa na uzito wa kilo moja! (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, wakulima wanaonewa sana, lakini vile vile, wakulima hao wana ukosefu wa mafunzo, kwa mfano, kama viuatilifu, vimekuwa vikienda vya aina mchanganyiko, lakini Maafisa Ugani hawakai *site*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka jana nimefanya ziara Mikoa ya Simiyu na Shinyanga, nimetembelea wakulima wa pamba, wamekuwa wakilalamika Maafisa Ugani hawakai *site*. Matokeo yake viuatilifu vinaletwa, lakini hakuna mafunzo yanayotolewa, wanachanganya visivyo, matokeo yake inaonekana haifanyi kazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ni sawa na hospitali, unakwenda unapewa dawa, halafu huambiwi unaitumiaje.

Matokeo yake utaitumia visivyo, ikikudhuru ndiyo unakuja kugundua kwamba kumbe nilitakiwa niitumie hivi. Naomba elimu itolewe kwa ajili ya matumizi ya viuatilifu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile, kuna suala la hao wanunuzi, tuna wanunuzi wengi na wanakwenda hata kununua pamba nchi jirani. Inasemekana kwamba, wanapokwenda nchi jirani wanawasaidia sana wale wakulima wa kule, lakini wakulima ambao ni wazawa, wakulima wetu wa Tanzania, pamoja na kwamba hao wafanyabiashara ni Watanzania, hawawasaidii hata kwa pembejeo, lakini wanapotoka nje ya nchi wanakuwa wanawasaidia kwa kila kitu. Sasa hii inatupa wasiwasi kwa nini wanarudisha mikono nyuma kwa Watanzania wenzao, na wanaweka mikono mbele kwa wakulima wa nje. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Wizara ifuatilie suala la kilimo cha Mkataba. Kilimo cha Mkataba sisemi kama kiondolewe kabisa, hapana, lakini ninachosema, basi mkulima aachiwe kuchagua, asilazimishwe aende kwenye kilimo cha Mkataba. Vinginevyo basi elimu itolewe kwa wakulima, kwa sababu watu wanaingia kwenye Mikataba ya hicho kilimo bila kujua madhara yake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, utakuta mtu ana pamba yake, amekuja Mwarabu mwingine kuinunua hiyo pamba, akija aliyeingia naye Mkataba, anamwambia ooo! Fulani ameshachukua, sasa hii inaleta *contradictions* baina ya wakulima pamoja na mnunuzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Sasa namwita Mheshimiwa Rebecca Mngodo.

**MHE. REBECCA M. MNGODO:** Mheshimiwa Naibu Spika, sijaona katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, ni namna gani Wizara yake itawasaidia wakulima wadogo wadogo ili waweze kutumia ardhi waliyo nayo, kama ni ndogo waweze kuzalishwa zaidi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tunajua kwamba, dhana ya kilimo kwanza ililenga kuhakikisha kwamba, kilimo cha wakulima wadogo, wa kati na wakubwa, kiwe cha kisasa na cha kibiashara ifikapo mwaka wa 2015. Mpaka sasa ni 2013, hatujaona mafanikio yeyote ambayo yametokana na dhana hii ya kilimo kwanza, badala yake tumeona kwamba ni biashara ya matrekta ilijiingiza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nitatoa mifano ya wakulima wadogo wadogo katika Wilaya ya Meru, Mkoani Arusha, ambao kihistoria walikuwa wamezaliwa katika hivyo vijiji, walikuwa hawajawahi kumiliki hata baiskeli, lakini wakaletewa mpango na utaratibu fulani uliojiingiza, wakakopeshwa matrekta kati ya milioni 25, 30 na wengine milioni 45.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapozungumza sasa hivi, wakulima hao wameangukia katika janga kubwa la hofu, wanaishi kwa hofu, wamerudi chini kuwa maskini, kwa sababu hawakupatiwa elimu yeyote walipokuwa wamepewa ile Mikataba. Cha kushangaza, ukiangalia mikataba ile ambayo imetolewa na Wakala kupitia Wizara hii ya Kilimo, imeandikwa kwa lugha ya Kiingereza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, wakulima wengine hawajafika hata darasa la saba, wengine hata la kwanza hawajafika, lakini wanaandikiwa mkataba wa mamilioni ya fedha kupewa trekta, mkataba ambao umeandikwa kwa Kiingereza! (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, huyu mkulima ambaye hajawahi kumiliki baiskeli anaona trekta, kwa vyovyote atasaini ule mkataba. Hivyo, kuna wakulima ambao wameangukia katika mtego huu, kupata matrekta, lakini wameshindwa kurudisha ile mikopo kwa wakati. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa tu hawakujua ile lugha iliyokuwa imeandikwa katika ile mitakaba na kipengele kimojawapo ni kwamba, wangerudisha hizo fedha kila mwezi. Je, mkulima ambaye anategemea kwanza mazao yake,

kwanza anasubiri mvua, aanze kulima shamba lake, aoteshe mazao yake halafu ndiyo akauze, apate fedha na ndipo aweze kurudisha fedha ile ambayo amekopa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa mkataba ambao umeandikwa kwa lugha ya Kiingereza, hajui kilichokuwa kimeandikwa, kwamba angerudisha kila mwezi. Kwa vile ameshindwa kurudisha kila mwezi, kilichotokea katika kijiji mojawapo huko Wilayani Meru ni kwamba, mkulima mmoja alishtukia kwamba, gari linapita na vipaza sauti, likitangaza kuuza shamba la mkulima huyo, na hivyo ikawa ni aibu kubwa kwake, amedhalilishwa na Serikali yake na kilichobaki ni aibu kwa yule mkulima.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi mkulima huyu kwa kweli anaishi kwa hofu, hatoki, akisikia king'ora tu anaogopa. Hivyo, napendekeza kwamba, mikataba hii iangaliwe upya. Tena mikataba hii iandikwe upya kwa lugha ya Kiswahili. Ni kweli kwamba, wengine walishindwa kulipa na muda mwingi umepita na hivyo wakatozwa faini. Mkulima mmoja alitozwa faini ya shilingi milioni tano, hakupewa hata risiti.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, haijulikani sasa, huku ni kumsaidia mkulima ajikwamue na umaskini, au huu ni mpango wa kuzidi kumgandamiza huyu mkulima na kumfanya aendelee kuwa maskini katika kijiji alichozaliwa na kuishi kwa hofu akiogopa kwamba, shamba lake sasa litakuja kuuzwa ili aweze kurudisha zile fedha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sana, Wizara kama haina habari na jambo hili, lipo linaendelea na wakulima wengi wamebaki kuwa ni ombaomba. Wakipata simu zetu sisi Wabunge wanabaki kuomba umsaidie kurudisha fedha milioni 20 ambazo sijui hata huyo Mbunge atazipata wapi kwa sababu tu ya mpango na utaratibu ambao haukutolewa kiuhakika kwa kutoa kwanza elimu kwa wakulima.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Rebecca. Mheshimiwa Selemani Said Bungara, atafuatiwa na Mheshimiwa Munde Tambwe na Mheshimiwa Mrema ajiandae. Mheshimwa Bungara!

**MHE. SELEMANI S. BUNGARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, nashukuru sana kupata nafasi hii. Pili, namshukuru Mwenyezi Mungu. Tatu naishukuru Serikali ya CCM kwa jinsi wanavyowafinya wanyonge, basi wanatupa nafasi sisi Vyama vya Upinzani kupata watu wengi katika sehemu hizi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naishukuru sana Kamati ya Kilimo, pia namshukuru sana Profesa Msolwa kwa taarifa yao waliyotoa katika Bunge hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la kwanza, nazungumzia Bajeti ya Kilimo na nanukuu taarifa ya Kamati kwamba, bajeti ya Kilimo ni finyu, inasema, mwaka 2009 Serikali walitenga asilimia sita, mwaka 2010 asilimia saba, mwaka 2011 asilimia 7.7, mwaka 2012 asilimia 5.4 na mwaka huu asilimia saba, lakini Kamati inashauri kwamba, Bajeti ya Kilimo ifikie asilimia 10.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ilani ya CCM ya mwaka 2005/2010 mliahidi kwa Watanzania kwamba, mtafikisha asilimia 10, lakini kutokana na matatizo ya Serikali na Chama cha Mapinduzi, kutokutekeleza ahadi zake, basi mpaka leo asilimia 10 katika Ilani hawajatimiza, wala Mkataba wa *SADC* hawajatimiza, hii inaonyesha CCM ina matatizo na Serikali yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naipongeza sana Kamati ya Kilimo kwa kuiambia Serikali ya CCM, mwaka unaofuata mtimize ahadi ya Sera yenu ya CCM au Ilani ya CCM na ahadi ya Mkataba wa *SADC*.

**MBUNGE FULANI:** Taarifa.

**MHE. SELEMANI S. BUNGARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, nawapongeza sana Wabunge wanaotukana katika Bunge hili. Nawapongeza kwa sababu ndiyo waliotumwa na wananchi wao waje kutukana ndani. Kwa hiyo, hawana kosa kama wakitukana, kwa sababu wametumwa na wapiga kura wao, nawapongeza sana. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu mimi nipo katika mpango wa stakabadhi ghalani, mwaka 2011 nilisimama hapa na nikaupinga sana mfumo wa stakabadhi ghalani katika zao la ufuta na kuna watu wakafikia hatua wakasema huyo huyo Mheshimiwa ana masilahi na zao la ufuta! (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini Mwenyezi Mungu kwa kuwa anampenda msema ukweli, mwaka 2012/2013, watu wa Kilwa au Halmashauri ya Kilwa tukaamua kuondokana na mfumo wa stakabadhi ghalani katika ufuta na tukapata bei nzuri, bei ya ufuta ikatoka sh. 1,000/= mpaka sh. 1,800/=.

Mheshimiwa Naibu Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Kilwa ilikuwa inapata ushuru wa shilingi milioni 70 mwaka jana tumepata shilingi milioni 370. Kwa hiyo, tumeshukuru sana kuondokana na mfumo wa stakabadhi ghalani kufutwa Wilaya ya Kilwa, mambo mazuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini leo nazungumzia stakabadhi ghalani na kuna matatizo mtu ukizungumzia habari ya stakabadhi ghalani kuwatetea wananchi, mnasema wana maslahi watu hao katika jambo hilo. Leo nina *form* za watu 5,508 wa Wilaya ya Ruangwa na Kilwa ambao hawautaki mfumo wa stakabadhi ghalani.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kwa heshima na taadhima upokee majina ya watu hao ambao hawataki mfumo wa stakabadhi ghalani na baada ya muda nitakabidhi ili Serikali ijue kwamba jambo hili sisemi Bwege, bali wanasema wananchi wa Mikoa ya Kusini hawautaki mfumo wa stakabadhi ghalani, nitakukabidhi baadaye, watu 5,208 wametia saini na kuna namba zao za simu kama una

wasiwasi utawapigia, hawautaki mfumo wa stakabadhi ghalani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wapo watu wa Ruangwa, Nachingwea, Tandahimba, Kilwa na kwa bahati mbaya kabisa sehemu zote hizo waliomba maandamano, Serikali ya *CCM* ikawaambia msiandamane kwa sababu mkiandamana watajua kwamba watu wengi hawautaki mfumo wa stakabadhi ghalani. Kwa hiyo, wakaona bora sasa wajiorodheshe! *(Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, watu wa Tandahimba, Nachingwea wapo humu na wa Liwale! Wakulima wa korosho siyo hawataki mfumo wa stakabadhi ghalani kwa sababu hawautakiutaki tu, hapana! *(Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka huu mpaka sasa hivi ninavyokwambia watu hawajalipwa malipo ya pili na Wilaya ya Kilwa kuna watu wamelipwa malipo ya pili, badala ya kulipwa sh. 600/=, wanalipwa sh. 250/=, naitaka Serikali ya CCM baki ya sh. 350/= iliyobaki mlipe lazima na kama hamkulipa, piga ua, tutaandamana lazima. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, Halmashauri za Wilaya zote zinazolima korosho hawajapata ushuru wa zao la korosho, kwa mfano kwetu Kilwa, Halmashauri yetu ilipanga tutapata shilingi milioni 50, lakini kutokana na mfumo wa stakabadhi ghalani kuwa mbovu hata senti tano hatupati. Tunataka Serikali ifidie pengo hilo kwa sababu wao ndiyo wanaolea mfumo wa stakabadhi ghalani. Tunawaomba sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukurasa wa 51, katika hotuba ya Waziri anasema, mfumo wa stakabadhi ghalani, hata hivyo mfumo huu unakabiliwa na changamoto zinazotokana na upotoshaji unaofanywa na walanguzi na madalali wanaojinufaisha na ununuzi wa mazao ghafi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri anaongopa tu, anaongopa tu! Mpaka sasa hivi mkulima wa korosho hajalipwa korosho yake na anavyolipwa analipwa pungufu. Unawaambia walanguzi wanasababisha mfumo wa stakabadhi ghalani usitakiwe. Sio walanguzi, ni mfumo wenyewe hautendi haki kwa wakulima.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba sana Serikali ya CCM, Serikali sikivu, Serikali yenye macho, Serikali yenye pua inanusa, Serikali yenye mdomo inalamba, lakini Serikali yenye mikono michafu ambayo haitendi haki kwa wananchi wa Tanzania. Tunaiomba Serikali ya CCM kama hamkujirekebisha mwaka 2015 kwaherini. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana! *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Huyo ni Mheshimiwa Selemani Said Bungara almaarufu kama Bwege. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Munde Tambwe, atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Augustine Mrema.

**MHE. MUNDE A. TAMBWE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kuchangia Wizara ya Kilimo.

**NAIBU SPIKA:** Wasaidizi humu ndani naomba ile *document* mtuletee mezani, Mheshimiwa Munde, endelea!

**MHE. MUNDE A. TAMBWE:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nianze kuisifu Serikali yangu ya Chama cha Mapinduzi, nia yake ilikuwa safi kabisa na nia yake ni thabiti ya kutaka kumkomboa mkulima na ndiyo maana ikaja na mpango wa *power tillers*, matrekta na mbolea za ruzuku. Nia ni nzuri kabisa, tatizo ni changamoto zinazojitokeza na changamoto hizi, sisi viongozi ni lazima tupambane nazo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, unaweza kuwa na nia nzuri hata nyumbani kwako, ukatoa wazo zuri lakini watu

wakaliharibu. Kwa hiyo, naisifu sana Serikali yangu, kwani kila siku imekuwa ikibuni mpango wa kuwakomboa wakulima. Hizi changamoto tunavyokabiliana nazo ndivyo tutakavyozidi kutatua matatizo yao na hatimaye watafanikiwa huko baadaye. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kuongelea suala zima la njaa, hata sisi Mkoa wa Tabora na Manispaa ya Tabora tunakabiliwa na tatizo la njaa. Tulikuwa na mahitaji ya tani 16,000, lakini mpaka leo Serikali imetupatia tani 700 tu, tunatakiwa tuongezewe tani kama 16,000. Kwa hiyo, niiombe Serikali kupitia Wizara ya Kilimo kwamba, tunaomba ituletee chakula hicho kwenye vijiji vingine hali ni mbaya sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze na suala zima la pembejeo za kilimo, Waheshimiwa Wabunge wengi wameongea kuhusu pembejeo za kilimo. Suala hili linasikitisha, halifuati kama Serikali ilivyokuwa inataka, vocha hizi watu wanapewa fedha wanakubali kwamba wamepewa mbolea, wakati si kweli. Naamini wazo la Serikali ni zuri, watu hawa wangepewa mbolea, mbolea hiyo wakailimia naamini *impact* ya chakula ingekuwa kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini binadamu ndiyo sisi na haya mambo tunayaharibu sisi wenyewe binadamu. Tunafika kule tunafanya vitu vingine, lakini naamini Waheshimiwa Wabunge wameliongea suala hili vizuri, Serikali imesikia na italichukulia hatua ili kuweza kumpatia *impact* mkulima na kuonesha juhudi za Serikali zinavyofanya kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini niiombe Serikali sasa kwa sababu tuna dhana ya Kilimo Kwanza basi twende na hicho kilimo kwanza kwa mpango wa kisasa. Kwa nini Serikali isijenge Maabara kila Mkoa ya kupima udongo ili kujua Mkoa huu unakubali mbolea ipi na Mkoa huu unakubali mbolea ipi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukijenga maabara ya kupima udongo pale Mkoani, basi Wilaya zote zitapima

udongo wake, ukiona kijiji fulani chakula hakiendi vizuri utachukua udongo utapima na ushauri utatoka kwamba, watu hawa mbolea hiii ndiyo inawafaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano kwetu Tabora, wananchi wengi hawapendi mbolea ya Minjingu. Sasa tunashindwa kuelewa kwamba hawaipendi tu kwa mazoea tu kwamba wamezoea mbolea ya *Urea* na kadhalika au hawaipendi kwa sababu haiwasaidii kwenye mazao yao, lakini kungekuwa na maabara ya kupima udongo tungejua kama Mkoa wa Tabora unastahili kupeleka mbolea gani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba sana tufanye hivi vitu kisayansi kidogo ili kuondokana na lawama ambazo hazina mpango wowote.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa na mabadiliko ya tabianchi. Mabadiliko ya tabianchi imekuwa ni tatizo kubwa, vipindi vya mvua vinabadilika na vipindi vya kulima vinabadilika na kadhalika. Unaweza ukaamua kwamba tunalima mwezi wa Kumi na Moja kumbe mvua isije mwezi wa Kumi na Moja. Kwa hiyo, tabianchi kwa kweli pia na yenyewe imechangia kuathiri sana suala zima la kilimo. Kwa hiyo, kilichopo hapa sasa ni kuhakikisha tunapata mabwawa ya kutosha ili kukabiliana na tabianchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tabora Manispaa katika Kata ya Inala, Kijiji cha Inala tulikuwa tumepewa bwawa mwaka 2010 lenye thamani ya shilingi bilioni moja na milioni hamsini na tisa. Lakini jambo kubwa la kusikitisha, sasa ni mwaka wa nne lile bwawa limekamilika kwa 37% tu. Ni kweli tupo *serious* na hiki kitu cha Kilmo Kwanza au tunaongea tu? Kwa sababu miaka minne huwezi kukamilisha bwawa kwa 37%. Kwa hiyo, namwomba sana Mheshimiwa Waziri aje na mpango atueleze kwamba hili bwawa litakamilika lini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimesikiliza hotuba ya Waziri Mkuu imetaja bwawa la Inala lipo kwenye mpango, lakini

nimefuatilia kuona mwaka huu tumetengewa shilingi ngapi kama lipo kwenye mpango. Kwa kweli sikuona hizo fedha zilizotengwa. Nimejaribu kumfuata Naibu Waziri wa TAMISEMI, Mheshimiwa Mwanri, nimemuuliza kwamba hili bwawa limetajwa kwenye hotuba ya Waziri Mkuu, lakini nimeangalia kwenye randama na kila sehemu lakini sikuona pesa tuliyotengewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Naibu Waziri ameniambia bado anaendelea kufuatilia na yeye hajaziona hizo pesa. Kwa hiyo, nataka Waziri wa Kilimo akija hapa anijibu kwamba tumetengewa shilingi ngapi, anipe na *action plan* ya kulijenga hilo bwawa na kulimaliza maana lina miaka minne sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini vile vile niishukuru Serikali yangu pia kwa sababu walituletea wataalam wa *JICA* kwenye hilo hilo bwawa, tukaja tukajengewa mifereji, lakini wataalam wale ardhi ile wakaipenda sana kwa kilimo cha mpunga. Wakawachukua wanakijiji wa kijiji kile wakawapeleka semina kwa ajili ya kilimo cha mpunga na wakasema eneo lile lina uwezo wa kutoa magunia 50 kwa hekta.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, wanakijiji wale wamefundishwa, mifereji imejengwa na ujenzi wa bwawa umesimama kabisa, ni kitu ambacho kinasikitisha sana kwani watu walishapata moyo mkubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, niiambie Serikali kwa ujumla na nafurahi Waziri Mkuu yumo humu ndani, niiambie Serikali kwa ujumla kwamba vitu vyetu vya Tabora vinakwamakwama sana. Sisi ndiyo tunaolima tumbaku, unashangaa *processing* ya tumbaku inafanyika Morogoro.

Mheshimiwa Naibu Spika, unabaki unashangaa na sisi Tabora tuna vijana na vijana hawa hawana ajira, kule Morogoro wanaajiri karibu watu 3000 katika msimu wa

tumbaku, barabara zinaharibika kwa kubeba magari mazito yaliyojaa tumbaku, kwa nini Tabora hawajengi Kiwanda cha Tumbaku? Tatizo ni nini?

Mheshimiwa Naibu Spika, nashindwa kuelewa kabisa, tumbaku nyingi inalimwa kwenye Mkoa wa Tabora, lakini Viwanda vya ku-*process* vipo Morogoro, unabaki unashangaa Tabora kuna nini jamani?

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi tunasafiri kutoka Tabora mpaka Nzega ambako ni kilomita 116, tunatumia masaa nane kwenye kilomita 116, barabara zinaharibika mno na hayo magari ya tumbaku, kwa nini msitujengee Tabora jamani? Sijui tatizo ni nini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli naomba kabisa Waziri atakapokuja hapa aje anijibu kwamba, hili bwawa linakamilika lini na Serikali imetenga shilingi ngapi, angalau nimeiona kwenye hotuba ya Waziri Mkuu ukurasa wa 30, lakini sijajua kwamba ni lini.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie na Wilaya ya Igunga, katika Wilaya ya Igunga alikuja Mheshimiwa Rais kwenye ziara. Alipokuja Mheshimiwa Rais wananchi wa Igunga wamemshukuru sana na wamempongeza sana Mheshimiwa Rais pamoja na Serikali yake kwa kutujengea Mto Mbutu kwani mto ule ulikuwa ni kero kubwa kwa wananchi na ulikuwa unasababisha mpaka mauaji ya wananchi. Kwa hiyo, tunaishukuru sana Serikali kwa kujenga daraja kubwa pale.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini wananchi wa Wilaya ya Igunga wakamwomba Mheshimiwa Rais, yale maji yanayotoka Mto Mbutu yanaharibika na yanamwagika bure na ukiangalia zama hizi ni zama za mabwawa, wakamwomba Mheshimiwa Rais awajengee bwawa kutokana na maji yanayotoka na kumwagika bure kwenye barabara huko.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, Mheshimiwa Rais amewakubalia kuwajengea bwawa la maji mengi yanayomwagika bure kutoka Mto Mbutu. Sasa namwomba Mheshimiwa Waziri wakati ana-*wind up,* aniambie Wizara yake ina mpango gani sasa wa kuanza kujenga lile bwawa na litaanza kutekelezwa mwaka gani na kwa kipindi gani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kusema hayo machache, nadhani wamenielewa vizuri, nasubiri majibu mazuri kutoka kwa Mheshimiwa Waziri na naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimwa Munde Tambwe. Mheshimiwa Augustino Mrema atafuatiwa na Mheshimiwa Moses Joseph Machali.

**MHE. DKT. AUGUSTINE L. MREMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kutoa mchango wangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kule Kilimanjaro tuna mazao ya chakula na mazao ya biashara. Kwa upande wa chakula mwaka huu tumelima ndizi, mvua zimenyesha vizuri na watu inaelekea watapata ndizi nyingi, pamoja na matunda na mbogamboga, kilio chetu kitakuwa ni tumuuzie nani, soko hakuna.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naendelea kukumbusha na nilisema nilipochangia kwenye Ofisi ya Waziri Mkuu kwamba madam Serikali imeamua kwa makusudi kuwapatia ajira watu wa Vunjo na Kilimanjaro, kuwapatia vijana wetu kazi, lile soko la Njiapanda, la mbogamboga ndizi na matunda, ningeomba basi lianzishwe na Waziri Mkuu alishaniahidi siku moja kwamba atatembelea Kilimanjaro na atakwenda kukagua tena hilo soko.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, kutokana na hii sera ya Kilimo Kwanza, watu wangu wa Kahe Vunjo wamelima mpunga mwingi sana, lakini bei ya mpunga ni ndogo na watu

wamekopa fedha kutoka kwenye mabenki. Sasa naomba lile soko la pili la nafaka la Lokolova nalo lingeanzishwa, kwani kuna watu wapo tayari kuwekeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, haya masoko yasichukue tena muda kwa sababu mnapotamka sera zinazopendeza watu, basi watu wanaingia kazini. Sasa isije ikaonekana ndizi hazinunuliwi wala hazina soko, wale watu wa Kenya, Somalia na Sudan ambao tulisema watakuja Himo au Njiapanda watakuja kwenye soko la nafaka la Lokolova, isije ikachukue tena miaka miwili au mitatu, *otherwise* sera hii itaonekana haina maana. Kwa hiyo, hilo naomba Serikali ilikazane.

Mheshimiwa Naibu Spika, zao la tatu ni kahawa. Sasa hivi bei ya Kahawa ni mbaya sana kule Kilimanjaro, makopesho ni sh. 2,000/= kwa kilo, wakati kilo ya nyama ni sh. 6,000/=, bei ya unga ni kubwa kuliko hiyo bei ya kilo moja ya Kahawa. Hali ni mbaya, watu wanadai mabaki yao miaka miwili au mitatu iliyopita lakini hawajalipwa. Kwa hiyo, hali si nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka jana nilizungumzia juu ya mdororo wa uchumi, nikauliza kwa nini watu wa pamba na wa tumbaku pia wamefidiwa? Kwa nini *KNCU* ya Kilimanjaro haikupata fidia? Sikupata maelezo mazuri, ingawa nilimfuata hata Waziri Mkuu nyumbani kumwomba kwamba, kama watu hawatapata fidia inayotokana na ule mdororo wa uchumi hali itakuwa mbaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi *CRDB* inawadai wakulima wa *KNCU* shilingi bilioni moja karibu na milioni mia nne, sasa hivi imeshafika shilingi bilioni moja na milioni mia sita. Fedha hizi ina maana watakatwa kwenye kahawa yao, ndiyo sababu hawapati mabaki na ndiyo sababu kahawa inakuwa chini, tatizo ni kama hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikaona niandike barua nijue tatizo ni nini, lakini nashukuru Wizara ya Fedha ilinijibu tarehe 22 Oktoba, 2012 waliniandika kwamba Dkt. Augustino Mrema, malipo ya fidia ya hasara inayotokana na mdororo

wa uchumi duniani kwa *KNCU,* tafadhali rejea barua yako namba hiyo Vunjo Dodoma/203 ya tarehe 6 Agosti 2012. Ni kweli kuwa *KNCU* iliwasilisha maombi ya fidia ya hasara inayotokana na mdororo wa uchumi.

Uchambuzi wa awali wa takwimu uliofanywa na Benki Kuu ya Tanzania ulionesha kuwa walipata faida ya zaidi ya shilingi bilioni mbili kwa kipindi cha mdororo wa uchumi duniani, hivyo hawakustahili kupatiwa fidia. Hii ni barua ya Wizara ya Fedha, kumbe *KNCU* walipata faida!

Mheshimiwa Naibu Spika, ndiyo sababu hata Waziri alipokuja kule nikamwomba atume wakaguzi, kile Chama kinasambaratika na kinadidimia, kumbe walipata faida ya shilingi bilioni mbili, nauliza kwa nini watu wanakopwa kahawa yao? Kwa nini hakuna mabaki? Kwa nini hakuna ushuru?

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nikaitaka Serikali ikague hizi shilingi bilioni mbili au hii faida iliyopatikana wakati wa mdororo wa uchumi, kinachoendelea pale *KNCU* kama ile *KNCU* hamtaimulika au hamtachukua hatua, basi wakulima wa Kilimanjaro watapata shida sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2008/2009 nilivyosoma barua hii ya Wizara ya Fedha kwamba, walipata faida, Serikali inasema baada ya *KNCU Limited* kupatiwa taarifa kuwa hawakustahili kupata fidia kwa sababu walipata faida ya shilingi bilioni mbili.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ikasema *KNCU* waliandika barua Wizara ya Fedha ya kulalamika kuyapinga maamuzi ya Benki Kuu, wanapinga kwamba walipata faida. Aidha, mawasilisho haya yalifanywa baada ya kupita kwa kipindi cha kushughulikia fidia kwa mdororo wa uchumi. *KNCU* ikawasilisha taarifa na takwimu za ziada, Wizara ya Fedha ilielekeza Benki Kuu ya Tanzania kufanya uchambuzi tena ili kujua kiasi gani cha fidia wangestahili kupatiwa kama wangewasilisha maombi yao kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kwanza mmesema *KNCU* walipata faida shilingi bilioni mbili, zipo wapi? Nataka Mheshimiwa Waziri aniambie kwamba wale wakaguzi aliowaleta pale Kilimanjaro na wakanihoji hizi hela zipo wapi? Kwa sababu tunachojua ni kwamba, mwaka 2008/2009 *KNCU* walipata faida, lakini baadaye wakatengeneza hesabu za pili, wakasema wamepata hasara wakiitaka Serikali ifidie Serikali na ninyi sijui mliwashtukia, sijui machale yaliwacheza, mkakataa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2009/2010 wakapata faida tena, lakini wakatengeneza hesabu zao kuonesha kwamba wamepata hasara, badala ya ile faida kulipa mabaki kilichojitokeza ni kwamba wamekwenda kuchukua mkopo *CRDB*.

Kwa hiyo, naomba waniambie kinachotokea kule Kilimanjaro ni nini? Kwa nini watu wanatengeneza hesabu wanaziona, wanazikubali na baadaye wanatengeneza hesabu nyingine za bandia na mnazikubali? Kwa mfano, hii barua inasema kwamba, hizi hesabu za pili zilionesha kwamba *KNCU* wangestahili kufidiwa shilingi 255,107,576/=. Hizi fedha pia Serikali hamkuzitoa mpaka leo, kwa nini hamkuzitoa? Hilo ni la kwanza nililotaka nimwombe Waziri wa Kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hiyo faida iliyokuwa inapatikana *KNCU* wakitengeneza hesabu za kwanza, lakini baadaye wanatengeneza hesabu za bandia, hesabu za pili na bado Wizara inazikubali tena, inakuwaje? Halafu wanasema hapa, kwa vile uchambuzi huu ulifanyika baada ya kipindi rasmi cha utekelezaji wa mpango, sasa kama wale jamaa wa *KNCU* wakati ule rasmi wa kutengeneza hesabu hawakutengeneza, wakaja kutengeneza baada ya ule muda kwisha, mmewachukulia hatua gani? Hilo la kwanza, nataka kujua kwanza ile ripoti ya ukaguzi...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Dkt. Augustine Mrema.

**MHE. DKT. AUGUSTINE L. MREMA:** Nashukuru. Nitaunga mkono hoja hii Waziri akiniambia ile taarifa ya ukaguzi ataileta lini na wale wahusika wa ile sekretarieti ya *KNCU* atawafanya nini?

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa nakushukuru sana. Mheshimiwa Moses Joseph Machali atafuatiwa na Mheshimiwa Ritta Kabati.

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa ili nami nichangie hoja ya Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu utajikita katika maeneo kadhaa. Moja, ningependa nichangie juu ya uwepo wa Chuo cha Kilimo pale katika Wilaya ya Kasulu ambacho kinapatikana ndani ya jimbo langu la Kasulu Mjini.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika, ione umuhimu wa kuhakikisha kwamba huduma muhimu katika Chuo hiki kama vile maji ya uhakika zinapatikana ili kusudi Walimu na wanafunzi wasiwe na kazi kubwa ya kusafiri umbali mrefu kwenda kutafuta maji. Maji ni tatizo na ni imani yangu kuwa Mheshimiwa Waziri akiweza kufanya ziara pale atakuwa amejionea mwenyewe kwamba hali ya chuo kile kwa kweli siyo nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kama vile tumewachukua wataalam mbalimbali kwa maana ya Mkuu wa Chuo na Wakufunzi wengine na wanafunzi wetu kwenda kuwa- *dump* mahali pale. Niombe wakati Mheshimiwa Waziri anafanya majumuisho yake aweze kutueleza ni hatua gani za haraka ambazo pengine Wizara yake itachukua kuhakikisha Chuo kile kinapata huduma ya maji haraka iwezekanavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia wana suala la changamoto ya mabweni. Ukifika pale utaona miundombinu ya mabweni kwa kweli ni dhaifu mno na hata hivyo bado haitoshi. Ni mabweni yaliyojengwa toka miaka ya 1980 huko ambayo yamechakaa kwelikweli na Chuo kiko porini. Mheshimiwa Waziri amefanya ziara na anatokea huko, niombe kwa kweli ajaribu kukipatia *priority* Chuo kile ili kusudi kiweze kuwa na hadhi ya Chuo. Hivi sasa hata shule zetu za msingi zinaweza zikawa na hadhi kuliko kile chuo.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la tatu kuhusiana na Chuo hicho. Wale watu ukijaribu kuangalia mazingira ya chuo kile ni kwamba, kiko kwenye *isolated area*, ni kama porini hivi. Pale hawana shule ya msingi, shule ya sekondari na pale tunajua wafanyakazi kwa maana ya Wakufunzi wa chuo kile nao wana watoto wanahitaji kusoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa Serikali iweze kutoa msukumo pengine kwenye Halmashauri yetu huko waweze kupata angalau hata shule ya msingi ili kusudi wale watoto wa wafanyakazi waweze kusoma kwa ukaribu, vinginevyo tutakuwa hatuwatendei haki.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili, baada ya kuzungumzia Chuo cha Kilimo cha Mbondo, Wilaya ya Kasulu, ningependa nijielekeze kwenye suala la pembejeo. Niungane na Waheshimiwa Wabunge kadhaa hasa ndugu yangu Ali Keissy Mohamed, kwamba, mfumo na utaratibu uliopo mbolea yetu inaonekana inahujumiwa. Kwanza inakuja kwa kuchelewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitatoa mfano, mwaka jana Mkoa wa Kigoma uliweza kupokea vocha tarehe 26 Agosti, zilifika mapema sana. Wilaya ya Kasulu tukazipokea vocha hizo tarehe 29 Agosti, lakini maajabu mkulima anaanza kupewa mbolea yake mwezi Desemba na Januari, wakati huo watu walishapanda mahindi na mengine yanaweza kunifunika hata mimi na urefu wangu. Hiyo mbolea ya kupandia ya Minjingu mazao tunaipeleka kwenda kufanya nini kama siyo kuwapatia ulaji? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niungane na Mheshimiwa Mohamed Keissy, kama haiwezekani tukazuia kuleta mbolea ikiwa imechelewa, naomba Serikali iachane na suala la kusema kwamba, inatoa ruzuku ya mbolea kwa ajili ya wakulima kwa sababu inakuwa haina tija. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niseme tu kwamba, mwaka jana ilibidi niwahamasishe wananchi wa Jimbo langu wakatae kuchukua hiyo mbolea ya kupandia Minjingu mazao ili kusudi hawa watu wenye Makampuni, Mawakala pamoja na kampuni ambayo mmeipa zabuni ya kuhakikisha ina-*supply* mbolea, wapate hasara. Pia waone uchungu wa kusafirisha mbolea kutoka huko Arusha na kuileta mpaka kwetu, labda inawezekana wakati mwingine mkakaa sawa, mkasisitiza, kama tatizo liko kule chini mtawasukuma *DALDO* pamoja na watu wake ili wahakikishe mbolea inawafikia wakulima.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka huu nitaanza mapema kuwazuia kama mbolea itakuja kwa kuchelewa kama wakati ule. Nitawazuia tena wananchi wangu, nitawaambia wasichukue, japokuwa bado kuna wananchi ambao siyo waadilifu. Tunapewa taarifa baadhi wanasainishwa ili kusudi wakubali kwamba, wamechukua mbolea, kumbe wanaichukua halafu wanawapelekea wafanyabiashara na kwenda kuuza kwa bei ya kawaida ya mbolea.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningeomba Mheshimiwa Waziri na Wizara yake wajaribu kukaa na kuangalia vocha zisije bila kuwa na mbolea, walete vyote kwa wakati mmoja. Kama vocha zinafika mwezi Agosti inakuwaje mbolea inakuja kumfikia mkulima mwezi Desemba au Januari? Hiyo mbolea ni ya nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, cha kusikitisha, nakumbuka siku moja nilikaa kwenye kikao kile cha Kamati ya Pembejeo tukiwa na Mkuu wetu wa Wilaya ya Kasulu. Afisa Kilimo huyu ambaye mnamwita *DALDO* anasema kazi ya ile mbolea ni kwa ajili kuimarisha mizizi pamoja na yale mazao. Mbolea

imeitwa ni ya kupandia na tumezoea tunaweka mbolea wakati tunapanda zile mbegu, lakini yeye anasema hata yale mahindi ambayo ni marefu kiasi cha kuweza kunifunika, ile mbolea bado inaweza ikatumika. Nimekuwa na wasiwasi sana, sijui pengine wataalam wa kilimo watusaidie, lakini *experience* inaonesha wakati ule tunapotia mbegu kwenye mashimo, ndipo halikadhalika tunaweka pamoja na mbolea.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini inapojitokeza mtaalam wa kilimo anasimama na kutetea kwamba, hata kama mahindi yamekuwa ni marefu kufikia kimo change, bado unaweza ukatumia mbolea ya kupandia, nakuwa na wasiwasi na utaalam wa huyu *DALDO* wa Halmashauri ya Wilaya ya Kasulu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba tujaribu ku-*check* kwani huku ni kutufanya wajinga. Sasa wakati ambapo mahindi yamekua, uweke mbolea ya kukuzia pamoja na ile ya kupandia wakati mmoja inawezekana wapi na wapi? Naomba tuliangalie hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ambalo ningependa kuzungumzia ni la *National Milling*. Hapa juzi ilijitokeza kwamba, pale Arusha kuna mtu mmoja inaonekana amepatiwa umiliki wa kiwanda kama ambavyo wanamiliki akina Bakhresa pamoja na wengine. Lakini inaonekana kuna mchezo mchafu, Yule mtu hajaweza kumilikishwa moja kwa moja kama ambavyo wamemilikisha watu wengine kama akina Bakhresa na wengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ningependa nijue tatizo ni nini kwa mwekezaji huyu ambaye ni Mtanzania na pengine anastahili kuwa na haki kama watu wengine? Tatizo ni nini, kwa sababu inasemekana kwa taarifa zilizopo, ameomba kumilikishwa lakini bado Serikalini kunasuasua. Ningeomba kupata ufafanuzi katika hili, ni sababu gani zinapelekea mtu huyu kuchelewa kupatiwa kiwanda hiki ili aweze kukiendesha kama ambavyo watu wengine wameweza kumilikishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ningependa kuweka msisitizo. Jana niliuliza swali hapa kwa niaba ya Mheshimiwa Mbunge wa Kasulu Vijijini, juu ya ujenzi wa Soko la Kimataifa la Mazao katika Wilaya ya Kasulu. Ningependa kwa kweli suala hili walipe msukumo. Wanaweza wakasema kama alivyosema Naibu Waziri jana wakati anajibu kwamba, tatizo liko kwetu. Naomba wa-*check* pia na huko kwao kwa sababu wanaweza kukuta pengine tatizo liko kwao huko juu.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala hili pia liende sambamba na suala la mazao. Kwa kweli tunalima sana katika Wilaya ya Kasulu, tuweze kuangalia pengine na masuala ya barabara. Mnapokaa huko kwenye vikao vyenu vya Baraza la Mawaziri muweke mkazo kwenye kuimarishwa kwa barabara ya Nyakanazi- Kidawe ili kusudi mazao haya sasa yaweze kusafirishwa kwenda katika Mikoa ya Mwanza na kwingineko. Jambo hili litaweza kusaidia.

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho kabisa ni suala la ushuru wa mazao. Mnaserma mnatoza kati ya asilimia tatu mpaka tano (3% - 5%). Ningeomba mlete marekebisho ya sheria. Hili suala la kusema asilimia tatu mpaka tano, unatoka kwenye kijiji kimoja kwenda kingine labda ni kilomita tatu au mbili, unakuta kijiji X wanatoza asilimia tatu. Unakwenda katika kijiji kingine kinachofuata kuna kama kilomita tatu au moja, unakuta watu wanatozwa asilimia tano. Hii ni *contradiction*. Lazima watu hawatakubaliana na utaratibu huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, niombe muiangalie sheria yenu, hili suala kweli lina upungufu. Naomba mlete marekebisho ya sheria hii. Sheria iweke bayana kwamba, tozo zote zitakuwa ni asilimia tatu au kama ni asilimia tano, baada ya kufanya *economic analysis*, basi wote watozwe kama ni asilimia tano, iwe ni asilimia tano. Suala la asilimia tatu na tano na kuiruhusu Halmashauri ifikirie itatoza kiasi gani, hili jambo bado halijakaa sawasawa na ndiyo maana wananchi wanalalamika. Kwa hiyo, kwenye ushuru wa mazao hilo jambo halijakaa vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa muda bado kidogo, nizungumzie suala la Ushirika. Ningeomba Wizara ijaribu kuimulika Ofisi ya Ushirika ya Wilaya ya Kasulu kwani inawanyanyasa sana wakulima wa tumbaku. Wakulima wa tumbaku wananyanyasika kwa sababu kuna fedha ambazo hawajalipwa za toka mwaka 2010/2011 kitu kama hicho, au mwaka 2011/2012. Hawajalipwa fedha zao na suala hili tumelifikisha kwa Mheshimiwa Waziri. Naomba suala hili tuliangalie na baadaye atupatie majibu kwamba limefikia wapi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Joseph Machali. Sasa namwita Mheshimiwa Ritta Kabati atafuatiwa na Mheshimiwa Halima Mdee. Mheshimiwa Ritta Kabati!

**MHE. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa hii nafasi ili niweze kuchangia katika Wizara hii ya Kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nianze kwa kuungana na wale ambao wamesema kwamba Wizara hii imetengewa fedha kidogo sana ukilinganisha na umuhimu wa kilimo katika kujenga uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kwanza nianze kuwatendea haki wananchi wangu wa Iringa. Nianze na kilimo cha umwagiliaji. Kwanza niishukuru Serikali kwa kuongeza eneo la kilimo katika kilimo cha umwagiliaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nianze kwa kuiuliza Serikali kwamba, je, ni vigezo gani vinatumika katika kutenga fedha kwa ajili ya miradi hii ya umwagiliaji? Vile vile ni kwa nini kuna baadhi ya miradi mipya ambayo inatengewa fedha wakati miradi ya zamani bado haijakamilika? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nini nasema hivyo? Katika Halmashauri ya Manispaa ya Iringa, Jimbo la Iringa Mjini ipo miradi ya muda mrefu sana ambayo kila siku

tumekuwa tukiilalamikia kwamba ile fedha ambayo inatengewa inakuwa haifiki. Uko mradi mmoja katika Kata ya Kitwilu, Kitwilu *Irrigation*. Huu mradi umekuwa ni wa muda mrefu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakumbuka Mheshimiwa Waziri wa Kilimo alipokuwa Naibu Waziri, niliishawahi kwenda mpaka ofisini kwake na kumpelekea mpaka andiko la huo mradi, lakini mpaka leo hii huu mradi bado haujaletewa fedha. Huu mradi unahitaji kama shilingi milioni 521.

Mheshimiwa Naibu Spika, upo mradi mwingine katika Halmashauri hiyo, Mkoga *Irrigation* ambao uko katika Kata ya Isakalilo. Huu mradi pia umekuwa wa muda mrefu sana. Wananchi wa Iringa wamekuwa wakiulalamikia. Kumekuwepo na uhamasishaji mkubwa sana kwa wananchi kuweza kuchangia miradi hii. Halmashauri pia imekuwa ikitenga fedha muda mrefu sana katika hii miradi miwili ya Kitwilu na Mkoga, lakini mpaka leo hii Serikali haijaweza kuleta fedha kwa ajili ya kuikamilisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Serikali iwe inaangalia hii miradi, hata kama ipo katika Halmashauri za Mjini, lakini ijue miradi hii ingeweza kuwasaidia sana vijana wengi hasa pale Iringa Mjini ambako kuna vijana wengi sana hawana ajira. Kukamilika kwa miradi hii kungeweza kusaidia kuleta ajira kwa sababu wanaweza kujihusisha katika miradi midogo midogo kama vile kulima mboga, matunda na kilimo cha mazao mengine ambacho kingeweza kusaidia vijana wetu kutokwenda kwenye miji mikubwa ambako wanapata matatizo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lipo jambo lingine ambalo ningependa liangaliwe katika Mkoa wetu wa Iringa. Katika Mkoa wa Iringa kuna kinu cha kusaga *(National Milling)*. Kile kinu kimechukua muda mrefu sana, kilikuwa kimeleta ajira kubwa sana kwa wananchi wa Iringa. Kuhusiana na kinu kile watu wanasema kwamba, uchumi mnao mmeukalia. (*Makofi*)

**MBUNGE FULANI:** Kweli.

**MHE. RITTA E. KABATI:** Ule ni uchumi ambao ungeweza kusaidia wananchi wa Mkoa wa Iringa, hususan katika Manispaa ya Iringa Mjini. Kimekaa muda mrefu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ningependa wakati Mheshimiwa Waziri anajibu atwambie, je, ni lini sasa kile kinu nacho kitatengewa fedha ili kiweze kufanya kazi ile kwa sababu hata ukienda kukitembelea mitambo imeshaharibika na majengo yameshaharibika. Huu ni uharibifu mkubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Serikali leo hii inijibu na wananchi wa Iringa waweze kujua kwamba, pale Serikali ina mpango gani wa kuwasaidia wananchi wa Iringa kuhusu ajira. Kama Serikali imeshindwa kufanya kitu chochote pale, basi tutafute mwekezaji ili aweze kuinua uchumi wa Iringa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niendelee pia kuzungumzia suala la viwanda. Jana Mama Madabida aliongea vizuri sana kwamba, Serikali yetu ina viwanda vingi sana, lakini viwanda vile vinatumiwa tofauti. Wananchi wanaomba lakini hawatumii kama vile ambavyo maombi yao yalionesha.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile kipo Kiwanda kingine cha Chai. Tumehamasisha sana wananchi wa Iringa hasa Kilolo huko walime kilimo cha chai, lakini kuna Kiwanda cha Chai pale ambacho pia kimekuwa cha muda mrefu na Serikali bado haijasema kiwanda kile kinafanyiwa nini ili kiweze kuwasaidia wananchi wa Iringa.

Mheshimiwa Naibu Spika, niulizie pia kuhusu ile Sheria ya Ushirika ambayo nilisikia ingeletwa hapa Bungeni ili ifanyiwe marekebisho kwa lengo la kuweza kuwasaidia wananchi ili waweze kunufaika na huu ukulima. Sasa ili kilimo kifanikiwe, ipo haja hii sheria iletwe hapa Bungeni ili tuifanyie marekebisho na maboresho ili iweze kuwasaidia wakulima kuliko kuwa kila siku tunalalamika lakini hatua hazichukuliwi.

Sasa hawa wananchi wetu tunawapeleka wapi? Kama tunasema kilimo kitawanufaisha, kitawanufaisha vipi wakati hivi Vyama vingine haviwakomboi wananchi? Sana sana wanakuja wajanja wachache, wanakwenda pale wanaanza kuwatumia wananchi kwa ajili ya kunufaika wao wenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, labda pia niongezee kutoa ushauri kwamba Serikali ingejikita pia kwenye uvunaji wa maji kwa sababu haya maji kama tungeyavuna yangeweza kusaidia wakati ule wa kiangazi. Tumekuwa na mikoa mingi ambayo ina kawaida ya kuwa na mvua nyingi, lakini hatujajiwekea utaratibu wa kuhakikisha yale maji yanavunwa ili yaweze kusaidia wakati ambao hakuna mvua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile ningeomba kuishauri Serikali kwamba ingeweza kuchagua baadhi ya Mikoa kwani kuna baadhi ina rutuba na mvua nyingi sana. Kwa mfano Mikoa ya Iringa, Njombe, Rukwa na Mbeya, ingewekwa maalum kabisa isaidiwe kwa kupewa pembejeo za kilimo za kutosha, zana za kilimo zikopeshwe kwa wananchi ili hii mikoa iweze kusaidia ile mikoa ambayo ina njaa. Tusingeomba msaada kutoka nje kwani kupitia hii mikoa kwa kuwasaidia wakulima wake ingeweza ikasaidia wananchi wa mikoa mingine wakati wa kipindi cha njaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, labda nitoe ushauri mwingine kuhusiana na kilimo kwanza. Najua Serikali yetu ina nia nzuri sana ya kuendeleza kilimo kwanza, lakini katika nchi zingine wanaangalia mazao yatakayowasaidia, labda wanakuwa na mazao mawili; zao moja la chakula na lingine la biashara. Mazao haya yakapewa kipaumbele cha hali ya juu, yakasaidiwa, yakafanyiwa kila linalowezekana ili kuhakikisha yanazalishwa kwa kiwango kikubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumesema ndiyo kilimo kwanza kinaanzishwa, mazao yamefikia wapi? Kwa sababu sasa hivi tumesema Kilimo Kwanza, lakini hatujaainisha.

Tunalima mazao mengi, hatuyapi kipaumbele, lakini haya mazao kama tungesema kwamba hili zao sasa linaingia kwenye huu mfumo wa Kilimo Kwanza la kilimo na hili la Kilimo Kwanza la biashara, pengine ingeweza ikatusaidia zaidi na tungekuwa na mafanikio makubwa zaidi kwa hii kauli mbiu yetu ya Kilimo Kwanza.

Mheshimwa Naibu Spika, vilevile labda nizungumzie kuhusu Vyama vya Ushirika, hizi *SACCOS*. Hizi *SACCOS* kwa kweli ni mkombozi wa Mwafrika, ni mkombozi kwamba tunaondoa umaskini lakini kuna vitu vichache ambavyo vinahitaji maboresho. Kwa mfano, hizi SACCOS zina Mkaguzi wa Ndani na Nje.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MHE. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Ritta Kabati kwa kuwasilisha matatizo ya wananchi wa Mkoa wa Iringa. Sasa ni zamu ya Mheshimiwa Halima Mdee atafuatiwa na Mheshimiwa Prof. Peter Msolla, Mheshimiwa Halima Mdee!

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru na mimi kupata nafasi ya kuchangia Wizara ya Kilimo.

Mheshimwa Naibu Spika, lakini kwanza niungane na wote waliochangia kuonyesha ni kwa kiwango gani Serikali haiko makini ama kwa kiwango gani Serikali haina dhamira ya dhati kabisa kuhakikisha kwamba kilimo ambacho kinaajiri Watanzania wengi kinapatiwa suluhu. Wote ni mashahidi, taarifa za Kamati zimeonyesha kwamba fedha zinazotengwa kwa miradi ya maendeleo kwenye kilimo ni fedha ndogo sana. Ukiangalia kwa mwaka jana tu tumepitisha karibia shilingi bilioni 120 za maendeleo, lakini kwa kuonyesha kwamba Serikali haiko makini, Serikali haimaanishi ama haitembei kwenye maneno yake, fedha

za ndani zilikuwa shilingi bilioni 14 tu, fedha za nje zilikuwa ni shilingi bilioni 106. Matokeo yake ni nini? Matokeo yake mpaka tarehe 19 Machi, 2013, fedha ambazo zimetolewa kiujumla wake ni shilingi milioni 22.9 tu, asilimia 19 ya bajeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hapa tunapiga ngonjera kwamba tuna nia ya kumsaidia mkulima, lakini swali ni kwamba tunachokisema ndicho tunachokitembea?

Mheshimiwa Naibu Spika, tuliambiwa kilimo kitakua kwa asilimia 10 inapofika mwaka 2015. Tunavyozungumza, bajeti ya kilimo ilikuwa asilimia 3.6, imekuja asilimia 4.3 imerudi asilimia moja. Uwekezaji hakuna, tunaambiwa uwekezaji unaongezeka, lakini kwa tafiti ambazo zimefanywa, zinaonyesha fedha nyingi ambazo zinaongezeka, ni fedha za matumizi ya kawaida, fedha za maendeleo bado hakuna ongezeko ambalo lina tija.

Mheshimwa Naibu Spika, sasa mimi nadhani kipindi cha kupigana *fixfix* hapa kina wakati wake. Wakulima wa Tanzania wamechoka ngonjera. Serikali imekuja na mpango wa *SAGCOT*, tumeambiwa mwaka jana zilitengwa shilingi bilioni 16, zimetoka shilingi bilioni 1.7. Huo ndio tunaambiwa ni Mpango wa Kukuza Kilimo Ukanda wa Kusini.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini Kambi ya Upinzani imezungumza kitu kimoja muhimu na naamini Serikali itasikiliza kwamba katika Mpango huu wa *SAGCOT* kuna wadau mbalimbali, *private companies* 17 duniani. Kuna Serikali ya Marekani, kuna Serikali ya Vietnam, lakini kitu ambacho kinatisha ni wadau ama aina ya makampuni ambayo wameingia kama wabia kati ya makampuni 17.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi naamini Serikali mnasoma, siamini kama mnaendesha Serikali halafu hamjui kinachoendelea duniani. Hakuna mtu ambaye hafahamu kampuni kubwa ya kuzalisha mbegu ya Monsanto, ni kampuni ya Kimarekani. Kwenye Mkutano wa mwaka jana wa *G8 Summit,* Kampuni hii inaji-*commit dollar billion* 50 kwa ajili ya kusaidia kufufua kilimo Afrika kwa kutumia hizi mbegu zinazotengenezwa kwenye maabara. Kwa hiyo, nina-*imagine*

Tanzania katika hizo *dollar* bilioni 50 ambazo tuna uwezo wa kuzitengeneza wenyewe kwanza tutapata mgao wa kiasi gani? Mbaya zaidi Kampuni inayokuja Tanzania leo, tunaipokea kwa mikono miwili, inapigwa vita duniani kote kwa sababu inawafanya wakulima wadogowadogo wawe wategemezi wa mbegu za kampuni za Kibeberu. *(Makofi)*

Mheshimwa Naibu Spika, ukienda India leo huyu Monsanto yupo India tokea mwaka 1949. Ukienda India leo Monsanto anafukuzwa kwa sababu amewafukarisha wakulima wadogowadogo wa India wanaoitwa *untouchables* ambao kwa Watanzania ndiyo hao wanaoenda kuathirika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukisoma *SAGCOT* kwa kina, *SAGCOT* inamwangalia kwanza mkulima mkubwa, halafu mkulima mdogo anawekwa pembezoni asaidiwe na huyu mkulima mkubwa. *(Makofi)*

Mheshimwa Naibu Spika, India wamewafukuzwa kwa sababu kwanza mbegu zao zinamfanya mkulima awe tegemezi, *the moment* ile mbegu inapandwa pale, mkulima hana haki ya kuirudia ile mbegu katika kilimo kijacho. Mkulima huyu pamoja na mambo mengine, anatakiwa alipe *royalty* kwenye hizi mbegu. Monsanto amepigwa vita katika nchi nane za Ulaya, Ufaransa ikiwa mojawapo na Ufaransa inasema kabisa kwamba huyu mtu mbegu zake zinasababisha sumu ambayo inafanya watoto wanaozaliwa wanakuwa mataahira, mbegu za Monsanto. Ukienda Argentina, Monsanto amepigwa vita, wala hatuhitaji kutumia nguvu nyingi unatakiwa u-*google*, andika Monsanto, utaona vielelezo kwenye *YouTube*, sasa *YouTube* msitumie kuwakamata akina Lwakatare, tumieni *YouTube* kujifundisha tunawasaidiaje wakulima wetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ukienda Peru, Monsanto amefukuzwa kwa sababu mbegu za viini tete anazozizalisha hazisaidii ardhi, hazisaidii mkulima, wanakuja na maneno matamu matamu lakini wanatuingiza karibuni. Leo tunaambiwa, wameshaanza kutumia hizi mbegu zake

kwenye zao la pamba. Tunasikia wakulima wetu wa pamba wanalia, lakini nina hakika kilio kinakuja zaidi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Baraza la Mawaziri ndiyo Washauri wa Rais, inawezekana Rais akaingizwa choo cha kike na hawa mabeberu nyie ndiyo wa kumsaidia! Anadanganywa kwa ahadi tamutamu, lakini kama India ilishindikana, kama Europe wamemkataa mwenzio, kama wakulima wa Marekani wanamkataa Mmerekani mwenzao, Tanzania kwa nini tunafungua milango? Tuna nia gani ya kuwasaidia hao wananchi wetu?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, mimi nilikuwa naiomba Serikali, hawa mabeberu wana mfumo wa kuingia kwenye *system* kwa kutumia rushwa, kwa kutumia *influence* kubwa ya fedha walizonazo, wana-*manipulate* viongozi ambao wapo madarakani. Siku moja nilisema, nyie wengi wenu hapa mko *above fifty* yaani mchoka, mnanielewa? Sasa msituharibie kizazi hiki. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimwa Naibu Spika, mnasema miradi ya wakulima, miradi ya vijana, nashukuru rafiki yangu Mheshimiwa Ester aliibua hili suala la vijana la kilimo lakini ukiangalia miradi ambayo imeelezwa hapa haishikiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo Mkuu wa Wilaya anasema kwamba jamani eti wale wawekezaji ambao wana maeneo yetu, ambao hawajayaendeleza tukawaombe, hivi Serikali unaenda kumwomba Mzungu ardhi kwenye eneo lako? Hii mikataba ya ardhi mnayoingia na hawa wawekezaji ni ya aina gani? Huu usiri huu umeghubikwa kiasi kwamba ardhi yetu inachukuliwa na wageni? Tukifika mwaka 2050, Watanzania tutakuwa milioni 150, tunaanza kuzalisha ma-*settlers* ndani ya Tanzania ninawaambia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Hoja yangu Binafsi ya Ardhi nilisema maeneo yote *strategic* mnawapa wageni, halafu mnasema mnawasaidia wakulima wadogowadogo, mgeni ana hekta 10,000, mkulima mdogo ana ekari moja umemwondolea umaskini au umemzidishia umaskini? Hekta

hizi 10,000 ndiyo wawekezaji hao wakubwa wa kigeni wanakuja na mbegu za sumu, mbegu zinasambaa kwa wakulima wadogowadogo. Kwa hiyo, badala ya Serikali kutuletea mipango ambayo haina kichwa wala miguu, watwambie kwenye Wilaya wamegawaje mashamba, wanawake wana kiasi gani, vijana wana kiasi gani, watwambie Wilaya fulani ina kitu fulani kinachoshikika.

*(Hapa kengele ililia kuashiri kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa...

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Siyo mnatutolea mifano mifano ya heka 100 na heka 10 hapa.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa...

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Naibu Spika, naamini ujumbe umefika. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Halima Mdee, kwa niaba ya Wabunge ambao wapo *above fifty,* nilihakikishie Bunge hili, taarifa nilizonazo ni kwamba wapo ngangari kabisa. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Kangi kwa kifupi sana.

## MWONGOZO WA SPIKA

**MHE. ALPHAXARD K.N. LUGOLA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Mwongozo wako. Bunge hili ni Bunge la Bajeti inayowahusu Watanzania na leo tunajadili bajeti ya Wizara muhimu, Wizara ya Kilimo ambayo ndiyo mwajiri mkuu wa Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini naomba Mwongozo wako, tunapokuwa tunaendelea na majadiliano ya Wizara hii ambayo ina masuala mengine mtambuka, ninaona Mawaziri wapo watano tu kwenye Bunge lako Tukufu na

Manaibu Mawaziri wapo tano tu kwenye Bunge lako Tukufu. *(Makofi)*

Sasa naomba Mwongozo wako, katika mazingira ya namna hii, tunapeleka *message* gani kwa Watanzania juu ya bajeti yao muhimu ya mwajiri mkuu, Wizara ya Kilimo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nilikuwa naomba Mwongozo wako kama kweli ni sahihi kuendelea kujadili bajeti muhimu kama hii tukiwa na Mawaziri watano tu na tukiwa na Manaibu Waziri watano tu. Naomba Mwongozo wako.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Lugola, nitautoa Mwongozo baadaye.

Namwita Mheshimiwa Profesa Peter Msolla atafuatiwa na Mheshimiwa Magdalena Sakaya. Mheshimiwa Profesa!

**MHE. PROF. PETER M. MSOLLA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuchangia kwenye bajeti hii ya Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika.

Mheshimwa Naibu Spika, nianze kwa kutamka kwamba mimi naunga mkono hoja iliyopo mbele yetu kwa sababu usipounga mkono unakwenda wapi? Kazi yetu sisi kama Wabunge ni kuishauri Serikali na kuisimamia lakini siyo kazi yetu kupinga tu, ukiishauri Serikali ni sikivu na watafanya yale yanayotakiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuchangia kwangu, kwanza, nianze kuzungumzia juu ya kilimo cha chai. Chai inalimwa na Mikoa mingi na chai ina faida kubwa mbili. Moja, bei yake hapa duniani, ni moja ya zao la biashara ambayo bei yake imebakia inatabirika wakati wote na haishuki ovyo. Kwa hiyo, anayelima chai anakuwa na uhakika wa kupata faida. Pili, ndiyo zao pekee ambalo mkulima anapata zao kila wakati, siyo zao la msimu. Ni zao ambalo

ukishapanda ukishaanza kuvuna, ni kwamba wakati wote wewe utaendelea kuvuna kwa miaka na miaka hata vijukuu watakuja kuvuna. Mazao mengine utalima kwa msimu, utavuna utapumzika. Kwa hiyo, ukiwa mkulima wa chai, ni sawa na mtu aliyeajiriwa ofisini kwamba kila mwisho mwa mwezi wewe unawaza kupata fedha zako.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini katika nchi yetu, wakulima wa chai wapo wengi wakubwa lakini wapo na wadogo wadogo. Kwa bahati mbaya sana, Bodi ya Chai hapa nchini imeweka msimamo wa kuwasimamia zaidi wakulima wakubwa na kusahau wakulima wadogo wadogo ambao ni wengi.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuishukuru Serikali kupitia Wizara hii ya Kilimo, Chakula na Ushirika kwa kuanzisha Wakala wa Chai wa Wakulima wadogowadogo wa chai ambao kwa kweli wamekuwa wakisaidia sana wakulima wadogo. Bahati mbaya sana huu Wakala hauna bajeti ya kutosha na hususani bajeti ya maendeleo ili kusudi waweze kufikia sehemu mbalimbali wawasaidie wakulima ili kusudi sekta hii iweze kukua.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la pili, ni ukosefu wa viwanda kwa ajili ya wakulima wadogowadogo. Hivyo basi, wakulima hawa wadogowadogo wa chai hawapo katika ule mnyororo wa thamani, wao mara nyingi wanalima halafu wanamuuzia mkulima mkubwa, wao wanakuwa kama ni manamba wanalipwa ile *farm gate price* ambayo ni kidogo sana. Hapa nchini kwa sasa hivi tuna viwanda vya wakulima wadogo wadogo kama vitatu tu navyo ni kwa ubia lakini wenzetu wa Kenya wana viwanda 65 vya namna hiyo ambavyo vinaendeshwa na Wakenya wenyewe na wanahusika katika mlolongo nzima wa mnyororo wa thamani na mapato yao ni mazuri sana kwa sababu wao wanahusika katika uzalishaji, usindikaji na vilevile kupeleka sokoni. Jambo hili lingefaa sana kwetu sisi Watanzania kuanzisha utaratibu wa namna hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, maeneo mengi yanafaa

kwa kilimo cha chai lakini nizungumzie Wilaya ya Kilolo. Wilaya ya Kilolo ina eneo kubwa takriban hekta 20,000 ambazo zinafaa kwa kilimo cha chai. Kwenye miaka ya 1980 kilijengwa kiwanda ambacho kwa bahati mbaya hakikufanya kazi na watu walihamasika sana, wakalima chai lakini baada ya pale walikataa tamaa na ndiyo zao pekee la biashara. Tulipata bahati ya kutembelewa na Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 8 Agosti, 2008 takribani miaka mitano iliyopita, alipotembelea yale mashamba pamoja na kiwanda cha zamani alisema kiwanda hicho kifufuliwe au kijengwe kipya. Juhudi za wananchi kule zimeendelea na sasa hivi kuna miche mingi na mashamba mengi yamefunguliwa lakini kwa bahati mbaya juhudi za kupata kiwanda mpaka sasa zimekuwa zinakwenda polepole sana. Ningeomba sana Wizara ione namna gani itashirikiana na wananchi wa Kilolo ili kuboresha hali hii. Pengine ningerudia kwa kusema kwamba hili ni eneo la *SAGCOT* vilevile. Kwa hiyo, ushirikiano na huu mradi SAGCOT katika zao hili ungeweza kutusaidia sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo linguine napenda kuzungumzia juu ya Sheria ya Manunuzi ya mwaka 2004. Sheria hii napendekeza ingeangaliwa upya kwa sababu kwanza, imepitwa na wakati, pili inachelewesha sana utekelezaji wake. Katika ile *tendering process* pekee yake inaweza kuchukua mwaka mzima lakini vilevile ni gharama kwamba wewe unayekwenda moja kwa moja dukani kupata huduma na ukizingatia kwamba asilimia 70 ya bajeti ya Serikali inakwenda kwenye Halmashauri na asilimia 30 kwenye Serikali Kuu, ile *process* ya ku- *tender* na mpaka upate huduma inachukua muda mrefu sana. Vilevile ni gharama, kwa mfano, yule mtu ambaye anataka kuchimba kisima cha maji moja kwa moja akampa mtu wa kuweza kuchimbia kisima, sana gharama yake ni shilingi milioni 40 lakini kupitia kwenye *tender* kisima hicho hicho utalipa shilingi milioni 400. Fedha nyingi zinatumika katika manunuzi ya huduma, vifaa na kadhalika. Angalia Wizara zote, Halmashauri zote, gharama yake ni kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimwa Naibu Spika, kuna kitengo kinaitwa TEMESA cha kutengeneza magari, ukienda na gari lako kwa

mtu binafsi, ile ya kwenye tenda gharama zake ni karibu mara nne. Ukisafiri wewe kama kiongozi wa Serikali unatoka hapa kwenda London, umepanda *business class,* wewe unayelipiwa na Serikali inakuwa Dola 8,000, lakini umesafiri na mke wako mmekaa kiti kimoja hicho hicho, yeye huyu unamlipia wewe Dola 2,000. Sasa Serikali inapoteza fedha nyingi sana katika utaratibu wa namna hii. Nashauri sheria hii iangaliwe upya ili tuweze kuokoa fedha nyingi na mambo mengi yangeweza kutekelezwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie juu ya kilimo cha umwagiliaji. Nilichangia hili wakati nachangia kwenye hotuba ya Waziri Mkuu, nikaeleza fursa zilizopo na eneo linalomwagiliwa, lakini kusema kweli bajeti kwa ajili ya eneo hili bado ni ndogo sana na maeneo mengi yanayofaa kwa umwagiliaji hayajafikiwa. Nitoe mfano tu wa Jimbo la Kilolo. Kata ya Mahenge kuna mradi unaitwa Mgambalenga katika mto Lukosi, Serikali ilikwishaahidi kujenga banio ili kuongeza eneo la umwaliaji la hekta 1,000 lakini mpaka leo hakuna kitu ambacho kimefanyika. Ukienda sehemu ya Nyanzwa ambako wanalima sana vitunguu na mbogamboga...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MHE. PROF. PETER M. MSOLLA:** ...nako liliahidiwa bwawa lakini bwawa hili mpaka leo halijawahi kujengwa. Ningeomba Serikali ione umuhimu wa kuangalia maeneo haya ambayo yangeweza kutusaidia sana. *(Makofi)*

Mheshimwa Naibu Spika, naona watu wengi hapa wanazungumza juu ya upungufu wa chakula katika maeneo mbalimbali...

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Profesa Msolla...

**MHE. PROF. PETER M. MSOLLA:** Mheshimwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Sasa ni zamu ya Mheshimiwa Magdalena Sakaya atafuatiwa na Mheshimiwa Ester Bulaya.

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kuweza kunipa fursa hii ili niweze kuchangia kidogo kwenye bajeti ya Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika.

Mheshimwa Naibu Spika, leo ni miaka mitano tangu Sera ya Kilimo Kwanza izinduliwe na Mheshimiwa Rais mwaka 2009. Miaka mitano ni muda wa kutosha kabisa kufanya tathmini ya mpango, utaratibu au mfumo wowote ambao unaanzishwa. Kwanza, tunapenda Serikali ituletee tathmini kwa muda wa miaka mitano tangu Sera ya Kilimo Kwanza imeanzishwa, ni mafanikio kiasi gani yamepatikana, tunachechemea, tunakimbia, tunatembea au tumekwama?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa bahati nzuri nilikuwepo kwenye uzinduzi ule na Mheshimiwa Rais alisema malengo ya kwanza ya Kilimo Kwanza tunataka tuhame kwenye kilimo kinachotegemea mvua twende kwenye kilimo cha umwagiliaji kutokana na mabadiliko ya hali ya hewa. Leo ndani ya miaka mitano najiuliza, Sera ya Umwagiliaji ni kwa kiasi gani miundombinu ya umwagiliaji imetengenezwa ndani ya nchi nzima. *(Makofi)*

Mheshimwa Naibu Spika, suala la umwagiliaji bado ni tatizo kubwa hata robo kwenye suala la kilimo hatujaweza kuingia kwenye suala la umwagiliaji. Hatuwezi kuwa na kilimo chenye tija kama hatuwezi ku-*invest* kwenye miundombinu ya umwagiliaji. Ukiangalia miradi mingi ya umwagiliaji inatengewa fedha za nje ambazo hazina uhakika, ukiangalia fedha ya ndani inayotoka kwenye miradi ya kilimo kwenye masuala ya umwagiliaji ni kidogo sana, *just a peanut* ambayo haiwezi hata kutekeleza hiyo miradi. Kwa hiyo, kama hatuwezi kutenga fedha ya kutosha ni tatizo kubwa litakuja kutukwamisha kwenye suala zima la kilimo.

Mheshimwa Naibu Spika, yapo mabwawa yamejengwa, yana miaka zaidi ya 10. Kuna bwawa la Kiloleni,

Wilaya ya Urambo lina zaidi ya miaka 10 halijakamilika. Naiomba Serikali ikakamilishe lile bwawa pale Kiloleni kwa Mheshimiwa Waziri wa Ushirikiano wa Afrika ya Mashariki ili wananchi waweze kulima kilimo cha mbogamboga vijana waondokane na umaskini.

Mheshimiwa Naibu Spika, fedha inayotoka kwenye vyuo vya utafiti ni kidogo sana, hatuwezi kuwa na kilimo cha kisasa kama hatuna utafiti. Mwaka jana nilizungumza kwenye Bunge hili, kuna vituo muhimu kwa kweli tena nika-*specify* kwenye Kituo cha Utafiti wa Miwa Kibaha. Kile kituo kinafanya utafiti wa kudhibiti magonjwa kwa njia ya kibiolojia na nikaeleza changamoto zake, matatizo yanayokibali kile Kituo na kinahitaji msaada wa Serikali. Cha kusikitisha hakikutengewa hata shilingi, hata *OC* ndani ya mwaka mzima wa bajeti ya mwaka 2011/2012. *(Makofi)*

Mheshimwa Naibu Spika, Kituo kile pamoja na kazi nzuri ambayo inatakiwa kifanye, kinaishi au kinajiendesha kutegemea fedha kidogo kutoka kwenye Bodi ya Sukari pamoja na wadau mbalimbali wa sukari. Hivi kweli Kituo muhimu kama kile, kinaendeshwa kwa kutegemea Bodi ya Sukari, Serikali haitengi hata *OC*. Naomba sana Kituo hiki kiangaliwe kwa jicho la pekee.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kituo kile hakina hata bustani yoyote hata ya mfano kwa ajili ya suala la umwagiliaji kuonyesha nini kinafanyika. Kuna bwawa zuri pale ambalo lina maji ya kutosha, wamekosa tu pampu ya kuwasaidia waweze kupampu maji kwa ajili ya masuala ya umwagiliaji. Walikuwa na jenereta pale imeibiwa, wamefuatilia *TANESCO* wamewaambia walipe shilingi milioni 40 waweze kupata jenereta nyingine na Kituo kile hakina hata shilingi. Naiomba Serikali itenge fedha mwaka huu inunuliwe hiyo jenereta kwa shilingi milioni 40 ili kile Kituo muhimu kiweze angalau kuwa na bustani za kuonyesha mifano kwa sababu wanafunzi wanafika pale, sisi tumefika pale Kamati ya Bunge hata bustani ya mfano hamna. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la mbegu. Hatuwezi kulima vizuri na tukazalisha kama hatuna mbegu bora. Kiasi cha mbegu kinachozalishwa ndani ya nchi yetu ni kidogo sana hata robo ya mahitaji hakifiki. Nitatoa takwimu. Mahitaji ya mbegu kitaifa Tanzania ni tani 120,000 kwa mwaka, mbegu za aina mbalimbali. Mbegu zinazopatikana ndani ya nchi, zinazozalishwa ndani na zile ambazo tuna-*import* kutoka nje ni tani 40,000. Mbegu zinazozalishwa hapa ndani peke yake, zinazozalishwa na Wakala wa Mbegu (ASA) pamoja na Kampuni ya binafsi, ni tani 18,000. Mbegu zinazozalishwa na ASA peke yake, Wakala pekee wa Mbegu Tanzania ni tani 6,000 tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunategemea asilimia zaidi ya 70 na zaidi kutoka nchi za nje. Tunajua matatizo ya kutegemea mbegu za nje, kwanza zinakuja na magonjwa *first of all* lakini la pili ni kwamba ni *very expensive,* wananchi wengi wanashindwa kumudu mbegu za nje kwa sababu ya ugali wake. Pia magonjwa mengi ya mazao yetu yanatoka nje kutokana na mbegu hizi tunazoagiza.

Mheshimwa Naibu Spika, naiomba sana Serikali iwekeze kwenye Wakala wa Mbegu (ASA, awezeshwe, azalishe mbegu za kutosha. Pili tunaomba *ASA* apewe mamlaka ya kufanya utafiti wa mbegu kwa sababu sasa hivi mafungu yote ya utafiti yanakwenda *COSTECH*. Tunaomba lile fungu la utafiti wa mbegu litoke *COSTECH* liende Wakala wa Mbegu ASA. Hii itasaidia Wakala huu kuweza kulima vya kutosha lakini pia kufanya utafiti na kutoa mbegu za kutosha lakini pia mbegu bora kwa ajili ya kilimo cha Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ushirika ndio njia pekee ya kuwakomboa wakulima wadogowadogo wa Tanzania. Vyama vya Ushirika vingi vimekufa kwa sababu ya viongozi wenye ubinafsi, waliokosa uzalendo, wenye uchu wa madaraka, wanaopenda kujilimbikizia mali. Ninasikitika sana na cha kusikitisha zaidi, watendaji wa Mabenki wanashirikiana na viongozi wa Vyama vya Ushirika, wanachukua mikopo mikubwa kwa majina ya Vyama vya

Ushirika, ile mikopo wanachama hawaijui. Matokeo yake, wanachama wanabambikwa madeni ambayo hawayajui. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, leo mwanachama analima mazao yake, analimia madeni ambayo hakunufaika hata na shilingi. Naiomba Serikali iseme leo hapa, Mabenki ambayo yameshirikiana na viongozi wa Vyama vya Ushirika, wakachukua mikopo mikubwa benki, wakanufaika wao wenyewe, leo madeni yale yamepelekwa kwenye Vyama vya Msingi, wakulima wamekatwa isivyostahili, wamebebeshwa madeni wasiyostahili, nini hatma ya benki hizi leo? Naomba Mheshimiwa Waziri akija kujibu aeleze ni nini hatma ya mikopo ambayo wamebambikwa wananchi ambayo haiwahusu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunafahamu kwamba zao la tumbaku kwa kiasi kikubwa linaingiza pato la taifa na lazima Serikali ikiri kwa hilo na kila mmoja anajua. Naomba Serikali iniambie leo, ni kwa nini wamekubali kwa miaka yote tumbaku inayolimwa ndani ya ardhi ya Tanzania, inanunuliwa kwa bei ya dola. Huwezi kutoka leo Tanzania ukaenda Marekani ukanunua hata peremende kwa hela ya Tanzania, kwanza hawaitambui. Tulikubali vipi mali yetu ndani ya nchi yetu inunuliwe kwa fedha ya dola. Dola imekuwa inamkandamiza mkulima siku zote, anauziwa pembejeo kwa kutumia dola, anauziwa mpaka kamba za kufunga tumbaku kwa kutumia dola, anauziwa mpaka gunia kwa kutumia dola, kila kitu anauziwa kwa kutumia dola wakati wa kupewa fedha, anapewa kwa kutumia Shilingi ya Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimwa Naibu Spika, tunafahamu uwezo wa wananchi wetu, kwa nini Serikali isipige marufuku, kwa nini Serikali inakubali wananchi wake wananyonywa na yenyewe inaona? Naiomba Serikali itujibu hapa ni kwa nini kwa miaka yote Makampuni ya kununua tumbaku yanatumia dola wakati huo wakijua kwamba dola sio fedha ya ndani ya nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi wakulima wengi wa tumbaku wanajiandaa kwa ajili ya msimu wa kuuza, wanasubiri masoko. Naiomba Serikali iwe makini mahali hapa, tunataka bei ya tumbaku iliyotamkwa iendelee kupanda na sio kushuka. *(Makofi)*

Mheshimwa Naibu Spika, bei ya tumbaku walipandisha *Grade One L10F* ikawa *US Dollar* 3.299 ya mwisho ni 0.388 lakini ukiangalia wakulima wengi wanauza madaraja ya kati hata tumbaku ingekuwa nzuri kiasi gani hakuna ambaye anaweza kupata hiyo *Dollar* 3.299, wengi wanauza *Dollar* 2.5, 2.6, 1.8 na hapo hajaingia *classifier,* kama hujamhonga *classifier* bado utauza mpaka 0.8, 0.7 na chini ya hapo. Naomba sana, wakulima wa tumbaku wanategemea sana Serikali kwa ajili ya kusaidia masoko yao.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kengele ya pili au ya kwanza?

**NAIBU SPIKA:** Ya pili. Ahsante sana Mheshimiwa Magdalena Sakaya, kabla sijamwita Mheshimiwa Ester Bulaya, nipitie tu kidogo Mwongozo alioutaka Mheshimiwa Alphaxard Kangi Lugola, nimhakikishie kwamba Waheshimiwa Mawaziri na Manaibu Mawaziri wapo, wengi wao wapo hapa Dodoma na tuelewe kwamba kila mmoja anajitahidi kuweka mambo yake sawasawa ili hivi karibuni wanapokuja mbele yetu hapa basi waje kikamilifu. Kwa hiyo, tujue kabisa kwamba wapo na wanafuatilia kwa ukaribu sana shughuli zinazoendelea. *(Makofi)*

Kwa hatua hii ni-*share* na ninyi kidogo uzoefu ambao unaendelea katika nchi jirani ya Kenya na mabadiliko ambayo yanatokea, sidhani kama kila mmoja anaelewa mabadiliko ambayo yanaendelea kule, wana Mabunge mawili sasa. Bunge la *Senate* na Bunge la Kawaida kama la kwetu. Katika moja ya mabadiliko makubwa ni kwamba katika Bunge lile kama la kwetu hilo la majirani, hakuna

Mawaziri ndani ya ukumbi wa Bunge. Mawaziri sio Wabunge, watakaoteuliwa kuwa Mawaziri watatoka nje ya Bunge na Mawaziri hao wataishia kwenye Kamati, hawatakanyaga kwenye Bunge. Mbona mnanyamaza sana, mnashangaa inakuwaje. *(Makofi/Kicheko)*

Kwa hiyo, katika Bunge jipya la Kenya hakuna kipindi cha maswali, kipindi cha maswali hakipo kwa sababu Mawaziri hawawezi kuja kujibu maswali Bungeni, maswali yote yanaishia kwenye Kamati. Sisi tuna Kiongozi wa Shughuli za Serikali Bungeni ambaye ni Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa Bunge lao wao wana *Majority Leader* ambaye anakuwa ni Mbunge wa kawaida. Upande wa Kiongozi wa Upinzani Bungeni kwa jina la kwetu hapa, wao kule ni *Minority Leader*. *(Makofi/Kicheko)*

Tuendelee na uchangiaji. Mheshimiwa Ester Bulaya atafuatiwa na Mheshimiwa Murtaza Mangungu na Mheshimiwa Shibuda ajiandae.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi.

Mheshimwa Naibu Spika, kabla sijajikita katika masuala ya vijana na kilimo, napenda Mheshimiwa Waziri akijibu awaeleze wakulima wa Mkoa wa Mara, mama zangu na baba zangu, wanataka kujua *status* ya viwanda vyao vile ambavyo vilikuwa chini ya *Mara Cooperative Union* vikoje kwa sababu vilichukuliwa na Serikali kama mufilisi na huu ni mwaka wa 18 hawajui *status* ikoje. Baba wa Taifa alisema enzi ya uhai wake waliovifilisi mnawajua, kwa nini msifilisi mali zao na matokeo yake mnafanya wakulima hivi viwanda ambavyo vilikuwa vinawasaidia hata katika kwenda kupata mikopo benki, sasa hivi hali yao hohehahe. Kwa hiyo, wakulima wa mkoa wa Mara wanataka kujua hilo. *(Makofi)*

Mheshimwa Naibu Spika, wanalima katika mazingira magumu kama ambavyo Wabunge wengine hapa wameendelea kusema masuala ya pembejeo

hayawanufaishi, vocha hewa, mawakala hawatimizi wajibu wao, Mheshimiwa Keissy hapa alipendekeza na mimi namuunga mkono. Kwa hiyo, wakulima wa Mkoa wa Mara wamekuwa wakilima kwenye wakati mgumu na ukizingatia wana bonde kule la Mto Mara, matokeo yake tu wanapata mafuriko baada ya Serikali kutumia kulima katika kilimo cha umwagiliaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia miaka miwili mfululizo nilizungumza katika Bunge lako Tukufu kwamba baada ya vijana kushindwa kunufaika kwenye sekta ya madini, sasa ni zamu yao kunufaika na ardhi yao kupitia sekta ya kilimo. Nashukuru Mheshimiwa Waziri ameliona hilo na wanasema mnyonge mnyongeni, haki yake mpeni, mimi nashukuru kwa kuliona, kuweka tu kwenye hotuba ni kwamba mnatambua changamoto za ajira kwa vijana na sasa mmeamua kuwasaidia vijana kujiajiri wenyewe kupitia sekta ya kilimo lakini kwa idadi hii, Mheshimiwa Waziri bado ni ndogo sana ukilinganisha na mamilioni ya vijana ambao wanahangaika kwa kukosa tu ajira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, matatizo ya ajira kwa vijana yanafahamika. Nilikuwa napitia takwimu mbalimbali ambazo nataka nichangie hapa inaonyesha kwa Mkoa wa Dar es Salaam peke yake ni asilimia 36, kwenye hii Mikoa mingine asilimia 15, vijijini ni asilimia saba. Sasa sio kwamba vijijini asilimia saba hakuna tatizo la ajira hapana, kule vijana wengi wamekimbia jembe la mkono ndio wako huku Dar es Salaam wako na kwenye hii Mikoa mingine wanakuwa Wamachinga lakini hata hao wengine waliokuwa kule ambao wanalima mashamba yale sio yao, ni ya wazazi wao. Wengine wamekuwa wakijishughulisha kilimo cha kuganga njaa tu. Wengine tunapokuja huku Dodoma na kurudi Dar es Salaam tunaona wale ambao wako Gairo kule wanauza viazi, nyanya, wako kule Mikese, yale mashamba sio yao, ni ya wazazi wao. Sasa Mheshimiwa Waziri ni vyema mkaweka mikakati ya kuhakikisha mnawawezesha hawa vijana badala ya kukimbilia mijini, badala ya kukimbia jembe la mkono, wanabaki kule na wanakuwa na ardhi yao na mnawawekea mfumo mzuri ambapo wanaweza wakapata vifaa vya kilimo

na pembejeo kwa ajili ya kuweza kujiajiri wenyewe na badala yake kuacha kukimbilia mijini, kuacha kukimbilia kwenye *centre* na wabaki kulekule vijijini na wasiishie kilimo cha kuganga njaa bali kilimo kiwawezeshe kujenga nyumba bora, kilimo kiwawezeshe kumudu milo mitatu kwa siku na kilimo kiwawezeshe kuwatajirisha kama ambavyo hata Azimio la Vijana linasema na ambalo tumepitisha kwenye Bunge lako Tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi vijana wameamka, mbali ya mifano ambayo ameitoa Mheshimiwa Waziri maeneo mengine pia na yenyewe yameiga na nilikufuata nikakwambia hata kule Bunda kwenye Jimbo la kaka yangu Alphaxard Kangi Lugola kijiji cha Kalukekere vijana ambao ni *graduate* tayari wameshaji-*organise* lakini wanakosa *support* ya Serikali. Mimi mwenyewe nilifanya ziara kabla sijaenda jeshini, nimeenda kutembelea yale mashamba. Hata ukiangalia kapampu walichonacho ni kidogo na wanafanya kilimo cha umwagiliaji, wanachukua maji kutoka kwenye ziwa. Sasa Mheshimiwa Waziri naomba na hawa vijana uwaangalie wa Mkoa wa Mara, Wilaya ya Bunda ambao wameshaanza na Mikoa mingine ambayo haipo katika mfano ambao umeweka hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania ina hekta 29,000,000 zinazofaa kwa kilimo cha umwagiliaji lakini hizi hekta zimejigawa, hekta milioni mbili ni zile ambazo piga ua, una uhakika wa kupata asilimia mia moja utakapo-*invest* kwenye kilimo cha umwagiliaji. Hekta milioni nne unaweza ukapata asilimia 70 mpaka 80. Hekta milioni 23 ni bahati nasibu, *either* upate au usipate. Sasa huku ndiyo wamekuwa wakisukumiziwa wakulima wetu, lakini haya maeneo nyeti wamekuwa wakipewa wawekezaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa leo tumeamua kuwawezesha vijana kujihusisha na kilimo. Mimi nakuomba Mheshimiwa Waziri, naomba kuwe na mgao sawa kwenye hizi hekta. Zile ambazo una uhakika wa kupata mazao na vijana wapate, si kwa wawekezaji peke yake wala kwa wakulima wakubwa peke yake, vijana wameamka na

wameamua kweli ku-*invest* kwenye kilimo. Naomba msiwa-*discourage*, naomba Serikali muwe *serious* muwawezeshe hawa vijana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, leo hii tunazungumzia kuagiza chakula nje, leo hii tunalamika bei ya vyakula kupanda siku hadi siku wakati tuna kambi za Jeshi la Kujenga Taifa kumi na tano. Serikali ina uwezo wa kuwezesha hizi kambi zetu ambazo wana nguvu kazi, vijana wanaoenda kwa mujibu wa sheria na wengine wanaenda kwa kujitolea, mwisho wa siku hawa vijana wanaenda mtaani hawana ajira, kwa nini Serikali isitumie rasilimali watu ambayo wako kwenye majeshi yetu haya ikawawezesha na wana uwezo wa kulisha taifa hili na wakauza nje ya nchi badala ya kuagiza sisi tukawa tunawauzia wenzetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nadhani kuna haja ya kuangalia kwa karibu hizi kambi zetu za Jeshi zina uwezo kabisa wa kutosheleza chakula na ikasaidia mfumko wa bei kuliko kuendelea kama Taifa kuagiza vyakula nje wakati kuna nchi nyingine zinatumia vyombo vyao vya ulinzi katika sekta ya kilimo kuondoa kabisa tatizo la katika nchi yao. Mheshimiwa Waziri ninaomba pia na hili mliangalie kwa sababu vijana wanaoingia kule ni wengi lakini si vyombo vyote vya ulinzi vina uwezo wa kuajiri, wanafundishwa mambo mbalimbali, kama kilimo. Sasa tukiliwezesha JKT lakini hata huko wanakorudi mitaani waandaliwe mazingira mazuri ya kwenda kujiajiri wenyewe na kujishughulisha na masuala ya kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nashukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi kwa mara ya kwanza kwa ajili ya *issue* yangu ya vijana, Mheshimiwa Waziri naunga mkono lakini naomba majibu sahihi lakini pia kama nilivyokwambia wazee wangu wa Mkoa wa Mara wanataka kujua *status* ya hivyo viwanda vyao vikoje kwa sababu miaka mingi imeenda lakini hawaoni kama kuna uwekezaji ambao unaweza ukawasaidia wakulima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Bulaya, sasa ni zamu ya Mheshimiwa Murtaza Mangungu atafuatiwa na Mheshimiwa Shibuda na Mheshimiwa Zainab Vullu.

**MHE. MURTAZA A. MANGUNGU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia katika hotuba ya bajeti ya Wizara hii ambayo imebeba naweza kusema sio uti wa mgongo tu pamoja na kichwa cha nchi yetu.

Mheshimwa Naibu Spika, nimeipitia bajeti iliyowasilishwa mbele yetu hapa lakini kwa masikitiko makubwa katika hotuba hii, ukurasa wa mbele kabisa ambao ndiyo ganda la hii hotuba kuna picha ya Mheshimiwa Waziri akimpa maelekezo Mheshimiwa Rais kuhusiana na mradi nadhani unaweza kuwa ni mihogo au sijui nini maana picha haitafsiriki vizuri.

**NAIBU SPIKA:** Akimpa maelezo.

**MHE. MURTAZA A. MANGUNGU:** Maelezo?

**NAIBU SPIKA:** Ndio.

**MHE. MURTAZA A. MANGUNGU:** Sasa nataka Mheshimiwa Waziri wakati anajumuisha hotuba ya bajeti yake, ningependa atueleze kwamba huwa kweli anasikiliza maelekezo ya Rais au anaamua vile ambavyo yeye anaona inafaa. Nasema hivi kwa maana kwamba mwaka 2009 Rais alikutana na viongozi wa Wizara pamoja na watendaji wa taasisi zote na yakafikiwa maelekezo 13 ambayo aliyatoa na nitayawasilisha kwako kwa maandishi na ningependa Bunge na Watanzania wajue kati ya yale ni lipi ambalo limetekelezwa na Wizara yako?

Mheshimiwa Spika, hali ya mfumuko wa bei ya chakula nchini ni mbaya sana. Wananchi wanapata shida, wananchi wanalalamika kwamba bei ya vyakula imekuwa ni kubwa, hailingani na uwezo halisi wa kipato walichonacho kwa hivi sasa. Mfumko wa bei ulifikia asilimia 19.5 na sasa

inasemekana umeshuka mpaka asilimia 9.8. Mimi nasema huu mfumuko unazungumzwa kitakwimu zaidi, hali halisi bado haijafanyiwa utafiti wa kutosha, kwa maana kwamba bei ya chakula bado iko juu.

Mheshimwa Naibu Spika, binafsi nilijiuliza maswali mengi inawezekanaje katika mambo ambayo hayanufaishi Watanzania wote kwa wakati mmoja, Serikali inakuwa rahisi sana kuwekea mfumo wa kudhibiti. Kwa mfano tumeweka udhibiti katika bei za mafuta, tumeweka udhibiti katika matumizi ya vyombo vya mawasiliano kama simu, tumeweka udhibiti katika nauli za mabasi na daladala. Kwa nini hatuweki udhibiti katika bei za vyakula ambapo Watanzania wote pamoja na hao wamiliki wa hizo taasisi nyingine wanatumia chakula? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaachia wananchi waendelee kuogelea na kukandamizwa na dimbwi la wafanyabiashara ambao wanapenda kupata faida iliyopindukia. Nchi nyingi duniani kama Indonesia, Malaysia India, wameweka mfumo wa kudhibiti bei ya chakula. Kwa nini Tanzania hatutaki, tunalazimisha hili liendelee kuwa huru na tunawaumiza wananchi?

Mheshimwa Naibu Spika, jambo ambalo na wewe Mheshimiwa Waziri nataka ujiulize. Leo hii ukienda katika eneo la Mtibwa, ukienda Moshi, ukienda Kagera, bei ya sukari katika maeneo ya viwanda vya sukari ni kubwa ukilinganisha na bei ya maeneo ambayo hayana viwanda vya sukari. Leo hii ukienda Zanzibar sukari ni shilingi 1,200/- wakati hawana kiwanda cha sukari, Dar es Salaam bei ya wastani ni shilingi 1800/- mpaka 2,200/-. Kwa nini maeneo ya Mtibwa, maeneo ya Kagera na maeneo ya Moshi, sukari ni shilingi 2,500/- mpaka 3,000/-, hili mnalitazama vipi? *(Makofi)*

Mheshimwa Naibu Spika, halafu hao wenye viwanda vya sukari, wanasema hatulipi wakulima kwa sababu sisi sukari yetu haijauzwa. Wanauza kwa bei kubwa na katika mfumo huo wa kuruhusu watu waagize sukari kutoka nje, vibali hivyo wanapewa haohao wanauza sukari kutoka nje

na haohao ndiyo wanakaa na sukari kwenye maghala. Hili mnalifikiria vipi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nizungumzie lingine. Katika kupunguza bei ya chakula nchini; mwaka jana Bunge liliazimia *NFRA* ipewe pesa za kusagisha unga katika kinu kile cha Iringa. Tulitumwa na Mheshimiwa Spika hapa, tukaenda kukagua kile kinu na taarifa tuliiwasilisha kwake na Bunge liliazimia *NFRA* wapewe pesa. Mpaka hii leo Wizara hii haijawahi kutoa hata shilingi kuwapa *NFRA*. Bei ya unga imefikia shilingi 1,200/- mpaka 1,500/-, tunawaonea huruma wananchi au tunapanga mipango kufuatana na fikra zetu zinavyotuendesha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo nataka nilizungumzie ni huu utaratibu wa kuanzisha programu nyingi. Nilisema tangu asubuhi wakati nahojiwa kwenye kipindi cha *TBC*, ukiangalia magari ya Waheshimiwa Mawairi hawa huwezi kukosa mkasi. Mara nyingi mimi nilikuwa najiuliza hawa wananyoana wenyewe? Nikagundua kwamba kumbe ile mikasi ni kwa ajili ya kuzindulia programu mpya kila siku, wanakata utepe, wanafungua programu. Sasa hizi programu, programu tu mpaka lini na wananchi wanaumia? *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimwa Naibu Spika, mfano mbaya wa programu hizi, mwaka 1982 mpaka mwaka 1990, Serikali iliingia mkataba na Wajerumani katika utafiti wa kilimo cha nazi. Mikoa yote ya Lindi, Mtwara, Pwani, Dar es Salaam, Tanga, Mafia, Unguja na Pemba, walikuja watu kufanya utafiti na wakaua minazi yetu ya asili wakaleta minazi mipya. Leo hii wakati tuna shida, wananchi wanapata taabu, hawawezi kujikimu Wizara inaleta hotuba hakuna hata nazi ambayo imezungumziwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa leo hii mnatuhamisha kutoka wapi tunaelekea wapi? Hili ni jambo la kusikitisha na kustaajabisha sana. Zao la nazi ni zao muhimu kwa uchumi wa wakazi wa Mikoa ya Pwani pamoja na Morogoro na mingine kama Mbeya, Tabora na kwingineko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme lingine kwamba katika suala la korosho ambalo limeanishwa hapa, nastaajabu kwamba kuna baadhi ya Wabunge wanapinga Vyama vya Ushirika havihusiki na kufifiisha uchumi wa wananchi kwa kuwanyonya na kuwanyanyasa kwa kushirikiana wao na madalali. Hili jambo ni la kweli kabisa kwamba Vyama vya Ushirika vinahusika, wananchi wanalipishwa madeni ambayo hayakuingia na dhamana inarudi kuwa ni mazao yao ambayo wanawasilisha kwenye vyama vile. Mfumo huu lazima uangaliwe ili wananchi iwe ni hiari yao, aidha kupeleka mazao kwenye Chama cha Ushirika au wapeleke wakauze katika mfumo huru kwa mtu yeyote kwa kulinganisha na mazao ambayo wanayatoa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni kuhusu huu msamiati wa ruzuku ya pembejeo. Naishauri Serikali na kuisisitiza na naiambia kwamba ufutwe katika misamiati yote. Kwa sababu hakuna mtu ambaye ananufaika na hizi pembejeo, hakuna mtu ambaye ananufaika na vocha, shusheni bei ya mbolea, wananchi waweze kunufaika. Leo hii tunazungumzia upatikanaji wa gesi katika Mikoa ya Lindi na Mtwara na Mikoa mingineyo, tunayo gesi ya kutosha, tuanzishe viwanda na Serikali badala ya kuelekeza hela kuwapa wafanyabiashara, iwekeze katika viwanda vya mbolea. Tanga kulikuwa na kiwanda, kifufuliwe na Mtwara kuna mpango wa kujenga kiwanda, kiwanda kile kijengwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, leo hii sisi wakulima kutoka Mikoa ya Lindi na Mtwara tumechoka kupewa pole bila ubani. Tunahitaji tupewe mipango ambayo itatukwamua tuzalishe chakula kinachoweza kutosheleza mahitaji yetu. Hata Tabora Mkoa ambao ni *potential* kwa kilimo, leo hii wanalalamika. Bunge lililopita na Bunge hili tumekuwa tunalalamikia sana ufaulu wa watoto. Moja kati ya mambo ambayo yanachangia watoto kutokufaulu ni lishe kutototosheleza, watoto hawezi kuwa na akili za kutosheleza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kule kwetu kuna msemo unasema kwamba shida ingekuwa sumu wengi wangekufa. Sasa nimalizie kwa kusema kwamba tujitahidi kutatua matatizo ya wananchi ili tuweze kuingia katika hatua zingine za kimaendeleo.

Mheshimwa Naibu Spika, mwisho kabisa ningependa kuuliza Mheshimiwa Waziri maana ukiwa katika biashara ya ushindani lazima uangalie na mpinzani wako anafanya kitu gani. Tumeona hapa katika hotuba aliyowasilisha Waziri Kivuli amesema kwamba kuna nchi kama Australia, Russia na nchi za Scandinavia zinalima korosho. Sasa tunataka kujua wanalima kwa kiasi gani na katika maeneo yapi ili tuone kwamba tunaingia katika ushindani gani wa kibiashara na wao.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Murtaza Mangungu, tunakushukuru sana kwa mchango wako katika eneo hili.

**MHE. MURTAZA A. MANGUNGU:** Mheshimwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Sasa ni zamu ya Mheshimiwa Magalle John Shibuda atafuatiwa na Mheshimiwa Zaynabu Vullu.

**MHE. JOHN S. MAGALLE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kupata fursa hii nami niweze kuchangia machache.

Mheshimwa Naibu Spika, kwanza kabisa, naomba kujielekeza katika mambo ambayo yatakuwa na mawazo ya fikra chanya kwa mambo mtambuka yaliyopo katika Wizara hii. Nitashauri mambo ya kuhimiza kwa dhamira ya kwamba kilimo kiwe ni kwa maslahi endelevu ya maisha bora

ya Watanzania badala ya kuwa malighafi kwa Walowezi wachache ambao wanapitia sasa dhana ya uwekezaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda vilevile kutumia fursa hii kusema kwamba, hakuna chema kisicho na kasoro na napenda kusema kwamba nitajielekeza katika kasoro ili ziweze kuboreshwa na kutafutiwa dawa.

Mheshimwa Naibu Spika, kwanza napenda kutoa ushauri ufuatao, naomba sana viongozi hasa Mawaziri mnapokwenda katika ziara zenu Mikoani na Wilayani, msiwe ni sikio sikivu kwa utashi wa mawazo ya Mkuu wa Mkoa au Mkuu wa Wilaya kwani taarifa nyingi mnazopewa ni za kulinda usalama wa Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya. Kwa hiyo, sasa hivi muwe na utaratibu mpya ambao mtavuna mawazo ya Madiwani, taarifa ya Madiwani na Wabunge ili muweze kuhakikisha kwamba mnakuwa na mawazo ambayo yana mtazamo chanya kwa maslahi ya jamii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda vilevile kuwashauri viongozi wa Serikali hususan Waziri wa Kilimo kwamba kilimo cha pamba kina mambo mengi ambayo yanahitaji Waziri ayafanyie kazi, umekuwa mshiriki na mdau wa kusikiliza mambo mengi, lakini sioni juhudi za Wizara yako kutatua matatizo hayo. Nasikitika kwamba wakulima walijengewa urafiki na TANU kwa Serikali yao na hivi sasa kisomo hicho cha urafiki kinaelekea kupukutika na kinatokota na mwisho wa yote ni kuwa na ufa ambao utazaa mifarakano ya kujutia na majuto ni mjukuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba Waziri wa Kilimo awaeleze Watanzania hususan wakulima wa pamba, tumefaidika nini na hawa wataalam, wamesaidia nini kilimo cha pamba, wamepunguza nini umaskini wa wakulima wa pamba, wanaongeza nini kwenye thamani ya zao la pamba kupata ubora na kupata maisha bora? Naomba sana uje uwaambie.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile pamekuwa na dhana ya kusema kilimo cha mkataba kina ubora, kina ubora gani na wapi? Kilimo cha mkataba wanaongeza madeni kwa wakulima na mkulima anayeshindwa kulipa madeni ya kilimo cha mkataba anakuwa na madeni ambayo yanabebeshwa na matokeo yake anakuwa ni manamba wa wafanyabiashara. Hakuna mfanyabiashara duniani ambaye ni mtaji wa kuondoa umaskini wa mtwana. Ninakuomba suala hili mkae mtafakari, mwache maneno matamu ya kutumia elimu za ma-*book* bila kujali uzoefu na ujuzi unaotokana na maarifa ya wakulima.

Mheshimiwa Spika, naomba hilo kulisema na nasikitika vilevile kutoa taarifa kwamba, ninashangaa sana panapotokea maafa ama chakula cha kupelekwa kwa ajili ya msaada kinakuwa ni nyenzo ya ulanguzi wa kisiasa. Hebu naomba Serikali iondoshe dhana ya chakula cha msaada kuwa ni nyenzo ya ulanguzi wa kisiasa. Leo kuna mafuriko Maswa lakini taarifa za athari ya mafuriko mbalimbali katika nchi wanaachiwa Wakuu wa Mikoa wafanye na watoe taarifa kwa kipindi wanachotaka. Naomba Serikali itoe Mwongozo na ikiwezekana itoe vilevile na Kanuni ya kwamba baada ya siku kumi taarifa ziwe zimefika ili waathirika wa maafa hayo wapate misaada ya uongozi na utawala bora. Naomba kasoro hizo ziondolewe haraka iwezekanavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumwarifu Waziri wa Kilimo kwamba nchi yetu hivi sasa bei ya zao la pamba kwa kweli ni fikra za kutangatanga kwa wakulima wa zao la pamba. Naomba basi Kamati inayohusika na masuala ya Bajeti pamoja na Serikali, mkakae mpitishe bei ya nyongeza badala ya kutuambia kuna rasimu. Kuweni na vitendo kazi kuliko kuwa na nadharia ya mitazamo ambayo ni lugha tamu lakini haina faida kwa maisha bora ya Mtanzania. Naomba balaa ya machukizo hayo myaondoe haraka iwezekanavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kusema kwamba kujenga imani ni rahisi lakini kuibomoa kuirejesha ni kugumu sana. Watanzania wanahitaji ombwe la kasoro la sikio la

kusikiliza matatizo ya wakulima lipatiwe jibu haraka iwezekanavyo. Mnazungumza uwezeshaji kwa wananchi, nadharia ziko nyingi sana lakini uhabarishwaji kwa wakulima ni kidogo sana. Naomba ujuzi wao wa Kiserikali wa wataalam wenu uwafikie wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiona kuna moto umezaliwa na cheche. Napenda kusema kwamba palipo na kiburi cha kujaribu kufunika fedheha ya taarifa zinazoonyesha kuna kasoro, matokeo yake huwa ni makubwa sana. Naomba Serikali inapopata kasoro zinazobainishwa na Wabunge au wanasiasa isichukie kwani Bunge ni sauti ya jamii na ni sikio la jamii na sisi Wabunge tunapotoa mambo yetu ya kuishauri Serikali, yasipokelewe na kubezwa kwamba ni mambo ya wanasiasa. Naomba hilo mnalojaribu kufanya kwamba Serikali ninyi ndiyo mna maono, ndiyo mna busara na hekima kuliko wanaoongozwa, ni kasoro na ni hitilafu kubwa sana katika utawala bora. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba Waziri wa Kilimo atuambie, hivi kilimo cha mkataba hadi leo kimesaidia kupunguza umaskini wa mkulima kwa kiasi gani? Nashangaa sana Mwenyekiti wa Bodi ya Pamba anaposema kwamba ni ukombozi. Ukombozi huo wa mbinu gani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile ninasikitika kusikia kwamba inatungwa Sheria ya Kilimo cha Mkataba kwa kupitia taaluma na mawazo ya wana taaluma bila kujali uzoefu na ujuzi wa walengwa kutumikia Sheria hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hakuna mahali popote ambapo mjeledi huibua werevu palipo na giza la ujinga. Nakuomba sana Waziri unapotunga Sheria kwa Wakulima, tambua kwamba wanadai na wana kiu ya kupata maarifa, uzoefu ambao utakuwa ni jumuisho la elimu na ujuzi, naomba sana hilo tafadhali.

Mheshimiwa Naibu Spika, maabara inapotambulisha kwamba Mfalme ana minyoo huwezi ukailaani na kusema kwamba inafedhuli ufalme. Wa kale walisema sauti ya *Victoria Federation* ndiyo ilikuwa ya ukombozi, nina- *declare interest* kuwa mimi ni mlezi wa Chama cha TAKOGA ambacho hivi sasa kinapigia kelele dhidi ya kupokonywa haki za wakulima na mapambano ya TANU wakulima wa pamba wanauliza mapambano na ahadi za TANU zimewekwa kwenye mfuko wa nani?

Mheshimiwa Naibu Spika, kilimo cha pamba ili kiweze kuwa na changamoto endelevu, ninaomba pamba iwe na ngao ambayo itakuwa ni ulinzi kwa wakulima. Hivi sasa wakulima wa pamba wanaishi na utumishi wa Bodi ya Pamba ambayo haina maslahi kwa wakulima wa pamba. Vilevile ninasikitika kusema kuwa kila mnapozungumzia mfumo wa maandiko ya kilimo cha pamba, hamuelewi kwamba kilimo cha mkataba hivi sasa ni giza na maneno yaliyoko katika maandishi ya kilimo cha mkataba hayana urafiki na yanaezua urafiki baina ya CCM na wakulima wa pamba na majuto ni mjukuu na mwanzo wa moto ni cheche.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna tabia giza za baadhi ya viongozi wa Halmashauri na ma-*DC* ambao ni balaa kwa sababu kila wanaposikia wakulima wanasema kwamba ujuzi huu mnaotuletea unaathari, wanawaambia fuateni la sivyo tutawaweka ndani. Sasa ubabe huo ninaomba uachwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba Mheshimiwa Waziri atuambie kwa nini *passbook,* mfuko wa kujitegemea hautaki kurejeshwa tunaletewa mfumo wa kuwekewa madeni kwa wakulima wa pamba. Ukweli una tabia ya kujirejea na kama hamtaweza kusahihisha hayo muelewe kuwa mnajenga hasira kwa wakulima wa pamba.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kusema kuwa kilimo cha pamba ni malighafi ya kisiasa na tunajiandaa kudai uongozi ambao utajali maslahi ya wakulima wa kilimo cha pamba. Napenda kusikitika kuwa unyonyaji unaoendelea hivi sasa wa taaluma ya kupitia amri za Wakuu wa Mikoa

kuwa marafiki wa wafanyabiashara wanyonyaji, hasara zake ni 2025.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba Serikali kupitia Wizara hii, itambue na kuthamini kuwa itasadikika tu kama itakuwa na sikio sikivu kwa wakulima na kujali kasoro zinazotambulishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri Serikali hii isiwe ndiyo ramli ya kuchagua maono yapi ndiyo yanafaa kutungiwa Sheria bila kupata maono ya wakulima. Serikali iache kuegamia mbinu za Sheria kuwa ndiyo zitakazoweza kuendeleza kilimo cha pamba. Duniani hakuna mjeledi ambao unaendeleza mtoto mjinga akawa mwelevu. Kwa hiyo, naomba Serikali isisigane na mawazo yanayotolewa na wanasiasa, Wabunge na Madiwani.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ninaomba sasa ijenge ukanda ambao utatambulika kuwa ni kwa maslahi ya wakulima na ukanda ambao utatambulika kuwa ni kwa maslahi ya wakulima wafugaji. Leo ninasikitika kutoa kilio cha wakulima wafugaji wa Kanda ya Ziwa ambao hivi sasa wanateseka na wanatokota na kaulli za uonevu zinazotolewa na watumishi wa Serikali. Naomba Serikali na Bodi ya Pamba waache kukingia kifua dhuluma zinazotendwa na hao wafanyabiashara. Sheria ninaomba ziwe ni kwa maslahi na ustahili wa maendeleo ya jamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu maono endelevu ya kuongeza uzalishaji, ninashauri Serikali itenge maeneo mapya ya kuifadhi ukanda wa wakulima wafugaji na ukanda wa wafugaji ambao ni wa mila ya kilimo peke yake na ukanda ambao utakuwa ni wa viwanda ili tusianze kuwa tunaingiliana na kuzozana. Nashauri haya yakitendeka amani na utulivu utakuwepo. Tengeni hifadhi mpya katika maeneo mapya, tusing’ang’anie kuwa sehemu moja kwa sababu ardhi ni kubwa na ni pana basi zindueni makazi mema ambayo yatajaa wakulima wa mila tofauti na kila mmoja ipewe uwezo wake. Wakulima wafugaji tutatumia uwezo wetu kuhakikisha kuwa pamba inakuwa.

Mheshimiwa Naibu Spika...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji).*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa muda wako umekwisha.

**MHE. JOHN S. MAGALLE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kusema kuwa Bunge hili vilevile tujielekeze kuwa na staha ya kusaidiana kuliko kuwa ni watu wa hila na visa. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa John Shibuda Magalle, kwa mchango wako kwamba kilimo cha 'nkataba' kimeshindikana sasa sijui huo muungano *wa* 'nkataba'*. (Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Zaynabu Vullu atakuwa mchangiaji wetu wa mwisho kwa asubuhi ya leo.

**MHE. ZAYNABU M. VULLU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipatia na mimi nafasi ya kuweza kuchangia hoja hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya yote, nianze kwa kutamka kuwa ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia ninapenda kusema kwamba Wizara kwa hakika imeweza kueleza mambo mazuri sana katika bajeti yake. Angalizo kwao ni kwamba waweze kuwasimamia watendaji. Watendaji wakiwa hawakufanya vizuri lawama zote huishia kwa wanaoongoza Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkoa wa Pwani na sisi ni waathirika wa matumizi ya stakabadhi ghalani lakini kabla sijaeleza yote, ninaomba ninukuu yaliyoandikwa kwenye kitabu cha hotuba, ukurasa wa 51, kipengele namba 96 kinasema, naomba kununukuu kwa ruksa yako:-

*''Wizara imeendelea kuhamasisha matumizi ya mfumo wa stakabadhi za maghala kwa lengo la kuwawezesha wakulima kupata bei nzuri katika biashara ya mazao. Hata hivyo, mfumo huo umekabiliwa na changamoto zinazotokana na upotoshaji unaofanywa na walanguzi na madalali wanaojinufaisha na ununuzi wa mazao kutoka kwa wakulima kwa kutumia mfumo usiokuwa rasmi. Aidha, watendaji wasio waaminifu wa Vyama Vya Ushirika, Wasimamizi wa Maghala na Taasisi za Fedha wamechangia kudhoofisha mfumo huo. Serikali itaendelea kuuboresha mfumo huo ili kuondoa kasoro zilizojitokeza ikiwa ni pamoja na kuwachukulia hatua wanaohujumu mfumo huo".*

Mheshimiwa Naibu Spika, haya ni maneno mazito sana. Serikali imeonyesha ni jinsi gani iko makini katika kufuatilia hili lakini hawa wanaofanya hujuma, kama Serikali imewabaini mpaka leo hii wamechukua hatua gani? Kwa sababu hawa ndiyo wanaowaumiza wakulima, hawa ndiyo wanaofanya Serikali inaonekana haitimizi wajibu wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, leo Serikali imesema dhahiri shahiri hapa kuwa hawa ndiyo wanaopotosha na wanaoharibu kazi na nguvu ya wakulima. Ombi langu wanaohusika watafutwe, wachukuliwe hatua na wakulima wahakikishiwe kwamba mfumo unaokuja na mazao yanayotarajiwa kuvunwa wakati unaofuata kwa kutumia mfumo huu wa stakabadhi ghalani basi wanapata fedha zao ili ziwaendeshee maisha yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakulima hawa wana mambo mengi sana ya kufanya, wakulima hawa hawana kazi nyingine zaidi ya kulima, sasa leo mtu analima, anavuna anategemea auze apate pesa lakini zile pesa hazipati kwa wakati unaostahili, anabaki na mazao ndani, pesa haipati, pesa zinakaa kwenye maghala lakini hazipati kwa wakati. Naomba Serikali iwe makini katika hili ili kuweza kuhakikisha wakulima wanapata pesa zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la Maafisa Ugani. Nina uhakika wenzangu humu ndani watakubaliana na mimi kuwa kuna maeneo mengine ajira hii haijawafikia. Maafisa Ugani wengine hawako kwenye vijiji vyetu na hata kama wakiwepo hawafanyi kazi zao kwa wakati na kwa mujibu unaostahili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ni vyema kwa maelezo waliyoyatoa katika hotuba yao, Serikali ihakikishe inazingatia na kufuata utaratibu waliotueleza kwenye hotuba ili tuweze kujua Maafisa Ugani wanafanya kazi zao kwa uadilifu. Pia siyo vibaya Maafisa Ugani hawa wakaa na wakulima wa eneo husika wakatoa elimu ya zao linalokubalika katika eneo husika badala ya watu tukisikia kwenye vyombo vya habari zao la alizeti lina pesa nyingi, linakubalika, mtu mwingine analima bila kuangalia hali halisi ya ardhi inasema nini na mvua zinaelezaje kwa zao husika. Kwa hiyo, ninaomba itolewe elimu ya mazao kutokana na ajira itakayopatikana kwa hao Maafisa Ugani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Serikali kwa kuongeza idadi ya wanafunzi katika sekta ya kilimo lakini ninaomba Serikali iongeze bidii kuhakikisha wanafunzi hawa wanaotoka katika sekta ya kilimo, wanaomaliza masomo yao, kuwe na msukumo kama unaofanywa kwenye Wizara ya Elimu na maeneo mengine. Kwa sababu wengi wao wanakuwa wako mitaani ama wajianzishie wenyewe vikundi ama wakawe wabangaizaji ambao hawana ajira inayoeleweka. Sioni sababu kwa nini hawa wasiwekewe utaratibu mzuri, wakashirikishwa na wakulima waliokuwa vijijini kule kwetu katika Mikoa yetu, wakaunda umoja wao kwa kushirikiana na wale waliokuwa kule tayari, wakatoa elimu yao na Serikali ikawekeza kwa hawa wanafunzi kama imeshindwa kuwapa ajira za moja kwa moja basi watoe utaratibu wa kusema watatoa mkopo iwe wa matrekta, iwe kumeongezwa *scheme* za umwagiliaji, washirikiane na wakulima wa maeneo waliyokuwepo ili tuhakikishe nchi yetu tunapata mazao ya kutosha. Tusipoangalia, wanafunzi hawa wanaotoka katika Vyuo Vya Kilimo, utakuja kuwa mwiba

usiotoka kwenye mguu au kama umeingia sehemu nyingine ikawa ni madhara makubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niombe Serikali pamoja na juhudi zake inazofanya ifike wakati sasa iwe na mpangilio wa kusema kuwa wanaohitimu katika vyuo vyetu vya kilimo, wapate ajira au wawezeshwe kwa mikopo kwa ajili ya kujiendeleza wenyewe. Hii itasaidia kwetu sisi sote, nchi yetu hapo miaka ya nyuma tulikuwa tunauza mazao yetu nje ya nchi iwe ya biashara au chakula. Kwa hiyo, tukiwawezesha hawa na mimi nina hakika Wizara hii kutokana na viongozi wanaoongoza, hili wanaliweza na kutakuwa na mafanikio makubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nijikite kwenye zao la korosho. Zao la korosho ni zao tunalolitegemea sana Mkoa wa Pwani, nimekuwa nikiliongelea kila mara ninaposimama wakati wa bajeti, iwe kupitia Wizara hii, iwe ni kupitia kwenye hotuba ya Waziri Mkuu. Naomba ufike wakati tusimame wawakilishi tunaotoka kwenye Mikoa inayozalisha korosho tuanze kusema kweli bei ya safari hii imemnufaisha mkulima, kweli mbolea imefika kwa wakati, kweli tunajivunia Serikali sasa hivi imetuletea viwanda lakini mpaka sasa hivi ninaposema hatuna viwanda vya korosho, hatuna viwanda vya matunda. Niiombe Serikali ihakikishe wale wanaosimamia masuala ya ugawaji wa mbolea na pembejeo zingine za korosho kama wameshindwa kazi, wawaweke pembeni wawatafute wengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hali kadhalika kwenye bei ya korosho mpaka sasa hivi bei ya korosho haina uhakika. Korosho zimekutana za mwaka juzi na mwaka jana lakini nina hakika kama Serikali italisimamia kwa uhakika na kwa umakini kwa kuangalia wale wanaofanya ubadhirifu basi hili zao litaweza kumnufaisha mkulima na atajikomboa kiuchumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, viwanda ndiyo mkombozi kwa mkulima. Kukiwa na viwanda bei itakuwa kubwa na itakuwa ya ushindani. Niiombe Serikali ihakikishe inatupatia

viwanda, tupate viwanda Mkoa wa Pwani, tupate viwanda na Mikoa mingine kutokana na mazao wanayozalisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mengi nilizungumza katika bajeti nyingine na mengi nilizungumza katika bajeti zilizopita lakini kama sikuzungumzia tena na bajeti hii suala la zao la nazi, nitakuwa siitendei haki nafsi yangu na wakulima wa Mkoa wa Pwani na Mikoa mengine inayolima nazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, zao la nazi, ni mkombozi mkubwa sana kwa wakulima. Kwanza niwaambie na kila siku huwa ninasema zao lile halina hiyana na binadamu, unavuna mara nne kwa mwaka mvua na jua wewe unavuna. Naomba suala la zao la nazi lipatiwe ufumbuzi, kama wenzetu waliweza kupewa fidia basi na wale wote ambao minazi yao ambayo imekufa na wao wafikiriwe kupewa fidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Zaynab Matitu Vullu kwa mchango wako.

Waheshimiwa Wabunge, naomba niwashukuruni sana kwa jinsi ambavyo mmeshiriki katika kuchangia hotuba hii ya Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika na Mheshimiwa Vullu alikuwa ni mchangiaji wetu wa mwisho.

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. MOHAMMED A. KEISSY:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashangaa sana baadhi ya Wabunge kutaka ushuru utolewa kwenye zana za kilimo kama vile tela za trekta, mtu anayenunua trekta ni mtu mwenye uwezo na trekta ni biashara, linaingiza pesa kuliko *tipper*. Mimi binafsi nilikuwa na trekta na tela, nilikuwa nafanya kazi *NMC* kusombea mazao, kusomba mchanga, mawe, tofali, kubebea kuni na pia kukodisha kulimia na leo hii kukodi trekta eka moja shilingi

30,000 - 50,000. Je, ukilima eka 10 – 15 kwa siku utakuwa umeingiza shilingi ngapi? Kwa hiyo, kila kitu kikisamehewa ushuru Serikali yetu itapata wapi pesa na huku hatuna maji, barabara, na kadhalika? Anayenunua trekta ni lazima kwanza naye alipe kodi maana anapata pesa. Leo mvuvi tu analipia hata kijimtumbwi kidogo kwa ajili ya uvuvi. Kwa hiyo, anayemiliki trekta alipie kodi, kwa sababu analifanyia biashara. Trekta halina masika wala kipupwe, ni kazi tu. Lazima wachangie katika mapato ya Serikali yetu,

Mheshimiwa Naibu Spika, fedha ya ruzuku ya mbolea na mbegu, elekezeni kwenye umwagiliani kuliko kunufaisha wachache ambao wanajitajirisha.

**MHE. DKT. PUDENCIANA W. KIKWEMBE**: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchangia katika maeneo haya yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ni kuhusu upatikanaji na ugawaji wa pembejeo. Serikali iangalie namna ya utoaji wa pembejeo kwa wakulima wadogo wadogo. Serikali imekuwa ikitoa ruzuku ya mbolea na mbegu kwa wakulima kwa kiasi cha eka moja tu. Ni vema sasa Serikali iangalie upya kwani kauli ya Kilimo Kwanza ni pamoja na kuzalisha kwa tija na ili kuwa na tija ni lazima kulima eneo kubwa na kama mkulima atapewa ruzuku kwa angalau eka tatu, kilimo kitakuwa ni ajira na pia mkulima hataweza kuharibu mazingira kwani hataweza kulima kwa kuhamahama. Kama lengo ni kuongeza tija na ufanisi, ni vema sasa ruzuku hizo zikatolewa angalau kwa eka tatu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili ni kuhusu Mfuko Maalum wa Kufidia Bei za Mazao (*Price Stabilization Fund*). Naipongeza Serikali kwa matarajio ya kuanzisha mfuko huo. Napenda kufahamu, je, mfuko huo ni kwa mazao gani? Je, wakulima ambao mazao yao yanakuwa yameharibika kutokana na hali ya hewa pamoja na kuliwa na wadudu kama vile viwavijeshi, watafaidika na mfuko huu?

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu ni kuhusu Bodi ya Nafaka ya Mazao Mchanganyiko. Pamoja na kwamba Serikali imekabidhi kinu cha kusagisha mahindi cha Iringa katika bajeti ya mwaka jana 2012/2013, Bodi hii kupitia kauli ya Mheshimiwa Waziri Mkuu iliahidiwa kupatiwa angalau shilingi milioni kumi (10,000,000/=) ili ianze kazi. Je, fedha hizo *(10 milion)* zilitolewa? Je, ni lini Bodi hiyo itaanza kutumia kinu hicho kibiashara kwa kushirikiana na *NFRA*?

**MHE. MARIAM REUBEN KASEMBE**: Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua nafasi hii kuchangia Hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Kilimo Chakula na Ushirika kwa maadishi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la kujitosheleza kwa chakula ni jukumu la kila kaya na Serikali husaidia pale ambapo hutokea upungufu wa chakula kutokana na maafa au hali ya hewa kuathiri mazao.

Mheshimiwa Naibu Spika, asilimia kubwa ya Watanzania hivi sasa suala la kilimo wamefanya ni kazi ya ziada na wengi wanaoshiriki kilimo ni wazee na akina mama waliopo vijijini. Vijana walio wengi na watu waishio mijini hawajishughulishi na kilimo, kila mmoja amekuwa akijishirikisha na biashara ndogondogo ambazo hazina tija na hazitoshi hata kuendesha maisha yao. Wale ambao wapo vijijini, kilimo chao si cha kisasa na wala mashamba si makubwa kwani wanatumia vifaa duni hivyo mavuno pia si yakutosha kwa familia kwa mwaka mzima.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hali hii, naomba niikumbushe Serikali na kushauri kuwa tuna Sheria ya Nguvu Kazi ambayo inamtaka kila mtu afanye kazi ya kujiingizia kipato hasa kilimo. Miaka ya nyuma sheria hii ilikuwa inatekelezwa na msimamizi mkuu wa sheria hii ilikuwa ni Wilaya kwa maana ya Mkuu wa Wilaya, Mkoa kwa maana ya Mkuu wa Mkoa na tulishuhudia kulikuwa kunafanyika misako mijini ya wazururaji kurudishwa vijijini ambako walikuwa wanapewa maeneo ya kilimo (mashamba) wakisimamiwa na Wenyeviti wa Vijiji. Kwa nini hivi sasa

misako hii haifanyiki? Serikali haioni nguvu kazi kubwa ipo mijini ambako hakuna kazi za msingi wazifanyazo? Kwa nini Serikali haifanyi misako au kushauri kwa vijana wetu kurudi vijijini?

Mheshimiwa Naibu Spika, Hayati Baba wa Taifa kazi hiyo aliifanya na aliweza kuwaondoa watu katika Jiji la Dar es Salaam na kuwahamishia vijiji vya Gezaulole, Kigugumo na kadhalika na wengine ambao hawakuwa tayari kwenda katika vijiji hivyo walirudi vijijini kwao kwa hiari na Serikali iliwagharamia usafiri tu. Je, Serikali yetu haioni huu ni mfano wa kuigwa na unaweza kupunguza msongamano wa watu mijini lakini vilevile itawafanya watu wawajibike katika suala zima la kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mchango wangu wa Hotuba ya Waziri Mkuu, nilizungumzia suala la tatizo la stakabadhi ghalani na Mheshimiwa Waziri alitoa ufafanuzi kuwa ataleta sheria hii Bungeni ili iweze kufanyiwa marekebisho kwa vipengele ambavyo vinaleta matatizo katika mfumo mzima wa stakabadhi ghalani. Suala langu kwa Mheshimiwa Waziri ni kutaka kujua sheria hii italetwa lini Bungeni ili iweze kutumika kabla ya msimu ujao wa korosho kuanza ili kuwaondolea kero wakulima wa korosho na kuwarudishia imani wananchi kwa Serikali yao?

Mheshimiwa Naibu Spika, suala hili ni muhimu sana kwa hatma ya zao hili kwani hali hivi sasa si nzuri kwa wakulima. Kwa hiyo, naiomba Serikali ifanye haraka marekebisho hayo kwa kushirikisha wadau wa korosho, tafadhali Mheshimiwa Waziri tuondolee kero hii ambayo ni ya muda mrefu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho nitaunga mkono hoja baada ya kupata majibu yenye matumaini kwa wakulima wa zao la korosho.

**MHE. MTUTURA A. MTUTURA**: Mheshimiwa Naibu Spika, moja ya kazi za Bunge ni kutunga sheria na sheria ikishatungwa Serikali inapewa jukumu la kusimamia ili

itekelezwe ipasavyo. Sheria ya Stakabadhi ya Mazao Ghalani ambayo ilitungwa na Bunge letu, kwa kipindi cha miaka miwili iliyopita mfululizo, Serikali imeshindwa kuisimamia sheria hii ili ilete manufaa yaliyokusudiwa. Naiomba sana Serikali kwa miaka miwili ijayo isitishe utekelezaji wa sheria hii kwa mazao yote ili kuinusuru CCM kwa chaguzi zijazo.

**MHE. KAIKA S. TELELE**: Mheshimiwa Naibu Spika, hali ya upatikanaji wa chakula katika Wilaya ya Ngorongoro hususani Tarafa ya Ngorongoro ni mbaya sana. Tarafa hii yenye wakazi takribani elfu sabini (70,000) ni hifadhi yenye matumizi mseto ya ardhi (yaani watu na wanyamapori kuishi pamoja bila kudhuriana). Wananchi hawahawa hawaruhusiwi kulima kutokana na Sheria ya Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo napenda kumshukuru Mheshimiwa Waziri yeye binafsi kwa kunisikiliza na kunisaidia mara zote nilipoleta kilio cha njaa cha watu wangu. Mara zote alikubali kutupatia chakula (mahindi) kutoka Wakala wa Hifadhi ya Chakula *(NFRA)* Kanda ya Arusha. Uthibitisho wa ukweli huu ni tani 726.400 iliyotolewa kwa Wilaya ya Ngorongoro na hivyo kuongoza Wilaya za Mkoa wa Arusha kupewa msaada wa chakula, nasema ahsante sana. Naomba pia uendelee kutupa kibali cha upendeleo cha kununua chakula kutoka *NFRA* – Arusha kupitia Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro au Baraza la Wafugaji Ngorongoro *(NCAA).*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kilimo cha umwagiliaji, naomba Wilaya ya Ngorongoro ipatiwe fedha ya kuanzisha skimu za umwagiliaji katika Tarafa ya Sale hususani katika vijiji vya Digodigo, Samunge (kwa babu wa Loliondo) Oldonyo-Sambu, Pinyinyi, Monie na Engaresero. Katika eneo la Lake Natron kuna Mito mikubwa katika maeneo niliyotaja inayotiririka maji mwaka mzima. Wakulima wadogo kutoka maeneo hayo ndio wanaolisha Tarafa za Loliondo na Sale katika Wilaya ya Ngorongoro kwa chakula na mbogamboga kutokana na kilimo cha umwagiliaji duni na wa mazoea (jadi).

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Tarafa ya Ngorongoro ni Hifadhi ambayo kilimo japo cha kujikimu hakiruhusiwi na kwa kuwa ukame wa mfululizo umekuwa ukiua mifugo kwa wingi ambayo ni tegemeo la wafugaji kimaisha na kiuchumi, na kwa kuwa ni haki ya msingi na ya Kikatiba kwa wananchi hao kupata chakula cha msaada, naomba Serikali iendelee kutoa chakula cha njaa/msaada bila kulazimika kupokea maombi kutoka kwa Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Ngorongoro au *RAS* – Arusha. Itoshe Mbunge, Mwenyekiti wa Baraza la Wafugaji na Mhifadhi Mkuu wa Ngorongoro kuleta maombi ya chakula cha njaa/ msaada au cha kununua kwako na kupewa kibali haraka. Utaratibu huu utapunguza urasimu na chakula kuwahi kuokoa maisha ya watu.

**MHE. DKT. AUGUSTINE L. MREMA**: Mheshimiwa Naibu Spika, nilimwandikia barua Mheshimiwa Waziri nikiomba kutokana na matatizo makubwa yaliyo katika Chama Kikuu cha Ushirika cha *KNCU*, Wizara yake itume Wakaguzi. Najua Wakaguzi walifika na kati ya watu waliohojiwa ilikuwa ni pamoja na mimi. Ninaomba kujua ukaguzi huo umefikia wapi kuhusu ubadhirifu unaokikumba Chama cha *KNCU* unaosababisha wakulima wa kahawa kukopwa kahawa yao, wakulima kushindwa kulipwa mabaki yao, ushuru na fedha za masawazisho ya bei na kadhalika. Je, taarifa hiyo ya ukaguzi itatolewa lini?

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja ya Wizara na ninampongeza Mheshimiwa Waziri kwa kazi nzuri.

**MHE. KHATIB SAID HAJI**: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa heshima, napenda kutoa mchango katika Wizara hii muhimu katika mustakabali mzima wa uhai wa nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imekuwa ikifanya jitihada nyingi katika kuhakikisha nchi yetu inajitosheleza kwa chakula ingawa bado kabisa hatujaweza kufikia malengo tuliyokusudia. Moja ya maazimio mazuri yaliyofikiwa katika makubaliano ya nchi wanachama wa *SADC* ni kuwa nchi wanachama zitenge katika bajeti zao wastani wa asilimia

kumi (10%) katika sekta ya kilimo. Hili ni jambo zuri ambalo angalau kwa kiasi fulani lilionekana kukisogeza kilimo katika lengo zuri lakini ni jambo la kusikitisha kwamba mpaka sasa nchi yetu haijaweza kufikia lengo hilo jambo ambalo halionyeshi hasa umakini wa Serikali uko wapi katika kulipa uzito stahiki jambo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Kilimo imekuwa ikitoa vibali vya uagizaji wa sukari kutoka nje ya nchi katika vipindi tofauti inapotokea hali ya upungufu wa sukari hapa nchini, jambo ambalo sio baya. Tatizo lililopo katika utaratibu huu ni pale Wizara inapokosa umakini wa kujua ni wakati gani hasa mahitaji ya sukari ya nje yanapohitajika mfano hai ni katika mwezi wa Februari 2013 ambapo Wizara ilitoa vibali vya tani sitini elfu kutoka nje na ukweli usiofichika ni kwamba katika maghala ya viwanda vya hapa nchini kuna mrundikano mkubwa wa sukari. Je, ni kweli kuna utafiti wowote ambao Wizara ilifanya na ikajiridhisha kwamba kuna ulazima wa kutoa vibali vya kuleta sukari hiyo?

Mheshimiwa Naibu Spika, athari itokanayo na jambo hilo ni kupelekea viwanda vyetu kukosa soko la bidhaa hiyo hasa ukizingatia sukari kutoka nje huwa inaondolewa kodi? Naomba Serikali iwe makini katika utoaji wa vibali vya kuingiza sukari kutoka nje. Iangalie ni wakati gani na mahitaji ya kiasi gani ili isije kuwa ni chanzo cha kuviua viwanda vyetu hivi ambavyo ni tegemeo kwa Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

**MHE. NYAMBARI C.M. NYANGWINE**: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutumia nafasi hii kuiuliza Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika maswali yafuatayo ili Mheshimiwa Waziri aweze kuyajibu wakati wa kuhitimisha hoja hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, umuhimu wa kilimo katika nchi yetu na nchi zinazoendelea kwa ujumla ni mkubwa sana. Umuhimu huo huonekana katika uzalishaji wa chakula cha binadamu na wanyama, uzalishaji wa malighafi kwa

viwanda vyetu, kilimo kutoa ajira na mwisho kilimo kukuza mtaji katika nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, maswali yangu ni:-

(i) Je, Serikali inalifahamu hilo kwa dhati? Inalishughulikiaje suala hili kwa wananchi wetu?

(ii) Je, vyuo vya kilimo katika nchi yetu vipo vingapi na vipo katika Wilaya au Mikoa gani? Je, vyuo hivyo vinatoa wataalam wangapi kwa mwaka na wameajiriwa wote na wanatoa mchango stahiki katika nchi yetu?

(iii) Je, hali ya hewa, mvua, joto na upepo huathiri vipi shughuli za kilimo hapa nchini? Serikali imejipanga vipi kukabiliana na majanga hayo ili kumsaidia mkulima?

(iv) Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha kuwa mazao ya chakula na biashara yanayozalishwa katika Wilaya ya Tarime yanapata soko la uhakika nchini Kenya?

(v) Ni taratibu zipi zinazofuatwa katika uagizaji wa mazao nje ya nchi na kuyaleta hapa nchini Tanzania? Ni kweli taratibu hizo huzingatiwa ipasavyo katika sehemu za mipakani mwa nchi yetu? Mbona taratibu hizo hukiukwa mpakani mwa Sirari Wilayani Tarime?

Mheshimiwa Naibu Spika, mazao ya biashara ni muhimu sana kwa uchumi wa nchi yetu. Je, wataalam wetu wanawashauri nini Watanzania juu ya mazao ya pamba, chai, katani, miwa, pareto, kokoa, karafuu, kahawa, ngano na mpira. Nina maswali kama ifuatavyo:-

(i) Ni sehemu zipi za nchi yetu zinazofaa kwa mazao hayo?

(ii) Serikali ina mpango gani madhubuti wa kuhakikisha kuwa mazao hayo yanalimwa kwa kiasi kikubwa hapa nchini?

Mheshimiwa Naibu Spika, China ni miongoni mwa nchi zenye kilimo cha mpangilio maalum na mapinduzi ya kijani, maswali.

(i) Je, Serikali inajifunza nini kutoka China?

(ii) Je, ni kwa nini Serikali isipeleke wataalam wetu China ili watoe utaalam wao katika sekta ya kilimo hapa nchini?

Mheshimiwa Naibu Spika, mpango wa Kilimo Kwanza unafananaje au kutofautianaje na mapinduzi ya kijani ya nchi ya China? Tunajifunza nini kwa ufanano au utofauti huo? Serikali ina mpango gani wa kuanzisha kilimo cha mkataba hususani katika mazao ya biashara hapa nchini?

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, naunga mkono hoja.

**MHE. HENRY D. SHEKIFU:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu wa kwanza uelekezwe kwenye kilimo cha mboga na matunda. Ili wakulima wadogo wa mboga na matunda waweze kunufaika na kilimo hicho, ni lazima wawezeshwe kwa kupata pembejeo za kilimo ikiwemo viwatilifu. Juhudi za wananchi kuanzisha *green house* kwa kusaidiwa na Serikali zimeonesha mafanikio, lakini mpango huo ni ghali sana. Kwa makusudi Serikali ianzishe mpango wa kusaidia vikundi vya vijana katika mashamba yao madogo madogo, wapatiwe pembejeo, wawezeshwe kulima mbogamboga na matunda yenye ubora wa kuuzwa nchi za nje kwa ushindani na nchi jirani ya Kenya na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, mpango wa *ASDP* bado haujaeleweka sana kwa watendaji hasa Maafisa Ugani. Elimu kwa wakulima na viongozi wa vijiji haijafika kikamilifu. Serikali kwa dhati na kwa haraka watafute wataalam wa kuandika michanganuo ya miradi ya umwagiliaji ili fedha za mpango

huu zisikae bure au kupotea. Kama inavyoonekana katika Hotuba ya Mheshimiwa Waziri, maeneo ya milimani kama Lushoto tungewezeshwa kujenga mifereji na mabwawa madogo madogo. Maafisa Ugani wapimwe kwa ubunifu wao na kuendeleza mipango ya kilimo vijijini. Kwa sasa maafisa hao wamejisahau kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mpango wa umwagiliaji, naiopongeza Serikali kwa kuamua makusudi kuongeza juhudi katika kilimo cha umwagiliaji ili kuongeza uzalishaji wa sukari, mahindi na mchele. Naomba Serikali iwe macho na wawekezaji wakubwa kupitia mpango wa "*Big Results Now*". Tumejifunza kutokana na hasara kubwa tuliyopata kutokana na udanganyifu wa ununuzi wa mashamba ya mkonge Mkoani Tanga na wawekezaji kutokomea na kuyatelekeza mashamba hayo hatimaye Taifa kupata hasara kubwa. Naomba maelekezo ya kina yatolewe kuhusu mpango wa "*Big Results Now*" katika kilimo cha kukuza mazao hayo. Tujifunze kwa matendo ya kina Chavda.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mpango wa kupima ardhi; Wizara ya Kilimo kwa kushirikiana na Wizara ya Ardhi kwa makusudi zitafutwe fedha, mpango wa matumizi bora ya ardhi vijijini pamoja na utoaji hati miliki ufanyike ili maeneo ya kilimo yatambuliwe na yalindwe. Kwa sasa maeneo mazuri ya kilimo hufanyiwa shughuli tofauti na kilimo. Wananchi pia wakipatiwa hati miliki za kimila wataweza kukopesheka na kuongeza uzalishaji katika mashamba yao. Kwa kufanya hivyo, umaskini utapungua sana na utatoweka.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

**MHE. ANASTAZIA J. WAMBURA:** Mheshimiwa Naibu Spika, malengo na mipango ya 2012/2013 yalitekelezwa kwa kuzingatia programu mbalimbali kama Malengo ya Milenia, *CAADP, TAFSIP*, Dira ya Maendeleo ya Miaka Mitano, Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo (*ASDP), CRMP* na yote izingatie sana masuala ya jinsia hasa walemavu, vijana na wanawake ili kuyainua makundi haya ya jamii kiuchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, idadi ya wanawake walioko kwenye mashamba darasa yaliyoanzishwa hairidhishi kwani ni asilimia arobaini (40%) tu, je, tatizo ni nini? Naiomba Wizara iondoe vikwazo vya ushiriki wa wanawake katika mashamba darasa kwa kushirikiana na Wizara ya Maendeleo ya Jamii. Ikumbukwe kwamba nguvu kazi zaidi ya asilimia hamsini (50%) katika kilimo inatoka kwa wanawake, hivyo ni vyema wapatiwe teknolojia za kilimo kwa asilimia zaidi ya hamsini (50%) kwani ukimuelimisha mwanamke umeelimisha jamii nzima.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kitabu cha hotuba imeonekana kwamba hadi Desemba, 2012 takribani shilingi bilioni 25.8 zilizokuwa zimetengwa kwa ajili ya umwagiliaji zilikuwa hazijatumika. Kwa kweli sababu zilizotolewa haziridhishi, kwani si kweli kwamba Serikali haikuzibaini sababu hizi mapema ili iweze kuzitafutia ufumbuzi. Napenda niongeze sababu nyingine kwamba ni watendaji kukosa ubunifu kufanya kazi kwa kukariri na kwa maeneo mengine ni kutothamini ubunifu wa wakulima. Nalisema hili kwani nimeshuhudia wakulima waliobuni mradi wa umwagiliaji katika eneo fulani lenye ukame lakini kuna chanzo kikubwa cha maji, wanalo tenki kubwa na pampu ya maji. Walichopungukiwa ni mabomba kwa ajili ya kusambaza shambani lakini wamepigwa danadana kwa miaka mitano sasa. *ASDP* haijawasaidia wala hawajaambiwa tatizo ni nini.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Serikali kwa kuanzisha program ya vijana. Tufike mahali sasa Serikali itekeleze program hii katika maeneo mengi zaidi lakini ianzishe na program ya wanawake katika maeneo mbalimbali ya nchi yetu. Kule Mtwara kuna vikundi vya wanawake wanalima ufuta na karanga Wilayani Nanyumbu, uyoga Wilayani Tandahimba-Masasi na Mtwara-Mikindani pamoja na kilimo cha mananasi Mtwara Vijijini, naomba Wizara iwasaidie kupitia *ASDP*. Katika kilimo cha uyoga tatizo kubwa ni ujenzi wa mabanda na mtaalam wa kutengeneza mbegu za uyoga kwani mama mmoja aliyegharamiwa kupata utaalam huu alifariki mwaka 2012.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie kwa kuishukuru Wizara kwa kuwapatia wananchi wa Kata ya Mahurunga mradi wa mashine ya kukoboa na kusaga kwa kufuata swali nililowahi kuuliza Bungeni. Wananchi wanashukuru sana kupata mashine ya kukoboa mpunga na kusaga nafaka kupitia *ASDP* kwani sasa wamepunguziwa mzigo wa kazi wa kutwanga kwa mikono na pia bei ya mchele imepungua kwani wanalima hapo hapo katika eneo lao na kukoboa kwa mashine yao ya karibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. MARYAM SALUM MSABAHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, wakulima wamekuwa wakilima kwa taabu na kupata pembejeo kwa tabu, cha kushangaza wafanyabiashara wamekuwa wakiwafuata kwenye mashamba yao. Wafanyabiashara hao wananunua mazao kwa bei rahisi (kuwakandamiza wakulima) kwa mfano wakulima wa vitunguu. Wafanyabiashara hao wakinunua vitunguu hivyo wanajaza rumbesa la vitunguu, gunia moja yanatoka magunia mawili ya vitunguu. Serikali haioni huku ni kumkandamiza mkulima? Ni lini Serikali itapitisha sheria ambayo inamnufaisha mkulima? Ni lini Serikali itachukua hatua madhubuti za kuwadhibiti hao wafanyabiashara ambao wanawanyonya wakulima? Naishauri Serikali kuweka kiwango maalum cha ujazo wa magunia kwa mfano gunia la ujazo wa kilo mia (100Kg) lisijazwe mpaka likawa gunia la ujazo wa kilo mia mbili (200Kg).

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna kero nyingi kwa Mikoa ambayo wanalima mahindi kwa wingi. Hawana soko la uhakika, hawana maghala ya kuhifadhi mazao yao. Msimu wa mahindi wanakuwa wakihangaika sana. Serikali haioni umuhimu wa kujenga viwanda vidogo vidogo vya *SIDO* vya (kusaga na kukoboa) na kuepuka mahindi haya kuuzwa nchi jirani kwa njia ya magendo. Vilevile vijana wanaweza kupata ajira kupitia viwanda hivi. Kuna baadhi ya Mikoa ina ukame wa njaa wataweza kunufaika kupitia Mikoa hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo lingine ambalo linaikumba Mikoa inayolima matunda kwa wingi msimu wa matunda, matunda hayo yamekuwa yakiiva na kuharibika mashambani. Hii inasababisha hasara kwa wakulima. Vilevile wakulima hao hawana soko la uhakika la kuuza matunda yao na hii inachangia wakulima kubaki maskini. Ni kwa nini Serikali isishirikiane na Shirika la Viwanda vidogo vidogo *(SIDO)* na kujenga viwanda vidogo vidogo vya usindikaji matunda? Wanaweza kutengeneza *juice* kwa kutumia matunda hayo. Ili kuwasaidia wakulima, viwanda hivyo vitachangia katika kupunguza umaskini kwani vijana wataweza kupata ajira kupitia viwanda hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la wakulima wa kahawa; kuna baadhi ya Mikoa ambayo inalima kahawa kwa mfano Mkoa wa Mbeya, na kadhalika. Wakulima wa zao la kahawa wamekuwa hawana soko la uhakika, baadhi ya wakulima wanauza kahawa hiyo kabla haijakauka na wengine kukata tamaa ya zao hili la kahawa na kuamua kung'oa kahawa hiyo na kupanda mazao mengine. Je, Serikali ina mikakati gani kuhakikisha inawatafutia wakulima wa kahawa soko la uhakika na kupata elimu ya kutosha kuhusu zao hili la kahawa?

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la vijana kutoka vijijini na kukimbilia mjini; naiomba Serikali iangalie vijana ambao wako vijijini ambao wanajishughulisha na kilimo. Vilevile Serikali iweze kuwawezesha vijana kwa kuwapatia mikopo yenye masharti nafuu, hii itasaidia kuepusha baadhi ya vijana kukimbilia mjini. Serikali ihakikishe hizi benki za wakulima zinafika vijijini na masharti ya riba yawe nafuu ili kuwanufaisha wakulima.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kilimo cha kisasa; ni takribani miaka hamsini ya uhuru kwa kweli zana za kilimo zimekuwa duni hasa kwa wanawake wanaoishi vijijini pamoja na vijana. Wamekuwa wakitumia jembe la mkono na kuteseka sana. Ni lini Serikali itatoa zana za kisasa kwa wanawake ambao wanateseka kulima na jembe la mkono mpaka leo?

**MHE. PROF. KULIKOYELA K. KAHIGI:** Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo kubwa linalokabili kilimo Tanzania ni mabadiliko ya tabia nchi ambayo tangu yaanze kutokea yameathiri misimu ya mvua iliyokuwa imezoeleka toka zama na zama. Kutokana na mabadiliko haya, tunakuta sehemu nyingi ama hazipati mvua za kutosha ama hata zikinyesha zinanyesha nje ya msimu na mara nyingine (kama inavyotokea sasa hivi huko Shinyanga) zinakuwa nyingi kiasi cha kuharibu mazao na hata kusababisha mafuriko.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa tatizo la mabadiliko ya tabia nchi litaendelea kuwepo kwa muda mrefu, Serikali ina mpango gani wa muda mfupi/wakati/ mrefu wa kuwaelimisha wananchi kuhusu mabadiliko haya na athari zake na njia bora za kupambana nayo? Waziri, katika hotuba yake, ukurasa wa 74-75, anasema Wizara "inaandaa mkakati na mpango kazi wa kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabia nchi katika Sekta ya Kilimo". Je, mkakati na mpango kazi huu utakamilika lini na utaanza kutekelezwa lini?

Mheshimiwa Naibu Spika, njia pekee ya uhakika ya kuhakikisha kuwa kilimo kinaendelea kwa tija ni kwa Serikali kuwa na mkakati wa kitaifa wa umwagiliaji ambao utatekelezwa hatua kwa hatua ili hatimaye nchi yetu iondokane kabisa na kilimo kinachotegemea mvua. Miradi iliyopo haitoshi kabisa kwa kuwa ni michache mno. Mkakati na mpangokazi wa umwagiliaji utaandaliwa lini?

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nitajielekeza kwenye matatizo yanayowakabili wakulima wadogo wa Wilaya ya Bukombe. Kwa mujibu wa utafiti nilioufanya katika miaka miwili (2011-2012), matatizo yanayowakabili wakulima wadogo ni haya yafuatayo:-

(i) Wakulima wengi hawana maarifa ya kilimo cha kisasa.

(ii) Ardhi sehemu nyingi imechoka, haina rutuba na wakulima wengi hawajui namna ya kurejesha rutuba ardhini kwa kutumia njia asilia.

(iii) Kutokana na mabadiliko ya tabia nchi, misimu ya mvua ni badilifu na wakulima wengi hawajui kwa hakika lini wapande mazao na wapandapo hawana hakika kama watavuna.

(iv) Maghala yaliyopo hayatoshi. Mathalani, katika maeneo ya Kata ya Namonge ambayo ni maarufu kwa kilimo cha mahindi na muhogo, kuna upungufu mkubwa wa maghala.

(v) Soko lisilo la uhakika wa bei. Tatizo hili linahusu mazao kama pamba na tumbaku.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ina mkakati gani kumsaidia mkulima mdogo kukabiliana na matatizo hayo (maarifa ya Kilimo cha kisasa, ardhi iliyochoka, mabadiliko ya tabia-nchi, upungufu wa maghala na tatizo la soko) na mengine yanayohusu zana bora?

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumalizia kwa kuiomba Serikali iangalie uwezekano wa kuwasaidia wakulima wadogo wa Bukombe na maeneo mengine ya Geita ili wawe wakulima stadi wa alizeti na muhogo (mbegu ya kisasa) ili yawe mazao ya ziada ya biashara. Mazao haya yataondoa utegemezi wa wakulima wa maeneo hayo kwa mazao ya biashara ya pamba na tumbaku.

**MHE. JOSEPH R. SELASINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, tangu zamani tulisema kilimo ni uti wa mgongo wa Taifa. Tena ajira kubwa ya Watanzania ni kilimo. Kutokana na umaskini wa kaya nyingi bado kilimo chetu ni duni. Katika hali hiyo, natoa ushauri kwa Serikali kuimarisha Ushirika. Katika historia ya nchi yetu Vyama vya Ushirika kama *KNCU, NYANZA* na kadhalika wakulima wanachama walipata fursa ya mikopo ya pembejeo na vifaa vya kilimo. Kama tutaimarisha ushirika ni rahisi sana hata kuunda vikundi vya vijana kwa

ajili ya kilimo cha biashara au ugawaji wa pembejeo. Kwa hali hiyo, naishauri Serikali kuweka mkazo kufufua Vyama vya Ushirika vya Msingi kama mkakati maalum wa kuwahudumia wakulima.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ni kilimo cha umwagiliaji. Baadhi ya maeneo katika nchi yamekumbwa sana na mabadiliko ya tabia nchi na kusababisha ukosefu mkubwa wa mvua. Hata hivyo kama *Scheme* mpya zitaanzishwa kwa kujenga mabwawa kwenye maeneo kama Rombo kwa kuhifadhi maji ya mvua hali ya kilimo chetu itabadilika na wananchi wanaweza kulima mwaka mzima bila kutegemea mvua.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, nashauri masoko ya mazao yaimarishwe hasa yale ya mpakani kama Tarakea na Holili, Rombo ili kudhibiti uvushaji holela wa bidhaa usiozingatia Sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile jitihada zifanyike ili mazao yetu yaongezewe thamani ili kudhibiti utoroshaji wa ajira za Watanzania na kuyafanya kuwa na thamani zaidi na kuhifadhiwa kwa muda mrefu zaidi.

**MHE. MUNDE T. ABDALLAH:** Mheshimiwa Naibu Spika, Bwawa la Inara Wilaya ya Tabora Manispaa lilitengewa shilingi 1.059 bilioni. Tumepewa shilingi 344 milioni tu mpaka sasa. Mmwaka huu tumeambiwa tumetengewa fedha na hotuba ya Waziri Mkuu lakini haionyeshi ni shilingi ngapi? Nataka kujua mpango kazi wa Serikali kuhusu bwawa hili la muda mrefu.

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wamejitolea kujenga mifereji na bwawa hilo lilikaguliwa na Wajapani *(JICA)* wamekubali kutusaidia na wamechukua wanakijiji 30 kwa gharama zao kuwapa semina ya kilimo cha mpunga na walitaka pale pawe mfano maana pana uwezo na kutoa gunia 50 kwa heka. Wananchi wa Tabora wanataka kujua msimamo wa Serikali na kujua wanapewa shilingi ngapi?

Mheshimiwa Naibu Spika, tunamwamini Waziri na Naibu kwa kazi yao na uwajibikaji wao. Nategemea ufafanuzi mzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

**MHE. DKT. MARY M. NAGU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nawashukuru Viongozi na Watendaji wa Wizara ya Kilimo na Chakula kuliweka Bwawa la Gidahababieg katika Kitabu cha Hotuba kwa mara ya pili kwani Bwawa hilo lilitajwa vilevile katika Hotuba ya Bajeti ya mwaka jana. Ninachoomba sasa ni utekelezaji uanze. Halmashauri ya Wilaya ya Hanang ilitayarisha *Project Writeup* kwa ajili ya Bwawa hilo. Ikiwa kuna mambo ambayo Wilaya inatakiwa kufanya ili kuanza ujenzi wa Bwawa uanze mara moja ijulishwe. Eneo la Wilaya ya Hanang lipo katika volcano hivyo maji ni ya shida. Naomba Waziri aeleze wakati wa kuhitimisha bajeti yake lini ujenzi wa Bwawa utaanza, itawapa matumaini.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru.

**MHE. KOMBO KHAMIS KOMBO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kauli ya Serikali kuhusu suala zima la Kilimo haliendani na matendo kwani kauli zote zilizotolewa kuhusiana na kilimo zimefeli na kamwe hazijawasaidia wakulima mfano Kilimo ni Uti wa Mgongo wa Taifa na Kilimo Kwanza. Sera hizi zimefeli na kubakia kuwa kumbukumbu kwenye mawazo na masikio ya Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, huwezi kuimarisha kilimo kwa kutumia vijembe vya mkono jambo ambalo limepitwa na wakati kutokana na sababu zifuatazo:-

(i) Chakula hakiwezi kutosheleza kutokana na ongezeko la idadi ya watu.

(ii) Ardhi kuchakaa kwa hali ya hewa joto duniani.

(iii) Ukosefu wa zana za kilimo za kisasa.

(iv) Serikali kutotilia maanani suala la kilimo kwa vitendo.

(v) Bajeti ndogo ambayo haikidhi katika shughuli za kilimo.

(vi) Tatizo la uhifadhi wa vyanzo vya maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, niliposema kwamba Sera ya Kilimo Kwanza na ile ya Kilimo ni Uti wa Mgongo wa Taifa ni kwamba Serikali imeshindwa kabisa kukiendeleza kilimo kwa vitendo bali inaendesha sekta hii kwa maneno. Umefika wakati sasa Serikali ikubali kuendeleza sekta hii kwa vitendo ili tuondokane na tabia ya uagiziaji wa chakula kutoka nje. Hili litawezekana endapo Serikali itakubali kuleta zana za kisasa za kilimo lakini vilevile itatunza vyanzo vya maji ambavyo vitasaidia katika umwagiliaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kukuza shughuli za kilimo badala ya kuendeleza kauli ya Kilimo Kwanza tutengeneze au tutumie Sera ya (Maji Kwanza) ili kuelekea kwenye kilimo chenye tija. Tutakapoendeleza sera hii, tutaanzisha ujenzi wa mabwawa ya maji yenye kina kirefu ambayo yatawezesha kuleta mapinduzi ya kilimo, kilimo ambacho kitaweza kutosheleza mahitaji ya wananchi na hata kupeleka nje na nchi jirani na hatimaye kukuza pato la Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni vyema kabisa wale wawekezaji wazalendo ambao wanataka kuwekeza katika sekta ya kilimo na ambao wamekuwa wakitoa mchango mkubwa kwa Taifa, wapewe fursa ya kuwekeza katika sekta hii ili kutoa nafasi za ajira kwa vijana wetu. Mfano, Said Salim Bakhresa ambaye aliomba kuwekeza katika Mkoa wa Rukwa ni mwekezaji mzalendo ambaye ameweza kulisaidia Taifa juu ya kuwapatia ajira vijana wa kitanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, kilimo kama kilimo ni ajira ambayo inamwendeleza mwananchi kimaisha, kielimu na kiakili pale ambapo kilimo hicho kitakuwa kinampatia

mavuno ya kutosha au mazao ya kutosha ambayo ataweza kuuza na kupata mahitaji mengine ya msingi.

**MHE. ALI KHAMIS SEIF:** Mheshimiwa Naibu Spika, nchi yetu imetangaza Sera ya Kilimo Kwanza, katika mkakati huo, je, suala la mbegu za mazao katika suala zima la kujitegemea limefikia wapi. Haifanani kwa sasa na miaka 50 tokea upatikane uhuru kuwa bado nchi yetu haijitoshelezi kwa mbegu. Ninaomba Waziri katika majumuisho yake anieleze kuna mkakati gani wa kuweza kujitosheleza kwa mbegu.

Mheshimiwa Naibu Spika, bado suala la umwagiliaji halijapewa uzito hasa ukitilia maanani na mabadiliko ya tabia ya nchi. Kilimo kwa wakati huu hatuwezi kupata mafanikio bila ya kuwa na kilimo cha umwagiliaji. Ongezeko la ekari za umwagiliaji kwa kila mwaka hazikidhi kuleta mapinduzi ya kilimo hapa nchini. Serikali imejipanga vipi katika kuhakikisha kuna ongezeko kubwa la ekari za umwagiliaji?

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna mgongano mkubwa wa maslahi baina ya kilimo na ufugaji. Hali hiyo imefikia hatua ya kuhatarisha amani baadhi ya maeneo katika nchi hii kwa sababu Wizara hii ni mdau kama ilivyo Wizara ya Mifugo na Uvuvi, imechukua hatua gani ili kuhakikisha hakuna mwingiliano wa maeneo ili kuepuka wakulima na wafugaji kupigana?

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inahimiza wananchi wakuze kilimo na katika hilo wananchi wanajitahidi. Tatizo lililopo, mazao yanapoongezeka wananchi au tuseme wakulima huzuiliwa kuuza mazao yao hususani chakula wanapotaka. Hili huwa haliwasaidii wakulima bali ni kuwavunja moyo wakulima. Haiwezekani wakulima wakauziwa pembejeo kwa bei wanazotaka wauzaji wenyewe halafu wakulima wakazuiliwa kuuza mazao yao wanapotaka ili wapate bei nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeanzisha Mfuko wa Mikopo ya Pembejeo ili kuwawezesha wakulima kupata

mikopo inayohusiana na kupata pembejeo za kilimo. Serikali tayari imeshatoa mikopo hiyo lakini urejeshwaji wa mikopo hiyo inasuasua hali ambayo ndiyo tabia ya baadhi ya wananchi wetu kutojali mikopo inayotolewa katika kuyalipa madeni hayo. Serikali ina mkakati gani wa kulipwa madeni hayo ili kuhakikisha mfuko huo haufi?

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

**MHE. RASHID ALI OMAR:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa, namshukuru Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema na Ukarimu kwa kuniwezesha kuwepo katika Bunge lako Tukufu ili niweze kuchangia bajeti hii ya Wizara ya Kilimo kwa njia ya maandishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kilimo ndio uti wa mgongo wa uchumi na maendeleo ya nchi zote maskini duniani na hata zile nchi tajiri ambazo humiliki viwanda mama. Nchi yetu ni miongoni mwa nchi maskini, kwa hiyo, naomba niishauri Serikali kama ifuatavyo:-

(i) Iandae mbinu mbadala katika kilimo chetu.

(ii) Iachane na kilimo cha wakulima mmoja mmoja kwa kutumia jembe la mkono.

(iii) Tujiandae na mashamba makubwa ya ushirika.

(iv) Kiwe kilimo cha umwagiliaji kwa uhakika na sio kubahatisha, mbegu bora, pembejeo.

(v) Kiwe kilimo kinachofanyiwa tafiti mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, asilimia 85 ya Watanzania wanaishi vijijini na hutegemea kilimo katika maisha yao ya kila siku. Hata watu wanaoishi mjini hutegemea mazao ya kilimo kutoka vijijini kwa sehemu kubwa ya mahitaji yao ya chakula.

Mheshimiwa Naibu Spika, inasikitisha kwamba Serikali haijasimamia rasmi juhudi za wakulima wetu katika baadhi ya maeneo ya Tanzania, wanayo mazao ya ziada, lakini hawana masoko ya kuuzia mazao yao kwa mfano Morogoro wamezalisha mpunga mwingi lakini wakulima wanalalamikia soko la kuuzia mazao yao hawana. Jambo la kusikitisha zaidi Serikali inaagiza mchele nje ya nchi Thailand na mchele wenyewe mbovu hata sio wa kiwango. Maeneo ya Songea mahindi ya wakulima yamerundikwa, wananchi hawana masoko ya uhakika.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niishauri Serikali kupitia Wizara ya Kilimo ijiandae rasmi kutoa fursa ya uwekezaji katika kilimo chetu na kusimamia na kuweka miundombinu bora vijijini kwenye maeneo ya kilimo kama vile maji, umeme, viwanda vya usagishaji pamoja na barabara.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba tujikumbushe Wosia wa Baba wa Taifa uliosema hivi: “Ili tuendelee katika nchi yetu tunahitaji mambo yafuatayo; Watu, Ardhi, Siasa safi na Uongozi bora”. Watu tunao vijijini na ardhi kubwa tunayo. Je, kama ardhi hii aliyotumilikisha Mwenyezi Mungu hatuishughulikii ipasavyo, je, uongozi bora na siasa safi itakuwepo?

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kwa heshima Serikali ijisahihishe katika suala zima la kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

**MHE. ANNAMARYSTELLA J. MALLAC:** Mheshimiwa Naibu Spika, nianze na upatikanaji wa pembejeo. Upatikaji wa pembejeo katika mwaka wa 2012/2013, mahitaji ya mbolea yalikuwa tani 452,200, mbegu ilikuwa tani 60,000 na madawa tani 328,586. Hadi kufikia Machi 2013, tani 240,350 za mbolea na tani 30,443 za mbegu bora zilifikishwa kwa wakulima. Ni kweli Serikali inaonyesha ni jinsi gani inavyotekeleza huduma za kilimo karibu na wananchi, lakini basi kuna watendaji wanaoikwamisha Serikali katika

kusambaza huduma hii kwa wakulima, kwani nchi nzima kilio ni kimoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, kilio hiki cha nchi nzima ni kwamba pembejeo zimekuwa hazifiki kwa wakati mfano mbolea, mbolea ya kupandia inafika wakati mkulima ameshapanda mazao yake tayari. Mbolea ya kukuzia inafika wakati mkulima anakaribia kuvuna mazao ambayo tayari yamekomaa bila rutuba yoyote na mazao mengine yameharibika kabisa na kusababisha kipato duni ambacho hakikidhi. Ili mkulima arudi kwenye nafasi nzuri na kuepuka njaa na umaskini mkubwa anaoupata mkulima kwa ajili ya kusubiria pembejeo kutoka kwa Wakala wa pembejeo ambazo zinatolewa kiubaguzi toka kwa Mawakala, naishauri Serikali katika kusambaza pembejeo, isitumie Mawakala tena, bali iruhusu wafanyabiashara kununua na kuweka kwenye maduka na kila mkulima anunue kwa wakati na kwa bei nafuu ambayo imepangwa na Serikali yenyewe ili kuondoa lawama kubwa inayobebeshwa Serikali kuwa pembejeo zinatolewa kwa ubaguzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imebuni mfumo mpya usambaji wa pembejeo katika msimu 2013/2014 ambapo wakulima kupitia vikundi na Vyama vya Ushirika watapata mikopo ya muda mfupi na yenye riba nafuu kwa ajili ya kununua pembejeo.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala hili la mfumo mpya Serikali ingeufikiria kwa kina, Wabunge tumehamasisha sana wakulima kuunda vikundi kama hivi lakini kikwazo kipo zaidi kwenye mabenki. Tunaomba Kamati zote na Wizara zinazohusiana na masuala ya kilimo kushirikiana na wakae pamoja na kulijadili suala hili la mfumo mpya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu zana za kilimo; pamoja na jitihada zote za Serikali kuendelea kuhimiza uingizaji wa trekta nchini, bado wakulima wengi nchini wanatumia jembe la mkono, ni wachache wanaotumia trekta kama wawekezaji wenye mashamba makubwa na pesa kubwa. Kwa mkulima wa kawaida bado ni kitendawili.

Serikali ikae ipange namna ya kumsaidia mkulima wa kawaida namna ya kumkopesha trekta na namna ya ulipaji angalau kwa awamu huku Maafisa Kilimo wakiwasimamia wakulima.

**MHE. MARIAM S. MFAKI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wa Wizara kwa maandalizi ya Hotuba hii ya Wizara na kufafanua mambo mengi. Naomba kuchangia machache.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Mkoa wa Dodoma hatuna zao maalum la biashara ni kwa nini Serikali haijafanya utafiti ili Mkoa nao upate zao la uhakika na wananchi wanufaike kwa kuongeza kipato chao?

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali iliahidi kutengeneza bwawa la Kwamtoro ambalo linaweza kusaidia kuendesha kilimo cha umwagiliaji, je kazi hii itaanza lini?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa wananchi wameelewa umuhimu wa kulima kwa matrekta na bado yanahitajika, hivyo Serikali ijitahidi kuyatafuta ili wananchi waendelee kuyapata kwa mkopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii asilimia mia kwa mia.

**MHE. AMINA M. MWIDAU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nimechangia kwa kuongea sikumaliza mchango wangu kutokana na muda, naomba niwasilishe mchango wangu kwa maandishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu hali ya chakula, kutokana na utafiti uliofanywa na Wizara hii ya Kilimo ambao uliitwa *"Comprehensive Food Security and Nutrition Assessment Report"* iliyokamilika Oktoba 2012 ilionyesha kuwa mwaka wa 2012/2013, Tanzania ingeweza kufikia asilimia 113% katika kiwango cha kujitosheleza chakula yaani *"Food Self*

*Sufficiency Ratio (SSR)*. Takwimu za taarifa hiyo ni kama Mheshimiwa Waziri alivyoziainisha kwenye hotuba yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata baada ya changamoto nyingi sana wanazopata wakulima hasa wadogo, Tanzania bado wakulima waliweza kuvuna 13.6 milioni MT kwa mazao ya nafaka na chakula ambacho si cha nafaka, wakati mahitaji ya chakula kwa mwaka 2012/ 2013 kwa Watanzania wote yalikuwa ni 11.99 milioni MT. Hii inaonyesha wazi kuwa tume-*overproduce* katika nchi yetu. Ukiangalia kwenye *Global Hunger Index*, 2012, Tanzania ilikuwa nchi ya 54 kati ya nchi 79 yaani tukitoka sisi ni Burundi wakati sisi tuna *political stability*.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Waziri akifanya majumuisho anipe majibu ya masuala yafuatayo:-

(1) Ni kwa nini Tanzania tunashika nafasi hiyo na bado tuna matatizo ya chakula mpaka inabidi kuomba chakula nje ya nchi wakati takwimu zinaonyesha kuwa tuna *overproduce?*

(2) Je, ni kwa nini mfumuko wa bei za chakula haushuki, sasa hivi ni asilimia 25.3 wakati tuna *overproduce?*

(3) Je, Serikali ina mpango gani (Mpango Mkakati) wa kupunguza mfumuko wa bei za chakula?

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo hili la mfumuko wa bei nadhani ndio sababu watu wengi wanakosa chakula na madhara makubwa yanawapata watoto *(Malnutrition).*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia kwenye *Demographic Health Survey, 2012* inaonyesha kuwa zaidi ya 50% ya watoto wote waishio Dodoma wana *malnutrition*, hii ni hatari.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, nimalizie kwa kusema kuwa ukuaji katika sekta ya kilimo katika pato la Taifa unapanda na kushuka na ili kilimo kitoe mchango

unaotakiwa katika vita dhidi ya umaskini kinapaswa kukua kwa zaidi ya 10% kwa mwaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kupungua kwa mchango wa sekta ya kilimo kwenye pato la Taifa, kilimo kina nafasi ya kipekee katika uchumi na maendeleo ya Taifa kutokana na ukweli kwamba zaidi ya asilimia 75 ya Watanzania wanategemea kilimo. Hata hivyo, uchambuzi uliofanywa katika nchi nyingi umethibitisha kuwa ukuaji wa pato la Taifa unaotokana na sekta ya kilimo una uwezo wa kupunguza umaskini zaidi ya mara mbili ya ule unaotokana na sekta nyingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nipendekeze kuwa; kwa kuwa Watanzania wameajiriwa na sekta ya kilimo, ni vyema Wizara hii ipewe kipaumbele kinachostahili ili kuweza kuwahakikishia wakulima na Taifa usalama wa chakula na kipato.

**MHE. ALPHAXARD K.N. LUGOLA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninayo mambo machache kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza itakumbukwa kuwa mwaka jana niliomba Mwongozo juu ya Sera na Sheria ya Mufilisi kwa Vyama vya Ushirika vinavyofilisika. Niliiomba Serikali kushughulikia suala la kilichokuwa Chama Kikuu cha Ushirika Mkoa wa Mara yaani *Mara Cooperative Societies Union* ambacho kimekuwa chini ya Mufilisi hadi leo ni miaka 18 umri wa Mtanzania kupiga kura. Mitambo katika viwanda vinne vya Kibara, Ushashi, Mugango na Tarime imeng'olewa na sehemu kubwa ni kuuzwa vyuma chakavu. Aidha, viwanda vingine vimekodishwa kwa Makampuni binafsi zaidi ya miaka 10. Je, ni ufilisi gani huu usio na kikomo kwani wanaushirika wana hamu ya kuendeleza ushirika wao. Naomba maelezo juu ya huu mustakabali.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili ni namna ambavyo Serikali inavyowachanganya wakulima wa pamba juu ya kilimo cha mkataba. Nasema kuwachanganya wakulima kwa sababu kwa upande mmoja wanahimizwa na

kuhamasishwa na Serikali wawe na ushirika na wakati huohuo wanahimizwa na kuhamasishwa waunde vikundi vya wakulima ndani ya kilimo cha mkataba. Kwa maoni yangu, hii ni kuwachanganya wakulima kwani kuunda vikundi vya wakulima kwangu mimi ni aina nyingine ya ushirika. Naomba suala hili Serikali iwe na msimamo wa namna gani bora ya kuwasaidia wakulima.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu ni kutelekezwa kwa miradi ya kilimo katika Jimbo la Mwibara ambayo ingeweza kupunguza tatizo la chakula ambalo limetufanya tuwe ombaomba. Zaidi ya shilingi milioni tisini zilitumika kuchimba lambo katika Kijiji cha Nansimo ili litumike katika kilimo cha mpunga na mahindi lakini lambo halitunzi maji kwani lilichakachuliwa na kutelekezwa na hivyo fedha za umma zimepotea. Nini kauli ya Serikali?

Mheshimiwa Naibu Spika, pia lambo la Kijiji cha Namhula ambalo lilitumia zaidi ya shilingi milioni sabini kwa ajili ya kilimo cha mpunga lakini limechakachuliwa na fedha zimepotea bure. Nini kauli ya Serikali?

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, wananchi wa Mwibara wana ardhi nzuri ya kilimo, wanachohitaji ni mradi mkubwa wa umwagiliaji, nini kauli ya Serikali juu ya kupatiwa mradi?

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, naunga mkono hoja.

**MHE. CYNTHIA H. NGOYE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninawapongeza Mawaziri wa Kilimo kwa kazi kubwa wanayoifanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa mchango wangu kwa maoni machache kama ifuatavyo:-

(a) Kutokana na umuhimu wa zao la chai kama zao la biashara hapa nchini, napendekeza Serikali ifikirie kutoa ruzuku ya mbolea ili wakulima nao wachangie kwa fedha kidogo kama inavyofanyika kwa mazao mengine. Kwa njia

hii, mkulima wa chai naye atapata unafuu wa kipato. Hali ya wakulima wa chai kimapato imeendelea kuwa duni kila mwaka.

(b) Kwa kuwa wakulima wa Wilaya ya Rungwe wameitika wito wa kulima zao la parachichi zilizoboreshwa, nashauri Serikali ianze kuwasaidia wakulima hao kwa kuwapatia wataalam watakaowaelekeza njia bora za kilimo hicho na kuwatafutia masomo nje kuliko kutegemea utaalamu wa wakulima wakubwa ambao hawatoshi.

(c) Usambazaji wa mbolea bado ni kikwazo kikubwa kwa wakulima wengi hasa kwa maeneo ambayo ratiba za kilimo ni tofauti na maeneo mengine ambayo msimu wa mvua unaanza Novemba. Mfano ni Wilaya za Rungwe, Mbeya Vijijini, Makete na Kilolo. Maeneo haya hayapelekewi mbolea ya kupandia kwa wakati na hivyo kuwasababishia kupata mavuno kidogo. Wizara ipange wataalam maalum watakaoratibu kalenda za kilimo kwa kila Kanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya ushauri huo, naunga mkono hotuba hii ya Wizara ya Kilimo.

**MHE. RAMADHANI HAJI SALEH:** Mheshimiwa Naibu Spika, kilimo ni uti wa mgongo. Usemi huu unadhihirisha kuwa kama tukijikita vizuri katika sekta hii ya kilimo basi uchumi wetu utakuwa na wananchi watafaidika na mazao ambayo watalima.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali bado haijawekeza katika sekta ya kilimo kwani ardhi ambayo tunayo hapa nchini bado haijatumika vizuri yaani ni robo moja ambayo inalimwa katika nchi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kilimo ambacho tunatumia hapa nchini hatuwezi kupiga hatua nzuri. Kilimo ambacho tunaweza kupiga hatua ni kilimo cha umwagiliaji. Kilimo hiki kitamwezesha mkulima kuweza kulima kila mara na kuweza kupunguza malalamiko ya mvua hakuna.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ijikite katika kilimo cha umwagiliaji na mfumo huu ni rahisi kutokana na mito mingi, maziwa mengi basi tuyatumie maziwa hayo kwa ajili ya kumwagilia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kilimo kizuri ndicho kinachotoa ajira katika nchi yetu, vijana wengi wanakimbilia mjini kutokana na kukata tamaa huko vijijini na kama Serikali itawekeza katika kilimo zaidi basi vijana wengi watabaki vijijini ili kuendeleza kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja.

**MHE. UMMY A. MWALIMU:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii na ningependa kumpongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri kwa kusimamia vyema utekelezaji wa Sera na Mipango mbalimbali ya nchi yenye lengo la kuimarisha ukuaji/uwekezaji katika kilimo na kuwepo usalama wa chakula.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo ningependa kupata maelezo ya Wizara kuhusu je, kuna mikakati gani mahususi ya Wizara inayolenga kuinua/kuboresha ushiriki wa wanawake katika kilimo?

Mheshimiwa Naibu Spika, kilimo ndio maisha ya Watanzania hasa wanawake walio vijijini. Takwimu zinaonyesha kuwa zaidi ya asilimia 80 ya wanawake vijijini wanajihusisha na kilimo hasa kilimo cha uzalishaji wa chakula.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni ukweli usiofichika kuwa wanawake wengi wanaojihusisha na kilimo wanakabiliwa na changamoto mbalimbali kama vile kukosa kumiliki ardhi (kutokana na mila na desturi kandamizi); kukosa zana za kilimo za kisasa, pembejeo na teknolojia rahisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati Wizara imeonyesha uwepo wa mpango wa kuwezesha vijana kushiriki katika kilimo, ninasikitika kuona kuwa hakuna jitihada kama hizo

zinazolenga wanawake, je, ni kwa nini? Hivi Wizara haitambui nafasi (muhimu) ya wanawake katika kuhakikisha uwepo wa chakula? Ni kwa nini Wizara haitoi kipaumbele kwa wanawake wakulima ambao ni zaidi ya nusu ya wakulima wadogo nchini?

Mheshimiwa Naibu Spika, ni wakati muafaka sasa Wizara nayo ikaweka mipango/jitihada mahsusi zinazolenga kuinua/kuboresha ushiriki wa wanawake katika kilimo. Napongeza jitihada za mashirika kama *Oxfam, Care International na World Vision* kwa kufanyia kazi suala hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. DKT. KEBWE S. KEBWE:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa vile wakulima ni takribani asilimia 80 ya watanzania lakini bado kilimo chao ni duni na mikopo haina uhakika, kwa nini wakulima wasipewe mazingira mazuri ya kilimo ili mikopo iwe nafuu? Mfano Wilaya ya Serengeti ni mkulima (mtu) mmoja tu aliyekopa trekta, hii haitasaidia kuinua ubora wa kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, watumishi wa ugani walioko vijijini wanateseka mno, hawana makazi mazuri, hawana usafiri wa kuwafikia wakulima ama wafugaji na kadhalika. Hali hii iboreshwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni vizuri taaluma ya kilimo na mifugo ipitiwe upya ili kuoana katika ajira na Wizara husika. Halmashauri zitambue Idara na Wakuu wa Idara za kilimo na mifugo wajitegemee kuliko *DALDO* kusimamia idara mbili tofauti.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa vile kuna hekta zipatazo milioni 29 za kumwagilia lakini ni asilimia nne tu zinazolimwa kwa umwagiliaji. Hali hii inatisha, kilimo cha umwagiliaji kipanuliwe na kuboreshwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, masoko ya mazao ya kilimo yapanuliwe na wakulima wasaidiwe na bei isimamiwe ili

kuondokana na dhuluma kwa wakulima. Hali hii ya masoko duni na bei ya chini iboreshwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, Vituo vya Kuwasaidia Wakulima na Wafugaji *(VTC's)* viboreshwe ili viwe katika hali nzuri ya kutoa huduma ya ugani vijijini ambako ndiko kuna wakulima wengi na wafugaji wengi.

**MHE. DEOGRATIAS A. NTUKAMAZINA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo pamoja na timu yake ya Wataalam kwa kazi nzuri wanayoifanya katika mazingira magumu ya bajeti finyu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kusema naunga mkono hoja. Naomba nijikite katika kukiangalia kilimo kama sekta muhimu ya kutukwamua kutoka katika dimbwi la umaskini na kutufikisha kwenye ile nchi ya ahadi ya uchumi wa kati ifikapo mwaka 2025 kama dira yetu ya maendeleo inavyotutaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, itakapofika mwaka 2025 kilimo kinatakiwa kiwe kimekwisha kuwa *mechanized* na siyo kwa jembe la mkono. Hali ilivyo bado ni ngumu. Kilimo bado ni cha wakulima wadogo wadogo – *Subsistence Agriculture*.

Mheshimiwa Naibu Spika, trekta zilizoletwa zilikuwa ni chache na za bei mbaya kwa wakulima maskini kama wa Wilaya ya Ngara. Ngara hawakununua trekta. Tunahitaji kuondokana na jembe la mkono kama kweli tuko *serious* na mchakato wa kupambana na umaskini.

Mheshimiwa Naibu Spika, bado pia tatizo la pembejeo za kilimo ni kubwa.

(i) Dhana ya kilimo kwanza itaendelea kuwa ngonjera kama hatutaondokana na jembe la mkono na kama wakulima wetu wadogo hawatapewa mbolea na

mbegu bora kwa wakati. Ruzuku ya pembejeo inatakiwa iwafikie wakulima wengi zaidi.

(ii) Serikali inatakiwa kuanzisha kiwanda mfano wa *Ubungo Farm Impliments* ya zamani ili kutengeneza zana zetu za kilimo kuharakisha mchakato wa *mechanization.*

(iii) Uhaba wa Maafisa Ugani ni *real*. Tunahitaji kuhakikisha kila Wilaya iwe na Maafisa Ugani wa kutosha na wanaoishi na wakulima na kuwaongoza katika matumizi ya mbolea na pembejeo nyingine. Maafisa Ugani wanahitaji usafiri wa kuaminika. Wawe na Mashamba Darasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mpango wa *SAGCOT* ni mzuri sana kwa maendeleo ya kilimo kwa ajili ya nchi nzima, tatizo lililopo ni kwa wananchi wa mikoa mingine kama Kagera kuona kwamba, mradi huu wa *SAGCOT* ulioanzishwa na Serikali ni upendeleo wa baadhi ya mikoa na kusahau mikoa mingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wangu ni kwamba, wakati tunakuwa na miradi mikubwa kama ya *SAGCOT*, wakati huo huo Serikali isisahau Mikoa mingine na Wilaya zingine ndogo kama Ngara ambapo pato la Manangara kwa mwaka *(IDP per Capita)* ni kati ya sh. 170,000 hadi 284,000 wakati wastani ya Kitaifa ni sh. 800,000/= na zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hapo hapo ifikapo mwaka 2025 nchi yenye uchumi wa kati – *per capital Income* inatakiwa iwe US$ 3000 na zaidi. Bado miaka 12 kufika 2025. Swali, tutafika wakati mategemeo yetu makubwa ni kilimo?

Mheshimiwa Naibu Spika, maana ya wendawazimu *(Insanity)* ni "kufanya jambo lile lile kwa kutumia mbinu zile zile na kutegemea matokeo tofauti" kwa kiingereza – *"Insanity is to do the same thing over and over again and expect different results".*

Mheshimiwa Naibu Spika, dhana ya Kilimo Kwanza lengo lake ni maisha bora kwa kila Mtanzania, lakini kwa kutumia jembe la mkono, huo ni wendawazimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naelewa sana tatizo la Bajeti finyu inayopewa Wizara ya Kilimo. Serikali sharti ijue vizuri vipaumbele vyake na kuvizingatia na kuelekeza mapato madogo inayoyapata katika vipaumbele hivyo muhimu zaidi ya vingine kama Elimu na Kilimo bila shaka na Nishati. Serikali iongeze Bajeti ya kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, Utafiti ni jambo muhimu sana katika kilimo, upewe fedha zaidi.

**MHE. ABDULSALAAM SELEMANI AMER**: Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote natoa masikitiko yangu makubwa kwa Serikali yetu kutenga fedha chache sana kwenye Wizara hii. Hii ni kwa sababu ya dhana kuwa, kilimo ndio uti wa mgongo kwa asilimia themanini ya Watanzania na dhana ya Kilimo Kwanza pia itafifia.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Wizara hiyo ya Kilimo, Chakula na Ushirika, kwa kweli Watendaji pia wanalalamika kuwa pamoja na bajeti waliyoomba mwaka 2012-2013 kupitishwa pamoja na uchache bado Wizara ya Fedha au Hazina wanachelewa kutuma fedha kwa wakati. Kucheleweshwa huko ndio chanzo cha kudorora kwa miradi na pia kuongeza gharama iwapo pesa hazipatikani kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, nia njema ya Serikali katika mpango wa kugawa pembejeo ilitia doa baya kwa Serikali. Lakini napenda kupongeza mpango huu mpya wa Serikali katika kugawa pembejeo. Nahakikisha kuwa mpango huu utaweza kusaidia sana kuwafikia walengwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitoe rai sasa kwa Wizara juu ya wakulima wa miwa katika Bonde la Ruhembe. Kiwanda cha Kilombelo (K II) iliyo chini ya Kampuni ya Ilovo

ndio tegemeo kwa kupata miwa toka kwa wakulima wa nje *(Outgrowers).*

Mheshimiwa Naibu Spika, wakulima hao wa miwa wanaweza kujimudu kimaisha kutokana na zao hilo la miwa; wakulima hao wa miwa hawana msaada wowote toka Serikalini katika mambo mawili. Kwanza, kuhusu pembejeo hakuna msaada wowote toka Halmashauri ya Wilaya. Katika hotuba ya Waziri ina mpango mzuri juu ya mikopo ya matrekta na pembejeo zingine kwa wakulima. Naamini kwa asilimia mia moja kuwa wangepata elimu au kuelimishwa juu ya mpango huo wa Serikali wangekopa na uwezo wa kulipa wanao.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la pili ni juu ya malipo ya miwa toka kiwandani, kwa kweli haueleweki. Pamoja na malipo ya kawaida kutoeleweka lakini kuna makato mengi sana kiasi cha kufanya mkulima mdogo kuvunjika moyo kwa kulima miwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sana Wizara ya kilimo kupitia Waziri husika kufuatilia na kutia maanani suala la wakulima wa Miwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru.

**MHE. MASOUD ABDALLA SALIM:** Mheshimiwa Naibu Spika, kilimo cha Maua hakijapewa nafasi ya kuendelezwa katika dhana nzima ya MKUKUTA. Inashangaza kilimo kinategemewa na zaidi ya asilimia sabini (70%) ya Watanzania katika kujipatia riziki zao. Kwa nini kilimo hiki kimeachwa na hakipewi nafasi, kwani tukijapanga vizuri katika kilimo cha Maua, wakulima watapata kipato chao cha uhakika na Serikali itapata fedha za kigeni. Nashauri Serikali kuangalia kwa kina jambo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakulima wengi wana malalamiko kutokana na kukosa soko la uhakika kwa mazao yao na hatimaye nchi jirani wanachukua chakula toka

Tanzania, huku sisi tukilia njaa siku zote na Serikali inalifahamu hili, lakini bado hakuna ufumbuzi wowote.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishauri Serikali kupanga mpango mkakati wa mbinu gani wa kuboresha mazao ya wakulima kupata soko la uhakika.

Mheshimiwa Naibu Spika, thamani ya baadhi ya mazao kama korosho unapungua kutokana na kuuza korosho zilizobanguliwa huku Viwanda vya Korosho vimebinafsishwa kwa wawekezaji wa ndani, lakini hadi leo viwanda hivyo havifanyi kazi na yamekuwa maghala. Hivyo, naishauri Serikali kuweza kuwasaidia wamiliki wa Viwanda vya Korosho ili vifanye kazi na wakulima wa korosho waweze kupata bei ya juu ili waondokane na umaskini.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. REBECCA M. MNGODO:** Mheshimiwa Naibu Spika, hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Kilimo haioneshi ni kwa jinsi gani wakulima wadogo wadogo watasaidiwa na bajeti ya Wizara yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakulima wengi wadogo wadogo kwa miaka mingi hawapatiwi elimu kupitia vyombo vya habari kwa mfano redio, jinsi ya kupata /kuzalisha mazao mengi kwa kutumia ardhi ndogo na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile Dira ya Taifa ya Kilimo Kwanza ambayo ililenga kuhakikisha kuwa kilimo cha wakulima wadogo, wa kati na wakubwa kinakuwa cha kisasa na cha kibiashara ifikapo mwaka 2015, mpaka sasa dhana hiyo haioneshi mafanikio yoyote.

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto kubwa ya Kilimo ni jinsi ya kuongeza tija kwa eneo dogo la ardhi kutoa mazao mengi hasa kwa wakulima wadogo wadogo. Tanzania bara ina jumla ya eneo la hekta milioni 29.4 linaloweza kufanya uzalishaji kwa umwagiliaji, lakini ni karibu eneo la hekta 330,000 tu sawa na 1.1% tu ya eneo linalofaa

umwagiliaji ndilo kwa sasa linafanya uzalishaji kwa umwagiliaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara hii ya Kilimo itilie maanani mpango wa umwagiliaji katika maeneo ya mabonde ili tupate chakula cha kutosha na hivyo tuweze kuepukana na dhana nzima ya wananchi kupatiwa misaada ya chakula kwani misaada ya chakula haiwafikii walengwa katika maeneo yote yanayohusika na kupatiwa misaada.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakulima wadogo wadogo wa nyanya huko Ngarenanyuki, Wilayani Meru, Arusha hawapati msaada wowote kwa Maafisa Ugani. Mashambani hawafiki lakini kila mwisho wa mwezi wanapokea mshahara ambao hawajaufanyia kazi. Wakulima hawa wanachukua mikopo kwa kilimo cha nyanya, wanaishia kupata hasara kwa kukosa Afisa Kilimo wa kuwapa elimu ya matumizi sahihi ya pembejeo na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, nyanya wanazolima hawana soko la uhakika. Kwa sasa wana soko Dar es Salaam, Mombasa na kadhalika na njiani wanapata usumbufu mkubwa kutokana na bidhaa yenyewe kuwa *delicate*. Nyanya zinaharibika njiani na hivyo kushindwa kurejesha mikopo waliyochukua.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa siku wakulima hawa wa Ngarenanyuki wanasafirisha zaidi ya *Fuso* 20 (ishirini) za nyanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Wizara hii ya Kilimo iangalie namna ya kuwasaidia wakulima wa Ngarenanyuki kwa kuwajengea Kiwanda cha Kusindika Nyanya kwa mkopo ili wapate faida zaidi na vijana wao wapate ajira za uhakika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna maeneo mengine pia ya nchi yetu yenye matunda mengi kama huko Muheza, Tanga. Viwanda vijengwe kwa mkopo kwa wakulima ili

waweze kutengeneza juisi badala ya kuacha matunda kuoza ovyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. MOHAMED H. MISSANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, sukari imejaa viwandani na wanashindwa kuuza kwa sababu ya sukari inayoingizwa kutoka nje ya nchi. Kwani vibali vinatolewa kuingiza sukari wakati viwanda vyetu vina sukari nyingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, athari ya hatua hii ni kwamba:

(1) Viwanda vitafungwa;

(2) Wafanyakazi watafukuzwa;

(3) Tutalimbikiza tatizo la ukosefu wa ajira; na

(4) Serikali itakosa kodi kutoka viwanda vya Sukari na wafanyakazi watakaofukuzwa kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sana Serikali iachane na kutoa vibali vya kuingiza sukari kutoka nje ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, bado tatizo la ndege waharibifu halijapatiwa ufumbuzi. Wakulima wanaendelea kuathirika na ndege waharibifu. Ndege hawa wanaharibu mazao ya biashara na ya chakula na hivyo kusababisha njaa na umaskini kwa wananchi. Mwaka jana Serikali iliahidi kununua Ndege *(Aeroplane)* kwa ajili ya kuangamiza ndege waharibifu. Je, Serikali imefikia wapi katika ununuzi wa ndege hiyo?

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ilishatoa kibali cha kuvuna ndege hawa ili vijana wawavune na kuwauza nchini.

Hivi sasa nasikia kibali hicho kimefutwa na mtu akikamatwa anavuna ndege anashtakiwa na kufungwa, naomba nipate maelezo juu ya kadhia hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya ya Ikungi, Singida ni miongoni mwa Wilaya iliyopata chakula cha msaada. Lakini:-

(a) Chakula kilichelewa sana;

(b) Chakula kilikuwa kichache hakikutosha kabisa; na

(c) Wananchi wameumia kwa njaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wanalalamika na kuona kana kwamba hicho ni kiini macho. Naomba dosari hizi zirekebishwe kwa msimu ujao.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. SHAFFIN A. SUMAR:** Mheshimiwa Naibu Spika, mwendelezo wa mchango wangu wa kuongea. Tumbaku ina madaraja 72, kila mwaka daraja linaongezwa, lakini ninapowatembelea wakulima maeneo mengi nawakuta na mafungu matano mpaka saba, sasa madaraja yote hayo kweli yapo? Mbona wenzetu wa Zambia wana madaraja 50 tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, wingi wa madaraja ya tumbaku ni njia ya kuwachanganya wakulima ili waibiwe na *classifiers* na Makampuni ya Tumbaku. Nchi yetu bei ya tumbaku iko chini sana linganisha bei zifuatazo:

| BEI YA TANZANIA | | | BEI YA ZAMBIA | BEI YA ZIMBABWE | |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | TANI | L 30 | US $ 2.739 | $ 3.65 | $4.99 |
| 2. | TANI | L 20 | US $ 3.01 | $ 4.25 | $ 5.11 |

Je, ni kwa nini bei yetu iko chini?

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri Halmashauri ya Tumbaku iongezewe uwakilishi kwani kwenye kupanga bei wakulima ni wachache, wanaohusika kupanga bei ni watu wa Maofisini ambao si wakulima na wala hawajui adha ya mkulima wa tumbaku, ni vyema sasa kila *Union* iwakilishwe na viongozi wawili wa wakulima.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia tumbaku inayonunuliwa kwenye maghala ya vijiji haikamilishi ununuzi mpaka ifike kituo cha Reli au Maghala ya Makampuni, hii sio sawa kwa kuwa makampuni yanakuwa na wawakilishi wao na ma-*classifier* wanakuwepo siku ya kuuza tumbaku (Soko) hata hati ya mauzo husainiwa *(PCN)* lakini malipo na kilo huhesabika baada ya kufikishwa kwenye maghala ya makampuni yao. Ni dhahiri kilo hupungua baada ya siku nyingi kuachwa kwenye maghala yao vijijini na kupungua kwa kilo za tumbaku husababishwa na makampuni, fedha hizo za pungufu ya kilo hukatwa kwenye ushuru wa Chama cha Msingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, huu ni wizi; mjengeko wa bei ya pembejeo nalo ni tatizo, Wizara ifuatilie kwa nini bei ya pembejeo inakuwa juu, bei ya kununulia $ 39.40, usafiri $ 7.66 na mengine mengi kama gharama, hivyo kufikia $ 53.90 je, usafiri wa $ 7.66 ni wa nchi gani?

**MHE. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ukurasa wa 15 unaelezea hali ya Kilimo nchini. Pamoja na Serikali kukiri kuwa Sekta hii ni muhimu katika uchumi na maendeleo ya nchi yetu kwa kutoa asilimia 75 ya ajira kwa Watanzania, nasikitika kusema pesa inayotolewa katika sekta hiyo bado ni kiasi kidogo sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Ushirika; Sheria ya Ushirika italetwa lini ili ifanye kuhamasisha *SACCOS* kuendelea katika maendeleo ya mjini na vijijini ili viweze kutoa huduma za kifedha kwa wananchi wengi zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, yapo mambo ambayo ningependa Serikali ifanye maboresho. Ipo Sheria ya Ushirika

inayosema lazima *SACCOS* zikaguliwe na Mkaguzi wa Ndani na wa Nje. Mkaguzi wa mahesabu wa Vyama vya Ushirika wa nje ni *COASCO* na Mkaguzi wa Vyama vya Ushirika wa ndani ni Ushirika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na wakaguzi hawa wawili Vyama vingi sana vichanga vinapata shida sana vingine kutoendelea na kufa kabisa. Wakaguzi hawa wanatoza gharama (ada) kubwa sana ya ukaguzi, kitu ambacho kinafanya baadhi ya Vyama kutokaguliwa kwa kuogopa ada inayotozwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia Wakaguzi hawa wamekuwa wakilazimisha Vyama hivi kutoa michango ya Semina mbalimbali wakifanya kama kitega uchumi fulani hivi. Kwa mfano, *COASCO* wakiandaa Semina, akimaliza, Ushirika nao wanaandaa semina, kama ile.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningeshauri kingekuwepo chombo kinachoratibu semina hizi na wakati mwingine watoe elimu bure kwa ajili ya kusaidia Vyama vichanga visivyokuwa na uwezo wa kulipia ada ya elimu hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Miradi ya umwagiliaji; niipongeze Serikali kwa kuongeza eneo la kilimo cha umwagiliaji. Lakini Serikali ingeweka wazi kuhusu vigezo vinavyotumika katika miradi inayoanza kutengewa pesa kwa ajili ya maeneo ya umwagiliaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nini Serikali huwa inaanzisha miradi mipya wakati miradi mingine ya umwagiliaji inachukua muda mrefu sana kukamilika na kusababisha nguvu ambayo wananchi na Halmashauri wamejitolea kutokuwa na umuhimu tena na kusababisha wananchi kutokuwa na imani na Serikali yao. Ningeomba kupata majibu kuhusu vigezo vinavyotumika kutenga pesa ya hiyo miradi ya umwagiliaji katika maeneo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu pembejeo za kilimo; hizi ruzuku za pembejeo za kilimo zimekuwa na malalamiko

mengi sana katika maeneo karibu yote. Naomba kuiuliza Serikali:-

(i) Je, tangu ruzuku za pembejeo za kilimo zimeanza kutolewa kuna mabadiliko yanayoonekana ukilinganisha na wakati kulipokuwa hakuna ruzuku hizi?

(ii) Je, Serikali haioni kuwa sasa kuna umuhimu wa kushirikisha wananchi ili wao wachangie kilimo mbadala kuliko kuendelea kutoa ruzuku za mbolea na mbegu? Mfano, nimesikia baadhi ya maeneo wananchi wakiomba Serikali iache kupeleka mbolea, badala yake wanataka wapewe mizinga ya nyuki ili kufanya sehemu hiyo iwe maalum kwa uzalishaji wa asali.

(iii) Serikali inatakiwa itoe taarifa kwa Umma ili kujua sehemu ambako trekta za Kilimo Kwanza zimetolewa kwa wingi ili iweze kufuatilia kujua uzalishaji wake ukoje ukilinganisha na sehemu ambazo matrekta hayakupelekwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. HAMOUD A. JUMAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue nafasi hii kumshukuru Mungu kwa kunipa uzima na afya, hivyo kuweza kupata nafasi ya kuchangia hotuba hii ya bajeti ya Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika kwa mwaka 2013/2014.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nimpongeze Mheshimiwa Waziri kwa hotuba yake nzuri na yenye kutekelezeka. Hakika kwa mipango hii ya Serikali itatatua matatizo yaliyopo katika sekta hii muhimu kwa Taifa letu. Pia nimpongeze Mheshimiwa Waziri kwa kuandaa bajeti inayoonesha malengo yatakayowasaidia wakulima kupata mazao bora kwa kutumia kilimo cha kisasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze kuchangia kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutambua umuhimu wa wakulima kote nchini kuwapa pole kwa changamoto zote wanazokabiliana nazo, ikumbukwe kwamba wananchi walio wengi ni wakulima na wafugaji ingawa kuna juhudi nyingi za Serikali za kuboresha kilimo, lakini kuna mambo mengi sana yanayohitaji kuangaliwa kwa umakini wa hali ya juu katika sekta hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, najua Serikali ina nia nzuri sana na wakulima kwani inatambua umuhimu wao katika nchi na hata ukizungumzia duniani kiujumla wakulima huthaminiwa sana na wana mchango mkubwa sana katika Taifa. Kutokana na kuboresha Sekta ya Kilimo, Serikali ilikuja na mkatati wa Kilimo Kwanza, lakini imeonekana mkakati huo kutokufanya vizuri kwani wakulima hawana elimu ya kutosha kuhusu kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ingependeza Serikali ianzishe mkakati wa elimu kwanza kwa kutoa elimu ya kutosha kwa wakulima, kwa kuwa wakulima hawa wanaokusudiwa katika Kilimo Kwanza hawana elimu ya kutosha kuhusu kilimo. Tukija na mkakati wa elimu kwanza itasaidia wakulima kupata elimu, kuelimishwa kuhusu kilimo bora na ndipo kupata tija na kilimo safi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kufanya hivyo itasaidia pia kuwapeleka wataalam wetu vijijini na kutoa mafunzo kwa wakulima. Napenda niikumbushe Serikali, tuna wataalam wengi wa fani za kilimo hapa nchini, lakini tuna tatizo moja la hawa watalaam, wakipangiwa kazi vijijini huenda kuripoti na baada ya muda wa mwaka mmoja au miwili huomba ruhusa ya kwenda kusoma na kuacha kituo hakina mtu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kufanya hivyo husababisha wananchi kukosa wataalam wa kuwapa elimu bora. Serikali inapowaruhusu hawa wataalam kwenda shule, basi naiomba, isisahau kupeleka wataalam wengine ili kuziba nafasi iliyoachwa wazi kwa kipindi hicho.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunakabiliwa na upungufu wa chakula nchini, kuna baadhi ya maeneo kuna uhaba wa chakula, kutokana na mvua hazikunyesha vizuri, mazao yamekauka pia kuna maeneo mengine mvua zimezidi kunyesha mpaka zikaleta athari kwa mazao, matokeo yake wananchi wamekumbwa na njaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Serikali kupitia Wizara kuchukua hatua za haraka kushughulika na kukabiliana na njaa kwa Mikoa ya hapa nchini. Pia nichukue fursa hii kuwapa pole mikoa yote iliyokumbwa na njaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jimbo la Kibaha Vijijini limebarikiwa na vitu vingi pamoja na ardhi yenye rutuba ambayo inakubali kurutubisha mazao. Kwa mfano, ukiangalia katika mabonde mazuri tuliyonayo, tunaweza kulima mpunga, mbogamboga, matunda, nyanya, mananasi, machungwa, maembe, matikiti maji na kadhalika, lakini wananchi hawa kwa kukosekana kwa soko zuri la kisasa na sehemu ya kusindikia mazao yao katika Mji wa Kibaha imekuwa inawasikitisha sana. Hata hivyo, wanaendelea kujishughulisha na kilimo na kuiamini Serikali yao kuwa itawasikiliza kilio chao.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Serikali kuwawezesha wananchi hawa katika jitihada zao hizi ili waweze kufikia malengo mazuri. Hilo tunaweza kulifanya kwa kuwakopesha fedha katika vikundi vidogo vidogo ili waboreshe kilimo chao na pia Serikali iwape elimu kuhusu kilimo cha umwagiliaji mwaka mzima, kwani kilimo cha kutegemea mvua kimeshapitwa na wakati katika dunia ya leo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naamini kuwa tukifanya haya yote, tutakuwa tumewasaidia kwa kiwango cha juu wananchi hawa ikizingatiwa kilimo ndio uti wa mgongo.

Mheshimiwa Naibu Spika, zao la pamba hapa nchini limekuwa likisuasua katika bei kwa muda mrefu sana na mpaka kufikia wakulima wake kubaki njia panda kwa

kutokujua nini msimamo wa Serikali yao. Kutokana na hilo, naomba kusema kwamba, kumetokea kama kujichanganya kwa Serikali, kwa Wizara kuahidi bei ya Sh. 1,100/= kwa kilo ya pamba katika mkutano wa nane wa wadau wa sekta ya pamba uliofanyika mwezi uliopita huko Mwanza na sasa kuidhinisha bei ya Sh. 800/= kwa kilo. Hii inawachanganya wakulima na kuwavunja moyo. Maswali magumu ni:-

(a) Nani atawafidia wakulima hawa kwa upungufu wa bei hiyo ambayo Serikali ina jukumu la kusimamia soko la zao la pamba ili kuepuka hasara; na

(b) Pia hitaji la mizani 10,000 ya kusambazwa katika vituo vya kununulia pamba ambapo hapa inaonesha kusuasua kwa tenda hiyo kukamilika ili mizani hiyo iwasaidie wakulima.

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri atufafanulie vizuri ili tuweze kupata majibu ya maswali hayo, kwani itawasaidia sana wakulima wa pamba na kunufaika na zao hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile naomba Serikali itupie vizuri jicho lake kwa haya madawa yanayotumiwa na wakulima kupulizia katika mazao. Kama mazao hayo hayatakuwa na athari kwa mtumiaji pindi yakivunwa na kumfikia, kwani imeonekana baadhi yana athari hutokea kwa mtumiaji baada ya kipindi kirefu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia naishauri Serikali kuangalia upatikanaji wa mbolea nzuri na zenye ubora ili wakulima wetu wapatiwe na ikiwezekana urasimu wa upatikanaji wa mbolea hizi usiwepo kabisa, kwani imegundulika baadhi ya Mawakala wamekuwa si waaminifu kwa maana hiyo hupandisha bei ya mbolea hiyo na kuwa usumbufu kwa wakulima.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo lingine linalowapata wakulima ni jinsi ya kuhifadhi mazao yao baada ya kuyavuna. Tumejionea sehemu nyingi nchini mazao yanahifadhiwa

kiholela na kuharibika. Serikali ijitahidi kutoa elimu ya kutosha kwa wakulima hawa ili tuweze kuwa na uhifadhi mzuri ambao utayafanya mazao yetu kuwa bora.

Mheshimiwa Naibu Spika, ikumbukwe mazao haya yanahitajika sana katika masoko ya nchi za nje. Tatizo kubwa ni namna gani mazao haya yataweza kupenya katika soko hili, lakini ingewezekana kwa kuvitumia Vyama hivi vya Ushirika ili kuwasaidia wakulima, lakini kuna malalamiko mengi kutoka kwa wakulima kwa maofisa hawa kutokuwa waaminifu, pia upungufu wa kiutendaji wa Vyama hivi vya Ushirika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inaweza kuchukua hatua za makusudi kuimarisha Vyama hivi kwa kuhakikisha watendaji wa Vyama hivi wanao ujuzi wa kutosha katika masuala ya kilimo, hususan masoko na biashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. HAROUB MUHAMMED SHAMIS:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu *(Subhanah Wataala)* kwa neema na rehema zake nyingi kwangu, familia yangu na Taifa letu kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, wimbo huu wa "Kilimo Kwanza," "Kilimo ni Uti wa mgongo wa Taifa" sasa umechosha masikioni mwa Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati umefika sasa kwa Serikali kutekeleza kwa vitendo falsafa hii ya Kilimo Kwanza ili kuwanasua watu wetu na umaskini uliokithiri.

Mheshimiwa Naibu Spika, utashi wa kisiasa unahitajika ili kilimo kiweze kuinuka. Serikali itenge fedha za kutosha kuwasaidia wakulima wadogo ili waweze kuendeleza kilimo chenye tija kwao na kwa Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali iweke mkakati madhubuti na wenye usimamizi wa kutosha kwa Maafisa

Ugani kufanya kazi za kuwasaidia taaluma wakulima wetu wadogo wadogo ili walime kilimo cha kisasa kwa lengo la kuongeza uzalishaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo, ni wajibu wa Serikali kutafuta masoko ya uhakika kwa mazao yanayozalishwa. Kuzalisha bila masoko ya uhakika ni kupoteza nguvu, fedha na ni kuwavunja moyo sana wakulima wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hayo suala la kuyaongezea thamani mazao ya kilimo ni jambo lenye umuhimu mkubwa sana katika kuinua kilimo, kukuza ajira na kuinua kipato cha wananchi wetu ili kuboresha hali zao za maisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni jambo la aibu sana kwa korosho zinazolimwa Mtwara zibanguliwe India, zifungashwe huko India na zisafirishwe Ulaya, Marekani na Arabuni kwa *Brand* ya India *that is Produce of India*...!! Hii ni fedheha na tunatangaza udhaifu wetu duniani na uzembe usio kifani.

Mheshimiwa Naibu Spika, bila mambo matatu ambayo ni; kuwasaidia wakulima kuongeza kilimo kwa kulima kisasa, kuwatafutia masoko na bidhaa au mazao ya kilimo kuyaongezea thamani, Serikali itakuwa bado haijakuwa na dhamira ya kweli ya kuinua kilimo nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu *SACCOS;* Vyama hivi vya Akiba na Mikopo bado tija yake haijaonekana. Watu wako hamkani na vikundi vya *SACCOS,* lakini bado hamjawaletea tija inayostahili. Tatizo lililopo hapa ni kuwa, vikundi hivi havikuanzishwa kwa nia ya kuwainua kiuchumi wananchi bali kuwainua kisiasa baadhi ya watu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili tupate tija ya kilimo na vikundi hivi ni lazima siasa yetu itumikie uchumi na si uchumi kutumikia siasa, hatutofanikiwa abadan!

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu stakabadhi ghalani; kauli ya Serikali katika Bunge hili ni kuwa mfumo huu ni mzuri bali unaharibiwa na watendaji wasio waaminifu wa Vyama vya Ushirika, wasimamizi wa maghala na taasisi za fedha! Je, Serikali kwa vile imeshaona upungufu na kuwatambua wafujaji, ni hatua gani wamechukuliwa wabadhirifu hao? Au Wizara ina maslahi binafsi katika ubadhirifu huo ndio maana wanashindwa kuchukua hatua za kinidhamu?

Mheshimiwa Naibu Spika, mazao ya jamii ya kunde yana soko zuri sana katika nchi za India na Asia ya Kati. Serikali itoe elimu kwa wajasiliamali wadogo wadogo juu ya namna bora ya ku–*export* mazao hayo ili kukuza soko la ndani na nje na kuinua kipato cha mkulima.

Mheshimiwa Naibu Spika, mfumuko wa bei, hasa bei ya chakula ni athari na hatari kubwa kwa jamii kubwa ya wananchi wetu. Chakula ni kitu muhimu sana kwa maisha ya watu na hivyo hakitakiwi kupanda bei mara kwa mara au kupanda sana. Athari zake ni kupungua kwa lishe bora kwa nguvu kazi ya Taifa na kushusha uzalishaji katika sekta zote, kwani watu wenye njaa ufanisi wao wa kazi unapungua sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, athari nyingine ni kushuka kwa kiwango cha elimu na ufaulu pia, kwani Mwalimu asiyeshiba anakosa nguvu ya kusomesha darasani na mwanafunzi anakosa nguvu ya *concentration* na hivyo kushindwa kumudu masomo yake vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Mungu ibariki Afrika, Mungu ibariki Tanzania na watu wake.

**MHE. JITU V. SONI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kupata nafasi hii kuchangia katika bajeti ya Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nichangie kwa kusema bajeti ya Wizara hii ni ndogo sana kulingana na mahitaji yaliyopo. Lakini hata hiyo kidogo iliyopangiwa

mtiririko wa utoaji wa fedha ni mbaya sana. Asilimia ya fedha hasa ya maendeleo inayotolewa kila mwaka ni ndogo. Pia miradi iliyoanzishwa na kupata fedha kidogo huwa inakwama sababu gharama ya utekelezaji inapanda, ni vyema fedha yote iliyotengwa itolewe kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, natofautiana na wachangiaji wenzangu kutaka kukwamisha bajeti hii, kila mmoja anataka katika kitabu au randama ioneshe mradi katika Jimbo lake au linalohusu wapiga kura wake. Kazi yetu sisi Wabunge ni kuishauri Serikali, kuisimamia na kupanga mkakati wa kuendeleza kila sekta kwa kuweka sera nzuri na kuweka mazingira rafiki ya kuendeleza kilimo. Hatutoi ushauri wa nini cha kufanya bali tunalalamika wote. Vizuri tutoe njia na mfano wa nini cha kufanya na kuboresha Sheria zilizopitwa na wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, nashauri Serikali iangalie na kuweka mfumo wa kushirikisha Idara mbalimbali za Serikali wakati wa kupanga na kutekeleza miradi. Idara zote husika zikishirikishwa miradi itakuwa na mafanikio na utekelezaji wake utakuwa rahisi. Utafiti uliofanywa na watafiti mbalimbali unaonesha kuwa idara mbalimbali za Serikali ngazi ya Taifa, Mkoa na Wilaya hazishirikiani na idara nyingi hazijui miradi inayotekelezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika azma ya kutekeleza Kilimo Kwanza, moja katika nguzo muhimu ni ardhi. Lakini hadi leo hii Wizara ya Ardhi si Wizara katika mstari wa mbele *(Lead Ministries)* katika utekelezaji wa Kilimo Kwanza. Nashauri Wizara ya Ardhi pia iwekwe katika orodha ya Wizara mstari wa mbele *(Lead Ministries)* na kuwashirikisha katika masuala yote ya Kilimo Kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa hapa napongeza wazo la kuwa na Sheria ya kulinda Ardhi za Kilimo. Ni vyema Sheria hiyo iletwe mapema Bungeni, tuipitishe mapema. Leo hii ardhi kubwa yenye rutuba na uwezo wa kuzalisha mazao mbalimbali na yenye vyanzo vya maji na maeneo oevu

yamegeuzwa kuwa makazi, viwanda na matumizi mengine. Sheria pia ya kubadilisha matumizi ya Ardhi iletwe mapema.

Mheshimiwa Naibu Spika, mifano mizuri ni eneo la Babati ambapo maeneo mazuri ya uzalishaji wa Mbaazi maarufu duniani yamekuwa makazi na maeneo ya kufyatua tofali ya udongo. Arusha, mashamba ya *green belt* na hifadhi ya maji ya chini ya ardhi, Burka *Coffee Estate*, Seliani, Mringa yamebadilishwa matumizi kuwa makazi, utalii, mashule na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia eneo lote kutoka Arusha hadi Usa *River* matumizi yamebadilika, shamba la Gomba ambalo lilikuwa linazalisha mazao ya bustani *horticulture* na kusafirisha nje limegeuzwa kuwa ploti za makazi. Mfano, India hata raia wa India ambao hawana historia ya kuwa wakulima hawaruhusiwi kununua maeneo ya kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri Serikali wakati wa kubinafsisha mashirika mbalimbali, mashamba na ranchi, waangalie vikundi vya wajasiriamali wa ndani ya nchi na wenye uzalendo na uzoefu wa kazi hiyo wapewe kipaumbele. Pia, mazingira rafiki katika uwekezaji katika kilimo yawekwe na fursa zitangazwe kwa Watanzania wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri Serikali iangalie namna ya kuboresha miundombinu ya uhakika vijijini katika sekta ya barabara, nishati, mawasiliano ili uwekezaji katika sekta ya kilimo ukue, pia miundombinu ya mabwawa, mifereji na fursa za kupata mikopo ya riba nafuu upatikane kwa wawekezaji wa sekta ya kilimo. Leo hii mazingira si rafiki katika uwekezaji wa kilimo. Miundombinu hii ingewekezwa vizuri na Serikali vijijini, viwanda vingi vya usindikaji vingewekezwa huko karibu na wakulima.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali iangalie masoko ya mazao ya kilimo, leo hii mazao mengi ya matunda hasa zabibu, maembe, machungwa na mananasi yanakosa soko na wakipata soko hulipwa bei ndogo na wazalishaji ambao wanaagiza malighafi yaani *(concentrates)* kutoka nje na

hupata msamaha wa kodi au kulipa kiwango kidogo cha kodi wakati wa kuingiza malighafi nchini. Hii hudumaza maendeleo ya Sekta ya Kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia fedha nyingi hutumika kuagiza matunda na chakula kutoka nje, tuangalie namna ya kuzalisha chakula na matunda hayo hapa nchini. Mfano, *apple*, zabibu, *peaches*, maziwa na viungo vya aina zote.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri Serikali iangalie namna ya kuboresha Vituo vyetu vya Utafiti. Bajeti inayotengwa kwa ajili ya vituo hivyo ni ndogo sana. Pia tafiti zilizofanyika huwa haziwafikii wakulima. Mbinu bora na aina mbalimbali ya mbegu, dawa na teknolojia katika kilimo viwafikie wakulima ili waboreshe kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, vituo zaidi vya kupima udongo vingewekwa kila mkoa ambapo hakuna vituo hivyo karibu. Kilimo cha kisasa kinataka upime udongo kila wakati ili kujua mahitaji ya mbolea na aina ya mazao yanayofaa kupandwa katika ardhi hiyo pamoja na utafiti wa hali ya hewa wa uhakika.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri Mfuko wa Pembejeo ungewezeshwa zaidi, umekuwa na mafanikio makubwa isipokuwa changamoto ya ukosefu wa fedha kukidhi mahitaji. Mfuko huu uongezewe fedha ya kutosha ili wakulima waweze kukopa na Mfuko utanue wigo hadi kukopesha umwagiliaji. Pia Benki ya Kilimo iharakishwe kuanza kazi na *TIB* iongezewe mtaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la ugani ni muhimu, Serikali iangalie kuongeza idadi ya Maafisa Ugani hadi kufikia idadi inayotakiwa. Wawezeshwe kuwa na nyezo za kazi, usafiri, vyombo vya kufanyia kazi, lakini muhimu ni elimu ya uhakika kwa Maafisa Ugani wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Chuo pekee cha Kilimo Tanzania *Sokoine Universty of Agriculture* hutoa mafunzo vizuri, lakini changamoto ya kutokuwa na vifaa vya

kufundishia mfano *agrimechanisation* hawana trekta *power tiller*, mifano ya vifaa vya umwagiliaji, *sprinkler set, drip set et cetera,* maabara ya kisasa ipo isipokuwa ni ndogo sana na haikidhi mahitaji ya idadi ya wanafunzi waliopo. Sekta ya *horticulture,* haina benki ya mazao na matunda aina mbalimbali kwa ajili ya mafunzo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri Serikali iangalie namna ya kuboresha chuo hicho kiwe katika viwango vinavyostahili. Pia bajeti iliyotengewa, hasa ya maendeleo ije kwa wakati. Leo hii fedha ya maendeleo ya mafunzo ya vitendo *practicals* kwa robo ya pili na tatu mwaka 2012 - 2013 ilikuwa haijafika hadi 30, Machi, 2013. Matokeo yake yanajulikana.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichangie Sekta ya Ushirika, hii ni njia moja ambayo imekuwa mkombozi wa wakulima, lakini leo hii wakulima hawana imani na ushirika. Ushirika umekuwa mzigo na unyonyaji wa wakulima.

Mheshimiwa Naibu Spika, naamini wakati wa mabadiliko ya Sheria ya Ushirika utakapofika, tutaweza kuchangia na kuiboresha Sheria hiyo ili Ushirika uwe na manufaa kwa mkulima. Nchi nyingi wamefanikiwa na Ushirika mfano, India, *Amul dairies* ni Ushirika mkubwa wa sekta ya maziwa na mifugo yenye faida kubwa, Viwanda vya Miwa asilimia kubwa ni mali ya Ushirika. Leo hii Serikali inalipa madeni ya Ushirika ili wakulima wapate haki zao. Je, ni wabadhirifu wangapi walitumia fedha na mali za Ushirika vibaya wamechukuliwa hatua za kisheria?

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kuwa *CAG* sasa atakagua pia Vyama Vikuu vya Ushirika. Naomba waanze na RIVACO Babati. Ina hodhi ardhi nyingi na kukodisha kinyume cha Sheria na kuwa na migogoro ya ardhi na wananchi wa jirani. Pia hakuna mapato na matumizi kwa uwazi kwa wanachama na hawapokei wanachama wapya. Naomba elimu kwa wananchi wetu katika Sekta ya Ushirika.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Serikali iangalie kwa umakini suala la usambazaji wa pembejeo hasa za ruzuku. Mfumo huo mpya unaopendekezwa uangaliwe kwa umakini na ujaribiwe katika eneo la mfano *(Pilot area)*. Mfumo unaopendekezwa ni mzuri kwa nadharia na utakuwa na changamoto wakati wa utekelezaji. Tuendelee na mfumo wa vocha kwa msimu huu wakati mfumo mpya unaandaliwa na kufanyiwa majaribio.

Mheshimiwa Naibu Spika, Taasisi za kifedha (mabenki) hazipo katika maeneo yote nchini. Pili, vikundi rasmi vya wakulima havipo vya kutosha vijijini. *VICOBA* vingi tulivyohamasisha haviko kisheria. Ni vyema Sheria ya kutambua *VICOBA* iletwe na vikundi hivyo ambavyo ni vingi vijijini na wana mitaji midogo waweze kupata mkopo kutoka taasisi za kifedha na watasaidia katika kukopa pembejeo kwa wanachama wao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyochangia katika Bunge hili katika vipindi mbalimbali na sasa Wabunge wengine pia kukubali hoja hiyo, ruzuku itolewe kwa wazalishaji na waingizaji wa mbolea na mbegu moja kwa moja. Bei ya mbolea na mbegu iwe chini na pasiwe na vocha, kila mkulima anunue kutokana na hitaji yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri mbegu inayozalishwa nchini iwe na viwango tofauti vya ruzuku na mbegu inayoagizwa kutoka nje ya nchi. Inayozalishwa hapa nchini ipewe ruzuku zaidi na itapata fursa ya kununuliwa kwa bei nafuu na kuingia katika soko. Hivyo hivyo, katika mbolea, kwa wale watakaobainika kusambaza pembejeo chini ya viwango na feki wachukuliwe kama wahujumu uchumi na wabanwe na kufikishwa katika vyombo vya Sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, nashauri Serikali iangalie na kufanya utafiti wa kina katika suala zima la kodi na tozo mbalimbali wanazotozwa wakulima. Kodi tulizoondoa katika bajeti ya 2012 - 2013 bado zinaendelea kutozwa. Mfano, matairi ya trekta, tela za trekta, majengo

ya kuhifadhi mazao, pampu za umwagiliaji na jenereta. Hii ni mifano michache.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakulima walipewa matumaini ya kufutwa kodi ya vipuri vya zana za kilimo na matrekta, lakini bado havijamnufaisha mkulima, Sheria hiyo ambayo anayestahili msamaha ni mkulima na si mfanyabiashara. Je, ni mkulima yupi mdogo anayeagiza vipuli hivyo? Wafanyabiashara ndiyo huagiza kwa niaba ya mkulima.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia tozo mbalimbali wanazotozwa wakulima na wakala mbalimbali *(regulatory bodies)* ni mzigo kwa mkulima, mfano, ushuru wa mazao, tozo ya zimamoto, tozo ya mizani, OSHA, ukaguzi wa *TOSCI, TBS, TPRI* na nyingine nyingi.

**MHE. NIMROD E. MKONO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nchi yetu hukabiliwa na ukosefu wa chakula mwaka hadi mwaka katika sehemu mbalimbali ukiwemo Mkoa wa Mara hususani Wilaya ya Butiama. La kushangaza ni kwamba, lipo eneo kubwa Wilayani Butiama ambalo linaweza kutumika kuzalisha chakula cha kutosha kukidhi mahitaji yote ya chakula Mkoani Mara na hata kuuzwa nje ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, utafiti uliofanywa na Kampuni ya *Domion* ya America mwaka 2006 – 2007 na kuwasilishwa Serikalini ulionesha dhahiri kwamba Bonde la Mto Mara ambalo sasa limejaa magugu mengi limekuwa kero kubwa kwa wananchi waishio kando kando ya Mto Mara kukumbwa na mafuriko ya maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na mafuriko ya Mto Mara, wananchi wengi waishio Kata ya Buswahili na Bwiregi, Tarafa ya Kiagata mwaka hadi mwaka hukumbwa na mafuriko ya maji ya Mto Mara na kusababisha hasara kubwa kwa n'gombe wao kufa na watu kupoteza maisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kampuni ya *Dominion Farm* ya America ilibuni kujenga mradi mkubwa uitwao *Mara*

*Swamp Project*. Chini ya mradi huu ilipendekezwa ujenzi wa daraja kubwa kuunganisha ukingo wa sehemu ya Nyamongo iliyoko Wilaya ya Rorya na majimoto ili kupatikana kwa *Dam* kubwa ambalo litapunguza umwagikaji wa maji kufurika maeneo ya Wegero, Kongoto, Buswahili na Bwiregi. Daraja hili lingewekewa *valve* kuruhusu maji kupita kwenye *channel* maalum kando kando zote mbili za bonde la Mto Mara.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kufanya hivyo basi, Bonde kubwa la Mto Mara lenye ukubwa wa takribani hekta 75,000/= lingeweza kutumika kwa kilimo kikubwa *(the Mara Farms)* na hivyo kuwawezesha wananchi wa Kiagata kuweza kulima kilimo cha kisasa na kufuga mifugo ya kisasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, *Group la G 8* linajua liliipa Serikali ya Tanzania fungu kubwa la fedha ili kuisaidia Tanzania kuimarisha kilimo. Je, Serikali inasema nini kuhusu *Mara Swamp River Project* ambayo ni muhimu sana Mkoani Mara na kwa Taifa zima? Je, ni lini basi Serikali itamega kiasi kidogo kuweza kufanya mradi huu ili wananchi wangu wa Kiagata waweze kutokana na madhara makubwa yatokanayo na ufurikaji wa Mto Mara?

Mheshimiwa Naibu Spika, nilishawasiliana na Wizara husika kuhusu mradi huu muhimu, sasa ningependa kupata tamko la Serikali kuhusu mradi huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na mchango huu, naunga mkono hoja iliyoko mezani.

**MHE. PROF. JUMA A. KAPUYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kwanza niwapongeze Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na timu yake ya Wizara kwa hotuba nzuri ya Bajeti waliyotuletea.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara hii kwa mwaka wa tatu mfululizo wamekuwa wanaahidi kujenga bwawa la maji ya kumwagilia, kunywa na ya mifugo katika Kijiji cha Ulindwanoni, Wilaya ya Kaliua. Wamethubutu hata kuonesha

fedha wanazokusudia kuanza nazo katika ujenzi wa Bwawa hili ambazo zilikuwa ni Sh. 500 milioni.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa masikitiko makubwa mpaka leo hakuna chochote kinachoendelea. Bajeti zinakuja na kupita lakini bwawa halichimbwi.

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri wakati anahitimisha hoja yake anieleze, ni lini ujenzi wa bwawa hili utaanza. Wananchi wa Ulindwanoni wameendelea kuishi kwa matumaini, lakini hakuna chochote, inakatisha tamaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. RIZIKI OMAR JUMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichangie kuhusu Bajeti ya Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, bado bajeti iliyotengwa kwa Wizara ni ndogo sana na kwa msingi huu Kilimo Kwanza kinaweza kikawa ndoto tu. Ili tuweze kufikia malengo yetu ni lazima Serikali itenge bajeti ya kutosha. Hii itawezesha Wizara kupata, kutoa huduma za kutosha za kilimo kama vile pembejeo kwa wakati muafaka na pia kuweza kutoa ajira kwa vijana wenye uwezo kama vile Maafisa Ugani ambao ni muhimu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, mbaya zaidi ni kwamba, hata hiyo bajeti ndogo inayotengwa haipatikani. Ukiangalia fedha iliyotengwa 2012/2013 kiasi kilichotolewa ni kidogo sana hivyo hatuwezi kufikia malengo.

Mheshimiwa Naibu Spika, fedha iliyotengwa mwaka huu wa 2013/2014 halikadhalika haikidhi haja ya mahitaji ya Kilimo Kwanza. Nakubali kwamba, Serikali ina nia thabiti, lakini mbona fedha ni ndogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kilimo kingeweza kuwakomboa vijana wengi kwani wangeweza kujiajiri wenyewe lakini kwa mwendo huu wakulima kwa kutumia

jembe la mkono haiwezekani kutatua tatizo la ajira na hatimaye wanakimbilia mijini na kuwa Wamachinga. Mbali ya hilo wengine wanazurura ovyo mjini na matokeo yake Taifa hili linazalisha vibaka wengi mijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala ardhi kupewa wawekezaji kwa mkataba mrefu (miaka 99), naomba Sheria hii iangaliwe tena upya ili ifanyiwe marekebisho hasa wawekezaji toka nje ya Tanzania.

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA**: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimpongeza Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, pamoja na wafanyakazi wote wa Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika kwa kazi nzito na muhimu kwa mustakabali mwema wa Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya ya Simanjiro imekuwa inakabiliwa na tatizo la njaa na kupelekea Serikali kulazimika kupeleka chakula cha njaa kutokana na ukame wa mara kwa mara. Kwa kuwa upembuzi yakinifu umekwishafanyika wa miundombinu ya umwagiliaji Ngage na Ruvu – Remiti, nashauri Serikali itenge fedha za utekelezaji wa miradi hiyo ya umwagiliaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara inafahamu maeneo muhimu kwa umwagiliaji ambao hivi sasa yanatumika japokuwa miundombinu yake siyo ya kisasa hivyo kupelekea uzalishaji usio na tija. Naomba niikumbushe Wizara hii kuwa Serikali ilikwishatambua maeneo hayo na kuahidi kuyaendeleza. Mabonde hayo yapo katika Vijiji vya Kuwani, Lemkuna Ngage, Ruvu Remit, Loibor Soil, Gunge, Msitu wa Tembo na Kambi ya Chokaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri Serikali kupitia Wizara hii itenge fedha kwa ajili ya utekelezaji wa miradi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, bado ni rai yangu kuwa, Serikali ipeleke chakula cha msaada Simanjiro pamoja na chakula cha bei nafuu ili kuokoa maisha ya watu wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali iangalie upya suala la mpango wa pembejeo kwani inaonekana kuwanufisha Mawakala na Watendaji wachache wasio na chembe ya uaminifu badala ya kuleta mapinduzi yenye tija kwa wakulima wadogo wadogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumekuwa tukisikia na kusoma juu ya kuwepo kwa mabwawa makubwa ya umwagiliaji na matumizi mengine ya binadamu na ufugaji (mifugo). Naomba Serikali itupatie mabwawa ya aina hii angalau moja kwa mwaka huu wa fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. Ahsanteni.

**MHE. PINDI H. CHANA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. Je, ni trekta ngapi zipo katika Halmashauri, je, ni Halmashauri ngapi zina matrekta. Kwa nini hadi leo watu wanatumia jembe la mkono kwa kiasi kikubwa? Yako wapi mapinduzi ya kilimo? Mbona Mikoa yenye njaa inaongezeka kadri siku zinavyokwenda *why?*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kupongeza sana Mikoa ya Kusini kwa kilimo cha mahindi, lakini pamoja na michango yao mikubwa bado miundombinu hairidhishi hususan barabara. Hivyo, naomba barabara ya Njombe Ludewa Manda Itoni ijengwe haraka kwani Wilaya inachangia sana pato la Taifa. Miradi ya Kilimo Kwanza *SAGCOT* itengeneze barabara hizo. Ili kilimo kiendelee kuwa endelevu na matrekta lazima tuweze kununua kwa wingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kiwanda cha jembe la mkono nchini kipo wapi? Nina taarifa kuwa hata jembe la mkono tunaagiza, je, ni kweli?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Ludewa wanazalisha sana mahindi, lazima miundombinu ya barabara itengenezwe, hivyo, barabara ya Njombe-Ludewa-Manda-Itoni ipewe kipaumbele kwenye miradi ya kilimo na *SAGCOT*.

Mheshimiwa Naibu Spika, je, nchi yetu inalindaje bei za wakulima wa ndani? Je, nchi yetu inapata mapato kiasi gani kutokana na *Export* ya Mazao? Kwa nini hatu-*export* viazi, mahindi na matunda? Kila Halmashauri inunue trekta kama *Landcruser* za Wakurugenzi. Mikoa na Wilaya zinazozalisha kilimo zipewe ruzuku ya kutosha na *Government interventions, Ring Fancing*.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. SALUM K. BARWANY:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nashawishika kutokuunga mkono Bajeti ya Wizara ya Kilimo mpaka pale Waziri wa Kilimo atakaponitosheleza katika mambo yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la stakabadhi ghalani; wakulima wa zao la korosho wamekuwa wakicheleweshewa malipo ya pili na kusababisha uadui kati ya Serikali za Mitaa na wakulima hao. Wakulima hawapati bei dira inayoamuliwa au kutangazwa, kwa mfano, bei dira ya mwaka 2012/2013 ni sh. 1,200/= kwa kilo. Lakini wakulima walilipwa Sh. 600/= kwa malipo ya awali, malipo ya pili wamelipwa sh. 200/= hadi sh. 400/=, badala ya Sh. 600/= iliyobaki.

Mheshimiwa Naibu Spika, utaratibu wa kulazimisha ununuzi wa korosho kufanywa na Vyama vya Msingi peke yake. Makato holela ya fedha za wakulima ni vyema wakulima wakalipwa bei dira kwa mkupuo sh. 1200/=.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la mashamba pori; maeneo yaliyokuwa yanazalisha zao la mkonge hasa Mikoa ya Kusini, zao hilo halilimwi tena na mashamba hayo kubaki ni mapori na kusababisha upungufu na ardhi na wananchi wengi kukosa maeneo ya kulima.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Wizara ya Kilimo iliunda kikosi kazi cha kuchunguza mashamba pori, lakini hadi hii leo taarifa hiyo imebaki kwenye majalada. Nahitaji kujua taarifa hiyo itatolewa lini na hatua gani

zinachukuliwa kwa lengo la kubadili matumizi ili wananchi waweze kupata maeneo ya kulima mazao ya chakula na ya biashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bajeti ndogo isiyokuwa na tija kwa Wizara ya Kilimo kinyume na makubaliano ya nchi za *SADC* angalau kufikia 10% kwa lengo la kuinua sekta hiyo ya kilimo.

**MHE. SELEMANI S. BUNGARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, suala la Stakabadhi Ghalani limekuwa kero isiyopatiwa ufumbuzi mwaka hadi mwaka. Wakulima wamekuwa hawapati bei dira inayoamriwa na kutangazwa na vyombo husika. Mfano, ni mwaka 2012/2013, bei iliyotangazwa ni Sh. 1,200/= kwa kilo, lakini wakulima walilipwa malipo ya awali ya Sh. 600/= na malipo ya pili Sh. 200/= hadi Sh. 400/=, kwa nini Serikali isiufute mfumo huu na kuandaa taratibu za kuanzisha mfumo mwingine ili kuwezesha wakulima wanufaike na mazao yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kilimo kutajwa kama majawapo ya maeneo ya vipaumbele. Naitaka Serikali ilieleze kwa kina Bunge lako Tukufu nini hasa mchango wa kilimo katika bajeti ya Serikali. Ni kiasi gani cha fedha za kigeni kinaiingizia Serikali yetu na katika pato la Taifa. Serikali ina takwimu za wakulima wangapi kati ya nchi yetu, wangapi wameacha kujishughulisha na kilimo kwa kuona hakuna maslahi.

Mheshimiwa Naibu Spika, usumbufu wa wanyama waharibifu ni tatizo kubwa kwa wakulima wa Wilaya ya Kilwa, ikizingatiwa kuwa Wilaya hii imepakana na Mbuga ya Selous. Wanyama kama tembo, nguruwe na panya wamekuwa wakishambulia mazao ya wakulima na kufanya uharibifu mkubwa wa mazao yao, wakati wakulima wakiwa hawana nyenzo za kudhibiti wanyama hao.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Serikali iwaambie wakulima wa Kilwa mpango uliopo wa kuhakikisha

wanyama hao hawafanyi uharibifu huo tena au nini wakulima hao wakifanye kudhibiti wanyama hao.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kadhia niliyoitaja hapo juu ucheleweshaji malipo kwa njia ya stakabadhi ghalani, lakini pia kuna tatizo la ucheleweshaji wa pembejeo mpaka inafikia mwezi Mei bado uhakika wa mkulima kupata madawa ya kupulizia kwenye mikorosho haupo, kwamba, hazijulikani zitafika lini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inawahakikishia vipi wakulima wa Kilwa na mikoa inayolima korosho, pembejeo zitafika kwa wakati na kwa bei zinazokidhi maslahi ya wakulima hao ili kuendana sambamba na bei ya mauzo ya zao hilo ambayo haieleweki.

**MHE.OMARY A. BADWEL**: Mheshimiwa Naibu Spika, nimesikiliza kwa makini sana na nimerudia kuisoma Hotuba ya Bajeti ya Waziri wa Kilimo na Chakula. Ninasikitika sana licha ya yeye mwenyewe Mheshimiwa Waziri kuitembelea Wilaya ya Bahi na kuona hali mbaya inayoikabili Sekta ya Umwagiliaji, hakuna mahali popote katika Hotuba ilipoelezea namna Wizara itakavyoisaidia Wilaya hii ya Bahi katika eneo hili la umwagiliaji hasa tukizingatia Wilaya hii ni kame na kilimo cha umwagiliaji ndiyo njia pekee ya Wananchi wa Bahi kupambana na umaskini.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Mheshimiwa Waziri atakapojibu hoja mbalimbali za Waheshimiwa Wabunge, anieleze mikakati ya Wizara ya kutatua matatizo yanayoikabili Sekta ya Umwagiliaji katika Wilaya ya Bahi.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la ujenzi wa mabwawa ya umwagiliaji ni jambo muhimu pia kwa maana ya uendelezaji na uongezaji wa tija katika kilimo cha umwagiliaji kwa wakulima.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa Mheshimiwa Waziri katika hotuba ameelezea juu ya Mradi wa Uchimbaji Mabwawa miongoni mwa Mikoa aliyoitaja na Mkoa wetu

wa Dodoma upo. Sasa kwa mahitaji ya uwepo wa mabwawa ya umwagiliaji katika Wilaya ya Bahi ambayo kwa sasa hatuna hata moja, naomba kupata ufafanuzi juu ya Mradi huo wa Mabwawa; je, Wilaya yangu ya Bahi itafaidika kwa kuchimbiwa mabwawa mangapi na katika maeneo yapi ya kilimo cha umwagiliaji?

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru.

**MHE. MCH. ISRAEL Y. NATSE**: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutoa mchango wangu kuhusu Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika, katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kilimo ni ukombozi wa Mtanzania maana ndiyo ajira kubwa hapa nchini. Kutokana na mabadiliko ya hali ya nchi, nashauri Serikali iwekeze zaidi katika kilimo cha umwagiliaji. Nchi yetu imejaliwa kuwa na maeneo mazuri ya umwagiliaji kwa mazao ya mpunga, mahindi na kadhalika. Hakika Tanzania hatuhitaji kulalamika kwamba, nchi inakabiliwa na njaa na hata kuagiza chakula kutoka nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ihakikishe kuwa *skimu* za umwagiliaji katika mabonde yote zinafanya kazi sawa sawa na wawepo wataalam wa kilimo katika maeneo hayo. Kwa mfano, kilimo cha umwagiliaji katika Bonde la Eyasi, kilimo cha vitunguu, mahindi mpunga na kadhalika; kama Serikali itawekeza zaidi, hakika suala la njaa itakuwa historia.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaiomba Serikali iwe na mkakati na mpango wa kulinda wakulima wake hasa pale wakulima wanapopata shida ya masoko na kushuka kwa bei ya mazao yao, Serikali i-*subsidize* tofauti hiyo. Hii ni namna pekee ya kumkomboa huyu mkulima.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ilinde kwa udi na uvumba mazao ya wakulima wake zaidi ya kuagiza tu chakula kutoka nje wakati chakula hicho hicho kipo hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Serikali ihakikishe kuwa, pembejeo zinawafikia wakulima kwa wakati mwafaka na ihakikishe mbegu bora zinawafikia wakulima na si bora mbegu, jambo ambalo limekuwa tatizo kubwa kwa ukombozi wa mkulima.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ifanye utafiti wa kina kuhusu udongo katika maeneo yetu ili kuwapa wakulima mbegu stahiki na mbolea stahiki kwa eneo husika kuliko hali ilivyo sasa ya kutoa *package* isiyo na tija.

Mheshimiwa Naibu Spika, kusudi la kuanzishwa kwa Vyama vya Ushirika kwa mfano, *KNCU, ARCU, BCU, SHIRECU* na kadhalika ni kumsaidia mkulima wa kawaida kwa kadiri siku zilivyokwenda. Serikali imekuwa legelege, ubadhirifu na wizi umekomaa hatimaye kubadili mamlaka hizi na hata kufa kabisa. Naishauri Serikali kuweka udhibiti thabiti katika kumlinda mkulima.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la umwagiliaji na uadilifu (weledi) ni muhimu sana kwa watendaji wetu ili kumkomboa mkulima.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ichukue hatua za makusudi kuwekeza katika kilimo kwa vipaumbele kama ni mpunga maeneo yote ya umwagiliaji, mahindi hivyo hivyo, muhogo na vivyo hivyo kwa mazao ya biashara kama pamba, kahawa na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama Serikali itakuwa makini, Tanzania ni nchi tajiri sana.

**MHE. ESTHER N. MATIKO**: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchangia Hotuba hii kwa kuangalia vipengele vikuu vitatu. Kwa kuzingatia kuwa kilimo ndiyo tegemeo la Wananchi wengi wa Tanzania ambao wanaishi vijijini na hivyo kuwa vyanzo vyao vikuu vya mapato (uchumi wa mtu mmoja mmoja na nchi kwa ujumla).

Mheshimiwa Naibu Spika, tunatambua kuwa nchi yetu ina ardhi ambayo inaruhusu uzalishaji wa mazao ya chakula *(food crops)* mbalimbali na mazao ya biashara (*cash crops*).

Mheshimiwa Naibu Spika, maeneo haya ni uwezeshaji wa kilimo bora na cha kisasa (kilimo cha umwagiliaji, mbolea, mbegu za kisasa na dawa); miundombinu pamoja na masoko; tathimini ya mazao mengine ambayo hayajapewa kipaumbele ili hali ni ya muhimu kiuchumi na kiafaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni ukweli uliowazi kuwa nchi yetu imebarikiwa kuwa na ardhi kubwa na Wananchi wake kutegemea kilimo kwa ajili ya kutatua matatizo yao mengi kama chakula, kusomesha watoto na kununua mahitaji mbalimbali ya kifamilia.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakulima hawa kwa kiwango kikubwa na hapa nazungumzia wakulima wadogowadogo (*small farmers*), ambao hulima kwa kujiwezesha wao wenyewe bila kupata ruzuku yoyote toka Serikalini na izingatiwe kuwa hata ruzuku zitolewazo zinakuwa na mizengwe mingi na hivyo kupelekea Wananchi kuchoka.

Mheshimiwa Naibu Spika, inasikitisha mara baada ya mahangaiko yote hayo, wakulima wakishavuna mazao, Serikali inawapangia ni wapi pa kuuza na ni lini wauze.

Mheshimiwa Naibu Spika, hili nitalizungumzia kwa masikitiko makubwa sana na kwa kurejea mfano wa Wananchi wa Tarime, ambao mojawapo ya mazao wanayozalisha ni mahindi na mihogo. Ambapo mazao hayo na hasa mahindi ni zao la chakula na ni zao la biashara pia.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitarejea matatizo waliyoyapata Wananchi wa Tarime (wakulima), wafanyabiashara wa mahindi, ambao ni Watanzania kutoka maeneo mbalimbali, wasafirishaji wa mazao (*transporter*). Ilikuwa mwezi wa 12, tarehe za kuanzia 24, 2012 hadi Januari

mwaka 2013, ambapo Watanzania waliojitolea kwa kujiajri wenyewe (wakulima kwa kulima mazao), wasafirishaji wa mazao wenye magari na malori na wafanyabiashara wa mahindi, walipata adha kubwa sana na hawa walikuwa wakikamatwa na kuombwa rushwa, wakigoma au kukataa kutoa mazao yao yanakamatwa na kupelekwa mpakani *TRA.*

Mheshimiwa Naibu Spika, ikumbukwe wafanyabiashara hawa wamelipa ushuru wa Halmashauri, wamenunua mahindi kwenye maghala ya wakulima na wafanyabiashara na kipindi hiki wakulima hawa walikuwa wameshaanza kuvuna mahindi ya msimu huo. Cha kusikitisha sana ni kuwa, hawa wafanyabiashara wamekuwa wakifanya biashara hiyo kwa muda mrefu na walianza kusafirisha mahindi Oktoba, 2012 kwa msimu mpya bila bugudha hadi karibu na sikukuu za mwisho wa mwaka ndipo tukashuhudia polisi wa *Barrier* ya Magena, Mto Mara na kwingineko, walianza kuwakamata wafanyabiashara hawa. Pia Maafisa wa *TRA* walikuwa wakiomba rushwa waziwazi na walithubutu hadi kuwaweka ndani madereva na wafanyabiashara, kwa kisingizio kuwa mahindi yametoka Kenya.

Cha ajabu hawakuwahi kutoa zuio lolote la kuingiza mahindi kutoka Kenya. Pili, hata kama mahindi yametoka Kenya, ushuru wa bidhaa ni *zero tariff* kwa mujibu wa Soko la Afrika Mashariki; sasa iweje *TRA* waingilie kati na kuwatoza *fine* zaidi ya dola 5000 za Kimarekani? Kwa wafanyabiashara, kwa roli moja bado mwenye roli naye alitozwa *fine*. Baada ya kufuatilia sana kwa Mheshimiwa Adam Malima na Katibu Mkuu, wote walisema hamna zuio. Cha ajabu baada ya siku mbili ilitolewa barua na Mkuu wa Wilaya, kwa madai imetoka Wizarani ya tarehe 1 Januari, 2012 ikionesha zuio la kuingiza mbegu za mahindi toka Kenya kwa kuwa zilikuwa na ugonjwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, cha ajabu walichokuwa wanakamata yalikuwa ni mahindi ya chakula na wala siyo mbegu na katika sakata lote hili hapakuwepo na mtaalam

yeyote toka Wizara ya Kilimo ambaye angeweza kucheki hayo mahindi kama kweli ni ya Kenya na kama kweli yalikuwa na ugonjwa. Hata wadau waathirika na zoezi hili haramu walipokuwa tayari kumgharamia Mtaalam akague, Uongozi wa Serikali; *DC, RC* na Watendaji wengine, walikataa na kudai ni lazima mahindi yote yasagwe unga tena baada ya kulipa *fine.*

Je, huyu mkulima na mfanyabiashara na msafirishaji anapata nini na ikizingatiwa faida kwenye zao hili siyo kubwa?

Kwa nini mtu alipokuwa akitoa rushwa aliachiwa kuondoka na mahindi?

Je, akitoa rushwa ndiyo mahindi yanakuwa hayana ugonjwa au zuio?

Je, kwa nini mahindi ya Tarime yananyimwa masoko ya kuuzwa wakati ndiyo zao tegemezi kwa Wananchi wale maana ni dhahiri baada ya usumbufu ule hamna mfanyabiashara atakayerudi tena kununua mazao?

Mheshimiwa Naibu Spika, ikumbukwe siku zote Kenya inachukua mahindi toka Tarime na wala siyo kweli kwamba mahindi yalitoka Kenya. Vilevile kulikuwa na Watanzania wenye uhitaji wa mahindi yale kama Musoma Vijijini, Ukerewe, Shinyanga na kadhalika. Napenda Serikali ituambie Wananchi wa Tarime wana haki sawa na hawa Watanzania wengine. Pili, Serikali iniambie ni vipi *TRA* wanaingia kwenye usafirishaji wa mahindi ambayo hayana ushuru? Je, Polisi wanahusikaje na *DC* na *RC* wanaingiaje? Je, hakuna mtaalam wa kilimo kwenye Halmashauri ya Wilaya ya Tarime? Je, Serikali itawapelekea masoko ya mazao yao? Je, kweli Serikali ilizuia mahindi toka Kenya na siyo mbegu?

Mheshimiwa Naibu Spika, ili tuwe na kilimo chenye tija ni dhahiri Serika inatakiwa ihakikishe kuwa, asilimia kubwa ya Watanzania wanapata na kufanya kilimo cha umwagiliaji kwa kuzingatia hali ya hewa ya nchi yetu katika maeneo

mbalimbali. Pia kwa kuzingatia vyanzo vya maji, changamoto zingine ambazo ni vyema Serikali izipe kipaumbele ni miundombinu ya barabara ili masoko kufikika kwa urahisi; umeme vijijini ili kuweza kuwa na viwanda vidogo vidogo na usindikaji; na masoko mbadala ili mazao yalimwayo yapate walaji na siyo kuozea ndani.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho ni kuhusu Zao la Bangi. Kwa maoni na ushauri wangu, napenda kuiomba Serikali kupitia Wataalamu wake, wafanye uchambuzi ili kuchunguza na kujua athari na faida ya Zao la Bangi. Ifanye hivyo kwa kuzingatia kuwa, kila zao lina madhara yake kama vile tumbaku, kahawa miwa na kadhalika. Zao hili siyo tu linaipatia nchi fedha nyingi za kigeni na hivyo kukuza uchumi, bali ni dawa ya magonjwa mengi, hutumika pia kutengeneza dawa za usingizi na mafua, husaidia kurejesha nguvu za kiume, inaongeza ujasiri na mengine mengi. Hivyo, natoa rai kwa Serikali kuzingatia umuhimu wa kutoa majibu wakati wa kuhitimisha, kwani tumeshuhudia hekta nyingi zikiteketezwa hasa Wilayani kwangu Tarime, Kata ya Susuni na Mwena, Bunda.

Majuzi nimeshuhudia Kigoma zaidi ya heka kumi na hilo zao la bangi hustawi kwenye maeneo mengi nchini; yaani ni zao ambalo ni stahimili kwa misimu yote ya mwaka. Naungana na Mheshimiwa Keisy, kuhusu kufikirika kwa zao hili na kwa niaba ya Wananchi wa Tarime, wanaomba uhalalishwaji wa zao hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho ni Zao la Alizeti. Hili zao ni muhimu sana na likipewa kipaumbele tutakomesha uingizaji wa mafuta ghafi ya kula kutoka nje *(crude vegetable oil, crude palm oil, crude sunflower oil na crude soyabeans oil)* kutoka Malaysia na Marekani. Naomba wakulima kupitia *SACCOS* zao wawezeshwe mashine za kuchujia mafuta *(oil prosessing plant)* ili waweze kulima na kusindika mafuta.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba majibu. Ahsante.

**MHE. NAOMI M. KAIHULA**: Mheshimiwa Naibu Spika, suala la kuthamini wawekezaji wa nje badala ya wazalendo wetu, katika siasa ni kilimo kulikuwa na mipango mizuri ya Serikali kuanzisha Mifuko kama ya *National Food Security Co-operation (NAFCO).*

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Kilimo kutokuwa na *intelligentia* yake kuona jinsi gani nchi inaweza kuhujumiwa na kuacha kujitegemea bali kuendeleza utegemezi kwa nchi za nje kutufanya sisi tuendelee kuwategemea kuwa masoko yao ya kudumu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nini Mashamba ya *NAFCO* yameachwa bila kusaidiwa? Tunapenda kukumbatia wageni na kudharau Wananchi wetu sisi wenyewe, hatuoni kuwa tunawanyima nafasi ya kupata uzoefu pia Wananchi waliokuwa wanazunguka mashamba haya, walikuwa wanapata uzoefu na maarifa. Ni muhimu kuyafufua kama kweli tunataka kuondokana na msiba huu wa njaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie suala la *SAGGOT* kuwa ni ukombozi wa wakulima; hii siyo kweli kwani kinyume chake ni uuaji wa wakulima kwenye maeneo yenye rutuba. Hivi kwa nini hatutumii *intelligence* kuona kuwa hawa wanataka kutufanya wategemezi wao; kwani kama alivyosema Msemaji wa Kambi ya Upinzani kuwa wenzetu India yalikwishawapata wakaacha nao.

Mheshimiwa Naibu Spika, pendekezo langu ni kuachana nao mapema kabla hatujaharibikiwa. Hawa Momsanto wanaowatumia eti kuendeleza kilimo, mbegu hizi hazijafanyiwa utafiti kiasi cha kwamba, wakulima wetu wakatayarishwa kujiwekea mbegu za akiba za asili.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la matumizi ya mbolea za kigeni hili ni balaa, maana kusema ukweli ni kwamba, ukitumia mbolea za kisasa zinaua soko la wakulima, kwa kuwa inabadilisha ladha ya chakula; hivyo, watu hawapendelei kununua mazao yazalishwayo kwa

*fertizers* na soko la Ulaya ndiyo kabisa hawataki mazao ya aina hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi kwa nini Serikali haioni umuhimu wa kuwahimiza Wananchi matumizi ya mbolea za asili mfano marejea? Wakati wa Baba wa Taifa, Siasa ni Kilimo, alisisitiza kufanya tafiti za mbolea za asili na kuwashawishi Wananchi katika kutumia mbolea za asili.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, nizungumzie suala la dawa lishe. Inabidi kuwa wabunifu katika mambo mengine ambayo siyo utamaduni kama vile tunavyohamasisha kilimo cha matunda, mbogamboga, tujielekeze kwenye kuwashauri watu wetu kulima dawa lishe; mfano, alovera, mchaichai na kadhalika. Mazao haya yana soko zuri ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba Serikali isipuuze maoni haya, ni kweli mambo mengi mazuri yalikwisha tambuliwa katika Siasa ni Kilimo na yalikuwa yanatekelezeka.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishauri Wizara ifanye yafuatayo:-

- Ifufue Mashamba ya Taifa yatawasaidia kuwapatia uzoefu wataalam wetu.

- Wakulima wahimizwe na kuwekewa sheria ndogo ndogo kuwa na maendeleo ya kilimo cha chakula, pia wawe na maghala kwa ajili ya akiba.

- Kuhimiza kutunza mbegu za asili kwa ajili ya misimu, kukomesha matumizi ya utegemezi wa mbegu.

- Kuwasimamia wakulima kujiunga katika ushiriki ili kuweza kupambana na walanguzi wa kimataifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, natanguliza haya machache. Naomba kuwasilisha.

**MHE. NAMELOK E. M. SOKOINE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri yafuatayo:-

- Serikali iangalie ni kwa namna gani Bajeti ya Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika inaweza kuongezwa.

- Kodi kubwa ya ardhi ambayo ni mzigo kwa wakulima wadogo na wakati.

- Ulinzi na uhifadhi wa ardhi ya kilimo, nchi nyingi Duniani hutenga maeneo ya ardhi yote inayofaa kwa kilimo na kulindwa kwa mujibu wa sheria. Tanzania hususan Mkoa wa Arusha, ardhi inayofaa sana kwa kilimo yakiwemo mashamba ya Burka, Lakilaki, Manyara, Gomba na mengine, yamebadilishwa matumizi na kuwa viwanja. Kama utaratibu huu hautaachwa, tutakuta ardhi inayofaa kwa kilimo imekwisha na hivyo Taifa kulazimika kuagiza chakula kutoka nje.

- Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono pendekezo la Mheshimiwa Waziri kutunga sheria ya kulinda ardhi ya kilimo na ubinafsishaji wa mali za Mashirika ya Umma.

- Kuna upungufu mkubwa wa maafisa ugani; Wizara iangalie namna ya kuwaajiri.

Sehemu kubwa ya vinu na maghala ya *NMC* yamemilikishwa *Bakhressa* na *Mohamed Enterprises*. Kinu cha Arusha kimekodishwa kwa *MONABAN,* ambao wamenunua na kuweka mashine mpya za kukoboa na kusagisha ngano. Je, Serikali inapatwa na kigugumizi gani kumwuzia au kumpa mkataba wa muda mrefu? Naishauri Serikali itoe kipaumbele kwa wazawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. ENG. RAMO M. MAKANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, dhana ya Soko la Dunia inapotoshwa kwani Duniani hakuna mahala pamoja pekee panapouzwa mazao. Utafiti wa masoko ndiyo jibu pekee.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ichukue hatua kwa soko la korosho kama ilivyofanya kwa tumbaku katika Soko la China. Wengi tuna taarifa za awali kuhusu uwepo wa soko (korosho kuhitajika) mahali kadhaa duniani.

Serikali (Wizara), iitishe kongamano la wazi kubwa litakaloshirikisha wadau wa korosho kwa upana wake, siyo wale wadau *(routine),* wanaoitwa na *CBT* peke yao mara kwa mara. Katika kongamano hilo, *experts* na kadhalika, wawasilishe mada zitakazokuja na majibu ya ufumbuzi wa changamoto katika Zao la Korosho. Msimu ujao wa korosho (Septemba na Oktoba), Serikali irudishe imani kwa wakulima wa korosho kwa kununua kwa wakati na kwa bei stahiki. Suala la viwanda kuongeza thamani; Serikali iweke mkakati wa kubangua korosho nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, stakabadhi ghalani; kwa kuwa hata Serikali inakiri kutofanya vizuri kwa dhana hii (mfumo huu) na sababu ni *interference* kutoka kwa baadhi ya watu wenye maslahi na mifumo ya zamani, basi ni dhahiri wote tunakubali kuna matatizo ambayo yanarudisha nyuma pato la mkulima. Kwa kuwa inaaminika kwamba, wabaya au wahujumu wa mfumo huu wanafahamika, basi Serikali haraka na kwa uwazi, ichukue hatua mahususi kukomesha haya. Kurekebisha sheria au kutazama upya kanuni ni sawa isipokuwa hatua hizo zitachukua muda mrefu. Hivyo basi, ni vyema Serikali ikakubali kuwa na kipindi cha mpito ambapo mfumo wa stakabadhi ghalani hautatumika mpaka utakaporekebishwa.

Mkulima alikwishabeba *risks* zake wakati analima hadi kuvuna mazao yake. Mfano, mvua zisizoaminika, hali ya hewa isiyotabirika, bei za pembejeo kuwa ghali na pembejeo zisizofaa na kadhalika. Siyo vyema na siyo haki kumbebesha tena *risks* za kibiashara anazopaswa kubeba mfanyabiashara, mnunuzi wa mazao yake.

Baada ya *research (market research)* sahihi na kwa wakati, bei ya soko ya korosho itajwe kuwa moja na mkulima auze kwa mara moja, aendelee na utaratibu wa

kujiandaa na msimu wa kilimo unaofuata. Vinginevyo, baada ya marekebisho makubwa, mkulima aone faida ya stakabadhi ghalani dhahiri, siyo maneno kutoka Serikalini huku akikopwa bila kulipwa au kutolipwa kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Serikali inakiri juu ya kuwepo kwa matatizo ya ubadhirifu, ukosefu wa ujuzi au weledi au utaalamu na kadhalika, Miongoni mwa Viongozi na Watendaji wa Vyama vya Ushirika; Serikali ifanye haraka utaratibu wa ukaguzi ili kubaini ubadhirifu, kuthibitisha na kuchukua hatua kali. Binafsi, siamini kwamba ukosefu wa sheria mahususi au upungufu katika Sheria ya Ushirika, eti ni kinga kwao. Sheria zingine za nchi zitumike wakati mapitio ya Sheria ya Ushirika yakiendelea. Serikali ifanye *staff audit;* kubaini viwango vya elimu na ujuzi miongoni mwa Viongozi na Watendaji. Tatizo hili liko wazi mno katika Chama cha Ushirika cha Tunduru *(TAMCU);* hatua za haraka zichukuliwe.

Wizi na ubadhirifu wa aina nyingine uliosababisha; kwa mfano, *TAMCU* isababishe Serikali kupitia Benki Kuu ilipe dhamana ya shilingi bilioni 2.6 hauwezi kuachwa hivi hivi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mfuko wa Uendelezaji Zao la Korosho *(CDTF),* ulianzishwa kwa Sheria ya Fedha, 2010, unapewa fedha nyingi sana kutokana na mauzo ya korosho ghafi nje ya nchi; ilipaswa kusaidia uzalishaji na uuzaji wa korosho.

(a) Nani anakagua fedha za *CDTF?*

(b) *CDTF* toka ianzishwe hadi leo imeshapokea kiasi gani cha fedha?

(c) Fedha hizo zimesaidia kukuza au kuendeleza Zao la Korosho kwa kiwango gani?

(d) Nani anapima utendaji wa chombo hiki?

Ni vyema kwa haraka Serikali ikachukua hatua kama ilivyowahi kupendekezwa katika mojawapo ya vikao vya

wadau wa korosho siku za nyuma. Chombo hiki kisipewe fedha zote, badala yake Halmashauri zipewe kiasi kikubwa zaidi, kwani wao ndiyo wanaoishi na wakulima wa korosho na matatizo yao. Pia Halmashauri ni wadau, kwani kodi ya korosho inategemewa. *CDT*F ikaguliwe na *CAG,* wanazopewa ni fedha za Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, pembejeo; *CDTF* haijawasaidia wakulima *by any standards*. Serikali itafute namna mpya ya kutafuta mbolea na madawa sahihi kwa maeneo tofauti. Wakulima washirikishwe katika kuamua ni aina ipi ya dawa au mbolea inawafaa, licha ya utaalamu kuongoza katika hili. Mbolea au madawa sahihi yapelekwe kwa wakati. Mbolea au madawa yauzwe kwa bei nafuu (inayofaa). Mfumo mzima wa upatikanaji na usambazaji wa mbolea, madawa na kadhalika, uangaliwe upya na urekebishwe ili kujibu changamoto zilizopo hivi sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, dhuluma, ujanja ujanja dhidi ya wakulima wa korosho, kuwakopa wakulima, kuwacheleweshea malipo, kuwakata makato yasiyo halali kisheria na yasiyowasaidia wakulima kuhamasika na kilimo cha korosho. Wakulima wa Tunduru warejeshewe fedha zote walizokatwa bila maelezo. Walipwe fedha zao wanazodai haraka.

**MHE. BETTY E. MACHANGU:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuipongeza Wizara hii chini ya Mheshimiwa Waziri Chiza, inaonesha matumaini.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuishauri Serikali kuweka msisitizo na usimamizi mzuri katika ufuatiliaji wa kilimo cha umwagiliaji. Yapo maeneo yana mvua za kutosha; mfano, Ruvuma, Rukwa, Kigoma, Mbeya na Iringa. Maeneo haya miundombinu iboreshwe ili wafanyabiashara waende kununua mazao na kuuza katika Mikoa yenye uhaba wa chakula; mfano, Mikoa ya Kaskazini (Manyara, Arusha na Kilimanjaro).

Mheshimiwa Naibu Spika, kupitia Sheria mpya ya *PPP (2010)*, Serikali isimamie uanzishwaji wa viwanda vidogo vidogo vya kuongeza thamani *(processing)* katika mazao yanayolimwa, badala ya wafanyabiashara kununua mahindi wanunue unga uliokwishapakiwa katika kiwango tofauti; kg 10, kg 5, kg 20, kg 50 na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, maeneo yaliyoathirika na ukame mfano Kanda ya Kaskazini, ifanyike *drip irrigation*. Inawezekana kabisa ikasaidia Wananchi wa maeneo haya wakavuna kutokana na mfumo tajwa ambao wataweza pata maji kutoka visima virefu vichache halafu maji yakasambazwa kwa mfumo wa *drip irrigation*.

Mheshimiwa Naibu Spika, viwanda vya matunda vilivyofungwa katika Mkoa wa Tanga vifufuliwe ili kuweza kusindika matunda. Wakulima wa maeneo husika wafundishwe jinsi ya ku-*sort,* ku-*grade* na ku-*pack* matunda ili pale inapobidi kupeleka nchi za nje, wapate bei nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, mabonde mazuri ya kilimo mfano yaliyopo Kilombero yatengwe *specifically* kwa wawekezaji wakubwa wa kilimo ili pamoja na kuongeza Pato la Taifa, yatoe ajira kwa wakulima wadogowadogo kwa kuwapa mafunzo au stadi mbalimbali za kilimo bora. Wawekezaji hao watoe ajira kwa vijana na mashamba madogo madogo, yagawe pia kwa vijana hao. Ufuatiliaji wa uhakika wa mikataba ya wakulima wazawa na wawekezaji uwepo ili kuondoa ugomvi utakaoweza kutokea na hivyo kuleta *frustrations* kwa wawekezaji (mfano Kine - Manyara).

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru Serikali kuona umuhimu wa Sheria ya Vyama vya Ushirika ya 2003. Yapo mashamba 41 ya Serikali yaliyopewa Vyama vya Ushirika Mkoani Kilimanjaro.

Mheshimiwa Naibu Spika, Vyama hivi vimeshindwa kuendeleza mashamba hayo na badala yake wameingia mikataba na watu binafsi, ambao hawalipi pango kama

mikataba inavyosema. Mashamba hayo yameonesha jinsi Watendaji wa Vyama vya Ushirika wanavyovihujumu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ipo *coffee curing* ambayo nayo uzalishaji wake umepungua sana na inatumia mashine za zamani. Serikali ilikubali kuwaunga mkono wanahisa wa kampuni hii ya usindikaji kahawa ili wauze sehemu ya *assets* zao (nyumba) na wapate fedha ya kununua mashine ndogo za kusindika kahawa kwa ufanisi zaidi. Hii ni kampuni yenye wanahisa. Wanahisa wamekubaliana katika mikutano yao mikuu, sioni sababu Serikali inapata kigugumizi cha kumruhusu *coffee curing* kuuza mali zake ili wanunue mitambo bora. Badala yake deni walilonalo la *TRA* na *NSSF* linazidi kukua kwa sababu ya uzalishaji mdogo wa kampuni hiyo na hivyo kushindwa kulipa deni.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi binafsi niliongea na Mheshimiwa Waziri Chiza, mwezi Februari, 2013, ambaye alinihakikishia Serikali haina sababu ya kuingilia mpango wa kampuni hiyo. Mpaka leo Serikali haijaandika barua kutengua barua ambayo iliandika kuzuia hatua iliyokuwa inachukuliwa na kampuni hiyo ya kuuza sehemu ya mali zake.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imefanya vyema kuanzisha masoko ya mipakani. Lipo soko la Lokolova linatarajiwa kujengwa eneo la Makuyuni Mkoani Kilimanjaro. Soko hili likijengwa kwa wakati litaokoa sana chakula kinachopelekwa nchi za jirani kinyemela. Nchi za Sudan na Sudan Kusini na Kenya watakuja kununua chakula, watalipa fedha za kigeni na nchi itapata pato na Wananchi wa maeneo yanayolima mazao mfano mahindi kwa wingi, watapata faida au bei nzuri kwa sababu *demand* itakuwa kubwa. Nashauri Serikali iweke umuhimu katika ujenzi wa Soko la Lokolova.

Mheshimiwa Naibu Spika, kilimo cha korosho Mkoani Mtwara kitaipa Serikali ya CCM tabu huko tuendako. Yapo malalamiko mengi kuhusu ununuzi wa zao hilo. Makato ni mengi hasa kwa malipo awamu ya pili. Serikali itafute soko la *once and for all,* kwa wakulima wa korosho huko Mtwara.

Inawezekana kabisa Serikali ikaitaka *NSSF* ikishirikiana na watu binafsi, ikaanzisha kiwanda cha korosho zikabanguliwa nchini tukapata ajira kwa vijana na wanawake, pato kwa wakulima na kukubalika kwa CCM.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. LOLESIA J. M. BUKWIMBA**: Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kumpongeza Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, kwa hotuba nzuri. Nampongeza Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara, kwa kazi nzuri. Katika bajeti hii ya mwaka 20134/2014, ninaipongeza Serikali hasa kwa wazo la kuanzisha Mfuko Maalum wa kufidia bei za mazao pindi bei za mazao zinaposhuka katika soko la Dunia. Ninalo swali ambalo ningependa kupata ufafanuzi; ni lini Mfuko huu unaanza rasmi; na je, kwa mwaka 2013/ 2014 zimetengwa fedha kiasi gani kwa ajili ya Mfuko huu?

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili, ninaishauri Serikali kuwekeza katika kuboresha viwanda vyetu; kwa mfano, katika Mkoa wa Mwanza kuna kiwanda cha *MWATEX* ambacho hakifanyi kazi. Kiwanda hiki kikiimarishwa, kitasaidia sana katika kuongeza thamani ya mazao hasa pamba. Kwa kuwa kila Kanda ina zao la kibiashara na karibu kila zao la biashara linakumbana na changamoto ya bei; mfano, pamba, kahawa, korosho na chai, ni vyema ukafanyika utafiti wa kutosha kwa ajili ya uwekezaji ili kuongeza thamani ya mazao yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la tatu, Serikali inatakiwa pia kuangalia mazao ya matunda. Nchi yetu tunayo matunda mbalimbali, karibu katika kila kanda, ni vyema uwekezaji ukafanyika katika kila Kanda kulingana na matunda yaliyopo. Mfano, Mkoa wa Geita, tunazalisha mananasi kwa wingi sana, tukiwekeza katika viwanda vya *juice* ya nanasi, tutaongeza thamani ya mazao na mkulima ataweza kunufaika zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, MKUKUTA lazima ulenge kuboresha kilimo ambacho kimeajiri zaidi ya asilimia 75 ya Watanzania.

**MHE. DKT. ANTONY G. MBASSA**: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze mchango wangu nikijielekeza katika suala zima la Mfuko wa Pembejeo. Suala hili limekuwa na maelezo mazuri kwa wakulima lakini matokeo mabaya ya utekelezaji. Suala hili wazabuni wamekuwa hawaendani kabisa na hali ya misimu ya wakulima wetu na vilevile mabadiliko ya hali ya hewa. Haiwezekani mipango ipangwe vizuri, lakini utekelezaji uwe wa kusuasua kila siku. Sehemu zote suala hili limekuwa si la tija kwa wakulima walengwa hususan wakulima wadogowadogo na ambao ndiyo walengwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hili suala la Serikali kusisitiza matumizi ya mbolea ya Minjingu kwa ajili ya kupandia na kukuzia, linawapa Wananchi hali ya sintofahamu. Haiwezekani Wananchi wapande mazao yao mwezi Septemba na mbolea iletwe mwezi Novemba au Desemba. Kama mbolea ya kupandia inachukua muda mrefu kiasi hiki; je, mbolea ya kukuzia italetwa lini? Kama huku si kumwacha njia panda mkulima bila ya usaidizi wowote na mbaya zaidi pembejeo zikiletwa hazirudishwi ilimradi tu mkulima amesainishwa!

Mheshimiwa Naibu Spika, mbali na mbolea kuletwa imechelewa, kuna suala la mbegu, Wananchi wamepewa mbegu bila kuambiwa ni aina ipi. Mbegu inayopandwa na kupendekezwa ni ile chotara, lakini wengine wamepewa mbegu ambayo ni kwa ajili ya mahindi choma! Sasa suala kama ni kumkwamua mkulima kwa mbegu hii ya mahindi choma utakuwa umemsaidia nini? Hakika suala hili la pembejeo lifanyiwe mpango mkakati wa haraka ili kurekebisha huu upungufu unaozidi kumkwamisha mkulima wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nipendekeze kuwa Mfuko huu wa Pembejeo au ruzuku hii ya pembejeo iwe ya

msaada zaidi kwa wakulima kuliko kuwa ya kiabiashara zaidi. Wataalam wetu wa kilimo watusaidie sana kwa kupambanua maeneo yanayohitaji mbolea na yale ambayo hayahitaji mbolea na yale ambayo hayahitaji mbolea ya viwandani, lakini pia hata mbegu zinazostahili katika maeneo husika. Hakika haya masuala yakifanyiwa kazi, naamini tutainua hali ya kilimo chetu na pia hata uwezo binafsi wa wakulima kiuchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, haya yote niliyoyaeleza ni hali halisi ya wakulima Jimbo la Biharamulo Magharibi. Haya yote hata yakifanyika vizuri, bado kuna suala la masoko ya mazao haya. Mkulima hajapewa mazingira mazuri ya mazao yake, leo hii hakuna soko, Maafisa Ushirika wetu hawasaidii katika hili. Haraka wakulima wanapozalisha mazao hujikuta wamefikiwa na walanguzi na hivyo kuuza pasipo utaratibu mzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata kwa mazao ambayo yanalimwa hakika bei hii yake imekuwa si ya kumwinua mkulima; mfano Zao la Muhogo leo hii muhogo. Leo hii muhogo wa Biharamulo unauzwa nchi za Rwanda, Burundi, Uganda na hata DRC, lakini muhogo huu haujamfaidisha mkulima kwa lolote, matokeo yake wafanyabiashara ndiyo wameneemeka na mazao ya wakulima hawa. Naiomba Serikali kupitia hawa Wataalam, kufanya juhudi za makusudi za kutafuta masoko, kuanzisha na kuhimiza Vyama vya Ushirika na Misingi. Hakika Maafisa Ushirika wakifanya kazi yao vizuri, wakulima wote wataondokana na umaskini huu walionao.

**MHE. ALBERT O. NTABALIBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuipongeza Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika, kwa kazi nzuri inayofanywa na Wizara, licha ya changamoto zinazoikabili Sekta hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kupata ufafanuzi kwa mambo yafuatayo:-

Kwanza, kuhusu masoko ya mazao ya kilimo kupitia Mradi wa *DASP*. Wizara imesema imekamilisha usanifu wa miundombinu ya masoko na Jimbo langu la Manyovu limepangiwa kujengewa soko la Mnanila; je, ni lini sasa soko hili litaanza kujengwa? Je, katika bajeti hii imetengwa fedha ya utekelezaji wa Mradi huu? Muhimu ni kwamba, Serikali imeahidi muda mrefu na Wananchi wanasubiri utekelezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, maombi langu juu ya soko la kahawa ni yafuatayo:-

Bei ya kahawa 2013/2014 imefikia shilingi 4500 badala ya shilingi 7000 - 8000 ya mwaka jana. Wakulima wametoa malalamiko; hivyo, naomba Serikali iangalie namna ya kuokoa zao hilo ili wakulima wapate unafuu. Naomba Serikali ilitolee tamko na wananchi wasikie. *Price Stability Fund* ndiyo jibu la wakulima.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inaombwa kutoa tamko la kutaka walioenda kutapeli wakulima wa Jimbo la Manyovu na Kigoma Kaskazini kwa kuchukua kahawa zao na hivyo kufanya wakulima washindwe hata kugharimia huduma za shule na afya kwa familia zao. Wakulima wanahangaika bila ya kujua la kufanya, naomba Serikali itoe tamko.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba programu ya kuboresha migomba iliyo bora, ambayo mbegu mpya imeanza kusambazwa katika Jimbo la Manyovu liwe zao lenye tija. Tunaomba Wizara ya Kilimo itumie wataalam wao ili wakulima wengi wafaidike na zao lipate bei kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba Wizara iniongezee wataalam katika Wilaya mpya ya Buhigwa kwani tuna wagani watano tu, kitu kinachoathiri kilimo ndani ya Wilaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Kigoma inajitosheleza kwa chakula na haijapewa chakula cha

msaada na Serikali; je, Serikali inawapongeza vipi Wananchi wa Kigoma?

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaiomba Wizara itume wataalam waje kufanya usanifu kwenye mabonde ya Tarafa ya Muyama – Buhigwe katika Kata za Mugera, Milelema na Biharamulo ili tuanzishe kilimo cha mpunga na mazao yatakayofaa. Hiki kitakuwa kilimo cha umwagiliaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, pembejeo ya mbolea inayotolewa inatumika hata kwenye kahawa. Serikali iangalie kama hakuna madhara yoyote juu ya matumizi hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, nawatakia Wizara ufanisi bora.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuunga mkono hoja.

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA**: Mheshimiwa Naibu Spika, natoa pongezi kwa Mheshimiwa Waziri, Naibu wake na Watendaji wote, kwa kuandaa bajeti hii na kuleta hapa Bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania haiwezi kuwa na kilimo cha kisasa, chenye kuwa na tija na kuwasaidia Wananchi kwa ujumla, kama Serikali haitatenga fedha za kutosha kwenye Wizara hii muhimu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo Serikali inalalamika vijana wamekimbia vijijini wanakwenda mijini kutafuta namna ya maisha baada ya kukaa mashambani na kuona kilimo cha kienyeji hakilipi na hakina tija! Matokeo yake, nguvu ya vijana ambayo ni ya kuzalisha inapotea mijini kwa kurandaranda na kujiingiza kwenye mambo ya ovyo, pombe, kuvuta bangi na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaitaka Serikali ihakikishe inatafuta pesa za kutosha kuwekeza kwenye kilimo. Pembejeo zitolewe kwa muda na za kutosha. Mfumo mpya

wa kutoa pembejeo kwa njia ya mikopo haujafanyiwa maandalizi yoyote na hivyo hautafanikiwa. Serikali isimamie kikamilifu mfumo uliopo wa kutoa ruzuku ya pembejeo, kutoa mianya ya wizi na kuwawajibisha watendaji wakati inajipanga kwa mfumo mpya.

Mheshimiwa Naibu Spika, bila umwagiliaji, kilimo chetu bado ni cha kubahatisha sana, hatuwezi kutegemea mvua leo wakati tunajua mvua zimekuwa chache kutokana na mabadiliko ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hakuna fedha za ndani zilizotengwa kujenga miundombinu ya umwagiliaji tangu Sera ya KILIMO KWANZA ianzishwe mwaka 2009. Leo ni miaka mitano, Sera ya KILIMO KWANZA haijatekelezwa kikamilifu, imebaki kwenye vitabu na mafaili ofisini.

Mheshimiwa Naibu Spika, hatuwezi kuwa na kilimo cha kisasa bila kufanya tafiti kwa kila hatua. Tunavyo vituo vya utafiti maeneo mbalimbali, fedha zinazotolewa kuendesha vituo hivi ni kidogo sana. Vingine vimedumaa kabisa. Wataalam walioko kule fani zao hazitumiki kuleta maendeleo ya Taifa hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kituo cha Utafiti wa Miwa Kibaha ambacho kina wataalam waliobobea kufanya utafiti na kupambana na magonjwa ya miwa kwa njia ya kibayolojia kimesahaulika kabisa; mwaka 2011/2012 hawakupewa *OC* hata shilingi moja, pamoja na kuwa kwenye bajeti hapa Bungeni walitengewa shilingi 40,000,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeacha Chuo au Kituo hiki kiendeshwe kwa fedha kidogo inayotolewa na Bodi ya Sukari na wadau wengine wa miwa. Hii ni hatari sana sana, kuna hatari ya Kituo hiki kufa.

Mheshimiwa Naibu Spika, uwezo wetu kama nchi wa kuzalisha mbegu ni mdogo sana. Kwa kiasi kikubwa wakulima wanategemea mbegu kutoka nje, ndani ya miaka

52 ya Uhuru na nchi inyotegemea kilimo, zaidi ya robo tatu ya mbegu tunategemea nje, hii ni aibu kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mahitaji ya mbegu kwa nchi yetu ni tani 120,000 kwa mwaka. Mbegu zinazopatikana ndani ya nchi ni tani 40,000 zikiwepo tunazozalisha wenyewe na zinazoagizwa na makampuni mbalimbali kutoka nje ya nchi. Kiasi tunachozalisha sisi wenyewe ni tani 18,000 tu ambazo zinazalishwa na Wakala wa Mbegu *(ASA)* na Mashirika Binafsi. Hivi kweli kilimo bila mbegu?

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua madhara yatokanayo na mbegu kutoka nje ya nchi. Kwanza, ni ghali sana, lakini pia magonjwa mengi tuliyonayo kwenye mazao yetu yametoka nje na mengi yamekuja kwa njia ya mbegu.

Mheshimiwa Naibu Spika, *ASA* wapatiwe uwezo wa pesa wafanye kazi kwa ufanisi, wazalishe mbegu za kutosha na zilizo bora. *ASA* ipewe pesa ya kufanya utafiti, pesa ya utafiti wa mbegu zinazopelekwa *COSTECH* zilipelekwe *ASA.*

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali iliambie Bunge ni kwa nini Zao la Tumbaku linanunuliwa kwa Dola ya Marekani? Kwa nini pembejeo zinakopeshwa kwa dola? Kwa nini pesa inalipwa kwa fedha ya Tanzania *(Tshs.)?*

Serikali inatambua uelewa wa Wananchi wake wa vijijini; kwa nini wanaunga mkono makampuni kuibia Wananchi wa Mkoa wa Tabora na Mikoa mingine?

Mheshimiwa Naibu Spika, Vyama vyote vya Ushirika vinakufa kwa sababu ya ubinafsi na ulaji wa Viongozi waliopewa dhamana ya kusimamia, uwezo mdogo wa Maafisa Ushirika na Wanasiasa kujiingiza kwenye masuala ya utendaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ilieleze Bunge ni hatua gani zilizochukuliwa kwa Mabenki yaliyoshirikiana na

Watendaji wa Vyama vya Ushirika kuchukua mikopo mikubwa na kubambika madeni hayo kwa Wanaushirika?

**MHE. ENG. GERSON H. LWENGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, naunga mkono hoja hii ya Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze mchango wangu namna Serikali inavyopaswa isimamie kilimo chenye tija. Tumeliongea na liko ndani ya Hotuba, lakini utekelezaji wake unahitaji mikakati zaidi inayoweza kutufikisha kwenye Malengo ya Milenia na Mpango wa Maendeleo Vijijini 2025.

Mheshimiwa Naibu Spika, lazima tuanze na kuwanyanyua hawa wakulima wadogo ambao ndiyo wengi wanaozalisha chakula. Zana za pembejeo ni duni, hakuna huduma za mabwana shamba ijapokuwa wapo kila Kata na hata vijiji, lakini hawasimamiwi. Mimi nalima kila mwaka zaidi ya ekari 500 Kijiji cha Matanga, Wilaya ya Dodoma, kwa zaidi ya miaka kumi, lakini sijawahi kumwona bwana shamba wa eneo hilo, pamoja na kijiji kuongoza kwenye uzalishaji wa mazao ya mahindi na alizeti. Nilichangia hoja hii kwenye Bajeti ya Wizara hii mwaka 2012, lakini sijaona hatua yoyote iliyochukuliwa na Wizara hii kwenye eneo hili, bila wakulima.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya yangu ya Wanging'ombe tunalima sana viazi mviringo, tatizo letu kubwa Wananchi wanapata tatizo namna ya kuuza viazi kwa vipimo vya gunia la kg. 100. Wanunuzi pamoja na madalali wamekula njama ya kumlazimisha mkulima auze kwa vipimo vya Lumbesa. Naomba Wizara itafute mbinu ya kuzuia utaratibu huu ili mkulima apate faida kubwa na kuweza kumwinua kiuchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ni mmojawapo niliyekopeshwa trekta na jembe toka mfuko wa pembejeo, lakini wana urasimu mkubwa sana, toka mkulima analeta ombi mpaka anafanikiwa. Pia masharti ya Mfuko huu kutaka kuwa na dhamana ya nyumba na kadhalika. Hatutaendeleza kilimo kwa kasi inayotakiwa. Nashauri hili lirekebishwe na pia

riba ipunguzwe ili Mfuko huu uweze kuvutia wakulima wengi zaidi na kwa namna hiyo Kilimo kitainuka.

**MHE. HEZEKIAH N. CHIBULUNJE**: Mheshimiwa Naibu Spika, naiunga mkono hoja ya Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika. Nyongeza ya mchango wangu ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kilimo na umwagiliaji ni muhimu sana katika maeneo kama ukiwemo Mkoa wetu wa Dodoma. Ukipitia Jedwali Namba Mbili la Skimu za Umwagiliaji zinazotekelezwa katika mwaka 2012/2013, utaona kwamba Kanda ya Kati iko skimu moja tu ya Kongwa. Naomba kupitia Bajeti ya mwaka unaokuja wa 2013/2014, Kanda ya Kati itiliwe maanani kwa kutupatia skimu za umwagiliaji zitakazoweza kutukomboa Wakulima wa Kanda ya Kati.

Mheshimiwa Naibu Spika, narudia kuomba na kusisitiza Serikali iangalie uwezekano wa kulifufua Bwawa la Skowa. Wizara inajua kuwa miundombinu mingi ya bwawa hili bado ni imara, isipokuwa kujaa tope kwenye bwawa hili ambako kunahitaji kuchimbuliwa. Ni tegemeo langu kuwa, ombi la Wananchi wa Chalinze ambako bwawa hilo lipo, litapokelewa na Wizara na kuwatekelezea ipasavyo.

**MHE. ZARINA S. MADABIDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mchango wangu kwa Waziri Mkuu, niliomba Serikali kuchukua Sekta ya Kilimo na kugeuza mamilioni ya ajira kwa vijana. Vijana ni asilimia karibu sitini ya Watanzania na ndiyo nguvu kazi ya nchi. Kilimo ni shughuli kwa Watanzania zaidi ya asilimia sabini na tano. Kwa hiyo, ni dhahiri ni lazima kipewe umuhimu wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, Watanzania kama wakulima, wengi wao bado wanatumia zana duni, mbegu zisizo na tija na ukulima usio wa kitaalam. Tunaweza kukuza sana uchumi wa nchi na watu binafsi na kuonekana iwapo Serikali itaingilia kati na kuwawezesha vijana kwenda kwenye

kilimo. Hakuna kijana atakayekwenda kwenye kilimo kisicho na tija, maana atatumia nguvu nyingi kwa mapato madogo na matokeo yake wanakimbilia mijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri Serikali iandae mashamba kwenye ardhi yenye rutuba na maji ya uhakika. Iandae ardhi kwa kulima kwa matrekta, wawape kwa mkopo mbegu bora, mbolea, dawa na hata mahitaji ya awali ili waweze kujikimu kwa mwaka wa kwanza. Gharama hizo vijana hao walipe kwa mikupuo mitatu (miaka mitatu), ya mwanzo. Tumeshuhudia jinsi wale vijana wa chuo kikuu walioamua kwenda kulima baada ya kukosa ajira mijini; mafanikio yao yametia hamasa sana kwa vijana. Sasa naomba Serikali itumie fursa ya hawa vijana kuweza kuingiza vijana wengi kwenye kilimo cha tija. Wakati ni huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kilimo cha matunda; Tanzania tumejaliwa matunda mengi ya kila aina; machungwa, ndizi, maembe, mananasi na kadhalika. Mimi nilikwenda Botswana, nilishangaa mashamba makubwa sana ya mananasi. Botswana ni nchi ndogo sana, ni vipi Tanzania na ardhi hii tuliyonayo tunashindwa kuwa na mashamba kama yale? Suala litakalokuja ni soko, tumeshuhudia matunda mengi yanaoza bila kutumika. Ni masikitiko makubwa sana, viwanda vingi vya Serikali vya kusindika matunda vimekufa vyote. Vile vilivyobinafsishwa aidha havifanyi kazi au kama vinafanya kazi wananunua kwa bei ndogo sana kiasi mkulima anapata hasara na kudharau au kutokuona tija kuendelea na kilimo hicho cha matunda.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ni mkulima wa maembe, zao hilo kama lingepewa maana lingeweza kuondoa umaskini. Mwembe mmoja wa kisasa unaweza kumtolea mkulima kati ya shilingi 150,000 - 300,000, kutegemeana na matunzo. Mkulima akipanda hata miembe ishirini tu anaweza kupata mpaka shilingi milioni sita kwa mwaka au wastani wa shilingi laki tano kwa mwezi, juu ya kima cha chini cha mshahara wa mtu mjini. Pamoja na miembe wakati wa masika, shamba lile lile mtu anaweza

kulima mazao ya chakula, lakini pia anaweza kufuga na mabaki ya mazao ya chakula ikawa ni chakula cha mifugo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi pamoja na kazi nyingine, kilimo ni *hobby* yangu. Nimekuwa nalima kwa zaidi ya miaka ishirini Wilayani Kibaha. Sijawahi kumwona bwana shamba zaidi ya mara mbili na mara zote ni baada ya sisi kutoa taarifa ya matatizo ya viwavijeshi kuvamia mashamba. Ni vipi mkulima ataendelea iwapo hana msaada wowote wa kitaalam?

Namkumbuka Mheshimiwa Barongo wakati akiwa Waziri wa Kilimo na *Slogan* ya Chakula Bora Shambani, Mvua za Kwanza ni za Kupandia.

**MHE. AUGUSTINO M. MASELE**: Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja ya Wizara. Kilimo ndicho kinachoajiri Watanzania walio wengi; hata hivyo, kilimo chenyewe kinakabiliwa na changamoto nyingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pembejeo za kilimo hazipatikani kwa wakati. Zana za kilimo hasa matrekta ndiyo hasa yanaweza kuleta Mapinduzi ya Kilimo nchini. Hata hivyo, yapo matatizo makubwa kwa wakulima walio wengi ambao ni wengi hawakopesheki, matokeo yake kuyapata matrekta yanapoingia nchini kupitia SUMA JKT.

Mheshimiwa Naibu Spika, Zao la Pamba ndilo uti wa mgongo wa uchumi wa wakulima katika Mikoa ya Kanda ya Ziwa, kwani ndilo zao la biashara. Hata hivyo, bei ya zao hili imekuwa haibadiliki kwa kuwa imekuwa ikipanda mwaka mmoja mwaka unaofuata inashuka. Kwa mfano, bei iliwahi kufikia shilingi 1,200, lakini mwaka uliofuata bei ikashuka mpaka kufikia shilingi mia sita tu kwa kilo. Hali hii imekuwa ikiwavunja moyo wakulima. Zao hili likiachwa kulimwa na wakulima, ipo athari kubwa kwa uchumi wa mkulima mwenyewe na kwa Taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, Taifa letu linakabiliwa pia na ukosefu wa viwanda vya kutengeneza nyuzi na nguo ili

hatimaye ziuzwe kwenye masoko ya nje na kulipatia Taifa letu fedha za kigeni. Hali ya hewa nayo imekuwa haitabiriki, matokeo yake vyakula vimekuwa vikilimwa na kukaushwa na jua na kwa hali hiyo imekuwa ikisababisha uhaba wa chakula kila mwaka. Katika Jimbo la Mbogwe na Wilaya ya Mbogwe, yapo maeneo yanayofaa kwa shughuli za umwagiliaji kwa kuwa yapo mabonde yenye rutuba.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishauri Serikali ifikirie uwezekano wa kutuma wataalam wake wafike kuitembelea Wilaya yetu na kuona uwezekano wa kuwekeza katika shughuli za umwagiliaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Serikali kwa kuja na wazo la kuwa na Mfuko Maalum wa kudhibiti kuyumba kwa bei *(Price Stabilization Fund*). Iwapo Serikali itafanikiwa katika hili kwani itakuwa ni ukombozi kwa wakulima wote wa mazao ya biashara hasa pale bei za masoko haya inapoanguka katika masoko ya ulimwengu.

Mheshimiwa Naibu Spika, upimaji wa ardhi na umiliki wa ardhi kwa kimila. Hati hizi zimekuwa haziheshimiwi na vyombo vya kifedha hasa mabenki kama dhamana ya kuwezesha kupata mikopo ili waweze kuboresha shughuli zao za kilimo na kuboresha maisha yao. Naiomba Serikali itoe tamko kwa vyombo vya fedha hasa mabenki kuziheshimu hati miliki za kimila na kuzipokea kama dhamana kwa mkulima wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishauri Serikali ilete Bungeni Sheria ya Ushirika Nchini ili kuimarisha Vyama vyetu vya Ushirika vihusike kikamilifu katika kumsaidia mkulima wa kawaida ili aweze kuboresha maisha yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. RITA L. MLAKI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchangia hoja ya Wizara ya Kilimo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, nampongeza Waziri na Watendaji wake kwa ujumla, kwa Hotuba nzuri. Naomba kuchangia kuhusu Serikali kuwasaidia Wananchi katika Sekta hii ya Kilimo. Kilimo cha kibiashara kiendelezwe ili kukuza uchumi wetu. Nchi yetu ina ardhi nzuri, yenye rutuba na ni kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali iwasaidie wakulima kuanzisha mashamba makubwa. Serikali ipime mashamba, itafiti mazao yapi yapandwe eneo hilo, ilete mtaalam, iweke miundombinu ya umwagiliaji na iwape wakulima hayo mashamba wayaendeshe. Vilevile Serikali idhamini mikopo kwa kuendeleza mashamba hayo. Mwisho, Serikali itafute masoko ya hayo mazao. Hiyo ndiyo kazi ya Serikali, natumaini Serikali imeona, kwa miaka hamsini tumesema kilimo ni *back borne* ya uchumi wetu, lakini mpaka sasa bado kinachangia asilimia ndogo katika uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Serikali kwa kusimamia kilimo cha chakula na nchi yetu haina shida ya chakula.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja.

**MHE. GOODLUCK J. OLE-MEDEYE**: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, nampongeza sana Mheshimiwa Eng. Christopher Kajoro Chiza (Mb) - Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, Mheshimiwa Adam Kighoma Ali Malima (Mb) - Naibu Waziri pamoja Katibu Mkuu, Wakuu wa Idara na Wenyeviti wa Bodi ya Watendaji Wakuu wa Taasisi na Watumishi wote wa Wizara, kwa kazi nzuri wanayoifanya, kusimamia Sera na Sheria, kutoa ushauri na huduma mbalimbali kwa wakulima wetu wadogo na wakubwa ili kuongeza uzalishaji wa mazao ya biashara na chakula na hivyo kutegemeza Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza sana Serikali yetu kwa uamuzi wake wa kuteua Kilimo kuwa moja ya sekta za kipaumbele katika Programu ya “TEKELEZA KWA MATOKEO

MAKUBWA SASA." Nina matumaini kuwa, chini ya uongozi wa Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri, malengo yaliyowekwa kwa Sekta hii yatafikiwa bila wasiwasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu upatikanaji wa pembejeo; naishukuru Serikali kwa jitihada inazofanya kuwapatia wakulima pembejeo za kilimo ili kuongeza uzalishaji wa mazao ya chakula na biashara nchini. Napongeza hatua iliyochukuliwa kuzuia usambazaji wa mbolea zisizofaa, unaofanywa na wafanyabiashara wenye tamaa ya utajiri kwa gharama ya uhai wa Wananchi wetu. Nashauri kuwa ili kukomesha tabia hii, Serikali irekebishe sheria ili kuweka adhabu kali itakayotumika kwa wale wote watakaobainika kusambaza pembejeo zisizofaa nchini. Makampuni hayo yapigwe marufuku kufanya biashara hiyo nchini. Adhabu iliyotolewa kwa makampuni yaliyobainika kama yalivyotajwa kwenye Hotuba ya Mheshimiwa Waziri, itolewe pia kwa wasambazaji wa mbegu na pembejeo nyinginezo. Mwaka jana nilishauri juu ya umuhimu wa Serikali kufanya uchunguzi wa udongo kabla ya kusambaza mbolea ili kujua aina ya mbolea inayohitajika na udongo unaohusika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kilimo cha umwagiliaji; kutokana na mabadiliko ya tabia nchi, mvua inaendelea kupungua na hivyo kuathiri uzalishaji wa mazao mbalimbali. Kwa kuzingatia kuwa mito mingi iliyokuwa ikitoa maji yaliyokuwa yakitumika kwa umwagiliaji imepungua maji au kukauka kabisa, nashauri kuwa Serikali ione uwezekano wa kuwekeza kwenye uendelezaji wa vyanzo vya maji ya chini ya ardhi kwa ajili ya kuendeleza kilimo cha umwagiliaji pamoja na kuchuja majitaka ili yatumike kwa umwagiliaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuzingatia uzoefu uliopo maeneo mengi ya nchi yetu ambapo mvua hunyesha nyingi mara moja kwa kipindi kifupi na hivyo inapokatika Wananchi huachwa wakiangalia mazao yasiyokomaa yakikauka. Nashauri kuwa Serikali isaidie kuwekeza kwenye ujenzi wa malambo na penye mito ijengwe mabwawa ili kuwezesha Wananchi kumwagilia mashamba yao na hivyo kuepuka adha ya kuomba chakula kila mwaka. Katika

Jimbo langu la Arumeru Magharibi, naomba Wizara itusaidie kujenga malambo kwenye Kata za Olkokola, Oldonyosambu, Mwandet, Musa, Kisongo, Mateves, Oljoro na Bwawani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu vijana katika kilimo; nampongeza sana Mheshimiwa Waziri na wasaidizi wake, kwa kuanzisha programu ya kuwezesha vijana kujiajiri kwenye kilimo. Nashauri kuwa Wizara ifanye programu hii kuwa endelevu ili vijana wanaomaliza masomo katika fani mbalimbali waweze kujiajiri badala ya kuzurura mijini kutafuta ajira ambayo haipo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu utafiti; nimeona kazi nzuri ya utafiti inayofanywa na wataalam wetu kwenye vituo vya utafiti ikiwepo Taasisi ya Utafiti ya Mikocheni kwa lengo la kupata mbegu bora zinazotoa matunda mengi zaidi. Hata hivyo, kwa sababu ya Serikali kusikiliza maoni ya watu wenye imani potofu juu ya athari za mbegu hizo kwa afya ya binadamu na mazingira, hadi leo matokeo ya tafiti hizo bado hayajaanza kutumiwa Tanzania, ingawa ziko taarifa kuwa nchi jirani zinatumia matokeo ya tafiti zetu. Nashauri kuwa ili kuongeza uzalishaji wa mazao ya chakula na biashara, pamoja na kupata mbegu zenye kustahimili ukame na magonjwa, Serikali iruhusu majaribio ya uzalishaji yaanze kufanyika kwenye baadhi ya maeneo nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu usalama wa chakula; Mkoa wa Arusha ni moja ya maeneo yanayokabiliwa na upungufu wa chakula kutokana na kutopata mvua za kutosha. Serikali imekuwa ikisaidia Wananchi kuwapatia chakula cha msaada na cha kazi kwa takriban miaka mitano sasa. Kero ambayo Watendaji wa Wilaya na Wananchi pamoja na Wanasiasa wamekuwa wakipata ni ghala la *NFRA* kutokuwa na chakula pale kibali kinapotolewa na Ofisi ya Waziri Mkuu. Mwaka jana mwezi Aprili, baada ya maombi kuwasilishwa na Halmashauri ya Wilaya ya Arusha na Ofisi ya Waziri Mkuu kufanya uhakiki, kibali cha kupata tani 1,200 kilitolewa. Hata hivyo, baada ya Wilaya kuteua msambazaji, alipofika *NFRA* aliambiwa chakula hakipo. Hali hiyo ilijirudia

tena mwaka huu ambapo hadi niandikapo maoni haya, ni sehemu tu ya chakula tulichopangiwa mwezi Februari, 2013 kilichopatikana na maelezo ni kuwa ghala halina akiba ya chakula. Je, kwa nini Serikali haina mpango mahususi wa kuhakikisha kuwa ghala linakuwa na chakula cha kutosha mwaka mzima?

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. MURTAZA A. MANGUNGU:** Mheshimiwa Spika, napenda kuwasilisha kwako mchango wangu katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika kuhusu Makadirio ya Matumizi ya fedha ya Ofisi yake kwa mwaka 2013/2014.

Mheshimiwa Spika, Wizara hii ndiyo inayosimamia uti wa mgongo wa nchi yetu. Zaidi ya asilimia 80 ya Watanzania wanaishi kutegemea kilimo.

Mheshimiwa Spika, kwa miaka mingi sasa toka uhuru wa nchi yetu, kumekuwa na jitihada za aina mbalimbali katika kuboresha kilimo. Licha ya jitihada hizi, bado hazijazaa matunda.

Mheshimiwa Spika, uvumbuzi wa gesi asili nchini unaweza kusaidia sana kuboresha kilimo nchini kama fursa hii itatumika vizuri na ipasavyo. Sekta hii inaweza kusaidia kuinua kilimo kwani upatikanaji wa umeme utasaidia sana kuyaandaa mazao ya wakulima kabla ya kwenda sokoni *(processed or semi processed)* ambapo thamani itaongezeka.

Mheshimiwa Spika, mfumuko wa bei ni asilimia 19.5 hadi 9.8. Serikali iweke mkazo na jitihada katika kupunguza mfumuko lakini pia kudhibiti bei ya vyakula kama inavyofanyika kwa bidhaa nyingine kama nishati, simu na usafiri. Nchi nyingi duniani kama Indonesia, India, Malaysia na Singapore zimeweka zuio katika bei za vyakula.

Mheshimiwa Spika, bei ya sukari nchini ni kitanzi kikali sana. Ukiangalia maeneo yanayozalishwa sukari (Kagera,

Mtibwa, Moshi, Kilombero) bei kubwa kuliko maeneo mengine ya nchi. Kwa mfano, Zanzibar bei ya sukari ni wastani wa Sh. 1,000/= hadi Sh. 1,200/= kwa kilo. Lazima jitihada za makusudi zifanyike kuhakikisha kuwa viwanda vya ndani vikidhi mahitaji na kutoa unafuu kwa wananchi siyo kuwawekea mazingira ya kutengeneza faida haramu.

Mheshimiwa Spika, ili kukabiliana na mfumuko wa bei, Serikali mwaka 2012 ilikubali kutoa pesa kuwa *NFRA* ili wasage mahindi kushusha bei katika soko. Hadi leo hakuna pesa za mtaji zilizotolewa kwao na usagishaji umebaki kuwa ni wafanyabiashara wachache ambao wanawania faida iliyopindukia.

Mheshimiwa Spika, mfumo wa ununuzi wa korosho uangaliwe upya na vizuri ili kuondoa kasoro zilizopo. Vyama vya Ushirika vinakuwa na madeni makubwa ambayo siku zote wanalipa kwa kutumia mazao ya wakulima.

Mheshimiwa Spika, pembejeo za kilimo na viatilifu *(sulphur)* zitolewe bure, lakini pia tuelezwe siku zote Bodi ya korosho huwa wamewapa wakulima gani pembejeo kwa maana maeneo mengi hakuna aliyepokea. Hii ni changamoto kwao kuweka mfumo unaeleweka maana wanaowakabidhi kazi mara nyingine hawafanyi inavyotakiwa.

Mheshimiwa Spika, mradi wa kuboresha kilimo cha minazi ilikuwa ni kwa lengo lipi? Maana wakati huu ambao tunapata shida katika kilimo, hatuoni msaada wowote kiasi kwamba hata Wizara imeshindwa kulizungumzia katika hotuba ya bajeti hii. Huu ni uonevu kwa maana mradi ule ulikuja kuua minazi yetu ya asili na kuwabana wananchi kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, maeneo mengi katika Mikoa ya Kusini kwa maana ya Lindi, Mtwara, Ruvuma na Pwani wananchi wanafanya kilimo cha kuhamahama. Hii inatokana na mbinu za asili kubadilisha mashamba kila msimu. Utaratibu huu unatugharimu sana kutokana na

kuweka jitihada za makusudi kuelimisha wananchi matumizi ya viatilifu na namna ya kushiriki kilimo bora chenye ufanisi na tija.

Mheshimiwa Spika, baada ya Mheshimiwa Rais kutathmini, aliamua kuitisha kikao muhimu na yafuatayo yaliyoafikiwa katika Kikao cha Tathmini ya Utendaji wa Serikali kilichofanyika Ikulu, Dar es Salaam, Jumatatu, Machi 2, 2009 kati ya Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete na uongozi wa Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika na Taasisi zake:-

(a) Kwamba viongozi wasijivue wajibu wao wa kusimamia maendeleo ya wananchi ya kuleta mageuzi ya kilimo kwa kutumia kisingizio cha dhana ya wananchi kuibua miradi yao ya maendeleo, kwamba ni wajibu wa viongozi kuwaongoza wananchi katika kuibua miradi ya kilimo yenye lengo la kuimarisha kilimo cha Tanzania;

(b) Kwamba nguvu mpya ielekezwe katika kuinua tija katika kilimo kwa kutumia zana za kisasa zaidi na mbinu bora zaidi kwa sababu ni Sekta ya Kilimo ambayo itawaondoa watu wengi zaidi katika umasikini nchini na kwa haraka zaidi;

(c) Kwamba nchi ijielekeze kwa dhamira kubwa zaidi katika kuhakikisha kuwa inajitosheleza kwa chakula hasa hali ya sasa ya matatizo makubwa katika uchumi wa dunia;

(d) Kwamba upatikanaji wa mikopo ndiyo mkombozi wa Sekta ya Kilimo na hivyo juhudi ziongezwe kuhakikisha kuwa Serikali inafanikisha uanzishaji wa Benki ya Kilimo, ili kufungua njia kwa wakulima kupata mikopo ya uhakika kuendeleza na kuboresha shughuli zao;

(e) Kwamba katika masuala muhimu yanayohusu Sekta ya Kilimo, viongozi wasichelewe kufanya maamuzi kwa sababu ni dhahiri kuwa kwa sasa kuna ucheleweshaji sana wa maamuzi muhimu katika sekta hiyo;

(f) Kwamba iandaliwe programu maalum ya kulifanya zao la muhogo na matunda yanayotokana na zao hilo kuwa la kibiashara zaidi;

(g) Kwamba ili kuziba pengo la chakula lililoanza kujitokeza nchini na kupunguza makali ya bei za vyakula kwa sababu ya mvua ya shaka, wafanyabiashara waruhusiwe kuingiza nchini kiasi cha tani 300,000 za nafaka kutoka nje kwa miezi mitatu hadi Mei 31, mwaka huu 2013, bila kodi wala ushuru;

(h) Kwamba nchi ijielekeze katika kuwekeza kwa umakini zaidi katika maeneo mapya, na hasa katika uendelezaji wa kusindika matunda na kuwekeza kwa nguvu zaidi katika kilimo cha maua kama njia ya kupanua wigo wa mapato ya Taifa na kuongeza ushindani wa uchumi wa Tanzania;

(i) Kikao hicho pia kilijadili kwa kina hali ya masoko ya mazao ya kilimo duniani katika hali ya sasa ya matatizo makubwa ya uchumi duniani, na kukubaliana kuwa upo umuhimu mkubwa wa kutafutwa njia za haraka kuwalinda wakulima wa Tanzania, na kwa kuanzia walindwe wakulima wa zao la pamba linalolimwa katika Mikoa 11 nchini na ambao bei yake imeshuka sana duniani;

(j) Kwamba bajeti ya Sekta ya Kilimo iongezwe katika Bajeti ya Serikali ya mwaka ujao, kama njia ya kuhakikisha kuwa sekta hiyo inapata raslimali za kutosha kuweza kutimiza wajibu wake kama mwajiri mkuu nchini;

(k) Kwamba sekta hiyo iongeze juhudi zake katika eneo la utafiti kwa sababu utafiti ni muhimu katika kilimo kama ilivyo kwa sekta nyingine zote nchini, na katika kutekeleza hilo, wale watafiti ambao wamefikia umri wa kustaafu lakini bado wana nguvu za kuendelea kufanya kazi, wabakizwe kazini kwa mikataba maalum.

Mheshimiwa Spika, ni vyema wenzetu wa Wizara wakatueleza lipi kati ya haya ambayo wametekeleza? Kama si kutuweka pabaya!

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE:** Mheshimiwa Spika, naanza kwa kuunga mkono hoja iliyoletwa mbele yetu. Baada ya kuunga mkono, naomba nichangie baadhi ya maeneo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni suala la kushangaza kwa Serikali kuja na Muswada wa kuanzisha Bodi ya Mazao Mchanganyiko huku ikijua haijawa tayari kuifanya Bodi hii kufanya kazi zaidi ya kuundwa kwa Bodi ambayo imekuwa mzingo kwa Serikali kwa kutumia pesa ya walipa kodi lakini bila kutekeleza majukumu ya kuwahakikishia huduma wananchi kwa yale mazao yasiyokuwa na soko la uhakika.

Mheshimiwa Spika, suala la mkataba tata la kuitaka *NMC* ya Arusha iliyokuwa inasaga na kuuza unga kwa bei nafuu na kuambiwa eti achukuwe mwekezaji ndiye asage na kuweka bei anayotaka bila kujali uwezo wa wananchi, eti awe analipa *milling charges* ambazo kwa taarifa niliyonayo mpaka sasa, pamoja na mkataba tata kiasi cha Shilingi million 500 kinadaiwa bila kulipwa. Taarifa nilizonazo, mwekezaji huyu anabebwa na Maafisa wa *CHC* kwa manufaa yao binafsi. Naitaka Wizara iingilie kati na kusitisha Mkataba huu ili mali ya Watanzania iwasaidie Watanzania kwa kupewa kinu hiki *NFRA* au Bodi ya Mazao Mchanganyiko ili sote tufaidike badala ya wajanja wachache kwa manufaa yao binafsi.

Mheshimiwa Spika, Sera ya Kilimo Kwanza inapaswa kutekelezwa kwa vitendo kwa kuhakikisha mapinduzi ya kilimo kwa michakato inaendelezwa kwa kuhakikisha matrekta yenye bei nafuu yanaendelea kupatikana hasa kwa Mikoa inayozalisha chakula kama Rukwa ambayo matrekta yasiyozidi 12 tu ndiyo yaliyopokelewa. Kiasi hiki ni kidogo hata

Wilaya moja tu ya Kalambo hayatoshi ukizingatia uhitaji wa Mkoa.

**MHE. LUCY P. OWENYA:** Mheshimiwa Spika, zao la ndizi linalimwa katika sehemu nyingi hapa Tanzania, lakini Serikali haijalitambua zao hili kama zao ambalo linaweza kuingizia Taifa pato kwa fedha za kigeni hata za hapa nchini. Zao hili nchi za nje ni la gharama kubwa, nchi za Ulaya zinaagiza kutoka nje ndizi mbichi na mbivu kutoka nchi za Karibeani (Tameika, Dominics na kadhalika) na nyingine zinatoka nchi jirani ya Uganda.

Mheshimiwa Spika, wafanyakazi kutoka Uganda wanakwenda Bukoba wananunua ndizi matoke halafu wana-*export to Europe,* zinajulikana zinatoka huko. Siyo hilo tu, wananunua kwa bei ya chini sana, lakini kule Ulaya Uingereza ndizi yenye chana moja ya ndizi tano ni Pound tano sawa na Sh. 13,000/= za Kitanzania. Hizi ni fedha nyingi sana, zingetosha kuwafaidisha wakulima wa ndizi. Je, Serikali ina mikakati gani ya kuinua kilimo cha ndizi kiwe katika zao mojawapo la biashara hapa nchini?

Mheshimiwa Spika, wakulima wamekuwa wakilima mahindi kwa juhudi zao, wengine bila kutumia ruzuku ya Serikali na wanalima kilimo hiki kwa kilimo cha biashara, lakini wakishavuna Serikali huingilia kati na kuzuia kuuza mahindi nje, ukizingatia mbegu za kisasa huwezi kuhifadhi kwa muda mrefu bila dawa na wakulima wengi hawana matanki ya kuhifadhia. Je, Serikali haioni kuwaingilia ni kuwanyanyasa wakulima waliolima kwa jasho lao? Je, ni kwanini Serikali ina-*export* madini kwenda nje ambayo yana thamani kuliko hata haya mahindi, lakini ikija kwa mkulima hausishwi na kujua haki yake ya msingi ya kufaidika na kilimo chake?

Mheshimiwa Spika, naomba majibu.

**MHE. VINCENT J. NYERERE:** Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua fursa hii kwa kutoa shukrani zangu za dhati kwako na kuwapongeza Waziri na Naibu Waziri kwa mipango thabiti ya utafutaji wa masoko nje kwa ajili ya

wakulima wa hapa nchini kama ilivyofanya kwa kuwapeleka wakulima *South Sudan (JUBA)*.

Mheshimiwa Spika, kwa utafutaji mzuri wa masoko kwa bei nzuri ndiyo njia pekee itakayomhamasisha mkulima kuliko kuwazuia kufanya kazi ya kuuza mazao yao pale ambapo wanadhani bei ni nzuri.

Mheshimiwa Spika, ipo hatari kubwa ya upungufu wa chakula duniani ifikapo mwaka 2025 na hii inatokana na kuwa, wakulima wakubwa na watumiaji wakubwa wa chakula (CHINA) kuacha shughuli za kilimo na kufanya shughuli za viwanda. Wengi wanahamia Mijini na kuondoka vijijini ambapo ukulima unatekelezwa na kuja kutafuta fedha kwa shughuli nyingine ambazo pia zinawapatia fedha nyingi sana na pia watahitaji kununua chakula.

Mheshimiwa Spika, hapa ndiyo mahali ambapo Taifa hili linalokuwa haraka sana kiuchumi hasa kwa kutegemea viwanda na kuacha mashamba watahitaji chakula kutoka dunia nyingine na hasa Afrika ambapo pia kama hatujaanza kuchukua hatua sasa, basi dunia itakuwa na janga kubwa la njaa ifikapo miaka hiyo.

Mheshimiwa Spika, hapa ndiyo muda wa kuanza kuonesha nia ya dhati ya ukulima endelevu kwa ajili ya biashara na uchumi wa mtu na nchi kwa ujumla kuinuka kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, bado kuna shida ya utumiaji wa madawa ya kuua wadudu mashambani, siyo tu kwa uingiaji wa madawa bandia, pia matumizi sahihi ya madawa hayo haujatiliwa mkazo, kwani yapo madawa mengi yenye mchanganyo tofauti na huku wakulima wengi wakiwa na uelewa mdogo sana na huku Maafisa Ugani kuwa mbali na wakulima.

Mheshimiwa Spika, napenda Serikali ichukuwe hatua za makusudi za udhibiti wa Maafisa Ugani ili wawe karibu sana na wakulima kwa ajili ya kuwasaidia wakulima.

**MHE. AMINA ABDALLA AMOUR:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Sekta ya Kilimo inachangia asilimia kubwa kwenye pato la Taifa na sekta hii pia inachangia ajira nyingi, nachangia yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, wakulima tayari wameshahamasika kwenye kilimo na wako tayari kulima kwa wingi ili Serikali isiwavunje moyo ni kuhakikisha viwanda vingi vipya vianzishwe na pamoja kukarabatiwa kwa vile vilivyokuwa vikongwe Serikali ielekeze kujenga viwanda hivyo kwenye Mikoa na Wilaya ambazo zinatoa mazao mengi.

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali, ujengaji wa viwanda viende sambamba na miundombinu ya barabara pamoja na umeme, kwa kuwa kujenga hivi viwanda bila kuwa na umeme ni sawa kutwanga maji kwenye kinu. Hii ina maana viwanda vitachakaa kabla ya kutumika.

Mheshimiwa Spika, pamoja zao la alizeti kuwa kubwa, lakini bado Serikali inatumia pesa zetu za kigeni kununua mafuta ya alizeti. Kwa nini Serikali isiyanunue haya mafuta kwa wakulima na kuyafanyia usanifu mzuri ili yawe ya kuvutia na baadaye tukauza nje ya nchi na umeme tukatumia sisi wenyewe?

Mheshimiwa Spika, wizi wa pembejeo unazidi kila siku. Pamoja na Serikali kukemea, lakini bado kuna Halmashauri zinaendelea na wizi wa pembejeo. Naiomba Serikali izidi kufuatilia na anaopatikana na wizi huu wa pembejeo wapewe adhabu kali iwe ni fundisho kwa wengine. Ile adhabu ya kuwahamisha kutoka eneo moja kwenda linguine imepitwa na wakati kwani kila siku wiziunazidi.

Mheshimiwa Spika, inasikitisha kuwa mpaka hii leo zao la korosho bado zinakobolewa nje ya nchi na matokeo yake nchi hizo zinapata pesa nyingi kuliko sisi Watanzania ambao tunawauzia hizi korosho tunazolima. Kwa nini Serikali isinunue hizi mashine za kukoboa korosho baadaye Serikali ikanunua korosho kwa wakulima nah ii itaweza kumpatia

mkulima uhakika wa kuuza korosho zake nah ii itawaanya wakulima kulima korosho kwa wingi na ia Serikali itaweza kupata pesa nyingi za kigeni.

Mheshimiwa Spika, kilimo pamoja na kuchangia asilimia kubwa, lakini naamini ingeweza kusaidia zaidi kama tungekuwa na mipango mizuri kwenye Sekta ya Kilimo. Naiomba Serikali, badala ya kung'ang'ania mazao hayo hayo kila siku ikaamua kuiga mazao mengine ambayo nchi za wenzetu wanalima. Sisi tunayo ardhi kubwa na mazao mengi, ukiyapanda naamini yanakubali.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa bajeti ya kilimo ni ndogo, naiomba Serikali iitazame Wizara hii kwa makini na kuweza kuiongezea pesa.

**MHE. ENG. ATHUMAN R. MFUTAKAMBA:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Spika, katika ukurasa wa 17 na 18 wa hotuba ya Mheshimiwa Waziri hauzungumzii Bwawa la Goweko/Nsololo ambalo tangu mwaka 2008. Imeelezwa kwamba upembuzi yakinifu wa kanda ya Umwagiliaji ya Magharibi ilisemwa mwaka 2011 tathmini ya athari za kimazingira inafanyika. Bwawa hilo sasa halionekani hata kwenye hotuba hii. Naomba maelezo ya kina ili wana Igalula wajue umwagiliaji, unyweshaji mifugo maji ya kunywa na ufugaji samaki utawasaidiaje wananchi kupiga vita umaskini?

Mheshimiwa Spika, napenda kuongelea Kilimo cha Umwagiliaji Mto/Mbuga ya Iwembele, Igalula/Singida Magharibi/Igunga.

Mheshimiwa Spika, ziko hekta 10,000 katika bonde hili, lakini Wizara iko kimya. Umwagiliaji utaongeza uzalishaji wa mpunga kwa mwaka mzima, maji yakitegwa kwa malambo na umwagiliaji wa visima *(Boreholes).* Wizara itafiti Bonde hili na kuzalisha Mbunga kisasa na kutumia.

Mheshimiwa Spika, mbegu Bora na mbolea pia kwenye *value chain* ya mpunga, ukoboaji na upakiaji kwenye magunia na viroba na mifuko, mchele wa Igalula (Loya, Miswaki) uuzwe badala ya kuuza mpunga. Ajira itaongezeka Jimboni Igalula na Halmashauri itapata *(Cess)* pato na *Service levy* kusaidia miradi ya jamii.

Mheshimiwa Spika, mbegu za Sero5 (Mpunga) Igalula ziletwe na *AFDB* wana fedha za mashamba ya mfano *(Pilot projects)* ili uzalishaji uongezeke kwa eka.

**MHE. MICHAEL L. LAIZER:** Mheshimiwa Spika, kwanza nianze kwa kuunga mkono hoja ya Waziri. Pamoja na kuunga mkono hoja, niseme changamoto chache kwenye Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, katika suala zina la pembejeo, bado mfumo siyo nzuri kutokana na uwazi kutojulikana wazi. Pembejeo zinazopatikana, haziletwi kwa wakati. Kuna ucheleweshaji mkubwa wa mbegu za kuotesha mkopo wa fedha za kilimo, baadhi ya Halmashauri hawataki kuwadhamini wakulima kupata matrekta ya kulimia na kushindwa kuondokana na jembe la mkono.

Mheshimiwa Spika, napenda kukujulisha kwamba Wilaya ya Longido siyo ya wafugaji tu, kuna baadhi ya Kata za wakulima, mfano Kamwanga, Lerangwa, Olmolog, Ketumembeine na Engarenaiborne Gilay. Tingatinga zote hizi ni za wakulima. Kwa hiyo, basi kwenye bajeti hii Serikali itekeleze pembejeo kwenye maeneo nilizozitaja ili waachane na jembe la mkono.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza, Kata ya Tingatinga ni wakulima wa umwagiliaji. Ombi langu ni kuwasaidia wakulima hawa waweze kuongeza kilimo kwa ajili ya umwagiliaji ili kuwezesha Wilaya ya Longido ambayo ni kame iweze kupata chakula cha kuwauzia wananchi wengi kutoka kwa wakulima.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa inawezekana kuwa na mabwawa ya umwagiliaji katika vijiji vinavyapata maji ya umwagiliaji kwenye Mto Engarenanyuli na Mto Simba toka mlima Kilimanjaro, wanaweza kuwa na mabwawa ya umwagiliaji. Naomba fedha kwa mradi huu.

Mheshimiwa Spika, wakulima ambao wanazalisha chakula kingi pamoja na wafanyabiashara wananyimwa kuuza nje. Tatizo ni kwamba biashara ya mazao, wafanyabiashara wengi wanategemea kwa maisha yao. Wananchi wa Namanga sio wakulima wala sio wafugaji, wanategemea biashara huku wananyimwa kuuza mazao nje. Kwa kuwa Wakenya wanakuja kununua mazao na kupeleka kwao bila kizuizi huko kwao, wananchi wafanyabiashara waruhusuwe nao kufanya biashara kama wenzao wa jirani.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hotuba ya Waziri wa Kilimo.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Spika, mfumo mpya wa usambazaji wa pembejeo unatia shaka kama utaweza kuwa na matokeo chanya. Kwa kuwa mfumo huu unapangwa na Wizara bila kuwashirikisha wadau wakiwemo wananchi wenyewe, mara nyingi mifumo inayoandaliwa na Serikali bila kuwashirikisha huwa mibovu sana. Mfumo wa awali ulikuwa ni ufisadi mkubwa na malalamiko lukuki toka kwa wananchi, lakini Serikali inatueleza kuwa pembejeo hizi zitatolewa katika vikundi na Vyama vya Ushirika.

Mheshimiwa Spika, Wizara ilipaswa kutathmini: Je, ni wakulima wangapi wapo katika vikundi hivyo? Lakini pia imani ya wananchi katika Vyama vya Ushirika haipo tena kutokana na Vyama vingi kuwa na migogoro mingi na ubadhirifu mkubwa wa fedha za wanachama wake. Hivyo Serikali badala ya kutoa mfumo mbadala ambao ni shirikishi, badala yake mnaleta mfumo ambao utakwenda kuleta migogoro zaidi na kuwa wa kibaguzi.

Mheshimiwa Spika, mbolea zinazotolewa zimekuwa na urasimu mkubwa na ucheleweshaji sana, hivyo kuwasababishia wananchi usumbufu. Lakini pia mbolea inayotolewa katika maeneo mengine, haiendani na udongo wa maeneo hayo. Pia siyo hitaji la wananchi husika. Serikali ni vyema sasa ishirikishe wananchi katika kujua ni mbolea ya aina gani wanahitaji na kwa wakati gani. Uwazi katika suala zima la mbolea ni muhimu sana.

Mheshimiwa Spika, mikakati dhabiti ya kujenga miundombinu ya Umwagiliaji katika maeneo mbalimbali hapa nchini ni njia pekee itakayoondoa utegemezi wa chakula cha njaa kwa wananchi wetu. Utegemezi ni adhabu na namna ya kulemaza wananchi, lakini haimaanishi wananchi wafe na njaa, la hasha. Ni kuwa na mkakati wa uhakika katika kujenga Skimu za Umwagiliaji ili wananchi wengi zaidi wazalishe chakula cha kutosha mwaka mzima. Hivyo ni wakati sasa Serikali iweke nguvu kubwa ya fedha katika kujenga miundombinu ya umwagiliaji.

Mheshimiwa Spika, Maafisa Ugani katika Halmashauri nyingi nchini hawatekelezi majukumu yao ipasavyo na hata wananchi kukosa huduma na kukosa ushauri mbalimbali wa kitaalamu kuhusu matumizi bora ya pembejeo za Kilimo. Hivyo Wizara kwa kushirikiana na Halmashauri iweke vigezo vya kupima utendaji kazi wa Maafisa Ugani kwa utaratibu wa karibu wa Mkurugenzi wa Halmashauri.

**MHE. GOSBERT B. BLANDES:** Mheshimiwa Spika, naomba nimpongeze Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika yeye binafsi, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara hii kwa kazi nzuri wanayoifanya. Pia nawapongeza kwa kuleta hotuba vizuri ya bajeti. Ni kwa sababu hiyo naunga mkono bajeti (hoja). Pamoja na kuunga mkono ninayo machache ya kuchangia ili kuboresha hotuba ya bajeti ya Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, mnyauko wa migomba (Mnyanjano) Mkoa wa Kagera umekumbwa na tatizo la ugonjwa wa mnyauko wa migomba uitwao mnyanjano.

Tatizo la ugonjwa, hili ni janga kubwa sana kwa Mkoa wa Kagera, unaotegemea zao la ndizi kwa ajili ya chakula cha kudumu, pia zao la biashara. Natambua juhudi za Serikali za kupambana na ugonjwa huu, pia nampongeza Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika - Mheshimiwa Christopher Chiza kwa kuutembelea Mkoa wa Kagera na hususan Wilaya ya Karagwe ili kujionea hali halisi ya janga hili. Pamoja na juhudi zote hizi, bado ugonjwa huu unashambulia migomba kwa kasi ya ajabu. Naishauri na kupendekeza Serikali itangaze ugonjwa huu kuwa ni janga la kitaifa na kuelekeza fedha za kutosha ili kuokoa migomba katika Mkoa wa Kagera na pato la Taifa.

Mhehimiwa Spika, utaratibu wa Stakabadhi ya Mazao Ghalani ni mzuri na wenye kumnufaisha mkulima dhidi ya ulanguzi wa mazao yao. Naomba Serikali iongeze juhudi na kasi kwa kueneza utaratibu huu Mkoa wa Kagera hasa Wilaya ya Karagwe kwani utaratibu huu bado haujafika.

Mheshimiwa Spika, napongeza kwa utaratibu mzima wa kukopesha matrekta kwa wananchi kwa ajili ya kuboresha kilimo, kwa kuwa wananchi wengi wamekopa trekta hizi na bado wapo wengine wengi hawakupata, lakini bado wanayahitaji. Hivyo, nashauri Serikali iagize matrekta na nyenzo nyingine za kutosha kwa ajili ya kukopesha wakulima. Pia kwa kuwa wahitaji wengi ni wananchi wa vijijini wenye uwezo mdogo, nashauri wananchi wetu wakopeshwe bila ya kutanguliza fedha za awali, bali wakopeshwe moja kwa moja bila kianzio na warudishe kadri wanavyozalisha.

Mheshimiwa Spika, kutokana na mabadiliko ya tabianchi, kilimo cha kutegemea mvua hakiaminiki tena, hivyo kutokuwa na tija. Nashauri Serikali itenge fedha nyingi na ije na mikakati ya kisasa kwa ajili ya kilimo cha Umwagiliaji.

Mheshimiwa Spika, mpango wa Serikali kuwapatia mbolea wakulima ni mzuri sana, lakini utaratibu wa kuisambaza ni mbovu, kwani mbolea haiwafikii walengwa, yaani wakulima badala yake wanaofaidi ni wafanyabiashara

(wasambazaji). Nashauri Serikali ibuni njia mpya na sahihi kwa ajili ya kuzuia wizi wa pembejeo.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Sheria ya kuanzisha Bodi ya Nazao Mchanganyiko ipo: Je, ni lini sheria hiyo itaanza kufanya kazi ili kukomesha ulanguzi wa wafanyabiashara wa kununua mazao mchanganyiko mfano karanga, maharage, mahindi, ulezi, kunde, na kadhalika kwa vipimo vya ndoo, debe, gunia, bakuli na kadhalika. Naomba Serikali itueleze hasa katika majumuisho ni kwa nini tunaruhusu wananchi wetu wanazidi kulanguliwa na kuibiwa?

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. HUSSEIN NASSOR AMAR:** Mheshimiwa Spika, napenda kusema kuwa siungi mkono hoja. Hii ni kwa sababu hotuba hii haijalenga sana kumkomboa mkulima hasa wa Jimbo la Nyangh'wale. Kuna changamoto nyingi kwa mkulima hasa suala la pembejeo kama mbolea na mbegu. Mbolea inachelewa kufika, pia mbegu zinaletwa hazina ubora na hili limejitokeza zaidi ya miaka minne sasa halijapatiwa ufumbuzi pamoja na malalamiko mengi toka kwa wakulima. Je, Serikali hailitambui hili?

Mheshimiwa Spika, pia suala la bei ya mazao hasa pamba kila mwaka inashuka bei. Je, ni lini sasa bei ya pamba itakuwa imara na kumpa kipato kizuri mkulima ili asikate tamaa kabisa na kilimo cha pamba?

Mheshimiwa Spika, Jimbo la Nyang'hwale linakumbwa sana na njaa na kupata chakula cha msaada toka Serikalini karibu kila mwaka. Je, kwa nini Serikali isije na mpango wa kilimo cha kumwagilia? Kwa sababu kuna mabonde mazuri na makubwa sana, pia mkondo wa Ziwa uko karibu. Mpango huo ni mzuri. Iwapo Serikali itafanya hivyo, basi suala la njaa litakuwa historia kwa Jimbo la Nyang'hwale. Ni aibu kubwa sana kwa Serikali kutangaza njaa kila mwaka Jimboni Nyang'hwale, ardhi yake ni nzuri sana, tatizo ni ukame kutokana na uharibifu wa mazingira.

Mheshimiwa Spika, namalizia kwa kusema kwamba naiomba Serikali ichukue ushauri wangu kwa uzito mkubwa kutokana na uhalisia wenyewe.

**MHE. HAWA A. GHASIA:** Mheshimiwa Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Mtwara imebahatika kuwa na maeneo ya umwagiliaji katika bonde la Mto Ruvuma na Kitere, lakini kiasi cha fedha kinachotengwa kwa ajili ya miundombinu ya umwagiliaji ni kidogo sana. Namwomba Mheshimiwa Waziri aiangalie Halmashauri hii kwa jicho la huruma ili kuboresha kilimo Mtwara Vijijini.

Mheshimiwa Spika, kwa miaka miwili mfululizo, soko la zao la korosho na upatikanaji wa pembejeo za korosho limekuwa ni tatizo sugu. Pembejeo zinafika chache na kwa kuchelewa. Soko la korosho ni mtihani. Ni lini Wizara itawaondolea wakulima wa korosho adha hii ili zao la korosho liweze kunufaisha wananchi.

Mheshimiwa Spika, suala la maghala ni muhimu kwa ajili ya utaratibu mzima wa stakabadhi wa mazao ghalani. Mikoa ya Mtwara na Lindi, maghala makubwa yote yaliuzwa kwa watu binafsi hali ambayo inapelekea Vyama Vikuu vya Ushirika kukodi maghala yaliyouzwa kwa bei ya chini kwa gharama kubwa kila mwaka, kwani Wizara isiziwezeshe Halmashauri za Lindi na Mtwara kujenga maghala yake ili kuweza kuwapunguzia gharama za kukodi maghala ambayo inapanda kila mwaka.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. SAID A. ARFI:** Mheshimiwa Spika, nianze na pembejeo na changamoto zake kama ifuatavyo:-

- Kamati za Vocha Vijijini kutokulipwa posho zao;

- Mkanganyiko wa malipo ya pembejeo kati ya Mawakala na Makampuni;

- Uwepo wa mbegu zisizokidhi ubora;

- Makampuni yaliyochaguliwa na Wizara kutokufika katika maeneo waliyopangiwa; na

- Bei kubwa ya pembejeo kwa wakulima.

Mheshimiwa Spika, labda sasa nizungumzie kuhusu Umwagiliaji na changamoto zake. Mosi, skimu zilizoombewa fedha na kukabiliwa na Serikali kutokutolewa kwa fedha kwa wakati au kutokupata fedha kabisa. Lipo tatizo kubwa la uhaba wa wataalamu katika ngazi zote, aidha, wataalamu hawa wana tatizo sugu la usafiri katika ngazi zote hususan Maafisa Wagani katika Kata ambazo zina maeneo makubwa wapewe usafiri (pikipiki), hakuna nyumba za Maafisa Ugani na hawapewi posho za muda wa ziada.

Mheshimiwa Spika, hakuna uwiano kati ya mahitaji ya pembejeo na upatikanaji *(denand/supply)* msimu uliopita Mkoa wa Katavi tulipokea mbegu vocha 3222380 kgs mbolea vocha 86707 ya kupandia na vocha 43353 ya kukuzia wakati mahitaji halisi ni mbegu za mahindi tani 806476, mpunga tani 392, mbolea ya kupandia tani 956.71 na tani 123 ya kukuzia. Hivyo basi, ili kupata tija, ni lazima upatikanaji wa pembejeo ukidhi mahitaji halisi.

Mheshimiwa Spika, ningependa pia kujua kuhusu Chuo Kikuu cha Kilimo Katavi, kama Wizara inafahamu chochote na mpango huo umefikia wapi hadi sasa? Kadhalika hatua iliyofikiwa ya kupewa hati vijiji vyote nchini ili kuwepo mipango endelevu ya matumizi bora ya ardhi.

Mheshimiwa Spika, mwisho, mpango wa kutoa pembejeo katika msimu huu za vocha kama umefanyika wa kutosha ili usiwe na usumbufu na ulete tija kwa wakulima. Kadhalika, kilimo cha Mkataba utafiti wa kutosha umefanyika, maana katika masikio ni mpango mzuri: Je, tumejifunza nini katika kilimo cha Mkataba ambao umekuwepo kwa zaidi ya miaka 40? Kwa zao la Tumbaku, unabadili hali ya maisha na ustawi kwa wakulima wa Tumbaku hapa nchini. Kilimo cha Mkataba ni aina nyingine

ya unyonyaji wakulima wetu nchini na kuwanufaisha Makampuni ya kigeni na Mawakala wao.

**MHE. CAPT. JOHN Z. CHILIGATI:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, napenda kusema, naunga mkono hoja hii. Aidha, napenda kutoa hoja zifuatazo:-

Mheshimiwa Spika, hali ya njaa na ufumbuzi wake maeneo ya ukanda wa kati, ikiwemo Wilaya ya Manyoni na hasa eneo la Bonde la Ufa, kila mwaka hukumbwa na njaa. Hata hivyo ipo mbuga kubwa inayoweza kuzalisha mpunga kwa wingi na kuondoa tatizo la njaa ya kila mwaka.

Mheshimiwa Spika, katika Bonde/Mbuga hiyo zipo skimu za Umwagiliaji tano ambazo ni Waraka, Udimea, Ngaiti, Chikuyu, na Mtiwe. Lakini skimu hizo zinategemea maji ya mvua. Hakuna Bwawa la kusaidia skimu hizo kufanya kazi kwa ufanisi. Kwa hiyo, ufumbuzi wa tatizo la njaa Wilaya ya Manyoni ni kilimo cha umwagiliaji, tukianza na skimu zilizopo.

Mheshimiwa Spika, mradi wa Bwawa la Mbwasa (Manyoni) ujenzi wa Bwawa hili ukifanyika litakuwa ni injini ya kilimo cha umwagiliaji katika Wilaya yetu. Mradi wa Bwawa hili hivi sasa unafanyiwa upembuzi yakinifu na Ofisi ya Umwagiliaji kanda ya kati kwa gharama ya Shilingi milioni 91. Kazi ya upembuzi yakinifu inatazamia kukamilika mwezi Agosti, 2013. Baada ya hapo, tunaiomba Wizara tusaidiane kutenga fedha za ujenzi wa mradi huu au kutoka Serikali au kutoka kwa wahisani wanaosaidia miradi ya kupiga vita njaa. Bwawa hili likikamilika, litawezesha kilimo cha umwagiliaji katika bonde hili la Suryngai lililopo Wilaya ya Manyoni na Bahi, na tatizo la njaa katika eneo hili litabaki historia na pia kilimo hicho kitaondoa umaskini katika eneo hilo.

Mheshimiwa Spika, kilimo ndiyo sekta pekee yenye uwezo wa kubadilisha maisha ya Watanzania 75% kwa muda mfupi iwapo tu Serikali itaweka uwezeshaji wa kutosha kwa wakulima. Maeneo yatakayowasaidia wakulima waongeze mapato yao ni haya yafuatayo:-

(i) Huduma za Ugani zisogezwe ili wakulima wapate kanuni za kilimo bora, ili ekari moja izalishe mavuno mara dufu.

(ii) Utaratibu wa mikopo ya wakulima uimarishwe ili uwafikie wakulima wengi zaidi kuhusu mikopo ya zana za kilimo na ya pembejeo.

(iii) Mfumo wa masoko ya mazao uimarishwe ili mazao yao yawe na masoko ya uhakika na bei za uhakika.

(iv) Kilimo cha kutegemea mvua hakiaminiki, wawekewe miundombinu ya Umwagiliaji.

(v) Viwanda vidogo vidogo vya kusindika mazao yao mwaka ujao wa fedha 2013/2014, Serikali itenge bajeti kubwa zaidi ili kukidhi mahitaji haya.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii.

**MHE. SALEH A. PAMBA:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. Nawapongeza sana kwa hotuba nzuri. Ninayo maoni yafuatayo katika Sekta ya Kilimo:-

Mheshimiwa Spika, nchi yoyote inayopinga katika maendeleo, lazima ihakikishe usalama wa chakula kwa wananchi. Ni vizuri yale maeneo yanayotoa mazao ya chakula kama Ruvuma, Rukwa na Iringa, lazima yapewe kipaumbele katika uzalishaji wa chakula. Lazima sasa tufikie hatua ambapo mabonde yote yawe yanatumika vizuri kwa uzalishaji wa chakula kama mahindi, sukari na mpunga. Mabonde kama Pangani, Kilombero, Rufiji ni lazima kuwahamisha wakulima wakubwa. Hatuwezi kuondoa tatizo la njaa/uhaba wa chakula kwa kutegemea wakulima wadogo wadogo tu.

Mheshimiwa Spika, ni lazima kujikita katika masuala ya utafiti wa mbegu bora na kupambana na maradhi ya mimea ili kuimarisha kilimo.

Mheshimiwa Spika, matumizi makubwa ya mbegu za *GMO* katika nchi nyingi yamekuwa mkombozi kuondokana na tatizo la chakula. Lazima sasa tuanze kutumia mbegu za *GMO* angalau kwa majaribio katika mashamba makubwa ili kuimarisha uzalishaji wa mazao ya chakula na mazao ya kibiashara kama pamba, miwa na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, Serikali itoe maamuzi kuhusu mashamba ya katani yaliyotelekezwa ili wananchi na wawekezaji wakubwa wapewe ili kuongeza uzalishaji. Uamuzi kuhusu shamba la Kilimangwido, Pangani, utolewe mapema ili wananchi wapate maeneo ya kilimo.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. MKIWA L. A. KIMWANGA:** Mheshimiwa Spika, nami napenda kuchangia hoja ya Waziri wa Kilimo nikitambua kabisa kwamba asilimia zaidi ya 80 hapa nchini ni wakulima. Hivyo Wizara hii ni muhimu kwa uchumi wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, katika Randama ya Wizara inaonyesha katika Idara ya Utafiti tunategemea fedha kutoka nje. Mimi binafsi, siafiki sana utaratibu huu, kwani ili kupata mavuno yenye tija na mbegu bora, utafiti ni muhimu sana. Hii inaonyesha wazi kama Wahisani hawataleta pesa hizo, hatuoni Idara hii ya Utafiti itashindwa kufanya kazi yake, na wakulima kukosa kupata ushauri kwa watafiti hao.

Mheshimiwa Spika, ningependa kufahamu hasa, hivi ni lini sisi kama Watanzania tutakidhi Azimio la Maputo la kutenga asilimia kumi ya bajeti yetu kwa ajili ya kilimo? Kwani mpaka sasa ni asilimia saba tu. Ni vyema sasa ili kuendana na Azimio hilo, Serikali ione umuhimu wa kuongeza fedha hiyo.

Mheshimiwa Spika, ni vyema sasa Serikali ikatoa mafunzo ya kutosha kwenye kilimo cha mkataba, kwani wakulima wengi hawakifahamu vizuri kilimo hicho, hasa wakulima wa pamba. Pia wale ambao wanafunga

mkataba na wakulima, wengi wao kutowalipa wakulima bei stahiki, kuwapa pesa kidogo katika kununua pamba. Maana yangu ni kwamba, huwalipa bei kidogo kuliko ilivyo sokoni. Huu ni unyonyaji. Ni vyema wakati wa ufungaji wa mkataba huo, kuwepo na Mwanasheria ambaye atamsimamia mkulima maslahi yake.

Mheshimiwa Spika, siku za hivi karibuni zao la dengu limekuwa na bei nzuri katika soko la dunia. Hapa nchini wakulima wanalima zao hilo bila utaalamu wowote hasa katika maeneo ya kanda ya Ziwa; Magu, Busega na kwingineko. Hivyo basi, Wizara ya Kilimo itatakiwa kufanya utafiti wa zao hili na wakulima hao wa dengu ili kuwatambua na kuwapa utaalamu wa kutosha. Kwani baadhi yao hulalamikia kutokuwa na ujuzi wala usaidiwaji wa kitaalamu wa Kilimo cha Dengu hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, ningependa kujua Serikali inalitumiaje Bonde la Ziwa Victoria kwa kilimo cha Umwagiliaji? Bonde hili ni kubwa sana, hivyo kama tutalitumia vizuri, Tanzania hasa Kanda ya Ziwa, watu hawatahitaji chakula cha msaada (njaa) kwa kanda nzima ya Ziwa. Namwomba Mheshimiwa Waziri wakati anapokuja kufanya majumuisho, anifungue macho kwa kunifahamisha Bonde hili wanalitumiaje?

Mheshimiwa Spika, ahsante.

**MHE. HAMAD ALI HAMAD:** Mheshimiwa Spika, naomba nianze kwa kuiambia Serikali kwamba, bado ndani ya Serikali ya CCM hakuna nia njema ya dhati ya kusaidia kilimo pamoja na wakulima wa nchi hii.

Mheshimiwa Spika, unaposema kwamba unampelekea mkulima pembejeo, maana yake pia unawapelekea mahitaji ya kuboresha kilimo chao ili kiweze kuleta tija kwa mkulima mwenyewe na hata Taifa. Hivyo basi, jambo hili ni lazima liende sambamba na wakati unaofaa. Mfano, kilimo kinaanza Oktoba, basi pembejeo ziende katika kipindi hicho na siyo miezi mitano baadaye.

Mheshimiwa Spika, wananchi wanalima kwa kuwa hawana namna nyingine ya matumaini ya maisha yao, lakini hawalimi kwa sababu ya Serikali kwamba inawawezesha. Ndiyo maana mazao yanajaa katika maghala na hata katika majumba ya wakulima wenyewe.

Mheshimiwa Spika, bei ya mazao inasikitisha kwamba Serikali kwa makusudi kabisa haioneshi jitihada ya kuwafanya wakulima waweze kujidai na faida itokanayo na kilimo chao (jasho lao).

Mheshimiwa Spika, Serikali inazuia chakula kisiuzwe nje ya nchi. Ni vyema, lakini na yenyewe hainunui mazao hayo na hata pale wanaponunua ni kwa bei ndogo sana ambayo haileti tija kwa mkulima, lakini pia haiwezeshi mkulima kulipa deni alilokopa kwa kilimo.

Mheshimiwa Spika, kama hilo halitoshi, mazao yamelundikana, hawana mahali pa kuuza mazao na Serikali badala ya kuyanunua mazao hayo na kuyahifadhi na pia kuwasambazia Watanzania ambao wana njaa katika maeneo mengine, lakini bila kujali kwamba Serikali inawahamasisha watu walime na kwamba wanathubutu kuagiza chakula (mchele) toka nje ya nchi *(Thailand).*

Mheshimiwa Spika, utaratibu huu ni kuwadhihaki wakulima wetu na hii inatia shaka kwamba wanaohusika hapa kuna dalili za 10% inayokwenda kwa hawa waagizaji.

Mheshimiwa Spika, kuna tabia kwa wanunuzi hawa wa mbegu bora toka kwa wazalishaji hao wa mbegu, kwamba hawana utaratibu mzuri wa kuwalipa wazalishaji, jambo ambalo linapunguza jitihada za wazalishaji na matokeo yake ni uhaba wa uzalishaji wa mbegu hizo.

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali kwamba isaidie kuweka shinikizo kwa hawa Mawakala wa mbegu na itengeneze utaratibu wa kuwabana Mawakala ili walipe kwa

wakati ili na wazalishaji nao wapate nguvu ya kuweza kuzalisha zaidi kwa faida ya wakulima wetu.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. CLARA D. MWATUKA:** Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii kwanza nikimpongeza Mheshimiwa Waziri na jopo lake kwa kazi njema yenye matumaini kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, nataka nichangie kwa machache nikianzia na suala la korosho. Ukweli, zao hili soko lake linawachanganya sana wakulima, kwani halina uhakika. Naamini wazi Serikali ilikuwa na nia njema kwa wakulima juu ya bei ambayo kila mara ilikuwa inabadilika katika msimu mmoja huo huo; iliona vyema kuanzisha Mfumo wa Stakabadhi Ghalani. Matokeo ikawa mpango siyo matumizi.

Mheshimiwa Spika, mfumo ulianzishwa bila kuwashirikisha wakulima, wenyewe walikuja kupewa taarifa ya kile kilichoamuliwa na Serikali tu. Karibu maeneo mengi watu walikataa ikawa ni lazima watake wasitake ili mradi Serikali imeamua. Leo zao hili halina tija stahiki kwa mkulima, makato ni mengi yasiyo ya makubaliano na wakulima wenyewe, hali inayowafanya kudhulumiwa haki zao.

Mheshimiwa Spika, vilevile hali ya kuwakopa na kisha kuwalipa nusu nusu, kwa kweli hali hii inarudisha maendeleo nyuma. Ni vyema wangepewa zote na ile *bonus* ndiyo ifanyiwe hayo mambo mengine.

Mheshimiwa Spika, mazao mchanganyiko kama vile mahindi, mpunga, mihogo, mtama pamoja na mikunde kunde kutokuwa na soko maalum. Naiomba Serikali itafute masoko ili wakulima wanufaike.

Mheshimiwa Spika, kilimo cha jembe la mkono sasa kimepitwa na wakati na kwamba ili kuinua kipato cha wakulima, ni vyema Serikali ifanye utaratibu wa kuwaletea wakulima matrekta ili wenye uwezo wayanunue. Kufanya

hivyo, wakulima watakuza kilimo kwa kuwa na mashamba ambayo yatapata na ziada. Vile vile hali ya upatikanaji wa mbegu za kisasa ni shida. Kwa kule Kusini, wengi wanatumia mbegu za asili zikiletwa madukani ni kwa majaribio tu (chache) na bei huwa ni kubwa sana. Kama vile mahindi kilo moja ni Sh. 3,000/=, hivyo naiomba Serikali iagize mbegu kwa wingi na wauziwe wakulima kwa bei ya kuwawezesha wao kuzimudu.

Mheshimiwa Spika, suala la pembejeo pia ni la muhimu na bei iwe ni ya kawaida.

**MHE. IGNAS A. MALOCHA:** Mheshimiwa Spika, naomba nichangie kwa maandishi kwa masikitiko makubwa sana, kutokana na Serikali kutotekeleza yale iliyoyapanga katika bajeti iliyopita mwaka 2012/2013 kutotekelezwa katika Halmashauri ya Wilaya ya Sumbawanga. Matokeo yake mipango ya kilimo kushindwa kutekelezwa kwa Serikali kutopeleka fedha kama ilivyopanga. Kwa mfano:-

Mheshimiwa Spika, miradi ifuatayo ilipitishwa katika bajeti ya mwaka 2012/2013. Cha ajabu, mpaka hivi sasa hawajapelekewa fedha hata robo moja.

Mpango wa Stakabadhi Ghalani vijjiji vitano mlipitisha Sh. 22,075,000/=; Mashamba Darasa Sh. 4,057,000/=; mradi wa matumizi bora ya ardhi vijiji vitatu, Serikali ilipitisha kutoa Sh. 10,549327/=; utafiti wa udongo katika Kata saba Sh. 19,991,497/=; kuanzisha ujenzi wa ghala katika Kijiji cha Kalambanzite Sh. 201,565,951/=; kuendeleza ujenzi wa Skimu ya Sakalilo Sh. 28,000,000/=; ujenzi wa banio katika mfereji mkuu Sakalito Sh. 234,375,000/=; ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji Skimu ya Malezi Sh. 22,000,000/=; na Ujenzi wa banio mfereji mkuu wa Skimu ya Umwagiliaji Maleza Sh. 281,250,000/=.

Mheshimiwa Spika, naomba nipatiwe majibu, kwanini hata katika bajeti hii hakuna fedha yoyote iliyotegwa? Maana yake ni nini? Naomba majibu.

Mheshimiwa Spika, naomba Serikali inipatie majibu, kwanini imeingiza mchele mwingi nchini, wakati ndani ya nchi tunao mchele mwingi. Naomba Serikali iniambie ni jinsi gani imejipanga kununua mpunga kwa msimu huu ambao zao hilo limezalishwa kwa wingi sana, na hasa katika Mkoa wa Rukwa na Katavi.

Mheshimiwa Spika, siungi mkono hoja mpaka nipate ufafanuzi katika yote hayo niliyoyaelezea.

**MHE. JOHN P. LWANJI:** Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali iongeze matrekta ya *Farm track* na *New Holland* iliyouza na kukopesha msimu uliopita hapa Dodoma. Matrekta haya yamehamasisha sana kauli mbiu ya Kilimo Kwanza kwa sababu ya bei zake nafuu na uimara wa matrekta haya kiasi kwamba hata mbuga zinalimika. Inaonekana awamu ya pili matrekta haya yamechelewa kufika nchini kitu ambacho kinaleta wasiwasi kwa wakulima waliokwishajiandaa kukopa na kununua matrekta haya. Naomba majibu ya Serikali: Je, ni lini matrekta mengine yataletwa nchini ili wakulima wajiandae mapema zaidi?

Mheshimiwa Spika, je, ni hatua gani ambazo Serikali imechukua kutatua tatizo la wakulima wa tumbaku kutolipwa msimu uliopita na hivyo kuviingiza Vyama vya Msingi kwenye mgogoro mkubwa na wakulima hao? Mfano ni Kata za Mgandu Mitundu Mwanagembe na Rungwa. Aidha, ni hatua gani zimechukuliwa kwa Watendaji wa Vyama vya Msingi ambao walituhumiwa kufuja fedha na kujinufaisha wao wenyewe na kuwaacha wakulima bila malipo ya jasho lao? Afisa ushirika wa Mkoa wa Singida na Mrajisi wa Vyama vya Ushirika nchini walilalamika sana kutowachukulia hatua zozote wabadhirifu wa fedha hizo. Naomba majibu juu ya suala hili ambalo limekuwa kero kubwa Jimboni kwangu.

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na malalamiko juu ya mbegu za mtama na mbegu za mboga mboga na matunda. Msimu huu wa mvua, waliopanda mtama walishangaa kushuhudia mtama haukuota, licha ya kunyeshewa na mvua

nzuri. Mfano huu ulitokea maeneo ya Tarafa ya Itigi na pia wananchi wanaolima mboga mboga na matunda wamejikuta wakiuziwa mbegu feki zisizokuwa na ubora wowote. Naomba majibu juu ya haya na kama unajua kuwa kuna malalamiko haya kutoka kwa wakulima.

Mheshimiwa Spika, Serikali iliahidi kuongeza fedha kuendeleza ujenzi wa Bwawa la Itagata, (Tarafa ya Itigi Wilaya ya Manyoni), naomba majibu kama ahadi hii imetekelezwa na kama bajeti imezingatia ukamilishaji wa Bwawa hili muhimu sana kwa wakulima na wafugaji.

Mheshimiwa Spika, mazao yanayostahimili ukame kama vile mtama na uwele unalimwa sana Mkoani Singida, lakini tatizo ni ndege waharibifu *(Queleaquelea).* Ndege hawa waharibifu wanaanza kula mbegu pale inapoanza kupandwa kwa makundi ya ndege hawa kufukua mbegu. Msimu huu wakulima walilazimika kupanda mbegu ya mtama na uwele mara mbili mbili. Hata mimea hii inapokua na kuzaa ndege, hurudi kwa makundi kushambulia.

Mheshimiwa Spika, naomba majibu kama Serikali imejiandaa kukabiliana na tatizo hili.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja ya Wizara hii.

**MHE. SELEMANI S. DAFO**: Mheshimiwa Spika, naomba kutoa maoni yangu kwa maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, matreka yaliyokuwa yanapatikana *SUMA JKT,* lini yataingia tena nchini ili wakulima wetu waweze kupata matrekta hayo kwa mikopo kama ilivyokuwa awali?

Mheshimiwa Spika, Kisarawe ina mabonde mazuri sana. Je, ni lini Serikali itaweka nguvu kwa uzalishaji wa mahindi katika mabonde ya Marui na Malizi?

Mheshimiwa Spika, wataalam wanaotoa mafunzo katika Vyuo vya Kilimo vya *Diploma* na *Certificate,* hawapati motisha kama ilivyo kwa wenzao wa *Reseach*. Naiomba Serikali itenge mishahara ya kutosha kwa wataalam wanaotoa mafunzo katika Vyuo vyetu vya Mafunzo.

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali iuwezeshe *TFRA* kuweza kufanya kazi yake ya kupambana na mbolea feki hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. DIANA M. CHILOLO**: Mheshimiwa Spika, napenda kutumia nafasi hii kwa njia ya maandishi kuwapongeza Mheshimiwa Chiza - Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, Mheshimiwa Malima - Naibu Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, Katibu Mkuu pamoja na wote walioshiriki kuandaa bajeti hii nzuri.

Mheshimiwa Spika, kilimo cha umwangiliaji ni ukweli usiopingika kuwa Serikali ikiamua kujikita kwenye kilimo cha umwagiliaji, tatizo la njaa tutakuwa tumelimaliza kwa kiwango kikubwa. Nasema hivi kwa sababu nchi yetu inayo mabonde mengi ambayo yakitengenezwa kuwa *scheme* za umwagiliaji tutaondokana na kilimo cha masika hadi masika. Tutakuwa na kilimo cha muda wote nchini kote, mfano Mkoa wa Singida kila Kata, kuna mabonde ya kutengeneza *scheme* za umwagiliaji ili kukusanya maji ya mvua yasiwe yanapotea bure wakati mvua zinanyesha.

Mheshimiwa Spika, bado kuna mabonde ambayo Serikali haijayatambua, naomba utafiti ufanyike tena ili Serikali iweze kuyatambua na kuyatengea fedha kwa lengo la kuongeza uzalishaji wa mazao ili kuondokana na njaa na kuinua uchumi wetu. Mkoa wa Singida yapo mabonde ambayo hayajatambuliwa na Serikali kwa kutengewa fedha.

Mheshimiwa Spika, bado kuna tatizo la Maafisa Ugani kukaa Mijini kwa sababu mbalimbali, mfano ukosefu wa

nyumba, maji, umeme, Zahanati na kadhalika. Naiomba Serikali kupitia bajeti hii kuhakikisha nyumba zinajengwa kila Kata na vijiji vile ambavyo hata nyumba za kukodi hakuna, mfano Mgungira Singida vijijini na kadhalika. Vile vile Serikali itenge fedha za kununulia pikipiki za Maafisa Ugani ili waweze kupata nyezo za kuwafikia wakulima kutoa taaluma zao na wataweza kulima mashamba darasa ambayo yatakuwa mfano kwa wakulima, tena liwe agizo kila Afisa Ugani awe na Shamba Darasa.

Mheshimiwa Spika, bado kuna tabia ya Serikali kuagiza vyakula nje ya nchi, mfano mchele, *juice* na kadhalika, wakati kuna mchele ndani ya nchi wa kutosha na matunda mengi ya kutengeneza juice nchini. Vyakula vyetu vinavyotokana na mazao yetu, ni vitamu sana, tena tunakuwa na uhakika kuwa havina madhara kiafya. Mchele upo kila Mkoa, hivyo Serikali ikiboresha kilimo cha mpunga kwa kuwapa wakulima mbegu bora, yaani hapatakuwa na haja ya kuagiza mchele nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, Mpango wa Vyama vya Ushirika kununua mazao ni mzuri sana na ni ukombozi kwa wakulima, kwani Vyama vya Ushirika husimamiwa na Serikali, hivyo mara zote hufuata bei elekezi. Hivyo, wakulima hawatadhulumiwa na Walanguzi ambao huwafuata mashambani kabla hawajavuna.

Mheshimiwa Spika, ninashauri Serikali kuviimarisha Vyama vya Ushirika na kutoa maelekezo kwenye mabenki yetu kuyakopesha Vyama vya Ushirika kwa wakati ili vyama hivi vinunue mazao kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali kutoa pia nafasi kwa wanawake na vijana ambao tayari wameamua kuwekeza kwenye kilimo. Mikopo hii ipunguze masharti na utaratibu wake uwafikie wanawake na vijana vijijini ili waweze kuelewa upatikanaji wa mikopo ya pembejeo.

Mheshimiwa Spika, ni ukweli usiofichika kwamba wanawake wameamua kuondokana na umasikini wa kipato kwani tayari wanaweza kusindika mboga kwa matumizi ya nyumbani na biashara. Kwa hiyo, naomba Serikali itoe msaada wa kuwapa elimu zaidi na kuwapa mikopo ya fedha.

Mheshimiwa Spika, kwenye Vyama vya Ushirika kuna aina ya wizi kwenye kuwapa mikopo wakulima; huwaongezea tarakimu, mfano mkulima anakopa Sh. 1,000,000/= tu, anapokwenda kurejesha mkopo anakuta tarakimu inasomeka Sh. 11,000,000/=. Hii ni dhuluma mbaya sana. Naiomba Serikali ifuatilie na kukomesha kabisa. Hii imekuwa ni kero kwa wakulima.

Mheshimiwa Spika, mwisho, napenda kumalizia mchango wangu kwa kuunga mkono hoja hii nikitegemea kuwa mchango wangu utatambuliwa na kufanyiwa kazi.

**MHE. PEREIRA A. SILIMA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa ya kuchangia hoja hii muhimu kwa uchumi mkubwa na mdogo. Nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa hotuba nzuri. Pamoja na hongera hizo, naomba nichangie kwenye maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, tatizo kubwa tulilonalo katika kilimo chetu ni tija (kiwango cha uzalishaji na kipato). Dunia naelewa inalo soko maalum la bidhaa kutoka kwenye kilimo hai (*organic products*). Ingawa siilewi kwa kiasi gani tumefikia soko la *organic products,* nashawishika kuamini kwamba bado fursa hii hatujaitumia ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, nchi yetu inatishiwa na kupotea kwa mbegu za asili na hata kupata chakula kutokana na umakini mdogo katika *Plant protection.*

Mheshimiwa Spika, leo hii mihogo, migomba, mpunga na mazao mengine yakiwemo matunda ya aina mbalimbali yanakabiliwa na maradhi ya mimea. Haya ni matokeo ya kuruhusu wananchi au wageni kuingia na miche au udongo au sehemu za mimea iliyoathirika kutoka nje.

Mheshimiwa Spika, ni rahisi kudharau kitendo cha kuingiza bidhaa au mimea kutoka nje, lakini lazima tujue kwamba adui mkubwa wa kilimo na wakulima wa Tanzania ni maradhi ya mimea. Tuangalie migomba kule Kagera na mihogo sehemu nyingine za nchi.

Mheshimiwa Spika, pamoja na juhudi zote, nashauri tuwe makini zaidi katika jambo hili.

Mheshimiwa Spika, tija *(productivity)* na ustahimilivu wa maradhi ya mimea linatukosesha fedha na hata kutishia njaa hapa nchini. Ni miaka mingi sasa hususan baada ya kuanza tatizo la tabianchi, tumeshindwa kuzalisha chakula katika maeneo mengi ya nchi. Tabianchi ni hali ambayo tunatakiwa tuirekebishe. Hata hivyo, kazi hii ni kubwa na ni shida kuifanya peke yetu.

Mheshimiwa Spika, ili Tanzania tuendelee kupata chakula kutokana na kilimo chetu, hatuna budi kuwekeza na kuongeza jitihada za utafiti na matumizi ya teknolojia. Watafiti ni lazima wajitolee kufanya kazi ya ziada hasa wale wanaofanya kazi ya *Breeding* ili tuongeze tija na uwezo wa kupambana na maradhi kwa mazao yetu. Tuwatunze na tuwape motisha ili wasaidie kwenye kazi hii muhimu.

Mheshimiwa Spika, wakati umefika wa kufanya mjadala wa kitaifa juu ya *GMO* ili pengine isaidie katika juhudi zetu.

Mheshimiwa Spika, kilimo kinakwazwa sana na upatikanaji wa maji kwenye kilimo chetu. Kutokana na tatizo la tabianchi, kilimo bila kutumia maji kimekuwa hakiwasaidii wakulima hata kupata mazao ya kutosheleza mahitaji ya chakula kwenye kaya zao. Pamoja na tatizo hili, bado hatujachukua hatua za kutosha kuwafanya wakulima wetu kutumia maji ingawa nchi yetu inapata mvua za kutosha bila mpangilio na pia tunayo mito na maziwa mengi. Tumetoa kauli mara nyingi kwamba *irrigation* itapewa kipaumbele ingawa bado hakuna hatua zinazofanana.

Mheshimiwa Spika, nashauri tuongeze uwezo wa kuvuna maji ya mvua na itoe elimu hiyo kwa wakulima.

Mheshimiwa Spika, *drip irrigation* ni teknolojia rahisi ambayo wakulima wadogo wanaweza kuimudu. Tuweke mkazo kwenye jambo hili ili ukombozi katika uzalishaji upatikane.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**NAIBU SPIKA:** Kwa hiyo, jioni tutaanza kusikia Waheshimiwa Mawaziri wakianza kupitia na kutupa majibu ya hotuba zetu mbalimbali. Ninawaomba mahudhurio yenu yawe mazuri ili tuweze kuifikiria na kuitendea haki bajeti ya Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika.

Baada ya maelezo hayo, ninaomba nisitishe shughuli za Bunge hadi saa kumi na moja leo Jioni.

*(Saa 6.55 Mchana Bunge lilisitishwa Mpaka saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11.00 Bunge lilirudia)*

*Spika (Mhe. Anne S. Makinda) Alikalia Kiti*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kipindi cha asubuhi, wachangiaji kutoka upande wa Wabunge walishachangia wote, sasa tunampa nafasi mtoa hoja, tutaanza na Naibu Waziri kwa dakika 20 na Waziri kwa dakika 40. Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** *Bismillahir Rahmanir Rahim.*

Mheshimiwa Spika, naomba uniruhusu nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, Subhanahu Wata'ala, *az-wajaa,* mwingi wa rehema, mwingi wa ukarimu, kwa fadhila zake na neema zake zote juu yangu, Alhamdullilah. Pamoja na kuwashukuru wewe na Naibu Spika na Wabunge wote waliochangia katika hoja hii na wale wa Kamati ya Kilimo waliotuwezesha kufika hapa tulipo leo. *(Makofi)*

Mheshimwia Spika, naomba pia nitumie nafasi hii kumshukuru Waziri, Mheshimiwa Christopher Kajoro Chiza na Wafanyakazi wote wa Sekta ya Kilimo, Taasisi na Idara zake zote nchi nzima popote walipo na wadau wote wa kilimo, kwa kazi ngumu wanayofanya lakini nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumekubaliana na Mheshimwia Waziri kwamba na mimi nichangie kwa kujibu baadhi ya hoja na nitajikita katika hoja mbili, tatu na yeye atakuja kuhitimisha hoja yetu kwa siku ya leo.

Mheshimiwa Spika, naomba nianze kwa kusema kwamba, nimesikiliza kwa karibu hoja za Wabunge, wote kwa pamoja tumesikiliza, lakini kuna wale walioingia mashaka kidogo kuhusu Wizara yetu na uwezo wake wa kuiongoza Sekta hii ngumu, kwa sababu wanasema labda hotuba yetu imekosa mwelekeo, labda hakuna maeneo kwenye hotuba ambapo tumesema tunakwenda wapi na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, mimi nikajiuliza jambo lenyewe lililokuwa linazungumzwa ni nini, maana ukitaka kuangalia mwelekeo tunaotaka kwenda ni lazima ujue kazi yenyewe tunayofanya ni nini. Nikaanza kwa kujiuliza kwanza hicho kilimo chenyewe ni nini.

Mheshimiwa Spika, ukishatambua kilimo ni kitu gani ndiyo unasema sasa hawa mabwana wamejipanga vipi katika kutekeleza hilo. Katika hilo la kutafuta kupata mafanikio kwenye kazi hii ambayo ni ya kihistoria, kwenye vitabu, *encyclopedias* na kadhalika, inasema kilimo ni kazi ya kwanza ya mwanadamu, imeanza mabilioni ya miaka iliyopita na imekwenda inabadilika siku hadi siku kwa namna hadi namna hadi hapa tulipofikia.

Mheshimiwa Spika, wanasema *it is development of time defined by climates, cultures and technologies.* Kwa hiyo, sisi kazi yetu kubwa kabisa kwa kila siku tunayokwenda tunamwomba Mwenyezi Mungu, atuongoze kwanza tufanikiwe usalama wa chakula; hiyo ndiyo kazi kubwa. La pili ni kupata uhimili wa Wananchi wa Tanzania wanaoishi kwenye mazingira ya uchumi wa kilimo, ambao kwa wastani *over Sub-Saharan Africa,* wengine wana asilimia 75, wengine wana asilimia 80. Sisi tunakubaliana kwamba ni asilimia kati ya 70 na 75 ya Watanzania wote. Sasa tukisema kwamba, Watanzania tupo 46 milioni leo hii, ina maana kwamba Watanzania wanaoishi kwa kutegemea uchumi wa kilimo moja kwa moja wanafikia kama milioni 33 hivi. Kwa hiyo, ni kuhakikisha uhimili wao wa maisha kwamba kwa kazi yao ya kila siku ya kilimo maisha wanaweza kuyakabili.

Mheshimiwa Spika, lakini kazi ya tatu ni kuhakikisha kwamba, tuna mfumo ambao ni *sustainable*, ni *ecology* ambayo kazi hii haiendi ikaharibu mazingira, ikaharibu uwezo wa Watanzania watakaoishi miaka 50 - 100 kufanya kazi hii hii ya kulima. Hiyo kwa kifupi ndiyo tunapojifunga sisi. Tumepokea hoja hapa kwamba, labda Wizara haikujikita vizuri kwamba mwaka huu haikueleza malengo yake.

Mheshimiwa Spika, tungeeleza malengo ya kazi zote za Wizara ya Kilimo, tungekaa siku nzima hapa, lakini naomba niseme moja tu. Naomba uniruhusu nizungumzie suala la kilimo cha uzalishaji; tuna uzalishaji wa mazao ya chakula na tuna uzalishaji wa mazao ya biashara. Huo uzalishaji wa mazao ya chakula hayo hayo unapokwenda ukazalisha ziada yanageuka kuwa mazao ya biashara. Mazao yetu ya chakula makuu ni mahindi, mpunga, mihogo, jamii ya maharage, kwa sasa tunakwenda na alizeti kwa Kanda ya Kati, ufuta umezungumzwa leo asubuhi na Mheshimiwa Bwege pale kwa ukali kabisa, mtama na uwele. Haya mazao tunayachukua kama mazao ya chakula lakini pia ni mazao ya biashara yanapozalishwa kwa ziada.

Mheshimiwa Spika, upande wa pili tuna mazao ya biashara, tunayo tumbaku, korosho, kahawa, pamba, nimeyapanga kwa ukubwa wa uzalishaji. Chai, pareto na *non traditional crops* kama choroko, dengu ambayo yanapata soko kubwa nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, sasa naomba nizungumze nijifunge katika mazao mawili. Kwenye mazao ya chakula; mahindi uzalishaji wetu leo ni tani milioni 5.2. Kwa tija ya magunia manne mpaka matano kwa ekari. Tija ya wastani ya mahindi ni magunia 15 - 20 kwa ekari. Sasa Wakulima wetu wanalima magunia manne mpaka matano kwa ekari; maana yake nini? Maana yake tunazalisha theluthi moja ya uwezo wa kuzalisha mahindi waliyokuwa nayo wakulima wetu. Sisi Wizara ya Kilimo kazi yetu ni kuhakikisha tunawapeleka Watanzania pale ambapo wataweza kufika kwenye uzalishaji wa magunia 15 kwa ekari. Tukifika hapo sasa maana yake ni kwamba, tutakuwa tuna uwezo wa kuzalisha tani milioni 15 za chakula Tanzania, bila kuwa na ongezeko la ekari, kwa maana ya ardhi au kadhalika.

Mheshimiwa Spika, kwa mpunga ni hivyo hivyo, tunazalisha labda tani milioni moja na laki mbili, sasa tuna tatizo gani. Kwa upande wa pili tuna mihogo; samahani kidogo, tunapozungumzia suala la mihogo mara nyingi linachukuliwa kama zao ambalo halikidhi mahitaji ya chakula.

Zao la mihogo kwa maeneo mengi ukiangalia takwimu za nchi zingine, Nigeria na kwingineko, unapofika kwenye zao la muhogo *it is defined as a food surviving crop* kwa maana ya kwamba iko kwenye mahesabu ya chakula kinachohimili njaa. Sisi Tanzania tunazalisha tani milioni moja laki nane za mihogo, uwezo wetu ni kuzalisha tani zaidi ya milioni kumi na mbili.

Mheshimiwa Spika, sasa anaposema mtu kwamba ninyi hamjui mnachokifanya; hapana! Haya ndiyo malengo tuliyojiwekea ya kwenda kufikia na namna ya kuyafikia sasa ndiyo kazi ya Wizara ya Kilimo kwa kushirikiana na wadau wote pamoja na Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Spika, kuna jambo hili la mazao ya biashara. Mazao ya biashara kama nilivyosema, zao kuu ni tumbaku, linaingiza dola milioni 177 kwa mwaka, linafuatiwa na korosho dola kama milioni 160 hivi, linafuatiwa na kahawa dola milioni 140, likifuatiwa na pamba dola milioni 60. Kwa nini?

Mheshimiwa Spika, kwa sababu yote haya tunayaona pia katika upande huu pamoja na uzalishaji ambao bado ni mdogo sana, kuna uwezekano wa kuongeza tija kwa kiasi kikubwa sana na hiyo ndiyo kazi ya Wizara ya Kilimo. Kwa hiyo, nilipenda tu kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, niseme kwamba, tunaposimama na tukasema kwamba labda Wizara ya Kilimo haina mwelekeo haijui kinachoendelea, siyo kweli, tumejipanga, tunajua hizi ni *targets* ambazo ni lazima tuzifikie. Kwenye mahindi ni lazima tufikie japo tani milioni saba au nane ndani ya miaka mitatu, mine, ijayo.

Mheshimiwa Spika, namna tutakavyoifikia hakuna utaalam ambao tunaubuni. Ukisoma vitabu vinakwambia *historically* kilimo kilianza kubadilika miaka 150 iliyopita, ikaja na *Green Revolution* miaka 30 – 40, akina Norman Warbarg wale Maprofesa walioleta *Green Revolution* miaka 40 iliyopita, hakuna kitu kipya tunacho-*invent*. Katika utekelezaji wa mipango yetu ni lazima tutatengeneza usimamizi ambao

utatupelekea kwamba wale Watanzania wanaoji-*engage* kwenye kilimo, kilimo kikubwa na kilimo kidogo, wote wanakuwa na uzalishaji ambao unakuwa na tija ambao unaweza kufanya kilimo kiwe endelevu.

Mheshimiwa Spika, limezungumziwa suala la uagizwaji wa chakula, limezungumzwa kidogo kwa hisia kali hasa kwenye mambo mawili, kwenye mambo ya mchele na sukari. Mbele yangu hapa nina kitu wanaita *life production cycle of paddy.*

Mheshimiwa Spika, mchele Tanzania unavunwa mwezi wa tano, wa sita, mpaka wa saba, kwenye mikoa yote; mvua iwe inanyesha mara moja ama mara mbili. Mwezi wa nane tunamaliza kuvuna mpunga. Serikali imeanza kutekeleza mpango wa kuagiza mchele mwezi wa 12, baada ya kuona kwa miezi minne mchele unauzwa siyo chini ya shilingi 2,500. Sasa tunajiuliza mchele unauzwa 2,500, unga unauzwa shilingi 800, lakini unga unazidi kupanda kwa sababu kwa kupanda bei ya mchele unga nao unapanda, watu wanakimbilia kwenye unga. Kwa hiyo, unga nao ukaanza kupanda *gradually* ukafika shilingi 1,400. Mfumko wa bei umefika *double digits, and advancing fast*. Sisi ni Serikali ya Wananchi, Serikali ya Watanzania hawa, unaacha mchele ufike shilingi 2800, unga ufike shilingi 1,600; watu wataishi vipi?

Mheshimiwa Spika, lakini nakubaliana na watu wanaosema kwamba, mchele ulikuwepo, kweli mchele ulikuwepo, kila *data* inaonesha kwamba mchele ulivunwa ndiyo lakini ulikuwa wapi? Ulikuwa hauletwi sokoni, kwa sababu watu walinunua mchele kwa bei ndogo kwa wakulima wakaukalia wakawa hawauleti sokoni ili upande bei.

Mheshimiwa Spika, sisi Wizara ya Kilimo tumejipanga na tunataka tushirikiane na wenzetu wa Wizara ya Viwanda na Biashara, tabia hii lazima tupambane nayo ikome.

Mheshimiwa Spika, kwenye bei ya bidhaa ya kilimo duniani kote, mkulima *margin* yake *minimum* ni *60 percent*.

Tanzania bei ya kilimo ukikuta kitu kinauzwa shilingi elfu moja, Mkulima anapata 300, asilimia 30 tu. Hapa katikati ni walanguzi, wachuuzi na wajanja tu. Sasa *do you want us as a responsible Government* tukae tuangalie hali hii? *It is impossible!*

Mheshimiwa Spika, ninawaomba sana Wabunge, watuunge mkono, ni vizuri tukakubaliana kwamba pale ambapo Wananchi walio wengi wanaumia, kwa mbinu za wajanja na walanguzi wa hapa na pale, mje mtuulize, mtuhoji hapa Bungeni, Serikali tuambieni ni hatua gani zimechukuliwa na tuwaambie ni kwa nini tumechukua. Mchele huu unaolaumiwa umeingia wa kwanza mwezi Februari mwishoni, lakini mchele umekuwepo *for the last six months* watu wameukalia hawautoi. Kigezo chake wanataka ufike shilingi elfu tatu; haiwezekani!

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni la sukari. Kweli tumekubaliana na wenzangu tukae na wazalishaji wa sukari, haiwezekani sukari inazalishwa Mtibwa, inazalishwa Kagera, kima cha chini unanunua shilingi 1,500. Ukiagiza sukari kutoka nje inafika Tanzania kwa shilingi 1,000. Wakulima wetu hawanufaiki nayo.

Mheshimiwa Spika, tumesema tujipange, Waziri kesho na kesho kutwa, atakaa na wadau wote wa miwa kuangalia ni wapi tunapokwenda, zao kuu kama miwa ambalo lina athari ya moja kwa moja kwenye mfumko wa bei, linaruhusiwa kwenda namna hii. Kwa hiyo, naomba niseme kwamba, tumekubaliana tunaendelea kulinda viwanda vya ndani ili sukari kwa kiasi kikubwa izalishwe ndani. Mahitaji yetu ya sukari kwa mwaka ni tani 450,000, tunazalisha kama tani 300,000, kwa hiyo, tuna *deficit* ya tani 150,000. Katika hizo laki moja ni sukari ya viwandani inaitwa *industrial sugar*, elfu hamsini ni sukari ya mezani inaitwa *table sugar*. Kwa hiyo, kila mwaka ni lazima tuagize tani elfu 50 za *table sugar* ili kufidia soko.

Mheshimiwa Spika, lakini kwa wenzetu hicho ni kiwanda kimoja tu na uwezo wanao na ardhi tunayo, kwa

hiyo, matokeo yake wenzetu wa *TIC* na Waziri Mkuu na Waziri wa Uwezeshaji - Mama Nagu na wengine, wanafanya kazi ya kufungua milango ya uwezeshaji na uwekezaji kule Mkulazi na Malagarasi. Tunategemea kwamba, tutapata viwanda vya sukari japo vya kuzalisha tani laki mbili ndani ya miaka mitatu, minne na tutaondokana na hii adha ya kuagiza sukari kutoka nje. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nimesema kwamba tunazalisha mahindi ya kutosha lakini mahindi mengi yanatoka nje kwa sababu wakati sisi tunazalisha mahindi wenzetu wanakuwa bado wamechelewa. Tunazalisha tani milioni 5.2 lakini tunajikuta kama mwaka huu tena kinga ya kununua mahindi *NRFA* imekuwa kidogo ina tabu. Naomba niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kwamba, tumejipanga kama Wizara ya Kilimo kwamba huko tunakotaka kuelekea ni lazima tuongeze uzalishaji kutoka tani milioni 5.2 hadi tani milioni 6.2 ndani ya miaka mitatu ijayo. Inawezekana kwa matumizi ya *input*, pembejeo bora na misingi bora na ulimaji wa zana na kadhalika wala si kwa kiasi kikubwa hicho tunachotarajia, lakini ni vyema tukubaliane wote kwamba tunapokwenda huko tufuate ushauri wa kisayansi.

Mheshimiwa Spika, kuna jambo ambalo limezungumzwa hapa ambalo kidogo labda nilisemee siyo zuri na kuna usemi mmoja Waingereza wanasema; *it is an act of extreme ignorance to expose ones own ignorance publicly in the guides of expanding knowledge*. Usisimame wewe mwenyewe, ukatabiri na ukasema, ukafoka kwa jambo usilolijua hadharani.

Mheshimiwa Spika, mimi siyo mtaalam wa kilimo, mimi ni Mchumi, lakini ninapotaka kulijua jambo ninakwenda kwa wenzetu nauliza, suala la mbegu nauliza, suala la matumizi ya mbolea na mengine. Kitu kikubwa kinachotupiga ni kwamba, huko tunakokwenda wakulima wetu saa nyingine wanapelekewa elimu halafu sisi Viongozi tunashiriki kuwaharibia ile elimu ambayo inapelekwa kule, kwa sababu sisi wenyewe tunakuwa na maslahi humo ndani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba niseme katika utafiti ambao unaheshimika Afrika Mashariki na Kati ni utafiti wa akina Dkt. Mwaka, Dkt. Ndunguru na Dkt. Kulaya. Watu wanatoka Kenya, Uganda kuja kufuata elimu yao, wapo Mikocheni pale, sisi wenyewe tunashindwa kuitumia kwa sababu blaa blaa imezidi mno katika mfumo wetu. Wizara ya Kilimo tumejipanga tunataka tutumie sayansi hii kwa manufaa yetu wenyewe, tutaongea lakini tukubaliane tu kwamba, jamani wakati umefika sasa sisi wenyewe tuwe wanufaika wakuu wa hazina ya elimu ile ya sayansi ambayo tunayo Mikocheni pale na maeneo mengine.

Mheshimiwa Spika, mwisho, ninaruka hili la ubinafsishaji wa mashamba ya kilimo, nadhani tutayazungumza huko mbele, naomba sana uniruhusu nizungumzie suala la ushirika. Tumezungumzia kwenye korosho, mimi ni mdau na mwathirika mkuu wa korosho kama alivyo Mheshimiwa Bwege, kama alivyo Mheshimiwa Mangungu, kama alivyo Mheshimiwa Juma Njwayo na Wabunge wenzangu wa Kanda ya Korosho. Jamani tukubaliane, mwaka huu tatizo la korosho ni stakabadhi ghalani au tatizo la korosho ni uongozi ndani ya korosho?

Mheshimiwa Spika, Serikali imetoa pesa za kinga ya zao *70 percent* iende kwenye zao la korosho ifike pale, zao likiuzwa asilimia 70 irudi Serikalini nyingine itakwenda Majaliwa. Pesa ile ilipokwenda ilipofika kule baadhi ya watu kitu cha kwanza mtu akanunua gari lake mwenyewe, la pili akaoa mke na tatu akachezea ngoma, ilipokuja wakati wa kulipa pesa, pesa za kulipa hakuna na umetumia pesa za Ushirika na mmekopa kwenye mabenki vibaya! (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nimekwenda Wilayani kwangu nimemwambia Mrajisi nenda kafanye ukaguzi Wilaya nzima. Usiku saa nane napigiwa simu; Mheshimiwa Mbunge tulikuwa wote lakini unasahau kwenye kampeni utatufunga utatupeleka Segerea!

Mheshimiwa Spika, tukubaliane, amesimama Mheshimiwa mmoja anazungumzia masuala ya kulaani

masuala ya stakabadhi ghalani; ni nani asiyejua kwamba kule kwao tunafahamu kwamba kuna magari ya Viongozi wa Chama chake yamekamatwa yakiiba ufuta? Tunapofika sehemu hii tukubaliane, mfumo wa stakabadhi ghalani umekuja kama mbadala wa mfumo uliokuwepo ambao ulikuwa unawakandamiza wakulima wa korosho wa Kagomba na Chibuga.

Mheshimiwa Spika, tumeleta mfumo wa stakabadhi ghalani, lakini kuna watu wanauumiza mfuko. Sasa tunasema, nimemwambia siku ile Mheshimiwa Balozi Baruwan, tumekubaliana kwamba, katika misingi hii mtatuona wabaya kwa sababu, haiwezekani pesa ya chama chako cha msingi ikaenda halafu wewe unakuwa Mwenyekiti wa kwanza unanunua gari! Kw mfano, kule Kusini kuna Mwenyekiti mmoja kanunua gari, halafu nyuma kaandika jina la gari kasema, USIUMIZE KICHWA; halafu baadaye yeye huyohuyo anakuwa wa kwanza kuja Wizarani pale Kilimo, anadai.

Mheshimiwa Spika, ushirika ni mfumo ambao umekuwa *tested* kwa wenzetu na unafaa, lakini unahitaji usimamizi mkali. Tunachofanya, nakubaliana na Mheshimiwa Conchesta, ulisema pale kwamba, lazima katika Sheria mpya ya Ushirika, adhabu ziwe kali. Mtu anayeogopa kuiba pesa ya ushirika, nakubaliana na Mama Clara alisema pia jana, katika Mfumo huu wa Stakabadhi Ghalani na Mfumo wa Ushirika kwa ujumla, tufike sehemu tukubaliane kwamba, kuiba pesa za Ushirika iwe kama umekwenda kwa Mungu umeiba hela. Uwe unajua kabisa kwamba, adhabu yake ni kali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa tutakapokuja na Sheria hapa mwezi wa nane, tusianze tena kusema haki za binadamu sijui zimevunjwa; hapana. Tukubaliane, Kiongozi wa Ushirika anapewa dhamana na Wanaushirika wenzake, wewe utakuwa Kiongozi wetu ututoe kwenye umaskini huu; sasa badala ya wewe kuwatoa kwenye umaskini, unawaongeza umaskini halafu unakimbilia Serikalini, unasema Serikali, kusema kweli, katika jambo hili na hili la tumbaku ambalo limejitokeza, watu wamewaibia, wamefanya uharibifu

mkubwa kwenye maghala ya tumbaku kule halafu wamewababambika watu wa maghala ya vyama vya msingi bilioni tatu. Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, amenituma niende na Wabunge wa Tabora, tutakwenda Tabora. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninasema tu kwamba, wale mabwana waliofanya uharibifu kwenye Vyama vya Ushirika vya Tumbaku, labda kama hawajasikia vizuri, lakini wataumia tu. Kwa sababu, huwezi kuchukua bilioni tatu, unawaumiza Wananchi, unawaumiza wakulima kwa sababu, umetengeneza *channel* wewe Kiongozi wa Ushirika na Benki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kumalizia kwa kusema, Sheria Mpya ya Ushirika inakuja. Nawaomba Waheshimiwa Wabunge, mridhie kwamba, matatizo mliyoyasema kwenye Ushirika tunayajua, tunayafahamu, lakini katika misingi hii ya Sheria ambayo ina miaka kumi sasa, tangu 2003, tuna nafasi mwaka huu sisi wote humu ndani kutengeneza mazingira ambayo Sheria ya Ushirika itakuja na itaongeza adhabu kali sana kwa watuhumiwa wote wanaoshiriki kuhujumu Ushirika.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Naomba kuunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Naomba na mimi nianze kwa kushukuru kwa kunipa nafasi hii, niweze kujibu baadhi ya hoja ambazo Waheshimiwa Wabunge, wamezileta hapa wakati wa mjadala. Nina uhakika ni nyingi mno, sitaweza kuzimaliza, lakini kama kawaida zile ambazo hatutaweza kuzijibu tutazijibu wakati wa Kifungu kwa Kifungu, lakini nyingi zaidi zitajibiwa kwa maandishi.

Mheshimiwa Spika, waliochangia kwa kauli humu ndani peke yake ni 47, kwa hiyo, ni dhahiri siwezi kabisa nikaanza wa kwanza mpaka nikawafikia wote 47. Waliaochangia kwa maandishi wako 85 na kila mmoja angependa nimjibu. Naomba niseme nawashukuru wote kwa

michango yao, yote ni mizuri na ninawahakikishia kwamba, mawazo yao na ushauri wao tutaufanyia kazi na ule ambao tutaona pengine uko pembeni na sisi tutawashauri.

Mheshimiwa Spika, naomba niishukuru sana Kamati ya Bunge ya Kilimo na Mifugo, inayoongozwa na Mheshimiwa Profesa Peter Mahamudu Msolla. Kamati hii imefanya kazi kubwa sana, tulianzia mchakato Dar es Salaam, tarehe 3, tarehe 4 na tarehe 12 tulifanyia hapa hapa Dodoma. Ushauri wao ni mkubwa sana na kwa sehemu kubwa umefanikisha sisi kukamilisha Hotuba yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wametushauri mambo mengi, labda nitaje machache tu kwa faida ya wale ambao wanakuwa wamesahausahau. Yako mambo makubwa sana ambayo yamezungumziwa na Waheshimiwa Wabunge na Kamati imeyazungumzia kwa kirefu, kama uteuzi wa Wadarajishaji, yaani *Classifiers,* kwenye tumbaku. Tumbaku hii ambayo tunaizungumzia na matatizo kule Tabora. Mambo ya utafiti, mambo ya uwekezaji katika kilimo cha umwagiliaji, upimaji wa ardhi na mashamba; na hili nitalizungumzia baadaye maana Msemaji wa Kambi ya Rasmi alilizungumzia kwa kuli-*support* bila kujua kwamba, mara nyingi analipinga.

Mheshimiwa Spika, wamezungumzia mchakato unaoendelea wa *Price Stabilisation Fund,* ambao humu sisi tumesema ni Rasimu kwa maana ya kwamba, bado kuna mchakato mbele yake. Rasimu ile itakapokuwa imekamilika ndiyo itaitwa sasa Mfuko, lakini kwa sababu iko kwenye mchakato bado ni Rasimu. Maana nimesikia watu wakisema sasa rasimu, rasimu, rasimu, lakini ni rasimu kwa maana ya kwamba iko kwenye *process.*

Mheshimiwa Spika, wamezungumzia pia kutazama upya Mfumo wa Stakabadhi Ghalani; na nitajitahidi niende mbio, kusudi nisiondoke hapa bila kuutaja Mfumo huu ambao tunatarajia kwenda nao. Wamezungumzia uendeshaji wa Vyama vya Ushirika, kama alivyosema Mheshimiwa Naibu Waziri. Wamezungumzia uanzishaji wa Tume ya Umwagiliaji, Tume ya Ushirika na Sheria zake ambazo tutazileta hapa

mwezi wa nane, *Inshallah.* Yote hayo tumeyazingatia na ninakushukuru sana Mheshimiwa Profesa Peter Msolla na Kamati yako, mmekuwa wa msaada sana kwetu.

Mheshimiwa Spika, sasa naomba nianze kueleza mambo ya jumla jumla. Kama nilivyosema, nikianza kusema kila mmoja itakuwa kazi. Liko suala la bajeti ya matumizi ya kawaida ikilinganishwa na bajeti ya maendeleo kuwa kubwa. Hii ni hoja ambayo kila mara inaletwa, mwaka jana ililetwa na mwaka huu pia imeletwa.

Mheshimiwa Spika, naomba niwafafanulie kidogo. Kwanza, nifafanue lile suala la *ten percent budget,* ambayo ndiyo maelekezo au ndiyo maazimio ya Maputo. Walio wengi wanalikosea jambo hili kwa sababu, kila mara wakifikiria *ten percent* ya bajeti, wanafikiria bajeti ya mazao. Kama hii ya shilingi bilioni 328 ambayo tunaomba wanaweka juu ya ile Bajeti ya Serikali, wanasema tayari ni bajeti ya Sekta ya Kilimo.

Mheshimiwa Spika, maana yake siyo hiyo. Tunapozungumzia kutenga kwenye Sekta ya Kilimo asilimia kumi, tunazungumzia kutenga kwa Sekta ya Kilimo kwa maana ya mazao, kwa maana ya misitu. Sekta hii, kwa ufupi tu, inayo Wizara nne ambazo zinaitwa Wizara Kiongozi za Sekta ya Kilimo; iko Wizara hii ya Kilimo, Chakula na Ushirika, Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Wizara ya Maji, Wizara ya Viwanda na Biashara na TAMISEMI. Sasa fedha zote zinazoingia huko kwenye kujenga barabara, *farm to market roads,* zote hizi zinaitwa zinakwenda kwenye Sekta ya Kilimo; ukizijumlisha ndiyo unapata fedha inayotengwa kwa ajili ya Sekta ya Kilimo.

Mheshimiwa Spika, sasa hili nimesema niwafafanulie tu, ili wale watu ambao wangependa waende kutafuta, waweze kujua maana yake ni nini.

*(Hapa Wabunge fulani walikuwa wanazungumza)*

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Aah, sasa mnaniingilia.

Mheshimiwa Spika, naomba unilinde.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, endelea kuchangia; mtu yeyote siyo sababu yakO.

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, sasa nije kwenye fedha za *OC – Other Charges.* Wenzetu hawa wamekuwa wakizungumza kila wakati kwamba, mbona fedha ya *Other Charges,* inaonekana kuwa ni kubwa kuliko fedha ya maendeleo?

Mheshimiwa Spika, kwa bahati nzuri sisi kwenye Wizara ya Kilimo, tunazo kazi ambazo zimekaakaa kimaendeleo. Kazi hizo zinapotolewa fedha, fedha zake zinakuja kwenye Fungu la Matumizi ya Kawaida na zinakuja zikiwa na maelekezo kwamba, ni *ring fenced.* Kwa maana ya kwamba, fedha hizi hazitumiki kwa mambo mengine yoyote. Kwa mfano, fedha za ununuzi wa chakula kama mahindi, fedha za ruzuku ya mbolea, fedha za madawa, fedha za vyakula vya wanafunzi na kadhalika. Fedha hizi zote ziko *ring fenced,* lakini zinakuja chini ya bajeti ya *OC;* na jumla ya fedha zote hizi, sikuvitaja vyote hivyo maana viko 12, najaribu kuokoa muda wangu, ni shilingi 203,776,042,600. Sasa ukichukua hii katika bilioni 210 ambayo tumeomba kama ni *OC,* fedha zinazobaki kama ni *OC per se* ni shilingi bilioni 6.4.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, hili niliona nilifafanue kidogo, ili tusiendelee kufikiri kwamba, labda fedha za matumizi ya kawaida zimekuwa nyingi mno.

Mheshimiwa Spika, naomba niishukuru tena Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji, kwa sababu wakati wa uchambuzi, ilipitia bajeti yetu ikaona umuhimu wa kuongeza eneo la pembejeo ambalo fedha hizo hazipo katika bajeti hii. Kwa bahati, baada ya kuliona hili, Kamati ile inaendelea na mazungumzo na Serikali, wanajaribu kutafuta huku na huko na *Inshallah,* tutapata majibu kabla ya Bajeti ya Serikali, kukamilika. Ninawashukuru *in-advance* kwa sababu, wameona kwamba, upo umuhimu pia wa kuongeza eneo hili kwa hiyo, mchakato huo bado unaendelea.

Mheshimiwa Spika, hapo kwenye madawati ya Waheshimiwa Wabunge, wataona kuna makaratasi ya *re-allocation,* nimeona niwaambie mapema. Sisi ndani ya Wizara tumeanzisha Taasisi inayoitwa *Tanzania Fertiliser Regulatory Authority;* kazi yake ni kudhibiti ubora wa mbolea. Sasa Taasisi hii ambayo kazi yake na makali yake mmeshaanza kuyasikia, wale ambao wamefungiwa maduka yao huko hasa katika Mikoa ya Nyanda za Juu Kusini, nadhani Taasisi hii ilikuwa na shilingi milioni 170 tu kwa *allocation* ya kwanza. Sasa baada ya kuona umuhimu wa Taasisi hii, tumefanya *internal re-allocation* ndani ya Wizara, tukatengeneza tena milioni 330, ili Taasisi hii iweze kuongezewa fedha kufikisha milioni 500, kwa hiyo, Tasisi tumewaongezea milioni 330, ndiyo hizo ambazo mtaziona kwenye madawati yenu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba sasa nizungumzie mfumo mpya wa utoaji wa ruzuku ya pembejeo. Mfumo huu kila mtu ameupigia kelele; ni kweli, nakubali hata mimi changamoto nimeziona. Tulianza zamani kabisa na shilingi bilioni tatu, tukaenda bilioni saba, tukaenda bilioni 21, tukaanza kupanda, lakini kelele ikaja hapa Bungeni wakasema hamuwezi kuanza na Mikoa minne tu ya Nyanda za Juu Kusini, tunataka kila Mkoa upate. Tulipoingia sasa kila Mkoa upate ruzuku ya pembejeo, tukaanza kupata ile hela ikawa kidogo, matokeo yake pembejeo ikawa kidogo.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hayo basi, hata pembejeo yenyewe kwenye mfumo huu wa vocha, ambao tunautumia, wote mmeujadili; kuna changamoto nyingi na nimezieleza kwenye Hotuba yangu ya Bajeti. Sasa tumeona afadhali tuanze kubuni mfumo mwingine; tumebuni mfumo mpya, lakini kwa sasa tunafikiri kwamba, tutakwenda na mifumo miwili *parallel.*

Mheshimiwa Spika, kwa nini twende na mifumo miwili? Kwanza, tuna fedha za *World Bank* bilioni 19 ndani ya bajeti hii; ambao nao wametupatia fedha hizi kwa ajili ya mfumo huo wa ruzuku ya pembejeo. *World Bank* mfumo wao ni wa vocha, huwezi kusema nachukua fedha zao niende tena

kwenye mfumo wa mikopo; wao hawatumii mikopo wanatumia *Voucher System.*

Mheshimiwa Spika, sasa sisi tukaona kama fedha zimeshakuja na ziko hapa, iko haja gani ya kuzipoteza. Basi, kwa hiyo, kwa maana hiyo, tutakuwa na maeneo hasa yale ambayo yalifanya vizuri kwenye mfumo wa vocha, vizuri *relatively* kuliko wengine, hao watapewa fursa ya kutumia *Voucher System.* Katika maeneo mengine, tunataka tuanzishe sasa utaratibu wa wakulima kukopa kupitia kwenye vikundi vyao, kupitia vyama vyao vya ushirika, vyama vyao vya ushirika wa kilimo na vikundi mbalimbali vya uzalishaji mali ambavyo vitakuwa vimetambulika.

Mheshimiwa Spika, changamoto iliyoko hapa ni vikundi hivyo, viko tayari? Mahali pengine viko tayari, mahali pengine haviko tayari, lakini sisi tunafarijika, kwa sababu tumeanza mapema na mfumo huu wa bajeti wa kuanza Aprili, ndiyo utakaotusaidia, kwa sababu kufika Juni, tutakuwa tumemaliza na wakati huo wa Juni, hakuna mahali ambapo wanaanza kulima. Sisi tunataka katika kipindi hiki na tukiwa hapahapa tutaitisha Mkutano Mkuu wa Wadau na ninyi Waheshimiwa Wabunge mtashiriki, Wakuu wa Mikoa watashiriki, Wakulima nao tutawaita, tuangalie ni njia ipi itakayoweza kutusaidia na hasa kwenye mfumo huu wa kutumia mkopo kupitia kwenye vikundi.

Mheshimiwa Spika, zipo taasisi ambazo ni lazima zishiriki; Mabenki; *CRDB, NMB,* lakini yako mabenki mengine yana mtandao mkubwa kuliko mengine; kwa mfano, *NMB,* ina mtandao mkubwa zaidi, lakini ziko benki nyingine hatujazizowea; Benki ya Ushirika ya Kagera kule, Benki ya Ushirika Kilimanjaro kule na Mufindi, tunataka tupanue wigo Mabenki haya yashiriki katika utaratibu huu.

Mheshimiwa Spika, ninachotaka kuwaomba Waheshimiwa Wabunge ni kwamba, tutakapoitisha Mkutano huu naomba mshiriki, mtoe mawazo yenu. Hatuji na *model* ya kusema sisi tuna-*impose,* yale mtakayotushauri na sisi tutayachukua. Tukishaboresha mfumo huo, ndipo tutasema

sasa twende na mfumo huu. Kwa hiyo, Mungu akipenda tutakwenda na mifumo miwili *parallel;* wa vocha katika maeneo yaliyofanya vizuri na mfumo wa mikopo ambao ndiyo tutakuwa tunauanza sasa; baada ya hapo tutaona tena mwaka mwingine tunaweza tukaendaje.

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumzie Miradi ya Umwagiliaji. Nilieleza katika Hotuba yangu kwamba, kwa kutumia teknolojia ya *GPS,* tumefanya tathmini upya katika nchi nzima isipokuwa Kanda mbili tu, tena maeneo machache, Kanda ya Mtwara na Kanda ya Mbeya. Eneo ambalo tumelibaini kwamba, linamwagiliwa hivi sasa ni hekta 450,392.

Mheshimiwa Spika, katika hizo wakulima wadogo wanalima hekta 389,529 na zilizobaki 60,863 ni za wakulima wakubwa, kwa maana ya wale wanaolima miwa, wanaolima mpunga kama *KPL,* wanaolima kahawa, wanaolima maua; hao ndiyo tunawaita wakulima wakubwa. Wote ukiwajumlisha wao ni hekta 60,863, hapa ni pamoja na wale wenye mashamba makubwa kama Kapunga, Mbarali, ambao tuliwapa mashamba kwa kuwabinafsishia.

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumzie Miradi ambayo haijatekelezwa. Kumekuwa na mawazo na hoja nyingi sana kwamba, mbona kwangu sijaona Mradi fulani, mbona kwangu sijaona Mradi fulani?

Mheshimiwa Spika, mwaka huu tumeamua kwamba, tunayo Miradi mingi ambayo ni viporo na sababu nilizieleza katika Hotuba yangu, ikiwa ni pamoja na mtiririko usiofaa wa fedha, taratibu za manunuzi. Tunatarajia kwa utaratibu huu wa kuanza bajeti mwezi wa nne, mwezi wa saba inawezekana tukaanza kupata fedha mapema. Kwa hiyo, tutakachokianza ni kutekeleza Miradi ambayo haikutekelezwa msimu uliopita. Siwezi kuitaja yote ni mingi sana; hili kabrasha, linazungumzia Miradi yote ambayo haikukamilika msimu uliopita, lakini tungependa tuikamilishe katika msimu huu. Waheshimiwa Wabunge wakipenda tutatengeneza nakala waipate yote.

Mheshimiwa Spika, naomba nieleze kidogo tu; kuna watu waliuliza kwamba, hivi hii watu wanaipataje Miradi? Kuna utaratibu fulani ambao unatumika?

Mheshimiwa Spika, hii Miradi iko katika *category* kama nne za kupata fedha. Iko Miradi ambayo inapata fedha ambazo zinaitwa *National Irrigation Development Fund,* ni fedha nyingi kidogo zaidi ya milioni 800. Iko *category* nyingine inaitwa *District Irrigation Development Fund,* hii ni chini ya hapo, lakini kama mmesoma vizuri Hotuba yangu, kuna Miradi ambayo inapata fedha kutoka Mfuko wa *Food Aid Counterpart Fund.* Uko mradi mwingine unaitwa *DASP* kwa kifupi na wote mnaufahamu.

Mheshimiwa Spika, labda nieleze kidogo tuliuwekaje huu Mradi au huu Mpango wa *DASP?*

Mheshimiwa Spika, huu Mpango wa *DASP* uko katika Mikoa ya Kanda ya Ziwa na tuliuweka makusudi na mimi mwenyewe nilishiriki katika kupanga Mpango huu kuupeleka katika Mikoa ile. Tuliuweka huko baada ya kuona mtawanyiko wa Miradi katika Mikoa katika nchi hii, mingi ilikuwa Kaskazini na mingine hapa katikati, Mashariki. Sasa tukaona ni vizuri Mradi huu uende katika maeneo yale, ili angalau watu wa Mikoa ile ya Shinyanga, Mwanza, Tabora na Kigoma, nao wapate Miradi hii.

Mheshimiwa Spika, ndiyo hapo sasa Miradi ile ambayo alikuwa anazungumzia Mheshimiwa Maige; kwa mfano, asubuhi iliibuliwa, sijui ilikuwa ni asubuhi au jana, lakini nataka nimfahamishe hapahapa kwamba, kupitia Wilayani na kupitia Mfuko ule ipo Miradi kadhaa ambayo imeibuliwa na yeye mwenyewe kwake kuna Miradi miwili; mmoja wa shilingi milioni 635 unaitwa Skimu ya Chela na mwingine unaitwa Wendela wa shilingi milioni 835.

Mheshimiwa Spika, ni kweli fedha hazitoshi kwa kulinganisha na ukubwa wa skimu hizi lakini tutakachokifanya ni kuendelea kutafuta fedha ili tuhakikishe skimu hizi zote zinakamilika. Kupitia utaratibu huo huo tunataka tuangalie

maeneo ambayo ni kame, kama Mabonde ya Manonga, Mabwawa ya Masembu aliyoyazungumzia pia Mheshimiwa simkumbuki vizuri lakini alizungumzia suala hili. Alizungumzia Mradi huo ulioko katika Bonde zima la Manonga. Sisi tunatazama bonde kama bonde na tunataka bonde lile nalo liweze kufaidi kutokana na fedha hizo za *DASP*. Kwa hiyo, nataka niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge hawa kwamba, Bonde la Manonga Mheshimiwa Azza Hillary, Bwawa la Masembo yote hayo tutayatengea fedha na yaendelee kutekelezwa.

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumzie maeneo yenye sura ya kijumla tena kidogo tu, nizungumzie soko la korosho. Mheshimiwa Naibu Waziri amelizungumzia lakini niongezee kidogo. Ninachotaka kusisitiza hapa, Wabunge wengi wameongelea hasa wanaotoka kwenye maeneo ya korosho akiwemo Mheshimiwa *Engineer* Ramo Makani na wenzake. Ninachotaka kusisitiza hapa ni kwamba, sisi katika msimu ujao tunataka tuangalie mambo makubwa mawili, moja ni mipango ya sasa au msimu ujao kwamba mkulima wa korosho tunamsaidiaje aweze kupata kipato halafu tuzungumzie mipango ya badaye maana ukizungumzia mipango ya kujenga viwanda huwezi kujenga viwanda kwa siku moja.

Mheshimiwa Spika, yapo mambo ambayo tunaweza tukafanya sasa hivi na tukamsaidia mkulima wa korosho, hata wa pamba na moja ambalo nimeliona ni katika mjengeko wa bei. Mimi nimepitia mjengeko wa bei ya pamba, nimepitia mjengeko wa bei ya korosho, kwa kweli ukiyatazama yako makato mbalimbali ambayo siyo ya lazima kumkata mkulima. Ukiyapitia makato yote hayo utakuta yako makato ya unyaufu, utakuta kuna kuchangia *union*, kuna *task force* zimeundwa shilingi moja moja kila kilo. Halmashauri nazo zinachangisha, mahali pengine nimeambiwa hata bodi, hili limenishangaza maana bodi tulishazikataza zisifanye hivi, bodi ya korosho, sasa ukijumlisha michango yote hiyo wanachangia shilingi 288 kwa kilo, yote hii wanamsukumia mkulima.

Mheshimiwa Spika, tunataka kuangalia mjengekeo wa bei huu tu-*revisit*, tupunguze na nina hakika wale wakulima wa Tunduru tukifanya hivi tutaweza kuwasaidia angalau wapate fedha ya kupeleka nyumbani, tofauti na vile ambavyo wanalazimishwa kufanyiwa makato.

Mheshimiwa Spika, haya mengine ya kutazama sasa tutafuteje masoko, nimepanga kwamba tutaitisha mkutano wa wadau na ninataka zamu hii siyo kila mtu anakuja anasema Serikali imejipangaje, siwezi kujipanga peke yangu na Wabunge tutawaita na wadau wengine na hata wakulima tutawaita, waje hapa tuzungumze namna ya kutafuta masoko, hata wewe ukiwa mkulima unaweza kutafuta masoko, mbona nimepeleka wakulima Sudan ya Kusini, wengine wametoka huko Manyara, Mbeya, wamekwenda Sudan kuangalia fursa za kilimo za mazao ya kilimo yale ambayo niliwaambia kwamba, kule Sudan mazao yetu yamejaa yanapelekwa na magari ya Tanzania ambayo wenyewe ni watu wa Kenya.

Mheshimiwa Spika, nataka wadau wote hawa tuwaite waje hapa tusaidiane kutazama jinsi gani tunaweza kusaidiana pamoja na Balozi zetu zilizoko nje ili kwa pamoja tutafute masoko ya mazao ya kilimo. Tumefanya hivyo na tumefanikiwa, juzi tumesaini mkataba na wenzetu wa China, wamekubali kununua tumbaku yetu. Kwa hiyo, tuna uhakika sasa tumbaku yetu itanunuliwa, hilo ni soko jipya na tutaendelea kufanya hivyo kwa mazao mengine.

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumzie suala lingine *specifically* hili la Mheshimiwa Zitto. Naomba uniangalie Mheshimiwa Zitto, kwa sababu kwa kweli lina msingi wake, suala hili limekuwa likiuliziwa mara nyingi kwenye Mfuko wa Pembejeo, kwenye utaratibu wa pembejeo na changamoto zilizojitokeza msimu uliopita. Tuliagiza *CAG* afanye Ukaguzi Maalum angalau tuibaini ni mianya ipi inatumika katika utaratibu wa vocha, nani anafanya hivyo, tuweze kumwajibisha. Sasa nafurahi kuwaambia kwamba, ukaguzi ule ulishakamilika, ipo ripoti yake ni hii ni kubwa kabisa, *CAG* ameshatuletea na pia imepelekwa *World Bank* maana nao

walitaka waone utaratibu huu wa vocha ni wapi umegubikwa na matatizo ya kiutendaji.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa mimi ndiyo niliomba kwa *CAG* afanye Ukaguzi Maalum, lakini pia na *World Bank* waliomba ripoti, wamepata nakala lakini siyo siri ripoti hii nilikuwa sijui nimpe nani mwingine tena, nilidhani labda tungeipa *POAC*, lakini sijui Kamati hiyo kama ipo na hata kama haipo inawezekana ipo Kamati nyingine. Kikubwa ni kwamba, ripoti imeshatoka na ipo, *it is ready for consumption*. Mheshimiwa Zitto nadhani hapa tuko pamoja.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, sasa ninaomba nijibu Hotuba ya Waziri Kivuli, Mheshimiwa Rose Sukum, nafikiri ndiyo Waziri Kivuli. Nimeamua kufanya hivi makusudi kwa sababu katika hotuba yake jambo la kwanza nilikuwa sielewi na anisamehe bure tu kama nitakuwa nimekosea. Yeye amesema; Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali itoe maelezo, lakini nikawa najiuliza hivi ni Kambi Rasmi ya Upinzani au Kambi ya CHADEMA maana sina hakika kama haya aliyoyasema ni ya Kambi zote. Nikiyatazama naona kama ni ya CHADEMA CHADEMA tu. Kwa hiyo, sina hakika kama ni ya Kambi Rasmi ya Upinzani.

Mheshimiwa Spika, vyovyote ilivyo, ndiyo maana nikasema nisamehe bure kama wote mlikaa sawa, lakini la msingi ni hivi; katika Hotuba yenu mmesema kwamba, Kambi Rasmi ya Upinzani inataka Serikali ieleze hizi nguzo kumi zimefikia wapi ukizingatia kwamba kufikia 2015 tulitakiwa tuwe tumetekeleza. Naomba nichambue kidogo nguzo ya kwanza, nilitaja ni Dira ya Taifa ya KILIMO KWANZA. Sasa nasema hivi; Dira ya Taifa ya KILIMO KWANZA utekelezaji wake ndiyo unaojenga misingi ya hatua na program nyingine hizi zinazoendelea na maendeleo ni mchakato, huwezi kusema kwamba sasa tulipanga tukifikia 2015 yale maendeleo tunapiga *full stop no development, is a process,* ni mchakato, ni tofauti na matukio. Matukio ni vile vitu vinavyotokea tu kama gari limeanguka ni matukio, mvua imenyesha ni mafuriko, lakini haya mambo ya maendeleo ni *process,* kwa hiyo, Dira ya Taifa tunayokwenda nayo ni endelevu.

Mheshimiwa Spika, alizungumzia pia nguzo ya pili akasema, kugharimia KILIMO KWANZA, tena akasema hili lililenga kuongeza Bajeti ya Serikali. Ndiyo hayo niliyojaribu kueleza mwanzo, lakini hata yeye mwenyewe akitazama mwaka jana tulikuwa na bilioni 288, mwaka huu tumekwenda na 328 hata kama ni kidogo hicho lakini bilioni 40 hapo zimeongezeka. Maana amesema Kambi Rasmi inataka tuelewe mnavyogharimia kilimo. Si hilo tu, tupo katika mchakato wa kuanzisha Benki ya Kilimo ambayo Benki Kuu inashughulikia na hivi sasa nimeambiwa wamefikia kwenye hatua ambayo wanateua bodi na muda si mrefu Benki ya Kilimo itaanzishwa.

Mheshimiwa Spika, kuanzisha Benki ya Kilimo nalo siyo tukio ni mchakato, ni *process,* huwezi kusema unaanzisha Benki ya Kilimo halafu unasema endeleo limeshakamilika tayari. Kwa hiyo, nataka tu Mheshimiwa Sukum, Waziri mwenzangu, uelewe kwamba, *development is a process* na siyo matukio.

Ulizungumzia nguzo ya tatu muundo mpya wa taasisi kwa ajili ya usimamizi na ukasema unashangaa unataka uambiwe muundo mpya Serikali imefikia wapi kwenye kuunda taasisi kwa ajili ya usimamizi. Sasa mimi nikajiuliza tena nikasema jamani sisi Waha tunasema ukiwa mwongo usiwe msahaulifu na ukiwa mgomvi ujifunze na kukimbia maana kuna siku ya kupigwa.

Mheshimiwa Spika, juzi tu Mheshimiwa Wasira hapa alikuwa akizungumzia kuanzisha *President's Delivery Bureau,* taasisi ya usimamizi, wote mlisimama hapa chombo gani mnaanzisha hapa, huku tena unasema mbona hamuanzishi taasisi za usimamizi! Sasa ni *contradiction;* huku unasema msianzishe *bureau* huku unasema mbona hamuanzishi taasisi za usimamizi mnataka muambiwe. Juzi mlisema hamtaki *President's Delivery Bureau* ianzishwe, hii ni taasisi ya usimamizi. Sasa mimi nasema unapoandika lazima uangalie yaliyotangulia na yanayokuja, ndiyo maana nimesema ukiwa mwongo usiwe msahaulifu.

Mheshimiwa Spika, mabadiliko ya mfumo wa kimkakati nimeeleza vizuri, alisema mwenyewe lengo ni kubainisha maeneo ya kipaumbele ili nchi ijitosheleze kwa chakula. Ninaomba tu Waziri mwenzangu asome katika hotuba yangu, ukurasa wa kumi na sita, kuanzia kipengele cha 3.1.1 ataona kwa ufasaha maeneo yametajwa hivyo hivyo kimkakati. Tatizo ni kwamba, mtu anaanza kuandika yanayotoka kichwani kabla hata hajasoma haya mengine, lakini naomba asome hotuba ile atayaona.

Mheshimiwa Spika, alisema pia kuna habari ya ardhi kwa ajili ya KILIMO KWANZA. Anasema hii ilikuwa kwa ajili ya kurekebisha Sheria ya Ardhi na kuharakisha kutenga ardhi kwa ajili ya uwekezaji, Kambi Rasmi ya Upinzani inataka kujua mchakato huu umefika wapi. Narudi tena pale pale kwamba, lakini hao hao ndiyo walikuwa wakisema mambo haya ya kutenga ardhi kwa ajili ya uwekezaji, michakato hii isimame, sasa leo hii anasema tunataka kujua mchakato huu umefika wapi, Kambi Rasmi ya Upinzani inataka kujua. Hivi sasa mbona ni *contradiction;* nasema ukiwa mwongo usiwe msahaulifu, ina maana kwamba wewe mwenyewe umeshaona kwamba kumbe kutenga ardhi ya uwekezaji ni jambo la maana, lakini mahali pengine unalipiga virungu unasema hapana, mimi sielewi.

Mheshimiwa Spika, ninachokitaka, Waziri mwenzangu ajaribu kuwa anasoma vitu kwanza akavielewa halafu akija hapa pale ambapo tumefanya vizuri anasema hongera, pale ambapo hatukufanya vizuri anasema hapa hamkufanya vizuri. Katika hili hukunitendea haki na ndiyo maana unaona na mimi nakugonga virungu kidogo kidogo.

Mheshimiwa Spika, vivutio kwa ajili ya kilimo, yeye anasema kwenye hotuba yake kwamba, hii ni pamoja na kuondoa vikwazo vya masoko, Kambi Rasmi ya Upinzani inataka kujua vikwazo gani. Viko vingi tumeviondoa; tumesema tuondoe ushuru wa maudhi kuanzia kwenye ngazi ya Halmashauri, tumesema tuondoe *road blocks,* lakini vikwazo vingine ambavyo tumetoa ninyi wenyewe ni mashahidi, tumeruhusu wakulima kuuza mazao yao nje, hicho

siyo kikwazo? Kilikuwa ni kikwazo, tumewaruhusu na baada ya kuondoa vile vikwazo wakulima wameuza mazao, wameona faida yake na ndiyo maana nimewaambia tumeweza kuwapeleka baadhi ya wakulima mpaka South Sudan; na kufuatia hilo mkulima mmoja aliporudi amemwandikia moja kwa moja Mheshimiwa Waziri Mkuu akasema, nimeona mambo ya ajabu kule South Sudan, mchele mzuri wa Tanzania, mahindi mazuri ya Tanzania, ndizi nzuri zinazotoka Bukoba, lakini wao wanasema zinatoka Uganda na wanaozipeleka ni Waganda na Wakenya, sisi hatujachangamkia fursa hii.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu ameniagiza nishirikiane na wenzangu tuunde *inter-ministerial task force* ya kuangalia fursa za kilimo katika Sudan ya Kusini baada ya mkulima huyo kuleta ripoti nzuri na baada ya *task force* ile au timu ile niliyoituma iliyokuwa na wakulima na wafanyabiashara, ikiongozwa na Naibu Katibu Mkuu wangu, *Engineer* Mbogo Futakamba na Wakuu wa Wilaya, kurudi na kuripoti mambo mazuri. Sasa ujue hata hivi vinaashiria vivutio katika kilimo Mheshimiwa Msemaji wa Kambi Rasmi ya Upinzani.

Mheshimiwa Spika, viwanda kwa ajili ya kilimo, tunaendelea na juhudi ya kutafuta uwekezaji ili tujenge viwanda, tutumie rasilimali tulizonazo, *minjingu phosphate,* gesi asilia. Mheshimiwa Waziri wa Uwezeshaji amejibu swali hapa vizuri, ameelezea fursa zilizopo lakini kama hiyo haitoshi, bado juhudi nyingi zinaendelea kufanywa. Nilieleza katika hotuba yangu kwamba, tumewasiliana na wenzetu wa *NSSF*, mimi niliwauliza hivi *NSSF* ninyi mnajenga maghorofa tu, wakasema hapana hata kilimo tupo na wakasema kama kuna mwekezaji wa ndani anayetaka kujenga kiwanda cha mbolea, kiwanda cha pamba, viwanda vya korosho, sisi tuko tayari kuweka asilimia 60 na yeye aje na asilimia 40 tuangalie namna ya kumsaidia hiyo ni fursa nzuri tu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, wako wengi wameanza sasa kujitokeza na nimeambiwa kule Shinyanga tayari kuna mwekezaji anaanza, siyo anaanza mazungumzo, maandalizi

ya kujenga kiwanda cha pamba, kimefikia asilimia 60. Kwa hiyo, siyo kwamba tumelala, tunajitahidi lakini hizi ni juhudi ambazo tunatakiwa tuzifanye sisi wote na tusiseme ni Serikali tu, ni Serikali tu.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na sayansi, teknolojia na rasilimali watu. Tunaendelea na utafiti mbalimbali wa aina za mbegu, sitaki kuyarudia yale ambayo niliyasema katika hotuba yangu, lakini nataka niwakumbushe kwamba, Mheshimiwa Rais mwenyewe kwa kupenda mambo ya sayansi na teknolojia za kilimo, aliagiza zitengwe bilioni 30 na fedha hizo zilipitishwa *COSTECH* kwa ajili ya kusaidia kwanza, kukarabati vituo vya utafiti, kusomesha watafiti, kwa ngazi za shahada na za shahada za uzamili. Hiyo ni kuonesha tu jinsi ambavyo tunaendelea kutekeleza nguzo zote hizi kumi na juzi wakati natoa hotuba yangu nimeeleza kwamba, tuna upungufu wa wataalam, wahandisi wa umwagiliaji na kwamba tumeandaa mitaala kwa kushirikiana na Chuo cha Ufundi cha Arusha na Chuo cha Rasilimali za Maji Dar es Salaam, tumeandaa mitaala mizuri ya *Civil Irrigation Engineering* na *next year* wataalam wataingia sokoni, wanaendelea kusomeshwa pale, hizi zote ni taratibu ambazo tunaendelea kuzifanya.

Mheshimiwa Spika, miundombinu kwa ajili ya KILIMO KWANZA, kazi hizi zinaendelea kutekelezwa, labda tu nimwambie Waziri mwenzangu kwamba, Kambi Rasmi ya Upinzani unapotaka kujua miundombinu usifikirie tu miundombinu ni ile ya umwagiliaji, hapana, hizi barabara zinazojengwa kuunganisha Makao Makuu yote ya Mikoa kwa lami unatoka Dar es Salaam mpaka Mtwara ni miundombinu, ambayo yote ina-*contribute to KILIMO KWANZA* na maana ya KILIMO KWANZA nataka nikupeleke shule kidogo; KILIMO KWANZA maana yake siyo kulima tu ni kwamba, sekta zote zinazoweza kuchangia kwenye *growth* ya kilimo ndiyo maana ya dhana hii ya KILIMO KWANZA.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, hata haya mabarabara yanayojengwa yote ni miundombinu, lakini pia yako mengine haya ya umwagiliaji, yako masoko kama yale aliyokuwa

anaulizia Mheshimiwa Machali yanayojengwa na *DASP,* hiyo yote ni miundombinu ambayo ina-*contribute* kwenye KILIMO KWANZA.

Mheshimiwa Spika, mwisho, alizungumzia uhamasishaji wa Watanzania kwa ajili ya KILIMO KWANZA. Labda nirejee tu kwamba, kwenye hotuba yangu nilizungumzia habari ya program*u* ya vijana katika kilimo, kwenye ukurasa wa 69, hii ni aina ya uhamasishaji, ni kweli ni wachache lakini ndiyo tunakwenda hivyo, ndiyo tumeanza huwezi ukaanza tu kruuu ukafika mbali, lakini uhamasishaji unaendelea na sisi wenyewe tunaamini tutafika mahali.

Mheshimiwa Spika kama bado nina dakika chache, naomba niseme jambo moja la tumbaku. Hili la tumbaku nataka nilisemee kwa sababu kama alivyosema Mheshimiwa Naibu Waziri, limetuletea hasara kubwa sana kule Tabora, wakulima walikuwa wanakopa bilioni 88 kupitia Vyama vya Ushirika, wakaja wakadanganywa na watu wengine, sijui wanaitwa nini, wakawalazimisha kukopa kupitia kwenye *Union* wakakopa bilioni 104, gharama zote hizo zinaelekea kwa wakulima. Haya tumeyaona, nimetuma wakaguzi wamekagua, lakini nimeona haitoshi.

Sasa naomba nisome tu angalau; maana nikisema naweza nikakosea yale niliyosema: "Mfumo wa kuagiza pembejeo kwa kuchukua makisio ya Vyama vya Msingi na kuyapitisha *Union*, halafu kuayakusanya kwa *APEX,* unaacha mianya mingi ya ubadhirifu kuanzia kwenye ngazi ya *Union* hadi *APEX.* Mfumo huu unamwumiza mkulima na kwa kuzingatia ushauri ulitolewa na Waheshimiwa Wabunge, Wizara yangu inaagiza yafuatayo: Moja, mfumo wa kukusanya makisio ya pembejeo kutoka Vyama vya Msingi kupitia *Union* kwenda *APEX* uvunjwe. Badala yake nimeagiza uwekwe mfumo utakaozingatia ufanisi zaidi na kuziba mianya ya ubadhirifu. Pembejeo ziagizwe na Vyama vya Msingi vyenyewe kwa kupitia *cluster*, yaani vyama vilivyo karibu kijiografia; mfano, Sikonge, Urambo na Tabora. *APEX* ibaki na jukumu la jukwaa la kitaifa la kukutetea na kuwakilisha wakulima katika ngazi ya Kitaifa na Kimataifa. Uchunguzi wa

awali unaonesha *APEX* haina uwezo na imechangia kuwepo kwa usambazaji na waagizaji wasio na uwezo.

Pili, *tender* za uagizaji na usafirishaji zifanywe na Kamati ya Wajumbe kutoka katika kila *cluster* na kusimamiwa na Bodi za *Union* na Bodi ya Tumbaku.

Tatu, Ushirika wa Tumbaku nchi nzima, utakaguliwa na siyo tu kwa kujificha, kwa kukaguliwa na *COASCO* pale tunapoona haukukaguliwa vizuri. *CAG* atakagua ushirika na hatua kali ikiwa ni pamoja na mrajisi kuingilia na kuwapeleka mahamakani zitachukuliwa.

Nne, mikataba yote ya maendeleo iridhiwe na Vyama vya Msingi na kutekelezwa na Kamati za *Tender* za *Cluster* kwa kushirikiana na Ofisi za Wilaya kwa mujibu wa Sheria.

Mheshimiwa Spika, bado nina dakika moja, naomba nimalizie kwa kusema hivi; ndugu zangu sisi humu sote ni Wabunge, tulipokwenda kuomba kula kila mmoja aliulizwa tumtume nani Bungeni, ukasema mimi hapa na wakakutuma ukaja. Sasa lilobaki watakuuliza tena kwamba, kule Bungeni ulifanya nini?

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, kengele ya pili hiyo; kila mmoja atajibu mwenyewe.

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa nafasi uliyonipa. Sasa naomba Wabunge wapitishe bajeti yangu ili tuweze kufanya kazi zilizopangwa.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

## KAMATI YA MATUMIZI

## MATUMIZI YA KAWAIDA

### Fungu 24 – Tume ya Maendeleo ya Ushirika

Kif. 1001 – *Administration and Human Resource Management* .... ..... ..... .... ..... ..... Sh. 1,353,064,000
Kif. 1002 – Finance *and Accounts Unit* ... Sh. 59,110,000
Kif. 1003 – *Planning, Monitoring and Evaluation Unit* .... ..... ..... ..... … .... .... Sh. 179,815,000
Kif. 1005 – *Legal Service Unit* … … Sh. 32,024,000
Kif. 1006 – *Procurement Management Unit* Sh. 50,720,000
Kif. 1007 – *Management Information Unit* … Sh. 39,410,000
Kif. 1008 – *Internal Audit Unit* ... … Sh. 31,390,000
Kif. 4001 – *Promotion Services Section* .... Sh. 360,380,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 4002 – *Cooperative Micro Finance Section* Sh. 362,410,000

**MHE. MOSES M. MACHALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Naomba tujielekeze kwenye kasma ya 221200 - *Communication and Information*. Naona matumizi yameongezeka kwa kiasi kikubwa kutoka shilingi 840,000 kwenda 4,640,000; naomba ufafanuzi ni kitu gani ambacho kinapelekea kasma hii fedha kuongezeka kwa kiwango hiki?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu hiki kina ongezeko kwa sababu kuna gharama hapa za matangazo ya machapisho ya Kanuni za Uendeshaji na Usimamizi wa *SACCOS* mbalimbali. Kwa hiyo, mwaka juzi zilikuwa milioni sita, mwaka jana zilipungua kidogo kulikuwa hakuna kazi hiyo, mwaka huu kazi imejitokeza ya kuchapisha kanuni, kwa hiyo, kuna ongezeko la gharama hizo.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 4003 – *Cooperate Banking and Investment Section* ... ... ... .... ..... ..... ..... Sh. 124,810,000
Kif. 4004 – *Cooperate Marketing and Information Section* ... ... .... ..... .... Sh. 120,610,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 4005 – *Registration Service Section* ... Sh. 304,630,000

**MHE. SUSAN A. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Naomba kupata maelezo ya *Subvote 221000 - Travel in Country*; kwa nini kifungu hiki kimeongezeka kwa zaidi ya shilingi milioni 70 ukilinganisha na mwaka jana? Nataka pia kujua ni kazi gani wanafanya watu wa usajili?

**MWENYEKITI**: Kitu kinaitwa *travel in-country*, maelezo.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA**: Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu hiki 221000, hasa ni tiketi za ndege, mabasi na posho za usafiri kwa Watendaji wa Tume ya Maendeleo ya Ushirika, kwa kufanya kazi zao ndani ya nchi. Fedha zimeongezeka ili kuimarisha udhibiti na uendeshaji wa Vyama vya Ushirika kwa kuzingatia sheria.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif.4006 – *Inspection and Supervision Services Section* .... .... .... .... ... ... .... .... ..... Sh. 2,764,732,000

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 43 - Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika**

Kif. 1001 - *Administration and Human Resource Management* ... .... ..... ..... ..... ..... ...Sh. 3,970,625,000

**MWENYEKITI:** Naomba niwaandike wale watakaochangia. Nitakuwa nao saba tu kufuatana na muda. Mheshimiwa John Cheyo, Mheshimiwa Dkt. Augustino Mrema, Mheshimiwa Jitu Soni, Mheshimiwa Ezekiel Maige, Mheshimiwa Zitto Kabwe, Mheshimiwa Amina Mwidau na Mheshimiwa Mwigulu Nchemba. Tunaanza na Mheshimiwa John Cheyo. Someni Kanuni.

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Wakati ninachangia juu ya pembejeo na zaidi pembejeo za pamba, nilimwomba Mheshimiwa Waziri, afafanue mambo mawili. Kwanza, haya mambo ya kuchukua mchango kwa wakulima wa pamba, mwaka uliopita karibu bilioni 12 zimechukuliwa kwa ajili ya kununulia pembejeo na Serikali nayo inaweka, halafu mkulima anaenda kuuziwa tena. Jambo hili nililieleza kwamba ni kama wizi vile.

Pia kwa pembejeo hujafanunua juu ya pembejeo za pamba, nazo zitakopeshwa kwa kupitia vikundi na kama ni vikundi mkulima ambaye ana uwezo anaweza pia akakopa? Ninaposema uwezo siyo kwamba mkulima ana heka 100 ni mkulima aliye na heka tano, kumi; na kama anakopa isiwe ya kuonjeshwa pembejeo lakini iwe ni kweli kuweza kumsaidia katika kilimo chake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa ufafanuzi kwa jambo hili.

**MWENYEKITI:** Mawaziri mtakuwa mnaandika, halafu mwishoni mtajibu.

**MHE. DKT. AUGUSTINO L. MREMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati nachangia nilieleza matatizo makubwa yanayokikabili Chama Kikuu cha Ushirika *(KCU)* na Wakulima wa Kahawa. Nikaeleza kutokana na ubadhirifu mkubwa na wizi ulioko ndani ya Chama kile, sasa hivi bei ya kahawa kilo moja ni shilingi 2,000, ambayo haitoshelezi kununua nyama. Nikaeleza wakulima wale hawajapata mabaki wala nyongeza, lakini tatizo kubwa ninaloliona hapa, ni lile ambalo nilimwandikia Waziri wa Chakula na Ushirika barua yangu ya

tarehe 8 Januari, 2013, nikamtumia tuhuma 23, zinazosababisha Chama kile Kikuu kife, kisambaratike. Kubwa pale nilimtumia pia barua ya Waziri wa Fedha ambayo nilikuwa nahoji kwa nini Wakulima wa *KCU* hawakupata fidia wakati wa mdororo wa uchumi.

Waziri wa Fedha akanijibu kwamba, *KCU* walipata faida shilingi bilioni mbili, kwa hiyo, hawakustahili kupata fidia. *KCU* waliposikia hivyo, walifanya mahesabu mengine wakasema wamepata hasara. Mimi nikamwomba Waziri aje kukagua kile Chama Kikuu cha *KCU,* hizo shilingi bilioni mbili ambazo Wizara ya Fedha wanasema tulipata faida ziko wapi na zilitumiwa na nani. Moja hilo.

Pili, hao watu wakaenda kufanya mahesabu mengine wakaonesha kwamba, wamepata hasara na ikaonekana Serikali ilikubaliana nao, wakawaambia basi mtapata fidia ya shilingi milioni 255. Namwomba Waziri ule ukaguzi ulioniambia utakagua Chama Kikuu cha Ushirika ili wale wazembe na wezi wote waliogushi hayo mahesabu waweze kuchukuliwa hatua umefikia wapi?

Jambo lingine ni kuhusu sukari *TPC* nashukuru ilifika, lakini *TPC* wamewafanya *KCU* wakala, lakini ...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mrema ni swali moja.

**MHE. DKT. AUGUSTINO L. MREMA:** Naomba anijibu hilo la Kahawa, nitakuwa nimeridhika, la *TPC* atanijibu baadaye. Asante sana.

**MHE. JITU V. SONI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naomba kuiuliza Serikali; je, itatuhakikishiaje kuwa msimu huu kwa kutumia ule mfumo wa zamani pembejeo zitawafikia wakulima wote Tanzania kwa muda mwafaka hasa Wilaya ya Babati ambapo msimu wa upandaji Mpunga unaanza mwezi wa kumi na kanda zile za juu kule mahindi wanapanda mwezi wa kumi na moja mwanzoni?

Hapohapo kwa kutumia huu mfumo mpya sasa; je, Serikali itakuwa tayari imeshapitisha ile sheria ya kuhakikisha kuwa *VICOBA* vinatambulika kisheria ili Wananchi wote Tanzania nzima waweze kukopa vizuri kwa kupitia huo mfumo mpya?

**MHE. EZEKIEL M. MAIGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi. Nilipochangia jana, nilieleza kwa dhati kabisa kwamba, sikuwa tayari kuunga mkono bajeti hii, sababu ya msingi ilikuwa ni mikakati ya Serikali ya kupambana na umaskini wa Wananchi wa Mkoa wa Shinyanga, ambao unatokana na kuanguka kwa Zao la Pamba, ambalo ndiyo kitega uchumi chao kikuu.

Vilevile nikaeleza kuhusu usalama wa chakula, *food security,* kwa Mkoa wa Shinyanga. Nimesikiliza majibu ya Mheshimiwa Waziri, niseme nimefurahishwa na Wananchi wangu naamini kama wamemsikia wamepata matumaini.

Nimesikia kwa upande wa pamba kwamba kuna kiwanda kinajengwa Shinyanga, ni jambo zuri. Vilevile nimesikia kwamba, natambua uwepo wa Mpango wa *Price Stabilization Fund* na nimwambie tu kwamba, pengine ni vizuri aka-*speed up*.

Kubwa zaidi ni suala la usalama wa chakula, katika historia yetu ya Wilaya ya Kahama, hatujawahi kuwa na skimu, nimesikia kwa mara ya kwanza ametaja kwamba Skimu ya Chela ambayo Mheshimiwa Waziri Mkuu tulimpeleka alipotembelea, kwamba sasa itapata shilingi milioni 630. Ni jambo zuri na Skimu ya Kahanga au Wendele nayo itapata shilingi milioni 825.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu suala hili ni kubwa sana, lakini kwa sababu hatua zimeanza kuonekana,

naona kabisa kwamba, pengine itakuwa siyo jambo la busara kuzuia hata hizi shilingi milioni 635 zisiende kwa kukataa bajeti. Hivyo, nakubaliana hizi shilingi milioni 635 ziende Chela na shilingi milioni 835 ziende Kahanga. Nimwombe tu sana Mheshimiwa Waziri, rafiki yangu, kama bwana Yesu alivyomwambia Mtume Yona kwamba, unanipenda lisha kondoo wangu, nimwombe Mheshimiwa Waziri kwamba, fedha zilizotengwa hizi kweli ziende.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru.

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la mbolea ya ruzuku na ruzuku ya pembejeo, Mheshimiwa Waziri ametoa majibu hapa na ametuonesha Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Nataka nimfahamishe Mheshimiwa Waziri, labda hajafuatilia na mimi ndiyo Mwenyekiti wa *PAC* na hiyo Taarifa inapaswa ije kwangu.

Nataka nimkumbushe Mheshimiwa Waziri kwamba, mwaka 2010/11, wakati akijibu swali la Mheshimiwa Raya Ibrahim Khamis hapa Bungeni, alisema kwamba, wamemwomba *CAG* afanye *Audit*. Mwaka 2012 wakati akijibu swali la Mheshimiwa Rose Sukum alisema, Taarifa ya *CAG* bado. Mwaka huu wakati anajibu swali la Mheshimiwa Mchungaji Israel Natse, kwenye Mkutano huu amesema kwamba, Taarifa ya *CAG* bado. Leo Waziri anatuonesha taarifa ya *CAG,* naamini ameipata sasa hivi hata yeye bado hajaisoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *CAG* katika Taarifa yake ya Serikali za Mitaa, kuanzia ukurasa wa 158 – 160, anazungumzia suala la wizi, ufisadi na ubadhirifu wa mbolea ya ruzuku, kuanzia ukurasa wa 387, ametaja Wilaya mbalimbali na namna ambavyo wizi wa mbolea ya ruzuku ilivyo. Bukombe, Chunya, Handeni, Kilwa, Kyela, Mbeya Vijijini, Liwale, yaani karibia kila Wilaya ya nchi kwamba mbolea ya ruzuku ina matatizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna haja ya kuendelea na mfumo wa mbolea ya ruzuku, kwa sababu, cha kwanza umewanufaisha wachache, lakini pili ni rushwa. Ni njia tu ya kuweza kupitisha fedha. Kule Iringa, katika Kijiji cha Kibena, kuna mwana mama ambaye alikuta jina la mume wake ambaye ni Marehemu miaka miwili iliyopita, katika orodha ya watu ambao wamepata mbolea ya ruzuku.

Kule Kasulu, Nabitale, zile vocha zikishatolewa Mawakala wanazichukua, wanazinunua Sh. 2,000/= toka kwa wananchi. Hakuna sababu ya kuendela. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2012 tumepanga Bajeti Shilingi bilioni 75 ya mbolea ya ruzuku, ilikwenda kwa watu wachache; mwaka huu tunapendekeza Bajeti ya Shilingi bilioni 75 tena, inakwenda kwa watu wachache. Fedha hizi kwa nini zisiende kwenye Miradi ya *Irrigation* ambayo itanufaisha watu wengi zaidi, tutajenga *Infrastructure* zaidi na tutaweza kupata fedha zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa naomba kwamba, haiwezekani tukaondoa umasikini Tanzania bila kuwekeza kwenye kilimo. Lakini hatuwezi kuwekeza kwenye mbolea ya ruzuku na pembejeo ambazo zinakwenda kuwanufaisha watu wachache! *(Makofi)*

Juzi taarifa imetoka, sisi ni nchi ya pili kwa umasikini toka chini. Burundi tu nao wanatuzidi, *Global Monitory Report*, asilimia 68 ya Watanzania wanaishi chini ya dola 1.25. Nilikuwa naomba na nisiporidhika na haya majibu nitatoa Shilingi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Amina.

**MHE. AMINA M. MWIDAU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante na mimi kunipa nafasi. Naomba Mheshimwa Waziri aniambie Serikali ina Sera gani juu ya kilimo cha maua na katika dhana nzima ya kukuza uchumi na kuondoa umasikini? Kwa sababu ukiangalia nchi kama ya Uholanzi, wanawake wana fedha kiasi kikubwa sana kutokana na Sera yao nzuri

inayowawezesha kulima kilimo hiki. Katika nchi yetu ni Kilimanjaro tu *so far* ndiyo kilimo hiki kinaendelea.

Sasa namwomba Mheshimwa Waziri aniambie kuwa Serikali ina Sera gani juu ya kilimo cha maua? Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Hata Arusha waanalima, sisi kwetu yuko mtu mmoja tu, Njombe. *(Kicheko)*

**MHE. MWIGULU L. N. MADELU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Mheshimiwa Waziri, ameelezea nia ya Serikali ya kuanzisha Benki kwa ajili ya kuwafaidisha wakulima. Lakini kwa jinsi ninavyojua Benki huwa siyo rafiki kwa watu masikini, na ukiangalia kwa Watanzania leo, wakulima wadogo wadogo ndiyo wanaohangaika sana na njaa, lakini wakulima wadogo wadogo vilevile ndiyo wale ambao hawana *Collateral*, ningeomba Waziri atakaposimama kujibu atuelezee na kuwaondoa hofu Watanzania, ni namna ipi Serikali imejipanga kuhakikisha kwamba wakulima wadogo wadogo hasa ambao wamekuwa wakihangaika na njaa ambao wamekuwa wakisubiria chakula cha msaada, ambao wamekuwa hawana *Collateral*, ardhi yao haijapimwa, ni kwa mazingira yapi Serikali imejipanga inapoanzisha hiyo Benki kwamba wataweza kinufaika wale wakulima wadogo wadogo na kuweza kupiga hatua?

Kwa sababu vinginevyo, tukianzisha tu Benki na tutaiita Benki, tutaendelea kufaidisha daraja lile lile ambalo wangeweza kukopa hata *NMB*, wangeweza kukopa hata Mabenki ambayo yapo. *(Makofi)*

Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Waziri aseme, Serikali itatumia utaratibu upi ambao utatuhakikishia kwamba wakulima wale wadogo wanaweza kuondokana na kilimo cha kujikimu kwa kupata kilimo cha kisasa ambacho kinaweza kikaenda kibiashara na wakakopesheka? Ahsante.

**MHE. MTUTURA A. MTUTURA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Katika michango ya Mheshimiwa Saidi

Mtanda na mchango wangu wa maandishi, na michango mingine ya Wabunge ambao wanatoka maeneo yanayolima Korosho, tulitaka ufafanuzi kutoka kwa Mheshimiwa Waziri kutokana na mfumo huu wa Stakabadhi Ghalani.

Mheshimwia Mwenyekiti, takribani miaka miwili mfululizo, mfumo huu Serikali imeshindwa kuusimamia, hatuelewi ni kwa makusudi au kwa bahati mbaya au kwa kukosa uwezo. *(Makofi)*

Sasa tunaomba ufafanuzi kotoka kwa Mheshimiwa Waziri: Ni mpaka lini wakulima wa Korosho watapata mateso ya kutouza Korosho zao na pale inapotokea wanauza, wanauza kwa bei ya chini kabisa, na pale inapotokea kuuza kwa bei ya chini hata malipo yale ya chini hayapatikani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa mfumo huu Serikali imeshindwa kuusimamia miaka miwili mfululizo, kwa nini Serikali isikubali kusitisha mfumo huu kwa miaka miwili ili ijipange ikusanye uwezo ndipo ianze kusimamia mfumo huu wa Stakabadhi Ghalani? Naomba maelezo ya Serikali. *(Makofi)*

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Katika mchango wangu nilizungumzia kuhusiana na wadau wa *SAGCOT* ambapo mmoja wao ni Kampuni kubwa ya mbengu ya *Mosanto***.** Pamoja na mambo mengine, nilieleza madhara mbalimbali ya mbegu zinazozalishwa na Kampuni husika, na vilevile nikatoa mifano ya nchi mbalimbali duniani, kuanzia Mabara ya *Europe*, Amerika, ambapo wameamua kupiga marufuku Kampuni husika kujishugulisha na shughuli zozote za uzalishaji wa mbegu sababu zimethibitika kuwa na madhara makubwa sana kwa wakulima masikini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbali na kuwa na madhara ya kiuchumi, lakini vilevile kuna madhara ya kiafya. Sasa ninafahamu kwamba *Mosanto* ni mmoja wa wadau, na

ninafahamu kwamba *Mosanto* ni mmoja kati ya watu ambao wametoa fedha takribani dola milioni 50 kwa Afrika, sijajua kwa Tanzania mchango wake utakuwa ni kwa kiasi gani katika kuboresha ama kuendeleza kilimo kwa lugha kwamba wanataka kuhakikisha kwamba Afrika inaondokana na njaa. Sasa nilitaka tu Serikali ituambie, msimamo wake kuhusiana na *Mosanto*, na kama haijafanya uchunguzi wowote kuhusiana na Kampuni hii inayopigwa vita duniani, na kama ina mikakati yoyote ya kuchukua dhidi ya huyu mbia ambaye tumeonekana kumkumbatia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka nipate huo ufafanuzi kwa sababu kwa taarifa ambazo zipo ni kwamba wameshaanza kuingia kupitia Pamba. Sasa inawezekana pamba tukaanza lakini tunaweza tukaendelea pia kwenye mazao mengine ikawa ni hatari kubwa sana kwa kizazi cha sasa, kizazi kijacho na mbaya zaidi ni hatari kubwa sana kwenye ardhi yetu ambayo historia zinaonyesha kwamba tukishaanza kutumia mbegu za aina hiyo, kuja kurudi katika mfumo wa kawaida inakuwa ni kazi sana. Lakini zaidi inamfanya mkulima mdogo awe mtegemezi wa mbegu za Mabeberu. Ule utamaduni wetu wa asili wa kulima mbegu na kuweza kupanda na kuja kutumia tena mbegu kwa miaka miwili ama mitatu unaweza ukaisha kutokana na mfumo huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nilitaja tu nipate kauli ya Serikali kuhusiana na hili. Niseme wazi tofauti na alivyojibu Mheshimiwa Naibu Waziri kiwepesi wepesi, hakuna mtu mwenye *interest* yoyote. Kwa hiyo, ajibu kwa maslahi ya Taifa. Ukiona watu wanapinga *GMO,* hawapingi kwa sababu wana *interest.* Kwa hiyo, nilitaka nipate majibu ambayo yana nyanja...

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Lembeli!

**MHE. JAMES D. LEMBELI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushuru. Katika mchango wangu wa kuzungumza, pamoja na mengine mengi, nilizungumzia matatizo ya Afisa Ushirika pale Kahama kwamba amekuwa ni chanzo cha wizi wanaofanyiwa wakulima wa Tumbaku.

Sasa katika maelezo ya Mheshimiwa Waziri, sijamsikia akizungumzia tatizo hilo. Naomba sana nisikie maelezo yake, vinginevyo msimamo wangu katika kutoiunga mkono hoja hii, utabaki pale pale. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Kwa sababu ya Afisa Ushirika mmoja! *(Kicheko)*

Haya, Mheshimiwa Ester Bulaya wa mwisho.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Katika mchango wangu nilizungumzia mambo mbalimbali lakini hasa suala zima la vijana kushirikishwa katika Sekta ya Kilimo na kuwasaidia kuondokana na tatizo zima la ajira. Nimeshangazwa kitu kimoja, nilimpongeza Mheshimiwa Waziri kwamba tayari wameshaanza kulifanyia kazi. Lakini *the way* alivyojibu, amejibu *by the way;* yaani, kama hakukuwa na ulazima wa kulijibu kiunaga ubaga suala hili vijana, na hasa ukizingatia kwamba watu ambao wanaathirika na tatizo kubwa la ajira ni vijana.

Hivi karibuni tumepitisha Mpango Maalum wa Kukuza Ajira kwa Vijana na ilikuwa wanaojihusisha na Sekta ya Kilimo pekee kabla hatujaleta *amendment* ya kuhusisha maeneo mengine. Lakini cha kushangaza, Mheshimiwa Waziri hajagusia kabisa huo mpango. Ameeleza tu ni vijana wangapi ambao wamewasaidia, kama Igunga na maeneo mengine. Lakini kuuzungumzia ule mpango ambao tumepitisha na Bunge lako Tukufu, wao kama wahusika kwenye Sekta hii ya Kilimo, na tulitegemea wauweke wazi kuanzia mwaka huu wa fedha, Mheshimiwa Waziri hajazungumzia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitegemea angeelezea katika maeneo yanayofaa katika kilimo cha umwagiliaji, katika utekelezaji wa mpango huu ni hekta ngapi ambazo zimetengwa kwa vijana. Lakini angeelezea kwa kuanzia Wizara yake imetenga kiasi gani, lakini amezungumzia tu hawa vijana tu sijui elfu ngapi ambao amewasaidia, lakini *specific* mpango ambao tumeupitisha, hakuuelezea kabisa.

Kama nilivyosema, wale vijana, wengi ambao waliokuwa huko vijijini, yale siyo maeneo yao! Ni ya wazazi wao!

Mheshimiwa Waziri, nakuamini sana. Naomba uwaeleze vijana wa Tanzania walioshindwa kupata ajira kwenye maeneo mengine wanatumia ardhi yao, na hasa ukizingatia tumepitisha ule Mpango Maalumu. Wizara yako imejipanga vipi kutekeleza mpango huu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

**MWENYEKITI:** Ahsante, majibu.

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na hili la Mheshimiwa Cheyo, la pembejeo. Alitaka kujua kama kule kwenye pamba pia tutatumia vikundi au mfumo gani. Mimi nilikuwa kule kwenye Mkutano wa wadau wa Pamba. Tulilizungumza kwa kirefu, tukafikia mahali ambapo tulisema wadau wenyewe tutakaa nao tuamue ni mfumo gani. Kama unakumbuka Mheshimiwa Cheyo, kuna wakati wengine walisema, Halmashauri zishiriki. Tukasema hapana, Halmashauri tusizibebeshe mzigo huo, haziwezi kupeleka pembejeo hizo.

Tukasema tutakaa na wadau wote ili tuone ni mfumo upi ambao unafaa kuwafikishia wakulima wa pamba. Kwa hiyo, suala hili liko kwa wadau na wewe mwenyewe ni mdau na siyo Serikali tu kuamua kwamba tutatumia mfumo huu. Kwa hiyo, mimi namhakikishia Mheshimiwa Cheyo kwamba hili litaamuliwa katika ngazi ile ya wadau ili liwe *effective*.

Pia nilitaka nimwambie kwamba katika kufuatilia masuala ya pembejeo, nataka nimhakikishie kwamba bado nia yangu ni thabiti ya Mfuko ule wa *CETF*, ambao ndiyo nao unahusika kushugulikia pembejeo, nao ufanyiwe ukaguzi kwa sababu una-*handle Public Funds.*

Mheshimiwa Mrema aliuliza kuhusu *KNCU.* Liko eneo ambalo amemwandikia Waziri wa Fedha, sasa hiyo barua, mimi sijui, labda Waziri wa Fedha amemwandikia, mimi

hajaniandikia. Lakini nizungumzie masula ya *KNCU.* Nilichokubaliana na Mheshimiwa Mrema ni kwamba, Vyama vya Ushirika vingi nchini vina matatizo. Vingi tu! Hata *KNCU* siwezi kui-*rule out*. Nimekwenda kule kusuluhisha mgogoro wao na *TPC,* nikajua kwamba mojawapo ya matatizo waliyonayo ni *weakness* ya *Management.*

Kwa hiyo, ninachoweza kumhakikishia Mheshimiwa Mrema ni kwamba, kama nilivyosema hapa nilipokuwa kwenye hoja, Vyama vyote vya Ushirika ambavyo vinalegalega vitakaguliwa. Kama *COASCO* haiwezi kukagua sawasawa, tumesema tutatumia vyombo vingine vya Serikali. Mimi naweza kutumia *Internal Audit System* ya Wizara yangu, inapokuwa haiwezi kufanya kazi hiyo, tutatumia tena *CAG* kuhakikisha kwamba Vyama hivi vinakaguliwa na hatimaye fedha hizi za wakulima zinajulikana jinsi zinavyotumika.

Kwa hiyo, hilo ndilo ambalo ningeweza kumwambia. Kuhusu fidia, naambiwa pia kwamba, hii fidia anayoisema Mheshimiwa Mrema, *KNCU,* nimeambiwa kwamba haikupata faida ya Shilingi bilioni mbili, bali ilionekana kuwa ilipata hasara. Katika awamu ya kwanza hesabu zao zilitafsiriwa kimakosa, lakini walistahili kupata fidia. Malipo hayakufanyika kwa sababu zililetwa nje ya muda. Sasa mimi nadhani, baada ya majibu haya niliyokupa, Mheshimiwa Mrema aanze kufuatilia mpaka ajue mwisho wake inakuwaje.

Mheshimiwa Jitu V. Soni, alisema mfumo wa zamani wa pembejeo uboreshwe ili ifike mapema. Mimi kinachonipa faraja ni kwamba, sasa hivi tumeanza vizuri, Bajeti mwezi wa Sita tutakuwa tumeshaikamilisha.

Tukishaikamilisha mwezi wa Sita, ina maana kwamba, kwanza *cash flow* haitakuwa kama ile ya zamani tena ambayo fedha zilikuwa zinakuja mwezi wa Nane, ku-*print* vocha zinachelewa. Tunaamini kwamba vocha zitakuja mapema, japokuwa hata msimu uliopita mimi nilijitahidi, mwezi Agosti, maeneo yote ambayo yanapata mvua za kwanza hata kule kwetu Kigoma, vocha tarehe 26 Agosti zilikuwa zimeshafika.

Matatizo yalianza na Wafanyabiashara tu hawa ambao wanapenda kujinufaisha wenyewe. Sasa namhakikishia tu Mheshimiwa Soni kwamba, tutajitahidi pembejeo zifike kwa wakati kwa sababu tunaamini fedha zitakuwa zimepatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu *VICOBA*; bado hivi *VICOBA*, mimi ninavyoelewa ni kwamba vinatakiwa viandaliwe kisheria ili vitambuliwe kwamba viko pale kisheria. Mpaka sasa *VICOBA* haviko kisheria. Kwa hiyo, ni jambo ambalo kwa kweli nadhani itabidi lifanyiwe kazi kwa sababu tukiingia mtindo kwa Mabenki kukopesha, ndiyo maana kwenye utaratibu tutakapokutana Mabenki lazima yashiriki. Mabenki yakivikubali *VICOBA*, tutakubaliana, lakini yasipokubali itabidi tuanze utaratibu wa kuvihalalisha navyo kisheria, labda kuviwekea Sheria Maalum au Sheria nayo ivitambue kama Vyama vingine vya Ushirika vilivyo. Kwa hiyo, hiyo ndiyo hatua nadhani tunaweza tukaichukua.

Mheshimiwa Maige yeye, namshukuru sana kwa kukubali kuunga mkono hoja ili fedha hizi ziweze kwenda.

Mheshimiwa Zitto, mimi naomba niseme hivi, katika fedha tulizonazo msimu huu, nimeeleza hapa, tuna Shilingi bilioni 19 za *World Bank.* Fedha hizi ni mahususi kwa ajili ya ruzuku ya pembejeo kwa kutumia mfumo wa vocha. *World Bank* hawatumii mfumo wa aina nyingine. Sisi tume-*debate* mara mbili, tatu, kwamba hivi hizi fedha tuzikose kwa sababu ya changamoto tulizonazo kwenye vocha? Sisi tumeona kwamba siyo busara! Fedha zipo!

Mheshimiwa Mwenyekiti, la maana hapa siyo kuziacha na kusema tuachane na mfumo huu. Mimi nadhani la maana ni kuangalia kama tulivyofanya ukaguzi na ripoti mwenyewe unayo, mimi nilipokujibu juzi kwamba sijaiona, ni kweli nilikuwa sijaiona. Maana yake kule Wizarani, Wizara ni kubwa pale, na mimi ni Waziri, ni mtu mkubwa pale. Nina mambo mengi! Nilikuwa sijaiona. Sasa nimeiona na ndiyo maana nikakwambia ripoti hii ipo hapa. Lakini ninachotaka

kusema ni hivi, mimi sidhani kama ni busara kusema kwamba tuachane kabisa na utaratibu huu.

Mimi nadhani tuangalie ripoti imesema nini, ni mianya ipi ambayo inaleta ubadhirifu tuizibe, tuone tutakavyokwenda, lakini kusema tu tuache wakati *CAG* ameshatuambia, mianya ya ubadhirifu ni hii, ni hii, ni hii; na maana ya *auditing* mimi ninavyoelewa ni kwamba ni pamoja na kukupa fursa ya kuangalia ni njia zipi zitumike kuziba mianya ya ubadhirifu.

Sasa tutajipanga vizuri na nimesema tutakuwa na Mkutano hapa, wadau wote mtakuja na Mheshimiwa Zitto utakuwepo hapa maana nimepanga tufanye tukiwa hapa Bungeni, nawaomba tuangalie, tujaribu tuone mianya yote tuizibe, tukifanikiwa jambo litakuwa zuri. Huko baadaye tukiona mfumo hautufai, tutauacha.

Mheshimiwa Amina alizungumzia Sera juu ya Kilimo cha Maua, hiki ni kilimo tu kama kilimo kingine. Kwa hiyo, Sera inayo-*govern* mazao haya ni Sera ya Kilimo, ambayo zamani tulikuwa na Sera ya mwaka 1997. Sasa Sera ya Kilimo tayari imepitishwa, na sasa hivi kinachofanyika ni kuitafsiri kwa Kiswahili ili iweze kueleweka. Tutakachokifanya tu ni kwamba, maua ni sehemu mojawapo ya mazao ya bustani, na sisi tunao mkakati wa kuendeleza mazao ya bustani.

Tunataka sasa tupanue mazao ya bustani, yasiwe tu ni Arusha na Moshi, yanaweza kulimwa mpaka kule Kusini. Sasa hivi tumejenga kiwanja cha Songwe, ambacho kitakuwa kiwanja kikubwa. Tunafikiri tutakitumia kwa manufaa ya mazao kama haya. Maana yake ukilima maua unatakiwa uyasafirishe mapema, siyo uyaweke kwenye Lori, upeleke Dar es Salaam, yatanyauka.

Kwa hiyo, lengo hapa sijui kama alikuwa ana maana ya Sera hasa, labda alikuwa anataka kusema kuna mkakati gani; mkakati ni kwamba mazao yote ya bustani tunataka kuyapa kipaumbele na mojawapo ni zao hili la maua na tunataka liende mpaka Mikoa ya Nyanda za Juu Kusini na

zitatumia *advantage* hii ya kuwa pia na uwanja ambao tunaujenga kule na barabara nzuri tulizonazo.

Mheshimiwa Mwigulu Nchemba alizungumzia Benki ya Kilimo ni lini itakuwa rafiki kwa wakulima? Mheshimiwa Mwigulu hii ni changamoto, lakini lengo la kuanzisha Benki ya Kilimo ni kwa sababu tulikuwa tunajua zipo Benki nyingi siyo rafiki wa wakulima.

Kwa maana hiyo, mchakato wote wa kuanzisha Benki ya Kilimo unakwenda katika misingi hiyo hiyo kwamba Benki hii iwe Benki ya wakulima. Kwa hiyo, matarajio yangu ni kwamba hii Benki itakuwa rafiki wa wakulima. Tutajitahidi tufanye kila linalowezekana kwamba wakulima wawezeshwe na waweze kupata mikopo kwa masharti nafuu katika Benki hii. Mbona kwenye mfuko wa pembejeo kuna masharti magumu, lakini wanapokuja wakulima tunarekebisharekebisha na tunapunguza angalau masharti yale yasiwe magumu. Benki hii ni ya Watanzania, ni ya wakulima, kwa hiyo, tunajitahidi iwe ni Benki rafiki kwa wakulima.

Mheshimiwa Mtutura alizungumzia kuhusu stakabadhi ghalani. Mheshimiwa Mtutura mimi nilisema kwamba stakabadhi ghalani nimekubali kwamba kuna changamoto nyingi na kila mtu ameziona. Ndiyo maana nilisema tumekubaliana na mwenzangu Waziri wa Viwanda na Biashara kwamba sasa huu mfumo tutaurejea halafu tutaandaa Wizara ya Viwanda na Biashara ambayo ndiyo *custodian* wa mfumo huu, itaandaa Muswada wa Marekebisho ya Stakabadhi Ghalani kuangalia kasoro zote zile kuhusu watunza maghala na kuhusu mianya yote ile inayosababisha mkulima apate matatizo.

Kwa hiyo, Muswada huu utaletwa ili kurekebisha utaratibu wa stakabadhi ghalani. Lengo letu tunataka baada ya hapo tu-*improve* zaidi tuingie katika mfumo wa *commodity exchange*, ndiyo lengo letu kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sijui kulikuwa na lingine tena!

**SPIKA:** La Mheshimiwa Halima Mdee, Mheshimiwa Ester Bulaya na yuko Mheshimiwa Lembeli hujajibu.

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa dada yangu naye Ester hajanitendea haki. Muda wenyewe uliuona pale ulivyokuwa. Kwanza hili jambo la ajira kwa vijana hata mwenyewe unaliona kwamba ndiyo lina-*surface* na tunalishikia bango. Kwa hiyo, sitarajii kwamba lingeanza kwa kasi kubwa uliyofikiria kwamba tuanze tu na kufikia vijana milioni mbili.

Mimi nadhani hata hatua hiyo tuliyofikia kama ulivyoanza kupongeza ni vizuri. Lakini ninachotaka kumhakikishia ndugu yangu Mheshimiwa Bulaya ni kwamba, mimi nimeshirikiana kwanza kwangu imeandaliwa *program* ya ajira ya vijana ndani ya Wizara. Hiyo ni vijana kwa maana ya kilimo tu. Lakini tunashirikiana pia na Wizara ya Kazi, angepewa nafasi Waziri husika angeeleza. Tuna *program* ambayo tumejiandaa kwa ajili ya kuhakikisha kwamba vijana hawa wanapata ardhi. Ardhi huwezi kuipata hivi hivi, ni lazima kwanza ipimwe na ikishapimwa ifanyiwe *titling* ili uweze kupata kitu ambacho ni *titled*. Kwa hiyo, program hiyo ipo ya kupima mashamba na sisi tumetenga fedha kwa ajili ya kupima mashamba. Vijana watapata ardhi halafu itapata *title* ili iwawezeshe hata kutumika kama *collateral* kupata mikopo kwenye mabenki na kwenye mifuko ya pembejeo.

Pia kuna mawazo mengine kwamba baadhi yao tuta-*borrow* utaratibu ambao tumeona kwenye nchi nyingine. Hata vyeti vyao vinaweza kutumika kama *collateral* yaani ukiwa na cheti tu cha *degree* unaweza ukaki-*hold* kikawa *collateral* ukapata mkopo. Kwa hiyo, Mheshimiwa Ester Bulaya tupo *serious* kabisa na jambo hili na ninakualika na nakuomba ukipata nafasi njoo Wizarani tusaidiane na wewe uchangie mawazo makubwa kama hayo.

**MWENYEKITI:** Bado wawili, Mheshimiwa Lembeli na Mheshimiwa Halima Mdee. Mheshimiwa Lembeli ni juu ya Afisa wa Ushirika anayeleta matatizo kule.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hili la Mheshimiwa Lembeli namwomba tu akubali kwamba masuala ya Watendaji ndani ya Ushirika ni kama yale tuliyoyazungumza, tunayafanyia kazi na Waziri ameshatoa maagizo, kuna lile suala la mgogoro wa Tabora, kuna Watendaji wa Ushirika ndani ya Mikoa ya Pwani, Mtwara na kadhalika. Kwa hiyo, tutalifanyia kazi katika kufanya *review* ya Watendaji wa Ushirika lakini Mheshimiwa Waziri labda atakuwa na maelezo ya ziada.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati najenga hoja pale mwanzoni nilisema tu kwamba ni vigumu kuzungumzia jambao ambalo linakinzana na ufahamu wako. Mimi nilitaka kusema tu jambo moja kwamba sisi katika kampuni ambazo tunafanya nazo mikakati ya kuendeleza *Southern Agriculture Growth Corridor of Tanzania - SAGCOT,* Monsanto ni moja na kama makampuni hayo yatakuwepo mengi, sasa *Monsanto is a multinational. The fact* kwamba *Multinational Health Controversies* kwamba ina migogoro ya hapa na pale, siyo kitu cha ajabu!

Mheshimiwa Mwenyekiti, *Coca Cola* ni ya *multinational* inajulikana dunia nzima, nayo ina migogoro ya hapa na pale. Sasa tunasema sisi wenyewe Watanzania niliposema vile nilisema kwamba ngome yetu katika tafiti za kilimo Tanzania siyo Munsanto ngome yetu ni watafiti sisi wenyewe tuliokuwa nao hapa Tanzania.

Pia watafiti wetu hawa siyo watafiti ambao kazi hii niliposema, wameanza leo na jana. Kenya, Uganda, Ethiopia na kadhalika kote wanakuja Mikocheni kuja kuonana na Dkt. Ndunguru, Kulaya na Asha, Rosheni na wenzake. Sasa ndiyo nasema tukikaa tunajifunga hivi kwa kutengeneza uwoga kuwatisha wananchi ni jambo la hatari. Mbegu za sasa hivi zinazotumika kwa mfano kwenye Pamba ni mbegu za Kyuton. Sasa Kyuton wamekuja pale, wao mbegu zile *as a high breed version* wanazitoa kwenye utafiti uliofanywa Ukiliguru. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nilikuwa nafikiri tu kwamba katika haya, wakati wenzetu wanafanya mikakati

ya kutumia mbegu bora, sisi tusiwatengenezee uwoga Watanzania. Tuamini kwamba mimi ni Mchumi na wewe ni Mwanasheria, lakini wapo wenzetu ambao kazi yao na maisha yao kwa miaka 40 iliyopita wamekuwa wanafanya tafiti ya vitu hivyo. Lakini tukianza leo sisi kujiona tunajua kuliko wao wenye mamlaka yao, tutakuwa tunafanya makosa makubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwamba Kurugenzi ya Tafiti ya Tanzania ya Wizara ya Kilimo ni moja katika Kurugenzi ambayo ina imani ya Wanasayansi dunia nzima. Tuwaache wafanye kazi yao na ni kazi yao kutulinda dhidi ya madhara ya aina yoyote ambayo tunakadiria yatakuwepo hayo na ni wajibu wenu ninyi Wanasheria kutulinda dhidi ya migogoro yoyote ya kisheria ambayo tunaona inaweza ikatukwaza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hao hao Monsanto ni Kampuni katika Makampuni makubwa ya Marekani, lakini pia wana migogoro ya kisheria na maeneo mengine. Hilo linajulika. Wajibu wetu sisi ni kujikinga na migogoro hiyo. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Kifungu kilichotajwa hapo juu kimeafikiwa?

**WABUNGE FULANI:** Ndiyoo!

**MBUNGE FULANI:** Bado swali la Mheshimiwa Zitto Kabwe!

**MWENYEKITI:** Aah! Mimi nilijua mmeridhika, maana nimeona mmepumzika kweli.

**MHE. ZITTO Z. KABWE:** Nilitoa taarifa kwamba nisiporidhika nitatoa Shilingi.

**MWENYEKITI:** Sasa nimeona hamchangamki, nikaona umeridhika. Haya, Mheshimiwa Zitto!

**MHE. ZITTO Z. KABWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sikuridhika na maelezo ambayo ndugu yangu Mheshimiwa Eng. Chiza amezungumza.

Kwanza, sawa kuna fedha za *World Bank...*

**MWENYEKITI:** Sasa tuwe *specific*, unataka sisi tusikie nini?

**MHE. ZITTO Z. KABWE:** Hoja yangu ni ile ile kwamba fedha ambazo zimepangwa kwa ajili ya pembejeo ya ruzuku zihamishwe zipelekwe kwenye miradi ya umwagiliaji kwa sababu imethibitishwa ya kwamba fedha hizi zinanufaisha watu wachache, zinaliwa na zinafanyiwa ubadhirifu. *(Makofi)*

Ninachotaka ni kumkumbusha Mheshimwa Waziri, Mjomba wangu kwamba Benki ya Dunia wanatupa mkopo. Hiyo fedha siyo ya bure, siyo *grant,* ni mkopo. Kwa hiyo, hatuwezi kusema kwamba tuzisiache hizo fedha kwa sababu tutakuja kuzilipa tu. Kwa hiyo, kuzichukua sasa na kuwapelekea watu wachache, tutakuja kuzilipa hapo baadaye. *(Makofi)*

Mheshimiwa Waziri anasema kwamba tunabadilisha mfumo, twende kwenye kuwapa Vyama vya Ushirika, lakini mara baada ya kusema hivyo kauli iliyofuata ni kwamba Vyama vya Ushirika vina matatizo, vina ubadhilifu na vingine kama vyetu kule Tabora, Bodi nzima imefukuzwa. *(Makofi)*

Kwa hiyo, ina maana tunahamisha kutoka kwenye mfumo mmoja wa kifisadi, tunapeleka kwenye mfumo mwingine wa kifisadi. Njia pekee ni kuondokana na kabisa na hizi fedha. Lakini bahati nzuri Naibu Waziri, Waziri ni *Engineer* wenu Mchumi, nionyeshe *evidence* mahali popote kwamba toka tuanze kutumia mfumo wa mbolea ya ruzuku na pembejeo za ruzuku ukuaji wa Sekta ya Uchumi umekua maradufu tunavyotaka. Hakuna *evidence!* Hakuna hata moja! *Growth rate* ya Sekta ya Kilimo imebakia *maximum 4.5%,* haijakua zaidi ya hapo. *Target* yetu ya MKUKUTA *8% to 10%,* hatujawahi kufika, na tuna *pump* pesa kila wakati, *60*

*billion, 60 billion, 75 billion, 75 billion!* Hatuwezi kuendelea kumwaga fedha za nchi hivi.

Natoa hoja na ninaomba Waheshimiwa Wabunge waniunge mkono ya kwamba fedha zote ambazo zimetengwa kwenye bajeti ya mwaka huu kwa ajili ya kutoa mbolea ya ruzuku zipelekwe kwenye umwagiliaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Hapana, tukubaliane. Kwenye Shilingi hawasimami. Kha! Anayesimana ni yule anayetaka kuzungumza. Mheshimiwa Keissy, Mheshimiwa Jenista Mhagama, Mheshimiwa John Chenge, Mheshimiwa Machali na Mheshimiwa Ole-Sendeka. Si nimewataja! Haya, Mheshimiwa Keissy!

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hata kwenye hotuba yangu ya kuchangia Wizara ya Kilimo nilipinga kabisa kuhusu ruzuku ya mbolea. Hizi pesa zinaandikwa hata kwenye makaburi, watu waliokufa miaka 10 iliyopita, ushahidi ninao. Hakuna tija imepatikana kabisa kutoka kwenye ruzuku ya mbolea. Nilishauri ziende kwenye *irrigation* kama alivyosema Mheshimiwa Zitto. Hatuwezi kukubali nchi yetu kuingia kwenye madeni, hakuna tija yoyote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hizi pesa zinaliwa na wachache. Ni mtandao wa wizi, wa fedha za Serikali! Tumekaa! Tangu nimeingia Bungeni nilikuwa mchangiaji wa kwanza kupinga fedha za ruzuku ya mbolea. Zimekwenda mpaka kwenye kijiji wanacholima mihogo, maiti zinaandikwa, lakini tuseme vipi? Sitakubali kabisa pesa ziende *irrigation* ili wananchi wetu wakalime. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatukubali! Suingi mkono mpaka fedha hizi ziende kwenye *irrigation*! *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ni hoja hiyo.

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namwunga mkono Mheshimiwa Zitto Kabwe mia kwa mia! *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Jenista!

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge tunatakiwa kuwa na busara. Busara yangu mimi niliyesimama, inanituma niseme yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la umwagiliaji kweli ni tatizo linalotakiwa kushughulikiwa na Serikali, lakini suala la kuwawezesha wakulima kupitia ruzuku ya mbolea, ruzuku ya mbegu na ruzuku ya madawa ni kipaumbele kabisa kwa Serikali yetu. Leo hii kwa sababu za kimsingi ambazo zimewafanya wakulima wakose kusimamiwa vizuri kwenye mfumo wa ruzuku hatuwezi kuchukua ndiyo kigezo cha kuondoa kuwasaidia wakulima wapate ruzuku ya pembejeo, ruzuku ya mbegu na ruzuku ya dawa na kuhamisha fedha hizo kupeleka kwenye umwagiliaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nashauri kwamba mambo haya yote mawili ni mambo ya msingi. Ruzuku kwa wakulima ibaki kama ilivyo, lakini isimamiwe inavyopaswa, na Serikali ijipange kutafuta kila njia kuboresha kilimo cha umwagiliaji. Hayo mambo yote ni ya msingi siwezi kabisa kuona kwamba suala la ruzuku, kwangu katika Jimbo la Peramiho tumenufaika. Naomba kila jambo liangaliwe kwa namna yake. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Chenge!

**MHE. ANDREW J. CHENGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda tu niseme kwamba navutiwa na hoja ya Mheshimiwa Zitto Kabwe, lakini siiungi mkono. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hivyo kwa sababu kwenye Kamati ya Bajeti eneo hili tumehangaika nalo sana. Kwa siku tatu tumekaa na Wizara hii pamoja na Kamati yetu ya Kisekta ya Kilimo, Maji na Mifugo. Tuliangalia mapendekezo

ya Serikali, kweli tunaona mfumo uliopo wa vocha una uzuri wake, lakini una upungufu pia. Hoja ambazo zimekuwa zinasemwa humu Bungeni na nje ya Bunge ni kwamba mfumo huo unahitaji maboresho makubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lililotusumbua kwenye Kamati ni kwamba, unapohama kutoka kwenye mfumo huu pamoja na upungufu uliopo, unakwenda kujaribu mfumo mpya, matayarisho yake ni bado hayajakaa vizuri. Kamati ya Bajeti imeishauri Serikali kwamba tusipoteze fedha za *World Bank* Shilingi bilioni 19.9 ni fedha nyingi, wao wanataka pesa hiyo pamoja na kwamba ni mkopo, ndiyo ni mkopo lakini tulikubaliana nao kwamba tutatumia kwa utaratibu wa ruzuku ya vocha.

Sasa tunasema zile fedha zetu mtakapofika kwenye ukurasa wa 236 mtaona zile pesa Shilingi bilioni 75 kwenye *crop development* za *World Bank* utazikuta kwenye *volume IV* ya maendeleo. Lakini sisi tunapendekeza hivi, katika zile pesa zetu, tuchukue nusu yake iende kwenye vocha, ziende sambamba na zile za *World Bank* na nusu nyingine tukaanze maandalizi kwa utaratibu wa mikopo hii ambayo inapendekezwa na Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sisi tunaamini tukienda namna hiyo tutaua ndege wawili kwa jiwe moja. Ninaiomba Kamati yako ituunge mkono kwenye Kamati ya Bajeti kwa sababu bado tunaendelea na mazungumzo na Serikali kwenye eneo hili kwa lengo la kuangalia uwezekano wa kuongeza fedha kwenye Wizara hii kwa upande wa kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. *(Makofi)*

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kuniona.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni ukweli usiofichika kwamba kama kuna mahali nchi hii inaibiwa, ni katika mfumo huu unaoendelea wa sasa na kwamba *report* ya *Controller and Auditor General* ambayo mmoja wa Wabunge aliinukuu

ndani ya ukumbi huu, ni ukweli unaodhihirisha na wamechelewa sana kuuona ukweli huu.

Sasa rai yangu ni kwamba ukipeleka fedha hizi ghafla kwenye umwagiliaji, mimi niliye na mto Ruvu nitanufaika. Lakini wale wengine wasiokuwa na mito ya kumwagilia ambao wanategemea mbolea ili waweze kupata chakula, nao utakuwa umewatupa. Kwa hiyo, bado nataka niungane na pendekezo la Mheshimiwa Chenge kwamba katika kuondoka kwenye mfumo huu, ni lazima maandalizi yawepo.

Kwa hiyo, bado ni rai yangu kwamba Serikali kabla hatujamaliza Mkutano huu itupe utaratibu ambao Bunge hili litaridhia juu ya namna ya kudhibiti fedha hizi zinazokwenda huko ili thamani halisi iweze kupatikana sambamba na kutupa mpango mahususi wa kuelekea kwenye utaratibu mpya, maana nao una mgogoro. Maana mkisema fedha zitapitia Benki kisha ziende kwenye Ushirika, utafanyaje kwa Wilaya nyingine zisizokuwa na Vyama vya Ushirika? *(Makofi)*

Kwa hiyo, bado nasema jambo hili bado ni bichi, lakini tusiamue ghafla kwamba fedha hizi zihame kwenda kwenye umwagiliaji kabla hatujapata undani wa mpango ambao Serikali inao. Ila naiomba Serikali ielekeze nguvu kuwabana mafisadi wote waliohusika katika kuchakachua mpango huu ambao una maslahi makubwa kwa nchi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Machali.

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tu niseme kwamba unapokwenda kukopa mahali popote halafu hujajua namna gani ambavyo unaweza ukautumia mkopo wako vizuri, utakuwa ni wendawazimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bunge lako limekuwa kwa nyakati tofauti Wabunge wakipiga kelele juu ya kuchakachuliwa au kuibiwa kwa hizi ambazo tunaziita ni

pembejeo za kilimo. Tumetoa mifano mingi kutoka katika maeneo ya Majimbo yetu. Mfumo uliopo haufai, haufai na hakuna na hakuna namna kwamba tunaweza tukadhibiti wizi wa mbolea. Hata hiki ambacho Mheshimiwa Waziri ametueleza kwamba leo watakwenda waanze kutumia Vyama vya Ushirika, kwanza naomba niseme kwamba ushirika nchini haujaimarishwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niseme kabisa kwamba, yeyote ambaye anapingana na suala la kwamba hizi pesa tusizipeleke kwenye *irrigation*, basi kuna uwezekana kuna baadhi ya watu wananufaika na suala hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Waziri atueleze kwenye ushirika watadhibiti namna gani? Wakati wametueleza kwenye tumbaku tu, kuna tatizo kubwa! Hata huko kwetu Kasulu ni matatizo! Waziri tumemweleza kwa nyakati tofauti kwamba watu wanaibiwa fedha zao. Hizi fedha watakwenda kuzi-*control* namna gani ili kusudi zisiingie kwenye mikono ya watu wachache? Hawa Ma-*DALDO,* hawa Ma-*DC* ambao ndio Wenyeviti wa Kamati za Pembejeo, ni saa ngapi wamekuwa malaika ili kusudi waende kusimamia fedha hizi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tuungane na hoja ambayo imetolewa na Mheshimiwa Kabwe Zitto, hizi fedha tukubali kuzipeleka kwenye *irrigation* ili tuondokane na suala la Bunge letu kuwa kama *rubber stamp* kwamba kila kinacholetwa na Serikali basi kipite kama kilivyo. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante.

**MHE. PETER J. SERUKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili ningeomba sana Waheshimiwa Wabunge tulitafakari vizuri sana. Mambo yote mawili ni mazuri sana, lakini najiuliza na kwenda mbali zaidi; hivi tunataka kwa leo Bunge hili tuhalalishe udhaifu wetu kwamba upo mtandao wa wizi? *Yes!* Tumeshindwa ku-*deal* nao? Kwa sababu jambo la mbolea tunakubaliana wote ni jambo jema ili tuweze kuwasaidia wakulima wetu. *(Makofi)*

Tunaposema maisha bora, hii ndiyo sehemu ya kuwasaidia watu wetu kwa dawa na kila kitu. Lakini leo mfumo huu una wizi. Hatuwajui wezi? Tuna TAKUKURU na viongozi, leo tunataka ku-*surrender* kwamba sababu wezi wapo, tumeshindwa kuwakamata, sasa tubadilishe mfumo twende kwenye umwagiliaji. Kwenye umwagiliaji nako wakiiba, itabidi tuache twende kwenye kitu kingine. Haiwezekani! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachosema, umwagiliaji tunautaka sana, na kwa kweli hata mwanzo nilitaka kusimama ili niiombe Serikali kwenye bajeti inayokuja mwaka kesho angalau tuanze hata na mabonde matatu *massive* katika *irrigation*. Lakini nasema Serikali ije ituambie itafanyaje kulinda fedha hizi za watu zisiendelee kupotea? *(Makofi)*

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, narudi palepale kama nilivyoeleza mwanzo. Tumepata Ripoti ya Mkaguzi. Ripoti ile imeainisha mianya. Hivi tulikuwa tunataka ripoti itusaidie nini? Maana ripoti ile *Management Audit* inatwambia katika mfumo huu maeneo haya, haya na haya, ndiyo mianya! Wizi hauko tu kwenye pembejeo, mbona uko kwenye maeneo mengi? Hata huko kwenye *irrigation* ukienda kuna wizi vilevile. Ndiyo! Wizi uko katika maeneo mengi. Kwa hiyo, siyo kwamba tukiacha hivi, ndiyo tume-*save*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado nasimama pale kwamba jambo kubwa ambalo tunatakiwa kuwatendea haki wakulima wa Tanzania ni kuziba mianya ile inayopelekea wizi katika ruzuku ya pembejeo. Twende na mfumo huu, tuangalie jinsi ya kuboresha, halafu tuangalie tena itakuwaje. Sioni kwanini tuipuuze ripoti ya *CAG? CAG* hajasema tuachane nayo, amesema mianya ni hii na hii, na wanaofanya makosa wachukuliwe hatua.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri Mkuu!

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba nimshukuru sana Mheshimiwa Kabwe kwa kusaidia

kujaribu kuonesha tatizo lilivyo kubwa katika suala hili la vocha. Ndiyo maana hata upande wa Serikali tuliona ni busara *CAG* afanye ukaguzi ili tuweze kubaini kasoro zote na hizo ndizo zifanyiwe kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitakuwa mtu wa mwisho kukubali kwamba pamoja na kasoro zilizopo, kwamba mfumo wa vocha haujawasaidia wakulima. Siyo kweli! Si kweli! Siyo kweli hata kidogo! Wapo wakulima wengi ambao wamenufaika sana na utaratibu huu. Mimi nataka niamini kwamba kama isingekuwa juhudi hata hizi kidogo ambazo zimeonekana, kwa hali ilivyo, hata tusingekuwa tumefika hapa tulipo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niliombe sana Bunge lako, tusije tukafanya uamuzi wa haraka haraka wa kuadhibu wakulima wale ambao tayari wameishaona faida kubwa ya jambo hili kwa sababu ya upungufu wa watu fulani. Ilimradi tumeishasaidiwa, kazi iliyobaki ni kusimamia vizuri zaidi utaratibu utakaotuwezesha kuwanufaisha watu wengi zaidi kuliko ilivyo hivi sasa.

Nakubaliana kabisa na alichokisema Mheshimiwa Chenge na Mheshimiwa Ole-Sendeka kwamba, pengine ingekuwa ndiyo mwelekeo mzuri wa namna ya kusimamia jambo hili. Vinginevyo tutarudi nyuma kwa kiasi kikubwa sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Labda niulize, hivi ripoti ya *CAG* nyie watu wote Wizara na *Public Accounts Committee*, mmeishaisoma? Naomba mnijibu hili swali. Waziri umeshasoma ripoti ya *CAG* ambayo umetuonesha hapa? *Public Accounts Committee* wameisoma? Mheshimiwa Zitto!

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesoma ndiyo maana nimeitumia.

**MWENYEKITI:** Aah, siyo kuisoma wewe, *Public Accounts Committee!* Siyo wewe, ni *Public Accounts Committee.*

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa naongea kama Mbunge wa Kigoma Kaskazini, siongei kama Mwenyekiti wa Kamati.

**MWENYEKITI:** Aah, basi hamjasoma ripoti hiyo. Haya eleza sasa waliyokutuma.

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nikubaliane kuna watu wachache ambao wanafaidika. Naomba ninukuu wanaonufaika: "Baadhi ya wajane katika kijiji hicho cha Kibena, (Jimbo lako Mheshimiwa Spika), Maria Fuwime alisema kuwa kwa upande wake ameshangazwa kusikia katika Mkutano wa Hadhara jina la Marehemu mume wake Yohana Mteve linasomwa na lipo kwenye orodha ya wananchi waliofaidika na mpango huo wa pembejeo." Kwa hiyo, wapo wanaofaidika. Hii ni taarifa ya Mwandishi Francis Godwin ambaye amefanya uchunguzi. Wapo wanaofaidika. Wale wanaogawa hizi vocha wanafaidika, lakini sio wananchi wengi wanaofaidika. Hili ndiyo tatizo ambalo tunalo katika mfumo mzima wa mbolea ya ruzuku. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia nikupe *reference* moja. Hii siyo mara ya kwanza tunabadilisha mfumo. Mwaka 2012 Mheshimiwa Waziri alisema, katika kukabiliana na changamoto hizo za wizi wa mbolea ya ruzuku, alijibu swali hapa Bungeni kwamba, msimu wa mwaka 2012/2013 Makampuni ya Pembejeo ndiyo yatakayoteua Mawakala wa Pembejeo. Huu ulikuwa ni msimu wa pili, imeonekana una wizi, una matatizo, bado mbolea haifiki kwa wakulima! Bado mbolea inafika imechelewa! Kwa hiyo, hamna mfumo tutakaobadilisha ambao utasaidia hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, narudia kwa Naibu Waziri ambaye ni mchumi mwenzangu. Miaka mitano kabla ya kuanza kutumia mbolea ya ruzuku, ukuaji wa sekta ya kilimo ulikuwa ni zaidia ya asilimia tano. Miaka mitano baada ya kutumia mbolea ya ruzuku ukuaji wa Sekta ya Kilimo ni wastani wa asilimia tatu. Ndiyo *evidence*! *Evidence base* ni *facts*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba tu nitoe Shilingi tuondoe jambo hili. Hatuwezi kuendelea kupoteza fedha za umma kwa ajili ya kuwapelekea watu wachache, Makampuni machache yanayoagiza mbolea na viongozi wachache wanaochakachua mbolea za ruzuku kwa wananchi. Hatuwezi kukubali kuendelea kupoteza fedha za umma. Naomba Wabunge wapige kura. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, wale wanaofikiri mara moja tuamue kwamba ruzuku iondoke waseme ndiyo. *(Kicheko/Makofi)*

**WABUNGE FULANI:** Aah, rudia. *(Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Narudia. Fedha zilizotengwa humu kwa ajili ya mbolea ya ruzuku ziachwe zitumike kwa ajili ya umwagiliaji, waseme ndiyo.

**WABUNGE:** Ndiyooo!

**MWENYEKITI:** Wanaosema kwamba utaratibu wa sasa wa vocha uendelee ili uboreshwe waseme siyo..., *no, no!* *(Kicheko)*

Wale wanaosema utaratibu wa mbolea sasa usiende kumwagilia ili utaratibu uweze kuangaliwa upya waseme..., *no,no*, narudia tena. *(Kicheko)*

Ngoja ikae vizuri. Wale wanaosema utaratibu wa kupeleka fedha yote kwenye umwagiliaji waseme siyo.

**WABUNGE:** Siyooo!

**MWENYEKITI:** Nafikiri waliosema siyo wameshinda. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Hamna. Tunapiga kura wapi?

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kukataliwa)*

*(Hoja ya Mheshimiwa Kabwe Z. Zitto ya kupeleka Fedha za Ruzuku ya Mbolea katika Umwagiliaji ilikatiliwa na Bunge)*

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**MWENYEKITI:** Basi Waandishi wa Habari watasema Mama Makinda kababaika, nini; si ndiyo wanavyopenda kuandika! Wakaandike vizuri! *(Kicheko)*

Tunaendelea.

Kif. 1002 - *Finance and Accounts............Tshs 1,404,605,000/=*

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 1003 - *Policy and Planning .............Tshs 1,569,362,000/=*

**MHE. MASOUD ABDALLA SALIM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Nipo hapo kwenye sera na mipango, kwenye *item 220900 - Training (foreign).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye mwaka 2011/2012 kulikuwa na sifuri, mwaka 2012/2013 sifuri, lakini mwaka 2013/2014 kuna Sh. 9,100,00/=.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kuelewa, ni mafunzo gani na ya aina gani mliyopanga kwa watumishi wetu nje ya nchi? Naomba ufafanuzi. Nashukuru.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hii *function* ya *training* iko kwenye maeneo mengine. Hapa kifungu hiki ni kwa ajili ya kugharamia tu mafunzo, *outfit allowance* na nini. Ni posho ndogo ndogo kwa ajili ya kuwawezesha wale wanaosafiri kwenda nje ya nchi. Kimsingi wale wanaotoka kwenda kwenye mafunzo kwa kila Idara wanagharamiwa na Idara zao wenyewe.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 1004 - *Agriculture Training Institute….Tshs 8,429,419,000/=*

**MHE. SELEMAN S. JAFO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nilitaka nipate maelezo katika kifungu hicho cha 1004, *item* ya 220300 - *Fuel, Oils, Lubricants* ambayo imepungua kutoka Shilingi milioni 316 mpaka Shilingi milioni 210 na nikijua kwamba eneo hili ndipo Vyuo vyetu vya mafunzo vinapata fedha kwa ajili ya kuendeshea shughuli mbalimbali hasa matrekta na vifaa mbalimbali vinavyohitaji mafuta.

Sasa kwa bahati mbaya sana Vyuo vyetu vimekuwa katika mazingira magumu sana. Nataka nifahamu ni kwanini karibu Shilingi milioni 100 imepungua katika eneo hilo? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Umetaja kifungu, lakini hujataja *small items.*

**MHE. SELEMAN S. JAFO:** Ni *item* 220300.

**MWENYEKITI:** Umekiona?

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Nimekiona.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Murji kwanza.

**MHE. HASNAIN M. MURJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *sub vote* 1004 - *Agriculture training*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mchango wangu wa maandishi, tuna vijana wengi wamemaliza Vyuo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Murji tuko kwenye Kamati ya Matumizi. Kwa hiyo, unapaswa kuwa *specific* ni kifungu gani unachokizungumzia? Siyo jumla tu.

**MHE. HASNAIN M. MURJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *sub-vote 1004*, kifungu 210100 - *Basic Salaries – Pensionable Posts*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwamba hizi fedha ni nyingi ambazo zinaelekezwa katika mshahara, lakini ni fedha ambazo ziko katika *training*. Tuna vijana zaidi ya 600 tangu mwaka 2011, mwaka 2012 na mwaka huu ambao wamemaliza Chuo cha Naliendele *MATIs* lakini hawajaajiriwa. Sasa hizi Shilingi bilioni nane bado kupeleka, ni sawa na kukalia bomu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka kujua: Je, vijana hawa ambao tayari Serikali iliwaahidi kwamba mara wamalizapo Chuo wataajiriwa, lakini mpaka leo hawaajiriwa...

**MWENYEKITI:** Katika kilimo?

**MHE. HASNAIN M. MURJI:** Naam!

**MWENYEKITI:** Wale waliomaliza Chuo ni kwenye Kilimo?

**MHE. HASNAIN M. MURJI:** Ndiyo.

**MWENYEKITI:** Chuo gani?

**MHE. HASNAIN M. MURJI:** Chuo cha Naliendele *MATIs*. Kuna vijana zaidi ya 600 tangu mwaka 2011, mwaka 2012 na mwaka huu hawajapata ajira.

**MWENYEKITI:** Haya, sawa tumekuelewa.

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Naomba nijielekeze kwenye kasma 220800 - *Training Domestic.*

Itakumbukwa wakati nachangia leo asubuhi nilizungumzia juu ya maendeleo ya Chuo cha Kilimo cha

Mbondo kilicho katika Wilaya ya Kasulu. Naona hapa kuna fedha kidogo zimeongezeka kutoka zile za mwaka 2012 ambazo zilikuwa kama Shilingi bilioni 2.637 na sasa ni Shilingi bilioni 3,133. Katika majumuisho ya Mheshimiwa Waziri sikusikia akizungumzia suala ambalo nilizungumzia la tatizo la maji ambalo linakikabili Chuo kile, tatizo la ukosefu wa shule kwa ajili ya wafanyakazi ambao wanafanya kazi katika Chuo kile ambacho kiko katika *isolated area*, eneo ambalo ni kama porini, tatizo la umeme na nikasema Mheshimiwa Waziri amefanya ziara katika eneo lile.

Sasa nilikuwa naomba nipate ufafanuzi iwapo Chuo kile kitaweza kupatiwa fedha kutoka kwenye hizi fedha ambazo zimetengwa katika kifungu hiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niishie hapo nipate ufafanuzi.

**MWENYEKITI:** Hilo la mwisho ndiyo swali. Naomba majibu.

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianzie chini, *Fuel, Oils, Lubricants - 220300*. Yeye alisema anaona imepungua, ndiyo imepungua. Hii ni fedha ya mafuta. Sasa kulingana na bajeti iliyopo, huwezi ukaendelea kutumia mafuta mengi. Kwa hiyo, tume-*cut down* gharama za uendeshaji ndiyo maana imepungua kutoka Shilingi milioni 316 mpaka Shilingi milioni 210.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikija kwa Mheshimiwa Machali, labda tu nimpe taarifa kwamba huko mbele tunapokwenda kwenye *development* ataona tumetenga fedha nyingi kama Shilingi milioni 500 hivi, ni kwa ajili ya kukarabati Vyuo, pamoja na Chuo cha Mbondo. Kwa hiyo, shughuli zile za Chuo cha Mbondo zimetengewa fedha kwenye *development*.

**MWENYEKITI:** Yuko mmoja, umemjibu? Murji!

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Murji alikuwa anauliza hapa kwenye kifungu hiki, nadhani alikuwa anaulizia 210100 - *Basic Salaries and Pensionable Posts* kwenye *Agriculture Training Institute.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu ni kwa ajili ya mishahara ambayo inatokana na waajiriwa wote kwenye Vyuo hivi. Sasa imeongezeka kwa sababu kutakuwa na waajiriwa na watumishi wapya watakaoingia kwenye Vyuo vyote 14 vya kilimo nchi nzima.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 1005 - *Internal Audit Unit ..................Tshs 296,744,000/=*

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 1006 - *Procurement Mgt Unit ..............Tshs 629,229,000/=*

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru.

*Sub vote 1006, item 210500 - Personal Allowances in kind*. Kwa miaka miwili mfululizo tulikuwa hakitengewi chochote, lakini mwaka huu wameomba Sh. 22,620,000/= nilikuwa nataka ufafanuzi.

**MWENYEKITI:** Ni za kazi gani? Anataka kujua hizi zimetengwa kwa ajili ya kitu gani?

**MHE. MASOUD ABDALLA SALIM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Niko hapo hapo kwenye kitengo cha manunuzi kwenye *item 229900 - Other Operating Expenses*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ilivyo katika mwaka 2011/2012 ni sifuri na mwaka 2012/2013 ni sifuri, lakini mara hii

ni Shilingi milioni 30 zimetengwa. Kwa uelewa wangu shughuli za Idara zinahitaji ushauri wa kitaalam na pengine kuna mambo mengine ambayo yanahitajika. Ningependa kujua ni ushauri gani wa kitaalam uliokusudiwa? Naomba ufafanuzi.

**MWENYEKITI:** Hizi fedha zina kazi gani? Ndiyo swali lenyewe. Naomba ujibu hayo maswali mawili.

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *210500 - Procurement Management Unit.* Zamani kitengo hiki kilikuwa kama *section* tu. Sasa kimepanda hadhi, kimekuwa *elevated.* Kinapokuwa *elevated* matumizi yanaongezeka hapa na ndiyo maana sasa unaona kimetengewa fungu.

**MWENYEKITI:** Hilo ulikuwa unamjibu Mheshimiwa Ester Bulaya aliuliza. Sasa lingine ni la Mheshimiwa Masoud na hicho cha Masoud ni kifungu kingine. Esther Matiko ndiyo umemjibu. Sasa ni Mheshimiwa Masoud, hamkuipata hiyo?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye hiki kifungu cha *other operating expenses* miaka miwili iliyopita kulikuwa hakuna matumizi yoyote, lakini mwaka huu fedha hizi zimetengewa fedha maalum kabisa kwa sababu kitengo hiki kimepewa kazi ya kutathmini mali zote zilizopo kwenye Idara ya Kilimo na kadhalika. Kwa hiyo, maelezo yake hapa ni kwamba kifungu hiki ni kwa ajili ya malipo ya utayarishaji wa kitabu cha utunzaji wa mali na uwekaji wa alama za vifaa kwenye Wizara. Hii ni kwa ajili ya *register* ya *property* na *assets* zote ndani ya Wizara.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 1007- *Government Communication*... Shs.210,687,000/=

Kif. 1008 – *Legal Unit* .................................... Shs.293,699,000/=
Kif. 1009 - *Mgt Information System Unit* ..... Shs.263,187,000/=
Kif. 1010 – *Environmental Mgt Unit* .......... Shs. 293,225,000/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 2001 - *Crop Development* .......... Shs. 97,201,090,000/=

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Leticia huwa tunasimama baada ya kusoma hesabu. Mheshimiwa Rashid, Mheshimiwa Machangu. Mheshimiwa Leticia kwanza.

**MHE. LETICIA M. NYERERE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu 2001 kasma 220800 – *Training Domestic* mwaka wa fedha 20212/2013 ilikuwa Shilingi milioni tatu, mwaka huu wa fedha wanaomba Shilingi milioni 130 na imeongezeka kama mara 43. Ningependa kupata ufafanuzi ni *training* gani ni au ni matarajio gani ambayo yamepelekea ongezeko hili kubwa ambalo ni mara 43?

**MHE. RASHID ALI ABDALLAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nipo kwenye kasma ya 221000 – *Travel-in-country* mwaka 2012 kulikuwa na Shilingi milioni 429 lakini mwaka huu ni Shilingi milioni 663 takribani nusu ya bajeti ya mwaka 2012. Ni kwa nini zikaongezeka fedha nyingi kama hizo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Rashid umesema nini hiyo?

**MHE. RASHID ALI ABDALLAH:** *Travel-in-country*.

**MWENYEKITI:** *Travel-in–country, okay,* nimeipata. Mheshimiwa Betty Machangu.

**MHE. BETTY E. MACHANGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naomba nijikite katika hiyo sub-vote 2001, yaani *Crop development*. Katika mchango wangu wa maandishi...

**MWENYEKITI:** *Sub-item* gani unayoitaka. Sema sub item hiyo; sasa *item* ndogo, ipi?

**MHE. BETTY E. MACHANGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nilikuwa naomba niulizie kuhusu *crop development* kama *crop development*.

**MWENYEKITI:** Hapana, huwezi. Fedha hizoyo wakati wa sera sasa. Nyie hamjajibu. Naomba mjibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza hili limeulizwa ni *training domestic*. Mwaka uliopita *component* hii ya fedha za mafunzo zilikuwa kwenye upande wa *development*, zilitengwa maalum kwenye upande wa *development*. Lakini sasa mwaka huu fedha zile zimerudishwa huku na kwa sababu *crop development* ndiyo katika Idara kubwa kuliko zote tulizonazo Kilimo hata kwa *OC* yake unaiona.

Kwa hiyo, na *reflection* yake kwenye *training domestic* unaiona ni kubwa kidogo. Lakini ni kwamba zilikuwa zinatengwa kwenye sehemu nyingine. Lakini mwaka huu mafunzo ndani ya Idara ya *Crop Development* yanaonekana yatatokea pale pale badala ya kuwekwa kwenye kasma nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha *travel in country* ni kwa ajili ya kugharamia safari za ndani ya nchi, ikiwemo Mikutano ya kikazi, bajeti imeongezeka ili kufuatilia kazi zilizopangwa kutekelezwa na kuhakikisha malengo yanafikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo hata iwe upande wa mbolea, madawa na kadhalika ufuatiliaji wake bajeti zake zote zipo katika fungu hili kusafiri katika nchi nzima na kwa maeneo yote ya nchi nzima.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 2002 - *Agricultural Mechanization .....* Shs.664,877,000/=

**MWENYEKITI:** Ah, jamani. Basi tunaendelea.

Kif. 2003 - *Agric. Land Use Plan. & Mgt.......*Shs. 671,935,000/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 2004 – *Plant Breedes' Unit ................* Shs.198,280,000/=

**MHE. LETICIA M. NYERERE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kifungu 2004, kasma ya 220600 - *Clothing, Bedding, Footwear and Services* mwaka huu wa fedha tofauti na mwaka 2012 ni Sh. 165/= yaani ni chini ya Sh. 200/= kama hii.

Kwa hiyo, naomba maelezo, ninapata shida kidogo bajeti inayopangwa kwa mwaka mzima inakuwa ni tofauti ya Shilingi milioni 165 ndogo ya Shilingi 200 hii hapa. *(Makofi/ Kicheko)*

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mambo mengine haya, unajua kuna suala la bajeti kuwa finyu. Sasa kama bajeti tuliyonayo haitofautiani sana na ya mwaka 2012 na inabidi angalau hesabu zikamilike. Hiyo tofauti ya Sh. 100/= ndiyo lazima iwekwe.

Sasa huwezi kusema unatupa pale tu kwa sababu ni Sh. 100/=, ni lazima iingie pale. Lakini kwa kifupi mimi nafikiri bajeti ni kama ile ile ya mwaka 2012.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 2005 - *Irrigation & Techn. Service ....* Shs 3,317,466,000/=

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 3001 – *Research Development .......* Shs. 16,512,795,000/=

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Machali, Mheshimiwa Susan Lyimo, Mheshimiwa Jafo, Mheshimiwa Machangu. Mheshimiwa Machali!

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Naomba tujielekeze pale kwenye *item* 220800 kwenye *training domestic*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa najaribu kuweza kufanya hesabu naona kuna uongezeko kubwa sana ambalo ni mara kumi ya kutoka kiwango cha mwaka 2012. Kutoka Shilingi milioni 13.5 kwenda Shilingi milioni 136.2. Ningeomba Serikali iweze kutupa ufafanuzi wa kina ni kitu gani ambacho kimetokea mpaka wanakwenda ku-*train* watu wengi kwa kiasi hiki na je, huko nyuma hali ilikuwa namna gani? Ningeomba tuweze kupata ufafanuzi.

**MHE. SUSAN A.J. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. *Sub-vote 220900 - Training Foreign.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naamini kabisa Kitengo hiki ni cha utafiti na tumekuwa kinapata matatizo makubwa sana ya masuala ya mbegu bora na mambo mengine yanayohusiana na kilimo.

Sasa nataka kujua tu, ni kwa nini watu wetu hawa hawaendi pia kufanya utafiti nje ili waweze ku-*compare* na hapa ndani kwa sababu nikiangalia kifungu hiki kimepata *zero* na siyo mwaka huu tu na hata mwaka 2012. Nilikuwa naomba kupata maelezo ya ufafanuzi kuhusu hilo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Jafo! Naomba m-*mark* mtayajibu.

**MHE. SELEMANI S. JAFO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nataka niulize kasma ya 270300 *current grant to non financial public units* ambayo inalenga katika *academic institutions*. Kuna upungufu wa karibu Shilingi milioni 800. Sasa nikiona katika fungu hili tunalenga hasa katika *research* na bahati mbaya vituo vyetu vipo katika hali mbaya sana. Sasa naona fedha nyingi ipungua. Nataka nijue ni kwa nini imepungua na kama ikiwezekana ni jinsi gani kama Kamati ya Bajeti inaweza ikasaidia eneo hili kuongezewa fedha hapo baadaye?

**MHE. BETTY E. MACHANGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niulize kwenye hiyo *sub-vote 3001* kasma 410400 *Acquisition of specialized equipment.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mashine hizi zipo mashine ambazo za ni za *Coffee Curing* kwa ajili ya ku-*process* kahawa na ku-*process* kahawa kumepungua sana Mkoani Kilimanjaro kwa sababu ya hizi mashine, ambazo wanatumia ni mashine nzee za zamani na wanataka kuuza mali zao nyingine kwa ajili ya kununua mashine ndogo ambazo ni *efficient* zaidi. Kwa sababu maeneo mengine ya Tanzania nao wamefungua *Coffee Curing*. Kwa hiyo, Kahawa inayokwenda Mkoani Kilimanjaro kwa ajili ya *processing* ni kidogo. Kwa hiyo, wanahitaji kununua mashine ndogo ambayo ni *more efficient* na ambayo itawapunguzia gharama kama za umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imekuwa ikiwakatalia. Je, wanataka waendelee kufilisika au Serikali inasemaje?

**MWENYEKITI:** Swali lako hapa ni hizi fedha zilizowekwa ni za kazi gani? Hii habari ya kufilisika nyingine, inatoka wapi? Naomba mjibu maswali.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Machali ameulizia kuhusu *training domestic*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye *training domestic* hapa kuna ongezeko, ni kweli kutoka Shilingi milioni 13.5 mwaka 2012 hadi Shilingi milioni 136 sasa kifungu hiki ni kwa ajili ya manunuzi ya vifaa vya mafunzo. Katika hii Idara ya Tafiti kwa maana vinakusanyika Vyuo vyetu vya Utafiti. Sasa bajeti yake kwa ajili ya kununua vifaa vya mafunzo jumla yake ni Shilingi milioni 136 kwa wanafunzi wa mafunzo ya muda mrefu na mfupi kutokana na mradi wa *ASDP* kukamilika kwa awamu ya kwanza, wanafunzi wanaoendelea na shahada ya uzamilivu kwa mwaka 2013 malipo yatafanywa kutokana na kifungu hiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la Mheshimiwa Susan Lyimo la *training foreign,* ni kweli hata mwaka 2012 fedha hizi hazipangwa. Hizi hapa labda zingehusu safari zinatokana na Watumishi ndani ya Idara hizi za Utafiti, lakini hata mwaka 2012 hatukufanya na hakuna sababu yoyote ya nyingine isipokuwa tu ni ufinyu wa bajeti na kwamba kama watasafiri tutaangalia kutoka kwenye utaratibu mwingine labda *financing* kutoka kwa wafadhili wengine na kadhalika. Lakini kwa fedha zetu wenyewe tulikuwa tumeshindwa kupeleka watu kuwasafirisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili la Mheshimiwa Jafo *item 270300 - current grant*. Hiki sasa ndiyo kifungu pana kama Shilingi bilioni 4.5. Hiki ni kifungu cha kuwawezesha Mashirika yale yanayoshughulikia utafiti ndani ya nchi yetu, ma-*TPRA, TFRA* na kadhalika. Lakini bajeti imeongezeka katika kifungu hiki kutokana na kuongezeka mishahara ya baadhi ya Taasisi.

**MWENYEKITI.** Imepungua.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** *I am sorry,* imepungua. Bajeti iliyotengwa kwa mwaka 2013 ni ndogo kutokana na ukomo wa bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ukiangalia hapa bajeti hii imetoka Shilingi milioni 4.7 mwaka 2011, mwaka 2012, ikaenda Shilingi milioni 5.2 tukashindwa kuifikia. Kwa hiyo, mwaka huu tumejielekeza kwenye ukomo ambao unaonekana ndiyo inaweza kukidhi mahitaji ya Taasisi hizo.

**MWENYEKITI:** La Mheshimiwa Machangu!

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho ni hili la Mheshimiwa Machangu, ameulizia kuhusu *acquisition of specialized equipment* ambapo bajeti ya mwaka huu ni Shilingi milioni 10.

**MWENYEKITI:** Ni *Acquisition of Office and General Equipment.*

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, alitaka 410400 - *acquisition of specialize equipment*.

**MWENYEKITI:** *Okay, okay, okay!*

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Sasa kifungu hiki ni kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya utafiti, kwa maana ya kwenye baadhi ya maeneo, lakini ni fedha ndogo. Kwa hiyo, kuna fedha nyingine ambazo zimekwenda kwenye *agricultural equipment* ambazo pia zita-*save* kufanya kazi pamoja na hizo Taasisi zetu za Utafiti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ndiyo maana unaona kuna fedha hii ndogo hapa.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, kwa mujibu wa Kanuni inabidi niongeze dakika 30 baada ya saa ya kuahirisha Bunge.

Kif. 5001 - *National Food Security .......* Shs. 111,217,095,000/=

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Leticia sasa nitakuwa nakunyima nafasi kwa sababu unasimama kabla ya wakati. Mheshimiwa Murtaza Mangungu.

**MHE. MURTAZA A. MANGUNGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nataka kupata ufafanuzi kwenye kifungu kidogo 270600 ambayo inaonekana kwamba kuna fedha nyingi zimeongezeka kutoka Shilingi bilioni 31 hadi Shilingi bilioni 110, fedha hizi zina matumizi gani na kwa nini zimeongezeka kiasi hiki?

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nami napenda kuuliza kifungu hicho hicho 270600 tupatiwe ufafanuzi hizo fedha zinapelekwa katika *Non-Financial Public Units (Agencies).* Ni *agencies* zipi hizo?

**MHE. RETICIA M. NYERERE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Lakini kilikuwa kifungu hicho hicho ambacho kimeishaulizwa.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hizi ni fedha za *National Food Reserve Agencies* - *NFRA*. Sasa kuna ongezeko hili kubwa kwa sababu mwaka 2012 fedha zilizotengwa tulikusudia tununue mahindi tani 200,000, tukaishia kununua mahindi tani kama 50,000 kwa sababu tulipokwenda sokoni tunakaanza kupambana na sekta binafsi na bei zikapanda ghafla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Serikali mwaka huu imeweka utaratibu kwamba tuwe na fedha za kutosha kuweza kwenda kushindana kwa bei hiyo ya soko ili na wakulima nao wapate manufaa makubwa zaidi ikiwa sisi ndiyo soko kubwa zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tumeweka hatua hii ili pia katika akiba tunayokusudia tuwe na uwezo wa kununua zaidi tani 100,000 ifikapo mwezi Julai na Agosti.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**MIPANGO YA MAENDELEO**

Kif. 1003 - *Policy and Planning* ............. Shs. 8,117,319,900/=

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Machali, Mheshimiwa Wambura na Mheshimiwa Lugola.

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Mimi nilikuwa na swali ndogo tu pale kwenye *item* 4488 kwenye *DASIP.* Naona pale kuna fedha za *local* ambazo zimetengwa Shilingi milioni 250 halafu pale kuna *forex* Shilingi bilioni 1,170. Swali langu ni kwamba hizi fedha zinatoka wapi? Je, ni mkopo au ni *grant?* Maana hakuna *description* pale. Ningeomba tuweze kupata ufafanuzi na ushauri wa

bure tu kwamba *next time* maana yake hii inajitokeza katika maeneo mbalimbali.

**MHE. ANASTAZIA J. WAMBURA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kifungu 4486 *ASDP* tukiangalia kwenye kitabu cha hotuba tunaona kwamba huu mradi wa *ASDP* awamu ya kwanza programu hii inakwisha Juni, mwaka 2013. Lakini sasa utaona kwamba hapa ndiyo fedha zimeongezeka zaidi. Ningependa kujua kwamba zinaongezeka kwa ajili ya nini?

**MHE. ALPHAXARD K. LUGOLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kujua hiki kifungu cha 4488 kinachohuhusu *DASIP*.

**MWENYEKITI:** Tayari kimeulizwa, majibu hayawezi kuwa tofauti.

**MHE. ALPHAXARD K. LUGOLA:** Mimi nina swali lingine tofauti na alilouliza mwenzangu.

**MWENYEKITI:** Haiwezekani! Hela ni hiyo hiyo tu basi. Ndiyo hiyo hiyo na sababu ni moja, haiwezekani kuwa zaidi. Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 4486 *ASDP* amesema ameona fedha zimeongezeka...

**MWENYEKITI:** Kwamba mradi unakwisha.

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Ndiyo mradi unakwisha. Lakini kinachotokea ni hivi, tunapoziomba hizi fedha kuna *activities* ambazo wakati mwingine unakuta hazijafikia wakati. Kwa hiyo, muda unaweza ukawa mradi unakwisha, lakini miradi iliyokuwa ndiyo iko kwenye *design* sasa imekamilika, inatekelezwa. Kwa hiyo, ndiyo majibu yake.

Halafu kifungu 4488 hili ni ongezeko la ujenzi wa miradi vilevile, hili ni *DASIP. DASIP* ilikuwa na matatizo hayo hayo

kwanza wakati inaanza miradi ilianza kwa kusuasua kwa ajili ya *design,* baada ya hapo sasa miradi ime-*pick up* ndiyo inajengwa sasa kwa haraka. Kwa hiyo, fedha inayotumika ni nyingi.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu Kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

Kif. 1004 – *Agriculture Training Institute*..... Tshs. 600,070,000/=

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa nafasi. Nilikuwa kwenye kifungu kidogo 2221, natambua kwamba fedha hizi ni kwa ajili ya ukarabati wa Vyuo kama ambavyo Mheshimiwa Waziri alipomjibu Mheshimiwa Machali kwenye suala lake katika *Volume II*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na Waziri kusema kwamba fedha zimeongezeka, mimi naona fedha zimepungua kutoka Shilingi milioni 100 na mwaka 2013 ni Shilingi milioni 40 ukizingatia kwamba Vyuo vyetu vingi vya Kilimo ni vichakavu sana. Sasa nilikuwa naomba maelezo ni kwa kiasi gani wanategemea kwamba fedha hizi zinaweza kukarabati Vyuo vyetu ambavyo ni vingi sana na ni vichakavu sana hali inayopelekea wanafunzi kuishi katika mazingira mabovu sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Jafo.

**MHE. SELEMANI S. JAFO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante na mimi nilikuwa katika eneo hilo hilo, kwa hiyo, sina la ziada.

**MWENYEKITI:** Basi tena, huwezi. Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha tulizonazo ni hizo unazoziona zimetengwa hapo Shilingi milioni 560 na ndizo hizo nilizomwahidi, nikamwambia Mheshimiwa kwamba huko mbele ataona Shilingi milioni 300.

**MWENYEKITI:** Siyo! Ni kifungu 2221, Shilingi milioni 40 tu.

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** *Agricultural Training!* Ndiyo, ndiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunayo programu ya kuendeleza zao la mpunga na tunafanya utafiti kwa ajili ya *systems of rice intensification.* Kwa hiyo, hizi fedha zimetengwa kwa ajili hiyo.

**MWENYEKITI:** Uliyomsemea Mheshimiwa Machali kwamba iko ya ujenzi, iko wapi?

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA**: Mheshimiwa Mwenyekiri, ya Shilingi milioni 500 pale ukienda chini 4486 utaona *Agricultural Sector Development Programme,* mwisho kabisa utaona Sh. 560,070,000/= hizo sasa ni kwa ajili ya ukarabati wa Vyuo vya Kilimo pamoja na Chuo cha Mugondo.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

Kif. 2001 - *Crop Development*................Tshs. 31,883,396,400/=

**MHE. BETTY E. MACHANGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuulizia kasma ya 6505 - *Lake Victoria Environment Management Project.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ziwa Victoria ni chanzo kikuu cha maji kwa Ukanda wa Ziwa na ni chanzo kikuu pia cha samaki ambao wanakuwa *exported Europe*. Lakini hivi karibuni tumeanza kusikia kwamba Ziwa Victoria samaki wanakwisha. Mwaka 2012 tumepewa Sh. 47,000,000/=...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Machangu mnapofika katika utaratibu huu, hakuna hotuba, ni kwamba hizi fedha mbona hazikutengwa, ile shughuli imeishia wapi? Lakini siyo

tena utuhutubie wenzio, siyo hivyo. Sasa ndiyo hilo analotaka kuuliza.

**MHE. ANDREW J. CHENGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kasma 4491 zile fedha za *World Bank* kwa upande wa ruzuku ya mbegu na mbolea. Nataka tu nijue hizi fedha Shilingi bilioni 19.9 au ni Shilingi bilioni 23 kama inavyoonekana kwenye kitabu hiki?

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nilipenda kuuliza kwenye kifungu kidogo 4495, katika Mradi huu wa *East Africa Agriculture Productivity Programme* hazijatengewa fedha zozote za ndani ila zimetengwa fedha nyingi za nje na utegemezi wa fedha za nje tumeona ina athari. Naomba tupate maelekezo kwa nini hazijatengwa fedha za ndani.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Naomba majibu?

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ngoja nianze na Mheshimiwa Paresso, fungu 4495 ambalo hatukutenga fedha za ndani zozote pale. Kwanza ni kwa sababu ya ufinyu wa bajeti, lakini pia huu mradi wa *EAAP* kwa bahati nzuri wafadhili wenyewe wanakubali kabisa kwamba *whether* tuna fedha *local* au hatuna, wao fedha zao zinatumika na haupo kwa ajili ya Tanzania tu, uko katika *East Africa* na nchi nyingine. Kwa hiyo, kutokana na ufinyu wa bajeti sisi hatukuweza kutenga na kwa kuwa haituathiri, tukaona ni sawa.

**MWENYEKITI:** Mengine yale? Ehe!

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye kasma 4491 Mradi wa Usalama wa Chakula *(Accelerated Food Security Project).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama alivyosema Mheshimiwa Mtemi Chenge - Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti, ni kweli kwamba fedha zile ambazo *World Bank* imetoa kwa ajili ya vocha za ruzuku zinakuja kwenye Shilingi bilioni 19.9

kwa ajili ya Mikoa 23. Lakini hapa *sub total* ya *figure* hiyo inasomeka 23 kwa sababu hapo katikati pana Shilingi milioni 700 kwa ajili ya kuandaa na kusambaza vijarida kwa ajili ya matumizi bora ya mbegu za mpunga na kadhalika. Hapo hapo kwenye kasma hiyo hiyo kuna fedha kama Shilingi bilioni 1.2 kwa ajili ya kuwawezesha Mawakala wa Pembejeo kuanzisha vijishamba vya mfano kwa ajili ya wakulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, pana fedha mbalimbali pana vikasma vidogo vidogo mbalimbali ambavyo vyote vina-*form part* ya hiyo *Accelerated Food Security Project* ambayo jumla yake inakuwa Shilingi bilioni 23.098 ambayo ina-*include* Shilingi bilioni 19.9 za mfumo wa vocha.

**MWENYEKITI:** Suala la Mheshimiwa Machangu alilosema katika *Lake Victoria Environmental Management Project,* mbona hakuna kitu?

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi huu wa *Lake Victoria* huko nyuma fedha zilikuwa ziko Wizara ya Maji. Sasa ilikuwa tunaletewa na sisi *component* yetu inayohusu *activity* ambazo ni za kilimo kilimo. Kwa mfano, wale wadudu wanaopandwa mle kwa ajili ya kula magugu, ni mambo ya kilimo. Sasa fedha hizi kwa mwaka huu hazikuletwa kilimo. Kwa hiyo, hatuna fedha hizo.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

Kif. 2002 - *Agricultural Mechanization*.....Tshs. 3,210,985,600/=
Kif. 2003 - *Agricult. Land Use Plan. & Mgt...*Tshs.930,000,000/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

Kif. 2005 - *Irrigation &Techn. Service*......Tshs. 26,391,716,100/=

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kifungu kidogo 4066. Nilikuwa naomba tu maelezo, wote tunajua kwamba fedha...

**MWENYEKITI:** Hatujakupata vizuri, wapi unauliza?

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Kifungu 4486.

**MWENYEKITI:** Ni *Agriculture Sector Development Program eh!*

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Ndiyo.

**MWENYEKIRI:** Ehe!

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, wote tunatambua kwamba kutokana na mabadiliko ya tabianchi, kilimo cha kutegemea mvua sasa hivi hakiwezekaniki tena zaidi ya kupata kilimo cha umwagiliaji. Lakini nikiangalia naona kwamba mwaka huu hakuna hata Shilingi moja iliyotengwa kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji kwa fedha zetu za ndani. Nilikuwa naomba maelezo kutoka kwa Mheshimiwa Waziri ni kwa nini hali hii iko hivi wakati wanajua wazi kwamba kilimo chetu sasa hivi kinategemea zaidi kilimo cha umwaliaji?

**MHE. ANASTAZIA J. WAMBURA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kifungu kidogo 4486 - *ASDP*.

**MWENYEKITI:** Kimeshaulizwa huwezi kuuliza tena.

**MHE. ANASTAZIA J. WAMBURA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu ni tofauti.

**MWENYEKITI:** Haiwezekani kuwa tofauti hela ni hizo hizo.

**MHE. ANASTAZIA J. WAMBURA:** Ni tofauti Mheshimiwa Mwenyekiti!

**MWENYEKITI:** Haiwezekani, ni hela za *foreign* kwa ajili ya *Irrigation*.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Ahsante Mheshimiwa Mwenyekiti. Nami niko katika *sub vote* hiyo hiyo. Nashukuru.

**MWENYEKITI:** Haiwezekani.

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa najielekeza kwenye hii *sub vote* 4493 ya *SAGCOT*.

**MWENYEKITI:** Sawasawa.

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia *SAGCOT* ni kama vile inapewa *priority* kubwa kuliko kanda nyingine kama za *Western Corridor* ambako tunatoka sisi huko Mikoa ya Kigoma na kwingineko. Nimejaribu kuangalia kwenye *sub vote* ambayo tumetoka, zimetengwa fedha kwa ajili ya *agriculture, land use planning and management.*

**MWENYEKITI:** Aaah, tunazungumzia hiki hapa ulichokisema sasa unatoka.

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, niko hapa hapa najenga hoja.

**MWENYEKITI:** Aaah, hakuna hoja hapa!

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, basi ngoja niulize swali.

**MWENYEKITI:** Ehe!

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa naomba Waziri aweze kutupa sababu ambazo zimeifanya Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika kutenga fedha nyingi sana kwa ajili ya *SAGCOT* na kusahau maeneo mengine kama *Western Corridor* ambayo naizungumzia kama kwetu Kigoma na kwingineko hasa kwenye suala la

*irrigation* pamoja na *technical services* kwa kuwa tuna mabonde mengi sana.

**MWENYEKITI:** Hilo siyo swali. Wewe ungesema kwa nini hizi fedha ziko hapa? Sasa mengine mbona sisi hatuyaoni, unayosema wewe? Haya uliza swali lako vizuri, kwa nini hela ziko nyingi au ziko pungufu?

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *issue* yangu ilikuwa ni hilo tu kwamba nataka nihoji kwa nini wanatenga fedha nyingi kwa ajili ya *SAGCOT* halafu kwetu wametusahau?

**MWENYEKITI:** Wapi nyingine umeziona? Mheshimiwa Naibu Waziri naomba ujibu mengine hayo. Jibu lile la kwanza la Mheshimiwa Susan Lyimo ndiyo lina-*cover* yote.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa pana fedha zimetokana na vyanzo viwili. Pana fedha zimetokana na Japan *Policy of the Human Resource and Development* - *PHRD* pana fedha za *ASDP* ambazo zote kama tulivyosema hizi fedha za *ASDP* ndiyo zinamalizia *ASDP* awamu ya kwanza. Kwa hiyo, zimetengwa Shilingi bilioni tisa, ziko kazi ya aina mbalimbali. Fedha hizo jumla Shilingi bilioni tisa zimetengwa katika jumla ya kazi kama 28 hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naogopa kuchelea kuzisoma zote kwa ajili ya muda lakini zote ni kugharamia kuwawezesha wakulima, mabwawa, mafunzo, umwagiliaji wa mpunga na kadhalika. Hili la pili la Mheshimiwa Machali, nilikuwa nafikiri Mheshimiwa alikuwa anataka kujua kwamba...

**MWENYEKITI:** Ehe, alitaka kujua nini?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Hizi Shilingi bilioni 17 kazi yake nini.

**MWENYEKITI:** Eeh, hilo ndiyo swali.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti kuna kujenga miundombinu ya umwagiliaji kule Sonjo, kuna kuanza ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji Ngalimila, kujenga miundombinu ya umwagiliaji Lupilo kule karibu na Kilombero kule ndani kwenye miradi ya Sukari, kujenga miundombinu ya umwagiliaji katika Skimu ya Utete hekta 1,000, kuwezesha *NFRA* kujenga ghala la kuhifadhi nafaka kwenye maeneo hayo ya *SADC* kwa ajili kilimo kitakachokuja na kuwezesha *RUBADA* kupima na kuweka maeneo hayo tayari kwa ajili ya uwekezaji kama Shilingi bilioni 2.3. Kwa hiyo, jumla yake ndiyo unapata hizo Shilingi bilioni 17 ambazo ni fedha za ndani.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

Kif. 3001 - *Research Development* ..........Tshs. 9,706,800,000/=

**MHE. LETICIA M. NYERERE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kifungu 3001 kasma ya 4486 *(Agricultural Sector Development Programme).* Mwaka huu, fedha nyingi ambazo zinategemewa kwenye huu mradi zinatoka nje ambazo ni Shilingi milioni 540 ambayo ni kama asilimia 60 ya fedha zote ambazo zinatakiwa kwa ajili ya *research development.*

Sasa swali, *in case* hawa Wafadhili wasipotoa hizo fedha ina maana *research* haiwezi kufanyika?

**MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, niko katika *item* 4495 - *East Africa Agriculture Productivity Program*. Hii ni *research* ambayo inasaidia wakulima wetu, ambao inasaidia maendeleo katika Afrika Mashariki. Naamini kwamba nchi za wenzetu wametenga fedha zao za ndani katika masuala mazima ya *research.* Lakini sisi tumetegemea hizi Shilingi bilioni nane kutoka *World Bank?*

Mheshimiwa Waziri *are serious with this?*

**MWENYEKITI:** Aaah! Wewe ungeuliza kwa nini hatujatenga *domestic?* Hawa wengine umeziona wapi?

**MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMED:** Kwa nini Mheshimiwa Waziri hatujatenga fedha za *domestic* hapa?

**MWENYEKITI:** Eeh, hilo ndiyo swali.

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, labda nianze na ile 4486. Jumla ya Shilingi milioni 790 hapo pana miradi mitano ambayo inatekelezwa. Kwa hiyo, hata ukitazama Shilingi milioni 790 siyo hela nyingi hizi kwa kukamilisha miradi mitano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kwa upande wa pili wa *East Africa Agriculture Productivity* nilieleza tangu mwanzo kwamba huu mradi una-*cover* nchi za Afrika Mashariki, nadhani na Ethiopia pia. Sasa wao kwa makubaliano tuliyofanya ni kwamba hata kama kuna *local component* au haipo, wao fedha zao zipo na tuna hakika nazo. Lakini pia ukitazama huko tulikotoka, tumetenga fedha nyingine za *research* kwenye vifungu vya *Reccurent,* hizi ni za *development*.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

Kif. 5001 - *National Food Security*................Tshs. 200,000,000/=

**MWENYEKITI:** Haya tuanze na Mheshimiwa Jenista Mhagama, Mheshimiwa Shekifu hapa ni kitu kimoja tu, mimi nakwambia nyie wote mtahangaika.

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni ufafanuzi tu. Kwenye *Volume II Food Security* imetengewa Shilingi bilioni 111.

Sasa kwenye kitabu hiki cha *Development Food Security* pale *Agricultural Sector Development Programme* imetengewa hiyo Shilingi milioni 200.

Nilichokuwa naomba ufafanuzi kwa Mheshimiwa Waziri ni kutaka kufahamu matumizi ya hii Shilingi milioni 200 itakuwa ni kitu gani? Labda ni kwenda kujibu tatizo la kununua mizani ili kurahisisha upimaji wa mahindi ya wakulima ama kazi zake ni nini? Nipate tu ufafanuzi kwa Mheshimiwa Waziri kwa sababu kule nimeona yale mabilioni mengi, sasa na hapa nataka ufafanuzi vizuri.

**MWENYEKITI:** Hizi hela ni za kitu gani?

**MHE. HENRY D. SHEKIFU:** Swali langu ni kama hilo hilo, kazi yake ni nini?

**MWENYEKITI:** Nilijua tu wote swali ni moja tu. Kwa hiyo, hamna namna.

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha hizi...

**MWENYEKITI:** Ni kifungu kimoja tu. Kwa hiyo, hakuna maswali zaidi ya hapo. Msikilizeni Waziri.

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA**: Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha hizi ambazo zimetengwa jumla ya Shilingi milioni 200 zina kazi kama tatu hivi. Moja ni kununua mashine kwa ajili ya teknolojia hizi za kufanyia kazi za usindikaji. Kazi nyingine ni kujenga wanaita *park house* sijui zinaitwaje Kiswahili!

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hatusikii!

**MWENYEKITI:** Kwa Kiswahili hivyo hivyo!

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA**: Kiswahili sikijui, lakini yote ni kwa ajili ya usindikaji wa mazao kama matunda. Kwa hiyo, hizi Shilingi milioni 200 ni kwa ajili kazi hizo.

*(Kifungu Kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

*(Bunge lilirudia)*

**T A A R I F A**

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA**: Mheshimiwa Spika, naomba kutoa taarifa kwamba Bunge lako Tukufu limekaa kama Kamati ya Matumizi na kupitia Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika kwa mwaka 2013/2014 kifungu kwa kifungu pamoja na mabadiliko yaliyoletwa na Hazina na kuyapitisha kwa pamoja. Hivyo, naomba sasa Bunge lako Tukufu liyakubali na kuyapitisha Makadirio haya.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika kwa Mwaka 2013/2014 yalipitishwa na Bunge)*

**SPIKA:** Napenda kuchukua nafasi hii kuwapongeza Wizara, Mawaziri na wataalamu wao kwa kazi njema. Kama walivyoona Waheshimiwa Wabunge walivyokuja juu na Kilimo, basi kipindi kijacho mjitahidi yale ambayo wamezungumza myazingatie tuweze kuendelea mbele zaidi.

Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge, sina matangazo, naahirisha Kikao cha Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 2.00 usiku Bunge liliahirishwa mpaka Siku ya Jumatano, Tarehe 24 Aprili, 2013 Saa Tatu Asubuhi)*